BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

2016 - 2020

1.	**Mhe. Zubeir Ali Maulid**	**-**	**SPIKA**
2.	**Mhe. Mgeni Hassan Juma**	**-**	**Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake**
3.	**Mhe. Shehe Hamad Mattar**	**-**	**Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni**
4.	**Mhe. Mwanaasha Khamis Juma**	**-**	**Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani**
5.	**Mhe. Balozi Seif Ali Iddi**	**-**	**MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda**
6.	**Mhe. Issa Haji Ussi Gavu**	**-**	**MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka**
7.	**Mhe. Haji Omar Kheri**	**-**	**MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi**

			ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
8.	**Mhe. Haroun Ali Suleiman**	**-**	**MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi**
9.	**Mhe. Mohammed Aboud Mohammed**	**-**	**MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais /Uteuzi wa Rais**
10.	**Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed**	**-**	**MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge**
11.	**Mhe. Mahmoud Thabit Kombo**	**-**	**MBM/Waziri wa Habari, Utalii, na Mambo ya Kale/Jimbo la Kiembesamaki**
12.	**Mhe. Riziki Pembe Juma**	**-**	**MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake**
13.	**Mhe. Balozi Amina Salum Ali**	**-**	**MBM/Waziri wa Biashara, na Viwanda / Uteuzi wa Rais**
14.	**Mhe. Balozi Ali Abeid Karume**	**-**	**MBM/Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo/ Uteuzi wa Rais**

15.	**Mhe. Rashid Ali Juma**	**-**	**MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Amani**
16.	**Mhe. Hamad Rashid Mohamed**	**-**	**MBM/Waziri wa Afya / Uteuzi wa Rais**
17.	**Mhe. Maudline Cyrus Castico**	**-**	**MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais**
18.	**Mhe. Salama Aboud Talib**	**-**	**MBM/Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati / Nafasi za Wanawake**
19.	**Mhe. Sira Ubwa Mamboya**	**-**	**MBM/ Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais**
20.	**Mhe. Juma Ali Khatib**	**-**	**MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Uteuzi wa Rais**
21.	**Mhe. Said Soud Said**	**-**	**MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Uteuzi wa Rais**
22.	**Mhe. Khamis Juma Mwalim**	**-**	**Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe**
23.	**Mhe. Mihayo Juma N'hunga**	**-**	**Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi**

				ya Makamu wa Pili wa Rais /Jimbo la Mwera
24.	**Mhe.**	**Shamata Shaame Khamis**	**-**	**Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Micheweni**
25.	**Mhe.**	**Harusi Said Suleiman**	**-**	**Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete**
26.	**Mhe.**	**Mmanga Mjengo Mjawiri**	**-**	**Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani**
27.	**Mhe.**	**Mohamed Ahmada Salum**	**-**	**Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/Jimbo la Malindi**
28.	**Mhe.**	**Chum Kombo Khamis**	**-**	**Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale/ Nafasi za Wanawake**
29.	**Mhe.**	**Shadya Mohamed Suleiman**	**-**	**Naibu Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake**
30.	**Mhe.**	**Lulu Msham Abdalla**	**-**	**Naibu Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo/ Nafasi za Wanawake**
31.	**Mhe.**	**Juma Makungu Juma**	**-**	**Naibu Waziri wa Ardhi,**

			Nyumba , Maji na Nishati / Jimbo la Kijini
32.	**Mhe. Hassan Khamis Hafidh**	**-**	**Naibu Waziri wa Biashara, na Viwanda /Jimbo la Welezo**
33.	**Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi**	**-**	**Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Mtopepo**
34.	**Mhe. Abdalla Ali Kombo**	**-**	**Jimbo la Mwanakwerekwe**
35.	**Mhe. Abdalla Maulid Diwani**	**-**	**Jimbo la Jang'ombe**
36.	**Mhe. Ali Khamis Bakar**	**-**	**Jimbo la Tumbe**
37.	**Mhe. Ali Salum Haji**	**-**	**Jimbo la Kwahani**
38.	**Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)**	**-**	**Jimbo la Kijitoupele**
39.	**Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil**	**-**	**Uteuzi wa Rais**
40.	**Mhe. Ame Haji Ali**	**-**	**Jimbo la Nungwi**
41.	**Mhe. Amina Iddi Mabrouk**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
42.	**Mhe. Asha Abdalla Mussa**	**-**	**Jimbo la Kiwengwa**
43.	**Mhe. Bahati Khamis Kombo**	**-**	**Jimbo la Chambani**
44.	**Mhe. Bihindi Hamad Khamis**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
45.	**Mhe. Hamad Abdalla Rashid**	**-**	**Jimbo la Wawi**
46.	**Mhe. Hamida Abdalla Issa**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
47.	**Mhe. Hamza Hassan Juma**	**-**	**Jimbo la Shaurimoyo**
48.	**Mhe. Hidaya Ali Makame**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
49.	**Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)**	**-**	**Jimbo la Mtoni**

50.	**Mhe.**	**Jaku Hashim Ayoub**	**-**	**Jimbo la Paje**
51.	**Mhe.**	**Khadija Omar Kibano**	**-**	**Jimbo la Mtambwe**
52.	**Mhe.**	**Machano Othman Said**	**-**	**Jimbo la Mfenesini**
53.	**Mhe.**	**Makame Said Juma**	**-**	**Jimbo la Kojani**
54.	**Mhe.**	**Maryam Thani Juma**	**-**	**Jimbo la Gando**
55.	**Mhe.**	**Masoud Abrahman Masoud**	**-**	**Jimbo la Bububu**
56.	**Mhe.**	**Miraji Khamis Mussa**	**-**	**Jimbo la Chumbuni**
57.	**Mhe.**	**Moh'd Mgaza Jecha**	**-**	**Jimbo la Mtambile**
58.	**Mhe.**	**Mohamed Said Mohamed**	**-**	**Jimbo la Mpendae**
59.	**Mhe.**	**Mohammedraza Hassanaali Mohamedali**	**-**	**Jimbo la Uzini**
60.	**Mhe.**	**Mtumwa Peya Yussuf**	**-**	**Jimbo la Bumbwini**
61.	**Mhe.**	**Mtumwa Suleiman Makame**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
62.	**Mhe.**	**Mussa Ali Mussa**	**-**	**Jimbo la Ole**
63.	**Mhe.**	**Mussa Foum Mussa**	**-**	**Jimbo la Kiwani**
64.	**Mhe.**	**Mwanaidi Kassim Mussa**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
65.	**Mhe.**	**Mwantatu Mbaraka Khamis**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
66.	**Mhe.**	**Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini**	**-**	**Jimbo la Dimani**
67.	**Mhe.**	**Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy**	**-**	**Jimbo la Chaani**
68.	**Mhe.**	**Nassor Salim Ali**	**-**	**Jimbo la Kikwajuni**
69.	**Mhe.**	**Omar Seif Abeid**	**-**	**Jimbo la Konde**
70.	**Mhe.**	**Panya Ali Abdalla**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
71.	**Mhe.**	**Rashid Makame Shamsi**	**-**	**Jimbo la Magomeni**

72.	**Mhe.**	**Saada Ramadhan Mwendwa**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
73.	**Mhe.**	**Said Omar Said**	**-**	**Jimbo la Wingwi**
74.	**Mhe.**	**Said Hassan Said**	**-**	**Mwanasheria Mkuu**
75.	**Mhe.**	**Salha Mohamed Mwinjuma**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
76.	**Mhe.**	**Salma Mussa Bilal**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
77.	**Mhe.**	**Shaib Said Ali**	**-**	**Jimbo la Chonga**
78.	**Mhe.**	**Simai Mohammed Said**	**-**	**Jimbo la Tunguu**
79.	**Mhe.**	**Suleiman Makame Ali**	**-**	**Jimbo la Ziwani**
80.	**Mhe.**	**Suleiman Sarahan Said**	**-**	**Jimbo la Chakechake**
81.	**Mhe.**	**Tatu Mohamed Ussi**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
82.	**Mhe.**	**Ussi Yahya Haji**	**-**	**Jimbo la Mkwajuni**
83.	**Mhe.**	**Viwe Khamis Abdalla**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
84.	**Mhe.**	**Wanu Hafidh Ameir**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
85.	**Mhe.**	**Yussuf Hassan Iddi**	**-**	**Jimbo la Fuoni**
86.	**Mhe.**	**Zaina Abdalla Salum**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
87.	**Mhe.**	**Zulfa Mmaka Omar**	**-**	**Nafasi za Wanawake**

Ndg. Raya Issa Msellem - Katibu

Kikao cha Tano – Tarehe 15 Mei, 2018

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Zubeir Ali Maulid) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kuwasilisha Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalu za SMZ kwa Mwaka 2018/2019. Naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

Mhe. Machano Othman Said (Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum): Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha Hotuba ya maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum za SMZ kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa Mwaka 2018/2019. Naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 141

Mabalozi wa Zanzibar katika Nchi za Nje

Mhe. Simai Moh'd Said – Aliuliza:

(a) Je, Tanzania ina mabalozi wangapi katika nchi za nje.
(b) Je, katika Balozi zetu za Tanzania, ni mabalozi wangapi wamechaguliwa kutoka Zanzibar.
(c) Je, serikali imefikiria kuishauri Jamhuri ya Muungano kuwa na Afisi ndogo ya Zanzibar katika kila Balozi zetu kwa malengo ya kuunga mkono Diplomasia ya Kiuchumi hasa ukizingatia Balozi zetu nyingi zimekuwa zikilalamikiwa Wazanzibari wanaoishi nje kukosa taarifa za Zanzibar pale wanapoenda na hata raia wakigeni wanapotaka kufanya safari za kiutalii.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Simai Mohammed Said swali lake Nam. 141 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, Serikali ya Jamuhuri ya Muungano inawakilishwa na Mabalozi 41 katika nchi mbali mbali Duniani.

(b) Mhe. Spika, katika Balozi zetu tunazoiwakilisha Tanzania, wapo mabalozi 9 walioteuliwa kutoka Zanzibar.

(c) Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar bado haijafikiria kuishauri Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kufungua Ofisi ndogo za Zanzibar katika Balozi zetu za Nje ya Nchi, kwani hadi sasa serikali haijapokea rasmi malalamiko yanayohusiana na Wazanzibari wanaoishi nje ya nchi kukosa taarifa za Zanzibar katika Ofisi zetu za Kibalozi.

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inachoweza kufanya kwa sasa ni kufuatilia suala la kukosekana kwa taarifa za Zanzibar katika Ofisi za Kibalozi, ili Wazanzibari, na wageni waweze kupata taarifa na kuzitumia taarifa hizo pale wanapozihitaji. Nakushukuru Mhe. Spika.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante sana Mhe. Spika, nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu mazuri, lakini nilikuwa na swali dogo tu la nyongeza lenye vifungu vya (a) na (b). Mhe. Spika, kwa kuwa Zanzibar tumekuwa tunategemea utalii moja katika nguzo yetu ya uchumi na katika nchi za Ulaya pamoja na za Asia sasa hivi kuna mwamko mkubwa sana katika masuala ya kutumia diplomasia ya kiuchumi hasa kwa upande wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(a) Je, kwa upande wa Zanzibar ni wachumi wangapi ambao wamepelekwa na SMZ au wamependekezwa na SMZ katika Jamhuri ambayo wanaiwakilisha Tanzania kwa upande wa Zanzibar katika Balozi zetu hasa katika kutangaza uchumi wetu wa Zanzibar.

(b) Kwa kuwa Jamhuri karibuni imetangaza utaratibu mpya wa kupata *passport* zetu kwa ajili ya rais wetu Tanzania. Sasa tuna Watanzania wengi hasa Wazanzibar ambao wanasoma wengine wanaishi katika nchi tofauti.

Je, ofisi yake kwa upande ambao inaratibu masuala ya muungano na inasimamia mambo yote haya wamejipangaje kuhakikisha kwamba wazanzibari ambao wanasoma wako nchi tofauti kama China, Malaysia pamoja na nchi katika Bara za Ulaya na India na maeneo mengine yanapohitaji *passport* mpya kama hawana mpango wa kurudi nchini katika 2019 kutokana na viwango vya kifedha watawasaidiaje kupata hizo *passport* mpya na utaratibu mzima wao ili isiwe kikwazo kwao wao. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Simai Mohammed Said swali lake la nyongeza pamoja na kwamba swali lake limekuwa refu lakini nitajitahidi kumjibu kadri ambavyo itakavyostahiki.

(a) Idadi ya wachumi Mhe. Spika tuache tulichukuwe hili twende tukatizame katika *database* twende tukatizame na wenzetu wa *foreign* tutizame *exactly* wachumi

wangapi waliokuowepo katika maeneo hayo, *exactly figure* kwa sasa hatuwezi kuwa nayo.

(b) Mhe. Spika, wenzetu wa Uhamiaji wametuwekea *grace period* kuanzia sasa mpaka kufikia katika mwaka 2021/2022, ili watu sasa waweze kubadilisha hizi *passport* zao lakini kwa Wazanzibar wote au Watanzania wote waliokuwepo nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wanawajibika au wanaweza kufanya taratibu kupitia ofisi zetu za Kibalozi zilizokuwepo katika nchi husika, ili wao sasa waweze kupata utaratibu wa kubadilishiwa *passport* zao watakapofika pale ofisi zetu za Kibalozi zinatoa maelekezo na utaratibu namna gani wao wataweze kubadilishiwa *passport* wakiwa huko lakini kwa hali yoyote tunaenda mpaka 2020 mtu *passport* ambayo anayo leo ana uwezo wa kuitumia mpaka 2020 ndio ambapo rasmi sasa litakuwa zoezi limekamilika. Nakushukuru Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuongezea majibu ya nyongeza ya Mhe. Simai Mohammed Said kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza nitanabahishe kwamba sisi Wazanzibari ni Watanzania ni ofisi zile za Kibalozi ziliopo katika nchi mbali mbali ni mali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Jamhuri ya Muungano wa Tanzania maana yake ni nchi mbili zilizoungana kuunda Jamhuri ya Muungano kwamaana iliyokuwa Tanganyika na iliyokuwa Jamhuri ya watu wa Zanzibar ndio tukafanya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kwa hiyo, ofisi zile za Kibalozi ni zetu pamoja, hazibagui huyu Mzanzibar huyu Mtanzania Bara wanatumia sheria moja, utaratibu ni mmoja. Kwa maana hiyo, Wazanzibar wote walioko katika nchi yoyote wanayo haki ya kutumia ofisi hizo za Kibalozi kama alivyo mtanzania mwengine yeyote kwasababu sote ni watanzania kwa mujibu wa Katiba na Sheria tunazo sifa sawa.

Kwa hiyo napenda nitoe wito kwa Wazanzibar walioko nje kuzitumia ofisi zetu hizi inapokuwa Balozi ametoka upande wa Tanzania Bara au ametoka Zanzibar wote ni Watanzania ni haki yao kutumia ofisi hizo. Pia, na niwaombe sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu waelewe hivyo, na vile vile tuna haki pale ambapo tunataka kutangaza shughuli zetu za kibiashara au za kiuwekezaji katika balozi mbali mbali tunaweza kufanya hivyo kama vile ambavyo wanaweza kufanya Tanzania Bara hakuna ubaguzi wowote katika kufanya hivyo, ni haki yetu ya msingi na tunawajibu kutumia. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, na majibu mazuri pia ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwanza niishukuru sana Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kukubali watanzania ambao wako nje ya nchi kubadilisha *passport* zao huko huko. Swali langu ni kwamba, pamoja na kukubaliwa huku lakini inachukuwa muda mrefu sana mtu kupata lile ombi lake sio kwamba mwezi zaidi ya miezi mitatu nafikiri ndio wanapata zile *passport.*

Je, kuna hatua zozote ambazo Serikali ya Zanzibar wanaweza kuchukuwa au Serikali ya Muungano, ili kupunguza muda wa upatikanaji wa *passport* hizo kwa watu ambao wako nje ya nchi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mhe. Mchano Othman Said kama ifuatavyo. Mhe. Spika, kwa kuwa utaratibu huu bado ni mpya nia na dhamira ni kutoa *passport* kwa muda mfupi na dhamira yetu ya kuanzisha *passport* mpya licha ya kwamba kulikuwa na upotevu ama kufanya *passport* za kufoji kwa *passport* zetu, lakini moja ni kutafuta utaratibu wa kurahisisha wananchi kuzipata *passport* hizo kwa wakati. Kwa hivyo, nataka nimuhakikishie Mhe. Machano Othman Said tutafanya kila jitihada kuhakikisha kuwa *passport* zinapatikana mapema iwezekanavyo kwa sasa ni upya, na hivi karibuni tu tunampango wa kupeleka mashine kwa upande wa Kisiwa cha Pemba na katika wiki ijayo utaratibu utaanza rasmi na kwa upande huo. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, swali hili ni sehemu ya sehemu ya Jamhuri ya Muungano ikiwemo Zanzibar au Wizara ya Muungano na swali la msingi je katika Balozi zetu Tanzania ni Mabalozi wangapi wametoka Zanzibar jawabu tumepata 9.

(a) Mhe. Spika, nataka kujuwa katika 9 hao ni sawa sawa na asilimia ngapi waliopelekwa huko, lakini hapo hapo ni sababu gani za msingi zinazopelekea Wazanzibar kutopelekwa Balozi za Ulaya na kuachwa Afrika.

(b) Ni sababu gani vile vile katika ajira katika ofisi za Mabalozi Wazanzibar hashirikishwi kwa kiasi kikubwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake moja la nyongeza kama ifuatavyo:

(a) Kwanza tumfahamishe tu Mhe. Jaku kwamba Ubalozi ni Ubalozi tu ukiwa Afrika ukiwa Ulaya ukiwa Amerika *stutas* ya balozi itabaki kuwa Balozi tu. Kwa hiyo, hakuna kigezo cha utenganifu wa aina yoyote eti huyu Balozi wa Afrika au huyu Balozi wa Ulaya. Kwa maana hiyo, sisi tunasema tu kwamba mabalozi wote wana sifa sawa, stahiki sawa na hadhi sawa ya ubalozi katika nchi zao.

Lakni pia naomba arejee swali lake la mwisho Mhe. Spika.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, nilimuuliza tumepata Balozi tisa tu Zanzibar ni sawa saswa na asilimia ngapi tulipataka katika Balozi 41 tu nafikiri kama hivi. Lakini sababu gani za msingi wazanzibar kutokupelekwa Balozi za nje tofauti na huko nyuma, vile vile hata katika ajira katika Wizara hiyo Wazanzibar wanakuwa kidogo katika watumishi wa Ubalozi.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub kwamba suala la asilimia kama ambavyo tumesema kwa sasa tuna jumla ya mabalozi 9 na katika jumla ya mabalozi 41 ndani ya Jamhuri lakini tumwambie tu kwamba tunapochaguwa Mabalozi tunachaguliwa Mabalozi kwa mujibu wa

Utanzania wetu hatuchaguliwi kwa namna ya sehemu mtu anapotoka huko ambapo anafikiria Mhe. Jaku Hashim Ayoub itafikia wakati tunatizama kwamba nani katoka Michamvi nani katoka Kizimkazi nani katoka Mwera. Kwa hiyo, tunapochaguwa Mabalozi, tunapoajiri katika sehemu zile tunachaguwa kwa mujibu wa sifa za Utanzania wetu ndio unaotupeleka kule. Nakushukuru Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, pamoja na majibu na maruzi sana ya Mhe. Naibu Waziri ningependa niongezee majibu majibu ya nyongeza ya Mhe. Jaku Hashim Ayoub kama ifuatavyo. Mhe. Spika, kama nilivyosema awali kwamba Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni nchi mbili huru zilizoungana zikaunda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tumejiwekea Katiba yetu na Sheria zetu na utaratibu wetu na tunamamlaka moja tunaufanya uteuzi huu mamlaka hiyo tunafanya kwa kushauriana kwa upande wa Zanzibar kwa maana na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Nataka nimuhakikishie kwamba wapo Wazanzibari ambao walichaguliwa katika nchi mbali mbali za Ulaya hata humu ndani tuna Mabalozi maarufu sana, tunao Mabalozi Mhe. Amina Salum Ali, tuna Balozi Ali Abeid Amani Karume, tuna Mabalozi waliostaafu, Balozi Seif Ali Iddi, tunae ndugu yetu ndugu Salum Ahmed Salum alikuwa Balozi ni maarufu sana Balozi Mohammed Ramia Abdiwawa nawengine wengi sana ambao wamekaa katika nchi za ulaya wamefanya kazi na tumefanya kazi kiundugu bila ya kuonesha Balozi huyu anatoka wapi. *(Makofi)*

Jambo la msingi hapa zinatizamwa sifa na uwezo wa mtu, wako Wazanzibari wengi sana wamepata mamlaka makubwa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ndio utaratibu wetu. Mhe. Spika, napenda nitoe wito tusitafute namna ambavyo tukatafuta kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri kuanza kugawanya wenyewe kwa wenyewe la msingi hapa ni kuimarisha umoja wetu, kuimarisha udugu wetu na kufanyakazi kwa pamoja. Ahsante sana Mhe. Spika.

Nam. 237

Kukosekana kwa Mashirikiano kwa Baadhi ya Sekta katika Suala la Ugatuzi

Mhe. Machano Othman Said – Aliuliza:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika mwaka wa fedha 2017/2018 ilianza kutekeleza kwa vitendo uamuzi wake wa kugatua madaraka kwa wananchi baadhi ya sekta, kama vile elimu, afya, na kilimo hatua ambayo imeleta mageuzi makubwa katika kuimarisha upatikanaji huduma hizo kwa wananchi kupitia halmashauri zao pamoja na uamuzi huo mzuri. Hata hivyo, zipo baadhi ya taasisi hizo hazijatoa ushirikiano mzuri kwa halmashauri hizo.

(a) Ni hatua zipi serikali imepanga kuchukua, ili kuona kwamba taasisi zote zinazohusika na ugatuzi zinatimiza wajibu wao ipasavyo.

(b) Je, serikali haioni kwamba wakati umefika kwa sekta ya maji nayo kugatuliwa, ili kuleta nafuu kwa wananchi.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Machano Othman Saidi swali lake Nam. 237 lenye vifungu (a) na (b) kwanza naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Mhe. Spika, katika utekelezaji wa Mpango wa Upelekaji wa Madaraka kwenda kwa wananchi (Ugatuzi) hakuna taasisi ambazo hazijatoa ushirikiano kwa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ.

Mhe. Spika, sekta zote zimekuwa zikitoa ushirikiano mkubwa hususan katika matayarisho ya uhamishaji wa watumishi, uandaaji wa bajeti na uratibu wa kazi za kila siku. Mikutano ya mashauriano imekuwa ikifanyika baina ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ na sekta hizo katika ngazi za viongozi na watendaji Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikao, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ itaendeleza mashirikiano haya kwa utaratibu wa kuwashirikisha pia wananchi kwa lengo la kuharakisha upatikanaji wa huduma.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mheshimiwa Machano Othman Said jibu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, naomba ieleweke kwamba katika Mkakati wa Ugatuzi *(D by D Strategy and The Road Map)* umeelezea bayana kwamba utekelezaji wa mkakati huu utakwenda hatua kwa hatua na utekelezaji wake ni lazima uzingatie sheria, sera, kanuni, miongozo na maagizo ya serikali. Kwa mantiki hiyo, hakuna sababu za msingi kwa serikali kuzichukulia hatua taasisi ambazo labda tu zitaoneakana haziendani na kasi ya ugatuzi.

Katika utekelezaji wa mkakati huo kumeainishwa pia mpangilio wa usimamizi pamoja na mikutano ya kiutendaji baina ya sekta husika na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ. Kwa kuwa Kamati ya Makatibu Wakuu ndio chombo dhamana cha kusimamia utekelezaji wa ugatuzi hivyo basi, uwajibikaji wakuu wa kisekta utaendelea kupata msukumo kupitia vikao vya Kamati hio.

Mhe Spika, kwa utaratibu huu ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ haifikirii wala haitarajii kwamba sekta zetu zitakosa kutoa ushirikiano au kutokubali na ushauriano katika utekelezaji wa ugatuzi.

b) Naomba nikiri kwamba kutokana na umuhimu wa sekta ya maji kwa jamii yetu ungekuwa vyema sekta hii nayo pia ikagatuliwa ili wananchi waweze kuibua mipango yao na pia kuharakisha ufumbuzi wa matatizo ya maji pale yanapojitokeza.

Hata hivyo, kama nilivyosema katika jibu langu (a) utekelezaji wa mkakati wa ugatuzi unafanywa hatua kwa hatua, ili kupata nafasi ya kujitathmini hata hivyo dhamira yetu ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kuwa kwa kadri mafanikio hayo yatakavyoonekana

ndivyo sekta nyengine zaidi zitakapoingizwa katika mpango huu ikiwemo sekta ya maji.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Spika, kwanza nimshukuru sana Mhe. Naibu Waziri, lakini pamoja na majibu hayo nataka kuumuliza swali moja la nyongeza lenye a na b kama ifuatavyo:-

a) Katika majibu Mhe. Waziri amekiri kwamba anapata ushirikano nzuri kutoka tasisi nyengine nataka kumuliza. Je, hivi wale wafanyakazi wa ugatuzi maslahi yao na mafao yao yote yameshahamishiwa katika wizara yake.

b) Ni nchi gani ambayo inafanya *D by D* ambayo sekta ya maji imeachwa nje katika ugatuzi.

Mhe. Naibu Waziri Ofisi ya Rais Tawala Za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe.Spika, kwa ruhusa yako naomba kutoa majibu ya nyongeza kwa Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:

a) Mhe. Spika, nakiri kurejea kusema kwamba kama nilivyoeleza katika majibu ya msingi kwamba hakuna taasisi ambayo mpaka sasa hivi inaendelea kuona kwamba haiwezi kwenda sambamba na maelezo yale serikali. Hivyo basi, nataka niseme kwamba maslahi ya wafanyakazi au ya watumishi katika sekta zilizogatuliwa tayari yameshaingizwa katika utaratibu kwa yale ambayo kidogo yameonekana hayajafanikishwa kwa kiwango kile usawa na taassisi nyengine, imetokana na kwamba kama tulivyosema kwamba tunaenda hatua kwa hatua.

   Lakini kubwa zaidi ni kwamba tumefanya mawasiliano na sekta husika, ili kuona kwamba hakuna tatizo lolote ambalo linaweza kuwakwamwisha utekelezaji wa ugatuzi katika sekta zote ambazo tumezigatua au zimegatuliwa. Hivyo, naomba nihakikishe kwamba mishahara tayari pamoja na mambo mengine yamezingatiwa na hatua nyengine katika kama tulivyosema hatua kwa hatua.

b) Kutaka kujua kwamba ni nchi gani ambazo zina ugatuzi kama ambavyo sekta ya maji kuona kwamba haijagatuliwa. Nirejee kusema kwamba Mhe. Mwakilishi kwamba sekta ya maji hata na sisi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idaraa Maalum za SMZ, kutokana na umuhimu mkubwa tungependa sana sekta ya maji nayo iweze kuingana na hizi lakini kama tulivyosema tunaenda hatua kwa hatua.

   Kwa kweli, ugatuzi wetu sisi au mfumo wetu wa ugatuzi tunaweza tukawa na tofauti na nchi mbali mbali kwa sababu tunaangalia geografia na nchi nyengine ambazo zimewe ku-*practice* kwa mfano kama jirani zetu Tanzania Bara sitaki niende mbali, wao wamegatua katika sekta hii ya maji iko katika ugatuzi. Lakini hata hivyo, wao kila mmoja ameangalia na mazingira na tafiti ambazo wataalamu wetu wametushauri serikali imeona kwamba iko haja kwenda hatua kwa hatua ili zile mapungufu na kasoro ambazo zimejitokeza katika sehemu nyengine au nchi nyengine sisi zisije zikaingia kwetu katika kuona kwamba tunaweza tukaona kwamba mambo hayande vizuri kama vile ambavyo tumetarajia.

Mhe. Hamad Abdalla Rashid: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii ya kuuliza suala dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri na kwakua kwenye jibu mama kakiri kwamba hakuna taasisi ambazo hazijatoa ushirikiano na wizara yake.

a) Ningependa kujua ni ufanisi kiasi gani uliopatikana tokea ugatuzi huu uanze.

b) Kwa kuwa, ufanisi huu upo ni lini katika Kituo changu cha Afya Kibokoni kule kwenye Jimbo langu la Wawi nitapata ufanisi huu kwa sababu hata kiti na kituo kile kinatoa afya.

Mhe. Naibu Waziri Ofisi ya Rais Tawala Za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe.Spika kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, naomba nirejee kusema kwamba kama nilivyotangulia kusema naendelea kusema, kwamba tunaendelea vizuri katika suala zima la ugatuzi na hadi sasa hivi ufanisi ambao umepatikana tumeweza kuona wazi wazi kwamba ni mkubwa. Na hadi sasa hivi tumewe kukarabati baadhi ya vitua vya afya, tumeweza kupeleka huduma katika shule zetu za msingi na huduma mbali mbali ambazo ilikuwa awali kwa kipindi kirefu ni kwamba zilikosekana kwa hali ya sasa hivi yapo mabadiliko makubwa.

   Nimuombe tu Mhe. Mjumbe pamoja na Waheshimiwa wengine basi kwa kuwa huko majimboni huo ugatuzi wetu ndiko uliko, basi ni vyema na wao wapige jicho katika mazingira yale ili kuweza kuthibitisha zaidi haya ambayo tunaendela kuyasema. Kwa hivyo, katika ufanisi tuko vizuri kwa sababu sekta tunazo, mipango yetu tayari tumeshaipanga kufikiwa pamoja, taaluma kwa wananchi inapelekwa katika maeneo mbali mbali na kwa kutumia vyombo mbali mbali.

b) Kituo cha Afya Kibokoni ambacho Mhe. Mwakilishi amekuwa akikipigia kelele sana, kwamba hadi sasa hivi kusema kwamba hakuna kiti wala hakuna meza. Mhe. Spika, nikwamba ugatuzi tumeanzaa nao na tuko katika hatua ya kufatilia pia kuona ni wapi ambapo panahitaji msukumo wa aina gani na kwa wakati gani.

   Kwa hivyo, naomba nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba sisi tumekabidhiwa ugatuzi lengo lake ni kwamba tuweze kuharakisha huduma za waananchi zile ambazo serikali imezilenga zipatikane kwa haraka zaidi, haimanishi kwamba taasisi nyengine zilikosa kufanya ama kukataa kufanya ila ni kwamba sisi tunakipokea kituo na *Inshallah* nataka nikupe matumaini Mhe. Mwakilishi kwamba kazi hiyo ya kuona kwamba tunafanya mabadiliko pindi mukitupitishia bajeti yetu hatua zitaanza kuchukuliwa.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, swali limechukuwa muda kidogo majibu yamekuwa marefu, naomba tuendelee, ili kuweza kuyamaliza maswali yote tuliyonayo kwenye order paper ya leo.

Nam. 39

Ukosefu wa Maktaba na Wakutubi katika Skuli za Serikali

Mhe. Ali Khamis Bakar – Aliuliza:

Pamoja na jitihada za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kutoa elimu bora katika ngazi zote za elimu, skuli nyingi Unguja na Pemba zinakabiliwa na ukosefu wa Maktaba sambamba na uhaba wa "WAKUTUBI" wenye sifa kwa skuli zenye maktaba.

(a) Je, ni lini wizara kwa kushirikiana na Shirika la Huduma za Maktaba itafanya tathmini ya skuli ambazo hazina maktaba ili kufanya mpango wa kufikisha huduma hiyo katika skuli hizo.

(b) Je, ni lini wataalamu wa maktaba wenye sifa wataajiriwa, ili kukabiliana na uhaba mkubwa katika skuli za serikali.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali – Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwalikilishi swali lake Nam. 39 lenye vifungu (a) na (b).

Kwanza naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama hivi ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba, pamoja na jitihada mbali mbali tunazoendelea kuzichukua za kutoa elimu bora katika ngazi zote za elimu, bado skuli nyingi Unguja na Pemba zinakabiliwa na ukosefu wa Maktaba sambamba na uhaba wa "WAKUTUBI" wenye sifa kwa skuli zenye Maktaba. Kwa kulijua hilo Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kupitia utekelezaji wa mradi wa *Global Partnership for Education* "GPE" 2014/2016 ililiwezesha Shirika la Huduma za Maktaba kufanya tathmini ya awali *"School Library Survey*" ili kuweza kujua uhalisia wa Huduma za Maktaba zinazotolewa katika Skuli mbalimbali za Msingi na Sekondari Unguja na Pemba sambamba na uwepo wa wakutubi katika skuli hizo. Tathmini hiyo ilijumuisha jumla ya Skuli 129 Unguja na Skuli 126 Pemba kama *Sample* na ilizingatia zaidi mambo yafuatayo: -

i) Kuangalia skuli zenye maktaba na zisizo kuwa na maktaba;
ii) Kuangalia idadi ya wakutubi wenye sifa;
iii) Kuangalia ubora wa huduma za maktaba zitolewazo katika ngazi za skuli na
iv) Kuangalia upatikanaji wa vitabu na machapisho mengineyo katika maktaba za skuli.

Baada ya maelezo hayo, sasa naomba kumjibu kama hivi ifuatavyo:-

(a) Matokeo ya tathmini yalionesha kwamba kati ya skuli 129 za Unguja, asilimia 89 ya skuli hizo hazina maktaba na ni asilimia 11 tu ya skuli ndio zenye maktaba. Aidha, kwa upande wa Pemba kati ya skuli 126 zilizofanyiwa tathmini, asilimia 92 ya skuli hizo hazina maktaba na ni asilimia 8 tu ndio zenye Maktaba. Pia, utafiti ulionesha kwamba takribani ya skuli zote hutoa huduma za maktaba kupitia vyumba visivyo rasmi vyenye mchanganyiko wa vitabu, vifaa vya kufanyia usafi na huduma za ghala.

Huduma ya kuazimisha vitabu hutolewa na walimu wa kawaida bila ya kufuata muda maalumu au mfumo rasmi wa kutoa huduma za maktaba. Kutokana na ukubwa wa tatizo hilo, wizara imeanza kuchukua hatua ya kuomba uajiri wa wakutubi waliohitimu katika vyuo hivi karibuni.

(b) Maombi ya uajiri wa wakutubi 41, yamewasilisha katika vyombo vinavyohusika kwa ajili ya taratibu za uajiri.

Mhe. Ali Khamis Bakari: Ahsante sana Mhe.Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba nimuulize maswali mawili yenye a na b kama ifuatavyo:-

a) Je, ni lini hayo maombi yamewasilishwa na hatua gani ya awajiri imefikiwa.

b) Katika idadi hii ya 25 ambayo imetwaja hapa mlipanga Unguja wawe wangapi na Pemba wawe wangapi. Je, idadi hii itatosheleza.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe.Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mjumbe maswali yake ya nyongeza kama ifuatavyo:-

a) Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, iliandikia Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora tarehe 9 Mei na wizara hiyo tayari imeshawasiliana imeshaandikia barua kwa Katibu wa Tume ya Utumishi kwa ajili ya hatua za ajira.

b) Napenda kurekebishwa kwamba ni wakutubi 41 sio 25 kama tulivyoandika hapa ni 41. Kwa hivyo, 32 hawa wataajiriwa na Idara ya Elimu Sekondari na wote hawa watakuwa Unguja wanne wataajiriwa na Idara ya Mafunzo ya Ualimu ambao itakuwa ni Pemba na wengine watajiriwa kwa ajili ya shughuli ya za skuli huko Pemba.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Spika, nashukuru kunipa fursa hii kuuliza swali la nyongeza, nachukua fursa hii kwa kumpongeza waziri kwa majibu yake lakini na mimi nina swali la nyongeza. Kwanza kabisa niipongeze Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa juhudi kubwa ambazo imechukuwa katika kujenga skuli za ghorofa ambazo zitapunguza ufinyu wa nafasi naipongeza sana na zinajengwa kwa kasi kubwa sana napongeza sana. *(Makofi)*

a) Nataka kujua je, katika skuli hizi mpya ambazo ni za kileo na zinakwenda na wakati mumezingatia kuweka hivi vyumba vya maktaba, ambavyo vingeweza kuleta sura nzuri katika skuli hizi.

b) Vile vile, katika idadi ya wafanyakazi 41 ambao amefanya marekebisho sasa hivi ametwambia hapo ambao wameandaa kuwaajiri. Je, wamefikiria katika skuli hizo ambazo zinajengwa zinazokwenda na wakati, wamefikia kuwaajiri wafanyakazi hawa wa maktaba

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

a) Ni kweli katika majengo haja mapya tisa ambayo yanajengwa Unguja na Pemba matano Unguja na manne Pemba yamezingatia kwa kina vyumba ambavyo vitatumika kama maktaba za skuli.

b) Skuli hizi nazo pia zitakapokamilka wakutubi wenye sifa watapelekwa katika skuli hizo. Kwa hivyo, hili tumelingatia ahsante sana.

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa: Ahsante Mhe. Spika, kwa kuniona kwanza nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri aliyotujibu, naomba kumuuliza swali dogo la kama ifuatavyo:-

Pamoja na majibu yake mazuri ambayo katueleza alikiri kwamba kuna tatizo la maktaba na wakutubi. Naomba kumuuliza kama wizara yake ina mikakati gani pamoja na tathmini ambayo walikuwa wamefanya ambayo itakuwa sahihi, ili kuondosha tatizo hili la maktaba katika wanafunzi wetu hapa kwetu Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

Ni kweli kwamba tatizo hili lipo, na katika kuzingatia kwamba kila skuli inakuwa na vyumba ambavyo vitatumika maktaba, tumetoa maelekezo kwamba skuli zote ambazo zitajengwa basi zizingatie suala la kutenga vyumba ambavyo vitatumika kwa maktaba, lakini si vyumba tu lakini vyumba ambavyo vitakuwa na vigezo kwa ajili ya kuhudumia maktaba. Kwa hivi sasa, baadhi ya skuli utakuta kuna chumba kidogo tu hivi ambacho kinatwa maktaba lakini hakiwezi kuwa na sifa. Kwa hivyo, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali itaweka vigezo maalum kwa vyumba vitatumika kama maktaba hii ni makakati mmoja.

Mengine ni kwamba katika skuli zote ambazo zitajengwa sasa swali hili la vyumba ambavyo vitatumika kama maktaba vitazingatiwa. Lakini jengine kubwa zaidi ni kwamba kuna mradi ambao tunauitwa *School Helps,* mradi huu utahusisha skuli kama 20 nao pia umetenga vyumba kwa ajili *school library* ahsante sana.

Nam. 98

Matengenezo ya Barabara ya Makangale

Mhe. Omar Seif Abeid – Aliuliza:

Wakati wa mvua za Masika kwenye maeneo ya Mkiang'ombe huwa hakufiki gari kutokana na kuwepo kwa mchanga mwingi sana. Na kwa kuwa eneo la Makangale Mnarani kipo kifusi kingi ambacho Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji walichimba kwa ajili ya kufanya matengenezo ya barabara hiyo ya Makangale na Mkiawang'ombe.

Je, wizara yako ina mpango gani wa kuifanyia marekebisho angalau kwa kuanzia na kifusi katika barabara hiyo, ili kupunguza kero kwa mama majawazito na wagonjwa ambao hufikia

kubebwa kwa kitanda wakati wanapobidi kuhamishiwa kituo kingine kwa kufuata huduma za afya.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji – Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suala lake Nam. 98 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Barabara ya Mkiang'ombe ina tatizo la mchanga mwingi uliojikusanya na huwa ni usumbufu kwa wapita kwa miguu na hata kwa gari. Hali hii husababisha usumbufu kwa wagonjwa wa kawaida lakini inakuwa tatizo zaidi panapokuwa na waja wazito wanapobidi kuhamishiwa kituo kingine kwa kufuata huduma za afya.

Mhe. Spika, kwa hali ya mahala hapo palivyo na usumbufu wanaoupata wananchi wa hapo, kifusi kinahitajika na wizara imeliona tatizo hilo. Lakini, kifusi anachosema Mhe. Mwakilishi kitumike kujaza sehemu hiyo hakipo tena kwani kilitumika kwa shughuli nyengine. Kwa hivyo, wizara imeona kuna haja ya kulitatua tatizo hilo kutokana na unyeti wake. Katika bajeti ya 2018-2019 kwa ajili ya dharura wizara kupitia Mfuko wa Barabara itapanga bajeti, ili kuitengeneza barabara hii ili iweze kupitika na tunusuru maisha ya watu wa Mkiang'ombe na vitongoji vyake.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa ruhusa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, tunamshukuru sana Mhe. Waziri kwa majibu yake na kukiri kwamba kweli Mkiang'ombe kuna tatizo, nakushukuru sana kwa jibu hilo. Kwa kuwa umekiri na tatizo umeliona lipo na kwenye bajeti hii umesema utajipanga kutekeleza kwa kutia kifusi katika ile barabara na kweli wananchi wangu wanakufa wanateseka sana na wewe ni mama ulipitia kwenye hali hiyo ya udaktari.

Je, ni lini utakwenda wewe mwenyewe kuliona lile eneo na hali ilivyo, ili utakapokwenda ukapata nguvu zaidi ya kuwahimiza wafanyakazi wako waweze kuchukua hatua ya kutia kifusi na kutengeneza barabara ile, ili kuokoa maisha ya wananchi kama ulivyosema kwenye jibu lako mama. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, tulipokwenda juzi kwenye sherehe nilipitia baadhi ya barabara na moja katika barabara niliyoipitia ni hiyo na nimeiona, nilivyosadifu kuja kuona ipo nayo katika maswali nikaweza kupata picha halisi. Hata hivyo, nimezungumza na watu wangu na wao wamenihakikishia kwamba tutajitahidi kwa kadiri tutakavyoweza, ili tuweze kuhakikisha kwamba hilo linafanikiwa.

Mhe. Hamad Abdalla Rashid: Ahsante Mhe. Spika, naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, kutokana na mvua kubwa zinazoendelea kunyesha nchini, barabara nyingi za Unguja na Pemba zimechimbuka vibaya na kwa kweli zinahatarisha hata usalama wa nchi.

Je, wizara yako itachukua hatua gani za dharura mapema iwezekanavyo, ili kuhakikisha barabara hizi zinapitika kwa unadhifu kabisa.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, naomba arudie swali lake.

Mhe. Spika: Mhe. Hamad Abdalla Rashid, zungumza kidogo karibu na *microphone* ili asikie Mhe. Waziri.

Mhe. Hamad Abdalla Rashid: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri kutokana na mvua kubwa za masika zinazoendelea kunyesha katika nchi hasa visiwa vyetu vya Unguja na Pemba, inaonekana barabara zote takriban asilimia 80 zimechafuka na zimechimbuka na zinahatarisha hata usalama wa wananchi wetu.

Je, ni hatua gani ya dharura ya makusudi wizara yako itachukua katika kuzitengeneza barabara hizi mapema iwezekanavyo?

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, hatua za makusudi tunazozifanya kwa kupita katika maeneo yote kutathmini, kuzinakili na kuzijua ni zipi na ni sehemu gani. Baada ya hapo tunaangalia kile kilichoharibika, mule ambamo munahatarisha maisha tumegeuza njia tumechukua kutoka kwenye njia husika na watu wanapita pembeni yake halafu tunaunganisha barabara kwa mbele. Tumeshafanya hivyo kwa baadhi ya sehemu na tutaendelea kufanya hivyo kwa mule mote ambamo kuna matatizo kama haya. Baadae tutakuta tuone sasa barabara zipi tuanze, zile ambazo zitakuwa zinahatarisha maisha ndizo ambazo tutaanza nazo mwanzo, mule ambamo mnatakiwa kufanywa matengenezo madogo madogo kwa kujaza tutajaza na baadae tutaendelea na barabara nyengine ambazo zimeharibika lakini ambazo hazihatarishi maisha.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwanza nimshukuru sana Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kwa majibu yake, lakini pia na juhudi zake ambazo amezionesha.

Mhe. Spika, wiki hii eneo la Mtoni Kwakisasi pamechimbika kiasi kwamba kuanzia juzi kwa wale wanaotoka Kaskazini foleni zinaanza Kwanyanya mpaka Kwakisasi na ambao wanatokea mjini foleni zinaanza Mwembe Makumbi njia ya Chumbuni mpaka Kwakisasi.

Je, serikali itafanya hatua gani za dharura kupahami sehemu ile ili kupunguza ule msongamano.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, sehemu zilizoharibika kwa kiwango kikubwa ni nyingi sio Kwakisasi tu peke yake, na humo mote tunamujua, kwa sababu hivi ninavyokuambia watu wamo njiani wanapita kufanya tathmini hizo. Kwa hivyo, tutajitahidi kwa kadiri ya uwezo utakavyokuwa na mvua ikiwa itapungua kidogo ili tuanze kuzihami hizo sehemu. Moja katika sehemu ambazo zitafanyiwa kazi ni hiyo ya Kwakisasi. *(Makofi)*

Mhe. Maryam Thani Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo. Kutokana na barabara yangu ya Gando ilikatika kabla ya mvua hizi za masika kunyesha na kwa sasa mvua hizi zinaendelea barabara hiyo imeongezeka, yaani haipitiki kabisa kwa miguu na hata kwa gari.

Je, wizara ina mpango gani wa kuijenga kabisa barabara ile ya Gando, ili wananchi na wafanyabiashara wapate kufanya biashara zao kwa vizuri. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, barabara ya Gando ndio barabara ya kwanza niliyoitembelea baada ya maharibiko. Katika kupita na kuangalia hata mimi niliyekuwa sijenda skuli nimeona kwamba barabara ile inatatizo. Kwa kweli, sio tu kuitengeneza, lakini pale ndio katika sehemu ambazo michepuko ya ile barabara inatakiwa ifanyike.

Wataalamu na walioko pale na hao waliojenga barabara wanasema wataitengeneza. Mhe. Spika, nimewakatalia nikawaambia hii hata mkiitengeneza, mimi sitowi idhini ya kutengeneza hii tafuteni utaratibu mwengine, kwa sababu tatizo lilioko pale litakuwa ni la kudumu, sehemu ile imejazwa na palikuwa pana shimo na mvua inaponyesha mchanga unachipuka kwa chini shimo linaendelea kutokea, itakuwa hivyo na mkandarasi aliambiwa haya akafanya ukaidi. Sasa kama yeye kafanya ukaidi mimi sifanyi ukaidi, njia itabadilishwa njia. *(Makofi)*

Nam. 171

Kuwaondolea Kero ya Maji Wanakijiji wa Mgambo

Mhe. Asha Abdalla Mussa – Aliuliza:-

Mhe. Waziri katika ziara yako Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini "B" Unguja aliahidi wananchi wa Kijiji cha Mgambo kuwa atawachimbia kisima cha maji safi, ili kuwaondolea kero hiyo ambayo ni ya muda mrefu sasa.

Je, ni lini ahadi hiyo itatekelezwa ili wananchi hao waweze kufaidika na maji safi na salama.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 171 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, napenda kumfahamisha Mhe. Mwakilishi kwamba, wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji inatambua ahadi ya kuwachimbia kisima wanakijiji wa Mgambo na bado inaendelea na juhudi za kuhakikisha kwamba kisima hicho kinachimbwa, ili kusaidiana na kisima kilichopo kuongeza nguvu na kuweza kuwapatia wananchi hao huduma ya maji safi na salama. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Asha Abdalla Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kuwa huduma hii ya maji safi na salama ni changamoto kubwa ambayo inawakabili wananchi wa Shehia ya Mgambo na ndipo Mhe. Waziri akaahidi kuwa ndani ya muda wa miezi mitatu watahakikisha kwamba wananchi hawa wanapatiwa huduma hii.

Je, ni sababu gani ambazo zimesababisha huduma hii kutokufanikishwa kwa haraka. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati: Ahsante Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Spika, kwa sababu tuna ahadi nyingi na tunatekeleza moja baada ya nyengine. Lakini kama tulivyokuwa tumesema hatujakusahau na tutalifanya ahsante sana.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati, kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, tunajua maji ni uhai na mtu unapomuahidi maji basi anakuwa keshakuwa na imani kwamba maji yale atayapata, lakini najua kwa utaratibu wa Mhe. Waziri na *speed* yake *Inshaa-Allah* maji hayo yatapatikana.

Mhe. Spika, mimi swali langu liko hapa. Kwa kuwa katika Jimbo langu la Kijitoupele kuna visima viwili vikubwa tu. Kisima kimoja cha Magirisi na kisima chenigne cha Kwarara Kwa Ngulangwa. Visima hivi vimeathiriwa au vimepata athari ya watu kuvihujumu kwa makusudi, na kisima cha Magirisi kilikuwa na maji mengi ya kutosha katika wadi nzima ya Kijitoupele na sehemu nyenginezo.

Je, kwa kuwa kisima hiki kilitiwa mawe kwa makusudi na kilitiwa magogo na majani kwa makusudi. Mhe. Waziri atawasaidia vipi wananchi hawa ili kuhakikisha kwamba wanapata maji ili waondokane na tatizo hili kwa muda huu mfupi.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati: Ahsante Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Spika, ni kwamba yeye mwenyewe ni shahidi jitihada ambazo *ZAWA* inafanya juu ya kurekebisha ile hali, nimwambie tu kwamba tutaendelea kujitahidi kuhakikisha kwamba huduma hii inapatikana kwa kila tutavyoweza. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Ali Khamis Bakar: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kuniona na kunipa nafasi ya kuweza kuuliza swali. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, na mimi naomba nimuulize swali moja dogo la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri katika mvua ambazo zinaendelea kunyesha katika nchi yetu, kuna kuna baadhi ya sehemu Unguja na Pemba ambazo mabomba yaliyopita katika ardhi yamechimbuka na watoto wanakwenda wengine wakiyakata na wengine wakiyachezea mabomba yale na kufikia hatua maji kuweza kupotea kwa wingi.

Je, ni hatua gani za dharura wizara yako itachukua ili kuyanusuru mabomba yale yasipotee, lakini vile vile na watoto wasiweze kuyaharibu, ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati: Ahsante Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Spika, nikubaliane naye kwamba mvua hizi kweli kuna mabomba yanachimbuka na tunafanya jitihada ya kuyakagua, lakini pia kujua nini tufanye kwa kila bomba husika.

Kwa mfano, kama bomba ambalo hivi karibuni tumesikia limepata athari, hili sababu yake ni mvua na tunaendelea kufanya kila linalowezekana ili kuyanusuru haya mabomba. Kwa kupitia nafasi hii basi tuwaombe wananchi, kwa sababu maeneo mengine inawezekana hatujayafikia wakiona kuna athari hiyo basi wafanye jitihada angalau ya kuziba chini kule mchanga au kitu chengine chochote ambacho kitahifadhi, hasa yale mabomba ambayo yanahitaji *support* chini, ahsante sana.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kwa kunipatia nafasi hii ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Mhe. Spika, niipongeze Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuchimba visima vingi Unguja na Pemba.

Lakini Mhe. Spika, kwa masikitiko makubwa sana huu ni mwezi wa tano wananchi wa Kiuyu Minungwini na Kiuyu Kigongoni hawapati maji, kutokana na mashine ambayo ilikuwepo pale kuharibika katika kisima chao. Mhe. Spika, tumeshafuatilia sana mimi na Mhe. Mwakilishi wangu wa jimbo pamoja na madiwani wa Jimbo la Kojani, lakini bado kero iliopo pale haijatatuliwa na wizara hii.

Mhe. Spika, naomba kumuuliza Mhe. Waziri je, ni lini kero hii inayowasumbua wananchi wa Kiuyu Minungwini na Kiuyu Kigongoni itatatuliwa. Jambo hili, Mhe. Spika nimeshalizungumzia sana tokea Baraza lililopita la mwaka 2010 mpaka lililomalizia mwaka 2015, lakini inaonekana bado serikali hawajataka kulitatua tatizo liliopo pale katika kijiji kile cha Kiuyu Minungwini.

Mhe. Spika: Uliza swali Mhe. Mjumbe.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Mhe. Waziri, naomba unipe majibu ya kutosha na yenye uhakika. Sitaki kudanganywa tena, ili wananchi wale na wao waweze kufaidika na matunda ya serikali yao.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, hiki ni kipindi cha maswali na majibu sio wakati wa bajeti. Wakati wa bajeti ya wizara bado. Lakini pamoja na umuhimu wa swali lako Mhe. Mjumbe, liko nje kidogo ya swali la msingi lakini nitamruhusu Mhe. Waziri ajibu kwa sababu ya umuhimu wake tu. Lakini swali lilikuwa refu sana na hukupaswa kutuhutubia. Mhe. Waziri majibu tafadhali.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati: Ahsante Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Ni kweli Mhe. Spika, nimepata taarifa hizo na siku kama ya pili leo ama ya tatu tayari tumezungumza na Mhe. Viwe Khamis Abdalla pamoja na Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Kojani ambaye ni mwakilishi wa jimbo husika.

Mhe. Spika, hivi karibuni *Director General* wetu wa *ZAWA* karudi India kwa ajili ya kuangalia ubora wa mashine. Tatizo liliopo pale ni *pump*, sasa tunataka tulitatuwe hili maana yake lisiwe kila siku linarudirudi. Kwa hivyo, nimuhakikishie tu kwamba baada tu ya *pump* kupatikana basi tatizo la pale litakuwa limekwisha, ahsante.

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi. Kwanza nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa majibu mazuri ambayo anajibu. Mhe. Spika, mimi swali langu lina vifungu (a) na (b).

(a) Mhe. Spika, eneo la Kijichi linapata mgao karibu siku sita ndani ya wiki hawajapata maji na tatizo kubwa ni ubovu wa mabomba. Je, ni lini mabomba yale Mamlaka ya Maji itakwenda kuyaziba.

(b) Mhe. Spika, tulifanya ziara na kamati yangu ya Ustawi wa Jamii tukakutana na baadhi ya madiwani wa Jimbo la Kijini na wakatulalamikia suala la maji safi na salama. Je, ni lini Jimbo la Kijini nalo litapata maji safi na salama.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati: Ahsante Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye vifungu (a) na (b)kama ifuatavyo.

(a) Mhe. Spika, wakati nafuatilia tatizo la Kijichi nilipata kesi hizo mbili, kesi ya *pump* na mabomba. Lakini kama nilivyokua nimesema kwamba jitihaza zetu tunazozifanya ni kuhakikisha wananchi wanapata maji, kwa hivyo hatuchoki katika kulifanya hilo.

(b) Mhe. Spika, nimshukuru Mhe. Waziri kwa sababu Kijini alikokutaja sio Makunduchi ni jimboni kwangu, muone kwamba hatupendelei na mimi pia kama Naibu Waziri nina tatizo hilo. Lakini Kijini ni kubwa, sasa ungesema tu ni eneo gani. Nafahamu kuna baadhi ya maeneo maji kidogo shida na ndio maana pia katika mtiririko ule wa ahadi wa kuchimba visima Kijini pia imo kwa ajili ya kulisaidia kupata hayo maji. Ahsante sana nakushukuru sana.

Nam. 32

Ununuzi wa Mitambo ya Kisasa ya Kusafishia Karafuu

Mhe. Shehe Hamad Mattar – Aliuliza:-

Zanzibar ambayo ni mzalishaji mkubwa wa zao la karafuu lenye ubora duniani kupitia Shirika la *ZSTC* limenunua mashine sita (6) za kupimia unyevu na mashine moja ya kusafishia ambayo ni ya kienyeji sana.

(a) Je, Shirika la *ZSTC* liko tayari kwenda Tanzania Bara katika maeneo ya *EPZ* kwa lengo la kujifunza na kuona mitambo ya kisasa ya kusafishia karafuu.

(b) Je, *ZSTC* baada ya kuiona mitambo hiyo ya kisasa itakuwa tayari kununua kwa ajili ya Zanzibar, ili kuziweka karafuu zetu katika hali ya usafi unaohitajika na kuweza kukabiliana na ushindani katika soko la dunia.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Mawaziri, yanapoulizwa maswali ya nyongeza yanayogusa majimbo yenu mjipange vizuri sana kuyajibu, kama ambavyo imemkuta sasa hivi Mheshimiwa. Mhe. Waziri wa Biashara na Viwanda majibu.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 32 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, shirika tayari limeshaiondoa mashine iliyokuwepo ambayo ni ya zamani na hivi sasa shirika lina mashine 5 za kisasa, ambapo 2 zimenunuliwa kwa fedha za shirika na 3 zimetolewa msaada na mmoja wa wanunuzi wakubwa wa karafuu Zanzibar.

(b) Mhe. Spika, kwa vile shirika tayari limeshanunua mashine hizo za kisasa za kusafishia karafuu, ambazo ndiyo pia hutumika katika nchi nyengine wazalishaji wa karafuu na ambao zinakidhi usafishaji wa karafuu zetu na zinatumia teknolojia rahisi zaidi, shirika linaona kwa hivi sasa halihitaji mashine nyengine. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwanza nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa majibu mazuri na yenye matumaini. Lakini Mhe. Spika, katika ziara yangu ya kikazi nilikuta mashine kama hizo za usafishaji wa karafuu pamoja na viungo vyengine vinatumika katika mashine hizo.

Je, mashine zilizonunuliwa zina uwezo wa kusafisha karafuu pamoja na viungo vingine au ni karafuu tu na kama hakuna mashine kama hizo. Je, kwa nini hatutafuti mashine ambazo zinaweza kusafisha zaidi ya kiungo kimoja, kama vile karafuu, vanila, choroko mashine kama hizo zipo.

Je, mashine hizo zina uwezo wa kufanya aina ngapi ya kusafisha viungo.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mhe Spika, tunayoizungumzia ni karafuu, karafuu ya Zanzibar inasifika duniani kwa *quality*, sasa analozungumza Mhe. Mjumbe ni kuchanganya Vanila na mambo mengine hatuwezi kufanya hivyo kwasababu unapochanganya utaharibu *quality* ya karafuu ya Zanzibar ambayo *the World leader. (Makofi)*

Mhe. Spika, vitu hivi unapochanganya kuna kitu kinatokezea kinaitwa *contamination* kwa hivyo hatuwezi kuchanganya vitu kwasabau itatokezea *contamination* na itaharibu ladha ya hiyo kitu. *(Makofi).*

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Mhe. Spika, Ahsante kwa kunipa nafasi ya kuweza kuuliza swali dogo sana la nyongeza, lakini kabla nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa majibu ya swali mama aliyoyato. Lakini niipongeze serikali kwa kuweza kununua mashine mpya za kisasa katika kusafisha zao la karafuu.

(a) Mhe. Spika, ni utaratibu gani wa kizabuni ambao ulitumika katika kuzinunua mashine hizi mpya.

(b) Mhe. Spika, mashine hizi zilinunuliwa nchi gani na kwa gharama gani. Ahsante.

Mhe Naibu Waziri wa Biashara Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi la nyongeza kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzanzibar ina utaratibu kwa mujibu wa sheria ya manunuzi kwa utaratibu uliotumika ni ule utaratibu wa Sheria ya Manunuzi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

(b) Mhe. Spika, swali hili naomba nimjibu kwa maandishi. Ahsante, Mhe. Spika.

Mhe. Shaibu Said Ali: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri, kwa ufupi na wenye kufahamika naomba kumuuliza swali dogo la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwa kuwa hili la karafuu huharibika wakati mkubwa linapovunwa wakati wa mvua hasa kule kisiwani Pemba katika msimu wa vuli. Je, wizara au serikali ina mpango gani wa kununua mashine ya ukaushaji, ili kupunguza hasara wanazozipa wakulima na taifa wakati wa kuvuna zao hilo wakati wa mvua.

Mhe. Naibu Waziri wa Biasharana Viwanda Mhe. Spika, arejee tena swali lake, ni mashine gani.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, washa *microphone* tafadhali.

Mhe. Shaibu Said Ali: Mhe. Spika, ni mashine ya ukaushaji wa zao la karafuu wakati zinapovunwa wakati wa mvua, kwa sababu zao hili huharibika sana wakati wa mvua na wala hazipati kukauka. Je, serikali ina mpango gani kununua mashine hii ili kupunguza hasara kwa wakulima na taifa kwa ujumla. *(Makofi).*

Mhe. Naibu Waziri wa Biasharana Viwanda: Mhe. Spika, napenda nimpongeze Mhe. Mwakilishi kwa swali lake zuri kwa kuonesha uzalendo kwa kulipenda zao letu kuu la karafuu la Zanzibar pamoja na kulinda hadhi.

Mhe. Spika, naomba ni mjibu kwamba hili ni wazo tunaomba tulichukue na wizara yetu tutalifanyia kazi. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante Mhe. Spika, nashukuru kwa kuniona. Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. waziri naomba nimuulize swali dogo la nyongeza.

Mhe. Spika, Mhe. Naibu Waziri katika msimu wa uvunaji wa karafuu kama alivyosema Mhe. Shaibu Said Ali kule Pemba huwa inanyesha mvua na kupelekea wakulima zile karafuu

kuharibika. Ni kiasi gani ya karafuu *grade III* ambao zilizoharibika kwa msimu uliopita lakini pia ni kiasi gani ya gharama waliopata wakulima wetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Biasharana Viwanda: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako vile vile Mhe. Suleiman Makame Ali nimpongeze kwa kuonesha uzalendo kwa kulipenda kulienzi zao letu.

Mhe. Spika, kwanza napenda nikwambie mimi mwenyewe nimetembea nakuona maeneo mengi yanayozalisha karafuu kule Pemba, tena kilikuwa kipindi cha mvua na taka nikwambie wakulima wetu ni wazuri sana katika kuzipenda na kulihifadhi hili zao, sio nyingi zinazoharibika kwa sababu wanalihifadhi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, sasa ukweli ni kwamba na *ZSTC* tunanunua karafuu kwa *grade I, grade II na* Mpeta, sasa zote huwa tunazinunua hakuna mwananchi karafuu ambazo sisi tunaziita zimeharibika zimeharibika hicho hakipo kwasababu hizo tunazinunu kwa *grade III* lakini zote tunazinunua. Mhe. Spika, Ahsante.

Nam. 14

Ujenzi wa Nyumba za Madaktari

Mhe. Simai Mohammed Said – Aliuliza:-

Mhe. Spika, kwa kuwa moja ya sifa ya serikali yoyote ni kuboresha huduma kwa jamii na kwa kuwa madaktari wetu ni tegemeo kubwa la wananchi.
Je, kwa nini Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar isifikirie kuwajengea nyumba za malazi (*Doctors Compound Area*) kama walivyofanyiwa wapiganaji wetu majeshi ili kuleta motisha kwao.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Simai Mohammed Said mfuatiliani wa matatizo ya wananchi wa Jimbo la Tunguu swali lake Nam. 14 lenye kifungu (a) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, lengo la Wizara ya Afya na maelekezo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kuhakikisha kuwa madaktari pamoja na baadhi ya wafanyakazi ambao huduma zao ni umuhimu wa peke katika utowaji wa huduma za afya wanapatiwa makaazi karibu sana na maeneo wanayofanyia kazi, ili kuwawezesha kutoa huduma kwa wakati unaostahili.
Mhe. Spika, napenda kulieleza Baraza lako tukufu kwamba baadhi ya hosptali na ya vituo vya afya Unguja na Pemba zipo nyumba za madaktari ingawaje hazitoshelezi kwa mahitaji ya wafanyakazi hao, kama vile Hospitali ya Kivunge, Hospitali ya Micheweni, Hospitali ya Vitongoji, Hospitali ya Wete, na Hospitali ya Makunduchi ambapo nyumba ilijengwa kwa juhudi nguvu za wananchi na wizara imo katika hatua ya kuikamilisha nyumba hiyo.
Mhe. Spika, katika miaka ya hivi karibuni Wizara ya Afya ilimiliki nyumba kwa ajili ya kuishi madaktari karibu kila wilaya na maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba. Hata hivyo, kutokana na utaratibu usio wa kuridhisha uliokuwa ukitumika kuzitambua na kuzitunza nyumba hizo zilipelekea kama kwamba sio nyumba za Wizara ya Afya na zinadhibitiwa na Wizara ya Afya na

zinathibiwa na watu binafsi, wastaafu, na baadhi ya wafanyakazi wengine kuthubutu kubadilisha mikataba ya nyumba hizo kutoka Wizara ya Afya na kutengeneza mikataba yao binafsi.
Mhe. Spika, wizara yangu baada ya kuligundua tatizo hilo imeweka mpango maalum wa kuzifuatilia nyumba hizo na inaendele kufanya uhakiki wa kina wa kuzitambua na hatimae hatua za kisheria zitachukuliwa kwa wanaohusika ikiwemo kuzirejesha nyumba hizo katika umiliki wa Wizara ya Afya. Hivyo basi, tunatoa wito kwa wake wote ambao wanatumia nyumba hizo kuanza utaratibu wa kuzirejesha Wizara ya Afya haraka iwezekavyo. *(Makofi)*
Mhe. Spika, wizara katika kutekeleza agizo la Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar Dkt. Ali Mohammed Shein la kujenga nyumba za kisasa kwa ajili ya madaktari kuishi karibu na maeneo yao ya kazi. Wizara imeanza kuchukua hatua kwa matayarisho ya kujenga nyumba hizo katika Hospitali ya Abdalla Mzee Mkoani, pia katika Mradi mkubwa wa Ujenzi wa Hospitali ya Binguni utajumuisha na nyumba za wafanyakazi madaktari ili kuondosha tatizo la makaazi kuwa madaktari watakao toa huduma katika hospitali hiyo. Ahsante. *(makofi)*
Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Spika, ahsante sana nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa majibu mazuri sana hadi kufika kunifilisi kuweza kuuliza swali la nyongeza. Lakini nitauliza swali moja kidogo la nyongeza na ni matarajio yangu nitapata majibu mazuri.

Sasa swali langu lipo hapa, kwa kuwa utawala huu hapa kwa serikali iliopo madarakani hivi sasa imekuwa imepata nafasi ya maendeleo, wizara nyingi hasa Wizara ya Afya kwamba imekuwa sehemu moja ambayo inafuatiliwa kwa nguvu kubwa sana Mhe. Rais wa Zanzibar mwenyewe na tunaona mabadiliko makubwa sana baina ya visiwa vyetu vya Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, kwa nini wizara yake isifanye juhudi za makusudi katika nyumba ambazo zimejengwa na Taasisi ya *ZSSF*. Katika zile ambazo zimepangwa kujengwa hapa Mbweni, Wizara ya Afya ikapanga mpango maalum kununua jumba moja ambalo pia katika *tower* zile 48 moja tukapata kwa ajili ya madaktari wetu bingwa na wale wa katikati ili tuweze kuwapatia ya malazi na motisha kwa madaktari wetu. Ahsante sana Mhe. Spika.
Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, Ahsante, namshukuru sana Mhe. Mjumbe kwa wazo na shauri lake hili.

Mhe. Spika, hili tushalizungumza kwenye vikao viwili katika vikao vya uongozi Wizara Afya lakini bado lalijapata muafaka vizuri. Lakini kutokana na ushauri wako ambao unaweza ukakubalika na ukatusaidia Wizara ya Afya na kuahidi kwamba tutajijadili kwa kina zaidi na hatimae tupate ufumbuzi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, tulikwama kwenye tatizo dogo kwamba kwenye masafa kutoka Hospitali ya Mnazi Mmoja na pale nyumba zilipo ni mbali, sasa tulitaka tuwe na majengo ambapo yatakuwa ni karibu zaidi na hospitali, lakini ikishindikana hivyo Mhe. Mjumbe wazo lako ni zuri na tunakuhakikishia kwamba tutalichukua na kulifanyia kazi ili tuweze kufanikiwa.*(Makofi)*

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, Ahsante sana, nimuombe tu Mhe. Naibu Waziri kwanza kakiuka Kanuni ya 37 Wajibu na Mipaka ya Kujibu swali nafikiri Mhe. Spika sitaki kuisoma kupoteza muda lakini inatakiwa Naibu Waziri ajibu kwa ufupi kachukua muda mrefu kujibu swali hili.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, naomba ulize swali.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, ahsante sana. Hoja yangu Mhe. Naibu Waziri, ni lini tutafatana mimi na yeye mguu kwa mguu mguu kwenda kuangalia Hospitali ya Kizimkazi Dimbani ambayo imekwisha na mpaka leo haijafunguliwa, wananchi wa Kizimkazi Dimbani wanahitaji matibabu na hospitali ishakwisha sababu gani za msingi kutofunguliwa hospitali ile.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, ahsante. Kizimkazi hakuna hospitali kuna kituo cha Afya.*(Makofi)*

Mhe. Spika, kama ni hivyo mimi niko tayari kufuatana na wewe, tusubiri tumalize katika shughuli zetu za Baraza, ili twende tukaangalie hicho ambacho anakizumza na hatimae kitapata ufumbuzi. Lakini nashauri wakati tukiende mimi na yeye basi tukimshirikishe na Mhe. Waziri au Naibu Waziri wa Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ ambayo inahusika na ugatuzi. Kwa kweli, yote ambayo tutayakuta pale hayatahusu Wizara ya Afya tu naamini kuna mambo ambayo yatamhusu pia na yeye, tusisubiri siku nyengine ukasema ni lini. Ahsante Mhe.

UTARATIBU

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: kuhusu utaratibu.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, hapana naomba ukae.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Mhe. Spika, ahsante, kwa kuniona na mimi. Kwanza ni mpongeze Mhe. Waziri kwa majibu yake lakini ningependa nimuulize swali dogo lenye kipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, kutokana na majibu mama Mhe. Waziri aliyojibu kweli nyumba hizi zinajengwa kwa ajili ya madaktari, ili kuweka ufanisi zaidi kwa wagonjwa wetu ambao watakutwa na shida kwa muda wowote. Lakini inaonekana kwamba hizo ambazo zipo, hizo nyumba ambazo zipo ndani ya vitu daktari ambazo wanakaa si zote ambazo zinatumika kukaa hao madaktari wenye ili kuondoa tatizo kwa wagonjwa wetu. Sasa kama wizara itachukua utaratibu gani kuhakikisha kila nyumba na kwa kila mfanyakazi wa kituo anafika kwenye, ili nyumba na anaishi ili kuondosha usumbufu kwa wagonjwa wetu. (*Makofi*)

(b) Mhe. Spika, nyumba hizi nyingi zao zinaonekana kwamba tayari zimekuwa chakavu na nyingi zao zinavuja. Je, kama wizara inachukua utaratibu gani wa kufanya marekebisho kila baada ya mwaka, kuzipitia nyumba zile kufanya ukarabati na matengenezo ambayo yatawa-*cost* hao madaktari ambao watakuwa wanazitumia nyumba zile. *(Makofi).*

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe Spika, ahsante naomba kumjibu Mhe. Hidara Ali Makame swali lake la nyongeza lenye (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, katika jibu langu la msingi nilisemba kwamba wizara ina mpango na inaendelea kufuatilia na kufanya uhakiki wa kina kwa ajili ya nyumba zote za Wizara Afya ambazo ziko mikononi mwa mwa watu au wafanyakazi.

(b) Mhe. Spika, Kwa hivyo katika ukakiki ule pia tumekusudia baada ya kuzibaini na kuzitambua zitafanyiwa ukarabati mkubwa, kwasababu tumebaini kwamba zote haziko katika hadhi ya nyumba ya kuishi watu au madaktari wetu. Kwa hivyo, nakuhakikishia kwamba zitakapo tu baina na kutambulika tukawanazo tutazifanyia marekebisho

makubwa, ili ziweze kuwa za kiwango na madaktari wetu waweze kuishi kutokana na hadhi yao.

Mhe. Nadir Abul-latif Yussuf: Mhe. Spika, *Bismilahi Rahman Rahiym*, Mhe. Spika ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Waziri wa Afya swali la nyongeza lenye (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, kwa kuwa Hospitali ya Mnazi Mmoja ni hospitali mama katika nchi yetu ya Zanzibar na ndio inayotegemewa na wananchi wote na kila siku wananchi wanakuwa wengi. Katika upande mpya uliojengwa wa upande wa bahari wa kushoto ni lini sasa Wizara yako itaweza kuchukua vile viwanja vya mpira vilivyokuwepo viwili ili ikaweka eneo kubwa kwa ajili ya hospitali ya Mnazi mmoja, na badala yake kuondosha usumbufu kwa siku za mbele.

(b) Mhe. Spika, niipongeze Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Mhe. Rais wetu Dkt. Ali Mohammed Shein kwa kujenga kituo changu cha Kikobweni cha Afya. Suala langu liko hapa. Mimi Mwakilishi wa Jimbo la Chaani nipo tayari kushirikiana na Wizara yako, kujenga Kituo cha Chaani Masingi upya kivunjwe, kijengwe upya na nipo tayari wakati wowote na sehemu ile ina raia zaidi ya 7,000 wanategemea kituo kile, na wanakwenda Kivunge na matokeo yake wanapata matatizo.

Je, ni lini Mhe. Waziri au Mhe. Naibu Waziri wa Afya tutakwenda pamoja na mimi ndani ya siku hizi kwa sababu suala ni muhimu kwenda kuona hali halisi na kutoa ufafanuzi jinsi ya kuanza kujenga kituo kile.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, napenda kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake la nyongeza lenye (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Hospitali ya Mnazi Mmoja imo katika mradi mkubwa wa ujenzi wa hospitali ile, kwa hivyo tunategemea sana kulitumia hilo eneo alilolisema pamoja na maeneo mengine, ili kuipangua hospitali ile kwa mujibu wa huduma ambazo zitakuwepo. Kwa hivyo, tegemea sana kwamba hilo eneo ambalo umelitaja tutalitumia napengine tutahitaji na eneo jengine la serikali ili kuweza kupanua ujenzi wa hospitali yetu ile *inshaallah*.

Lakini kuhusu Kituo cha Chaani ulichonieleza mimi niko tayari tutumie muda huu wa katikati baada ya kutoka saa 7, basi jipange tu ukiwa tayari niambie ili tuende. Lakini pia nashauri kama nilivyomshauri Mhe. Jaku Hashim Ayoub kwamba tukienda tumchukue na Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ anayehusika na ugatuzi kwa sababu naamini kwa tutayoyakuta kule hayatakuwa yangu mimi peke yangu. *(Makofi).*

Nam. 101

Ujenzi wa Viwanja vya Michezo vya Wilaya

Mhe. Suleiman Sarahan Said - Aliuliza:-

Naipongeza sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika juhudi zake za kuendeleza michezo na kufanya mipango ya makusudi ya kujenga viwanja vya wilaya, ili kuendeleza michezo.

(a) Je, suala hili limefikia wapi.
(b) Je, viwanja hivyo vitajengwa wapi kila wilaya eneo husika.
(c) Vitaanza lini kujengwa viwanja hivyo na lini vitamalizika.

Mhe. Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 101 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inapokea pongezi kwa juhudi zake za kuendeleza Michezo hasa katika hatua za uimarishaji wa miundombinu ya michezo na ujenzi wa Viwanja vya Michezo vya Wilaya, ili kuendeleza michezo.

(a) Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2016/17, serikali ilianza ujenzi wa Kiwanja cha Kitogani kwa hatua ya awali ambapo kwa sasa wananchi wameanza kukitumia lakini pia hatua za kukiimarisha na kukifanya kiwe cha kisasa zimeanza. Pia katika mwaka huu wa fedha 2017/18 serikali imeanza kufanya hatua za ujenzi wa viwanja viwili vya michezo vya Micheweni na Mkoani.

Awali wizara ilipanga kufanya ujenzi wa kiwanja cha Micheweni na katika Wilaya ya Kaskazini 'A'. Kiwanja cha Wilaya ya Kaskazini 'A' ujenzi wake haujaanza kutokana na hadi sasa eneo la ujenzi wa kiwanja hicho kutokupatikana. Hivyo ujenzi huo ulihamishiwa Kangani Wilaya ya Mkoani kwa vile walikuwa tayari walikamilisha upatikanaji wa eneo na yaani *"Site Plan".*

(b) Mhe. Spika, **v**iwanja vitano vitajengwa katika wilaya za Unguja na Pemba kama ilivyoainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya 2015 - 2020 kwa mpangilio ufuatao:-

i). Kitogani Wilaya Kusini Unguja - 2016/2017
ii). Kishindeni Wilaya Micheweni Pemba - 2017/2018
iii). Kangani Wilaya Mkoani Pemba - 2017/2018 iv). Viwanja viwili vilivyobakia ambavyo vinatarajiwa kujengwa Unguja vinategemea upatikanaji wa eneo.

Mhe. Spika, ujenzi wa kiwanja cha Kitogani kwa hatua ya awali umekamilika na unaendelea kutumika. Aidha, taratibu za ujenzi wa viwanja vya Wilaya ya Micheweni yaani Kishindeni na Wilaya ya Mkoani Kangani, vimeanza kufanyika na vinatarajiwa kumalizika mwezi wa Disemba 2018. Viwanja viwili vilivyobakia vinatarajiwa kujengwa mwezi wa Disemba. Ahsante sana.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru sana Mhe. Spika, nami nimshukuru sana Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri, ingawa humu katika wilaya sijaiona wilaya ya Chake-chake kiwanja chake lakini sawa wacha niendelee.

Nashukuru sana kwanza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mhe. Rais Dkt. Ali Mohammed Shein kwa juhudi zake za makusudi za kuvijenga viwanja hivi kila wilaya. Mhe. Spika, viwanja hivi lengo lake ni kukuza michezo hasa ya mpira wa miguu katika sehemu zote za ngazi za chini na kuja mpaka wilayani.

Mhe. Spika, juhudi hizi zimeendelea juzi tu tulikuwa na mechi zetu za Afrika Mashariki na tulikuwa na *Zanzibar Heroes* na matokeo yake tukapimwa vipimo vya kuongeza nguvu katikati ya mechi na tatizo lile likatupa *disappoint* sana kwa wachezaji wetu kutokukaa katika ngazi nzuri. Lakini majibu yake hatukupata kwamba sisi tulikuwa na makosa au hatukuwa na makosa au ilikuwaje. Vile vile, juzi tena timu yetu ya *Karume Boys* imekwenda Burundi na ikapata *sabotage* nyingine ya sababu ya kusema tumeongeza umri.

Viongozi wetu wa hapa wanasema wanasababu maalum kwamba wale wako kamili hawakupata sababu, lakini tatizo hili linajitokeza kila timu yetu ya Zanzibar inapokwenda nje. Lakini majibu ya serikali hatupati *feedback* yoyote kwamba makosa tunayo sisi au wale wanaotufanyia *sabotage* tunafanyaje suala hilo.

(a) Kwa hivyo, namuuliza Mhe. Waziri ana kauli gani kuhusu *Karume Boys* kwa sababu ya kutolewa kwenye mashindano hayo.

(b) Je, hivi viwanja vinavyojengwa vitakuwa chini ya ugatuzi wa Tawala za Mikoa au vitasimamia katika Wizara ya Michezo.

Mhe. Naibu Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi maswali yake kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwakilishi tumeanza na viwanja vitano, baadae tutaendelea hapo mbeleni lakini kwanza tumalize hivi vitano na tumejitahidi kugawa kila Mkoa alau wapate kiwanja kimoja.

(b) Kuhusu suala la Karume Boys, ni kweli kabisa serikali bado haijatoa tamko, kwa sababu hapa serikali haina fursa kubwa sana kwa sababu kile ni Chama cha Michezo kinaendeshwa na katiba zake na kina sheria zake, wetu sisi ni Katibu, Katibu ndiye anaetupa taarifa hizi zote.

Vijana ni kweli wamekwenda walikuwa ni wadogo *under seventeen* hawakutimiza ile miaka, na walipojaza zile fomu na kupeleka kwa sababu kama wangalikuwa wamezidisha miaka fomu zingerudi kabla vijana wetu hawajenda ile sehemu ya mashindano. Lakini wamefika kule mpaka wameingia uwanjani ndipo waliposomewa shitaka kwamba wamezidisha umri.

Kwa hiyo, mpaka sasa hivi tuwe na subira, tumekata rufaa labda niseme *ZFA* wamekata rufaa kwa hivyo tupo katika kusubiri majibu yatakayotoka kule ili tujue nini kinaendelea. Nashukuru sana.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante Mhe. Spika na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali m oja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b).

Mhe. Spika, mbali na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri. Katika majibu yake amesema kwamba serikali haihusiani na sakata hilo, hiyo ni kweli lakini hata hivyo timu za taifa ni timu za Wazanzibari wote ikiwa timu ya Taifa ya Tanzania ni ya Wtanzania wote. Je, kutokana na sakata hili ambalo limeikumba Zanzibar katika mashindano yale ya Burundi, na Katibu Mkuu wa Wizara aliipa chama au taasisi husika mwezi mmoja kutoa taarifa kamili kuhusiana na kadhia ile.

(a) Tunaiomba serikali itupe taarifa au maelezo ya kina kuhusiana na sakata lile.

(b) Mhe. Spika, tatizo hili limekuwa likiendelea kila wakati katika Chama chetu cha Mpira wa Miguu Zanzibar na chama hiki kimekuwa kina migogoro ya hapa na pale. Je, kutokana na kadhiya hiyo huoni kwamba kuendelea, kuendeleza kuidumaza na kuiangusha soka la Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Nassor Salim Ali swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

Maelezo ya kina kama nilivyosema kwamba tusubiri ile rufaa tuliyoikata majibu yake, kama wamekubali kosa ni la kwetu sisi basi viongozi wa *ZFA* inabidi wakae wajitathmini ule uongozi wao. Na kama ikiwa kosa ni lao wao basi tayari tumeshatumikia kipindi ambacho tumerejeshwa mashindano, tayari tumeshatumikia adhabu ya kwanza nafikiri kama kosa litakuwa lao wao basi adhabu ya pili nafikiri itafutwa. *(Makofi)*

Lakini nimwambie Mhe. Nassor Salim Ali kuwa uongozi wa *ZFA* wanapiga kura kila baada ya miaka minne. Kwa hivyo, tusubiri kipindi hiki wamalize baadae wapige kura niwaombe wale ambao ni wanachama wa huko kwenye vilabu wachague viongozi mahiri ambao wataweza kuliendeleza soka hili kutoka hapa na kuendelea mbele zaidi, kwa sababu wakishakumaliza huo uchaguzi wa vilabu utakuja uchaguzi wa wilaya baadae utakuja uchaguzi wa taifa. Kwa hivyo, nawomba wale ambao wanahusika wachague viongozi mahiri na sio kuchagua labda huyu fulani au huyu fulani. Ahsante sana Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Machano Othman Said: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii, naomba niulize swali moja la nyongeza lenye maelezo (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a. Katika majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri kuhusu viwanja alisema kwamba kuna viwanja vitano vitajengwa na serikali na viwanja vitatu akataja mpaka wilaya ambazo zitajengwa. Je, haoni kwamba hivi viwili navyo kimoja kikajengwa wilaya ya Magharib A.

b. Wakati wa ujio wa Rais wa *FIFA* Fankiro, Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo wa Zanzibar nae alishiriki, aliporudi alitwambia kwamba Zanzibar itapata viwanja viwili kutokana na mkono wa Rais wa *FIFA*. Lakini zipo habari zinazosema kwamba Rais wa *FIFA* alikusudia kwamba, fedha ambazo *TFF* wanapata kutoka *FIFA* ambao sasa hivi wana karibu bakaa kule *FIFA* ya *TFF* karibu dola kama milioni 6 hivi, hizo ambazo zitumike kujenga viwanja tisa Tanzania.

Sasa je, upi ukweli kuna fungu maalum limetengwa na *FIFA* kwa ajili ya viwanja au tamko lile linahusu zile zile fedha ambazo *TFF* wanapata katika ule mradi wao ndiyo ambao watengeneze viwanja na kama ni hivyo je Zanzibar watapata.

Mhe. Naibu Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo: Ahsante sana Mhe. Spika kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Machano Othman Said swali lake lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:

(a) Mhe. Mwakilishi, huko ambako bado hatujapata *site plan* viwanja hii itategemea na Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya watakapochangamkia tenda hii, kwa sababu sisi tumetoa fursa tunataka hivi viwanja vijengwe kila mkoa, Mkoa wa Magharibi tunaweza kujenga itategemea na yule Mkuu wa Wilaya atakavyochangamkia ile nafasi. Tunataka masharti yetu ya kiwanja kiwe mita mia 200 kwa mia 300, ili tuweze kupata ujenzi na majukwaa yake.

(b) Kuhusiana na hiyo pesa hili labda niseme tutalichukua ili tujue, lakini viwanja vya wilaya vinajengwa na serikali na bajeti ya serikali yenyewe na siyo pesa za *FIFA*. Nashukuru sana.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, tumemaliza maswali, Mhe. Jaku Hashim Ayoub nitakuruhusu baadae kidogo. Waheshimiwa Wajumbe, wakati wa maswali umekwisha nina tangazo, tangazo linatoka kwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ambae anawatangazia Wajumbe wa Kamati hiyo kukutana kwenye chumba chao cha mikutano mara tu baada ya kipindi hiki cha maswali na majibu. Mhe. Jaku Hashim Ayoub kuhusu utaratibu.

UTARATIBU

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika na mimi nakushukuru, naomba uniruhusu kutumia Kanuni ya 27(1) kwa ruhusa yako na ya 46 Kanuni za Kudumu za Baraza kuhusu Haki, Kinga na Fursa ya Wajumbe na Uwezo wa Baraza. Naomba uniruhusu niisome.

"Haki ya kupata taarifa na kujadili uhuru wa taarifa hizo ni haki ya Wajumbe wa Baraza hili kwa mujibu wa sheria namba 4 mwaka 2007 kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Baraza toleo la mwaka 2016".

Mhe. Spika, katika kipindi hiki mfano jana kumeonekana mtindo unaoota mizizi katika Baraza hili wa kuvunja wazi wazi haki hizi za Wajumbe na kutia aibu Bazara letu na kuonekana kwamba halifati sheria na kanuni zake zilizotungwa na wenyewe.

Mhe. Spika, kumekuwa na mtindo wa kutumia utaratibu wa kuweka hati mezani kuhusu hoja zinazotaka kutolewa taarifa na kusema Barazani na huku Wajumbe wa Baraza hili wakiwa na ripoti na taarifa hizo mikononi hasa zile hati ambazo wanalazimika kupatiwa kabla.

Mhe. Spika, mtindo huu unaanza kuzoeleka na kuonekana kama wa kawaida, wakati kinyume na sheria ya kanuni na taratibu za kibunge mbali mbali na tunavunja sheria ya kanuni zetu lakini pia tunavunja taratibu na mila desturi za Mabunge ya Jumuiya ya Madola ambayo Baraza hili linafuata Kanuni ya 154 naomba tuitizame inasemaje. Kwa vile Baraza hili ni Wanachama hai wa Jumuiya ya Mabunge naomba tuangalie Kanuni ya 154 Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, ungejaribu kufupisha kidogo kwa sababu tuna shughuli nyingine, muongozo wako unaoutaka ili niweze kukusaidia.

Mhe.Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana, Mhe. Spika mimi naomba kukumalizia ni dhahiri kwanza kiti kilikiuka masharti ya 67 ya kanuni ya kudumu na kwa kushindwa kusimamia kanuni ya matokeo ya Baraza hili, limepoteza muda, fedha na nguvu za Wajumbe imebidi kikao jana jioni kiakhirishwe. Hoja yangu Mhe. Spika, naomba nimalizie kwa kutaka kiti chako kitoe amri au rule.

1. Kwa kuwa utaratibu wa kuweka hati mezani kwa taarifa ambazo hazipo ni sawa na uvunjaji wa sheria na kanuni na utaratibu wa Bunge na mtindo huu uachwe usiendelee katika chombo hiki.

2. Kwa kuwa Kiti kiwe makini wakati wote kinapotakiwa kuamua, kusimamia kutilia nguvu kanuni hizi zisivunjwe na Mjumbe yoyote.

3. Haki za Wajumbe kupata taarifa zinazotaka kusemwa na kujadiliwa katika chombo hiki zilindwe kwa mujibu wa sheria wa kanuni na utaratibu wa kibunge.

Mhe. Spika, nataka mwongozo wa kiti chako.

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. Jaku Hashim Ayoub. Waheshimiwa Wajumbe pamoja na maelezo yote ambayo Mhe. Jaku Hashim Ayoub ameeleza na nadhani amegusa zaidi kile kitendo cha jana cha kuondosha kwenye *order paper* ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Nadhani kabla ya uondoshwaji ule Waheshimiwa labda nilizungumze kwa ujumla nisiende kwenye kipengele kimoja kimoja kama alivyoeleza Mhe. Jaku Hashim Ayoub. Ipo kwa mujibu wa kanuni vile vile nadhani kama utaangalia Mheshimiwa Jaku kanuni ya 27 (4) ambayo inasema shughuli za Baraza katika kila kikao zitatekelezwa kwa kufuata orodha ya shughuli au kwa kufuata utaratibu mwingine ambao Spika ataagiza ufuatwe kwa ajili ya uendeshaji bora wa shughuli za Baraza.

Waheshimiwa Wajumbe, tutaona kwamba shughuli zote tunazoziendesha zinakwenda kwa mujibu wa *order paper* na mambo yote tunayofanya kwa siku yote ni mwongozo ambao umo ndani ya *order paper*. Jambo lolote ambalo halimo kwenye *order paper* hatuwezi kuliendesha humu ndani kwa hiyo hata elekezo la Spika kumtaka Naibu Spika aondoshe ripoti ya *CAG* ni elekezo ambalo kwa mujibu wa katiba yale matakwa ya katiba serikali waliyatimiza, ripoti mimi nimeipokea lakini muda ambao nilikuwa nayo ripoti ya *CAG* haukutosha sana yaani Wajumbe wamepata muda mfupi sana wa kukaa kuiangalia ile ripoti.

Lakini, jambo jengine ni kwamba Wajumbe sina maana Wajumbe wa Kamati tu lakini pamoja na nyinyi wengine Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi mnatakiwa pia muwe mmepata ripoti ile sasa mimi nimeipata lakini ilikuwa bado sijasambaza kopi za ripoti ile kwenu nyinyi Wajumbe.

Waliobahatika kuona na Kamati ya Hesabu za Serikali na muda pia walioupata ulikuwa ni mdogo kwa hivyo nikaona ni busara ripoti ile tuiondoshe tuna muda mrefu sana hapa mpaka tumalize Baraza na matakwa ya Kikatiba yalikuwa yameshatimizwa na serikali, basi tupeane muda ili Wajumbe wote waweze kupitia ile ripoti waridhike, ili sasa waziri atakapokuja kuwasilisha ile ripoti hapa na Mwenyekiti wa Kamati atakaposoma ile ripoti yao ya kamati muwe na maswali ya kuuliza. *(Makofi)*

Ningeruhusu jana yafanyike yale bila shaka wengi wenu hamjapata *content* ya ile ripoti na msingekuwa na maswala ya kuuliza, nimefanya hivyo kwa ajili ya kukupeni muda ili na nyinyi muweze kuridhika na ndiyo katika uendeshaji mzuri kwa mujibu wa Kanuni Spika ana uwezo pia wa kuondosha shughuli kwenye meza. Kwa hivyo, nilimuagiza Mhe. Naibu Spika alifanye hilo aliondoshe hiyo ripoti ya *CAG* na serikali baadae wataleta kwa wakati muafaka ambao tutakubaliana na Baraza bila shaka mtafaidika na yale ambayo yatakuwemo kwenye ripoti.

Nashukuru sana kwa ushauri wako Mhe. Mjumbe, tunazidi kufuata masuala yanayohusu kanuni tunazifuatilia.

Kwa bahati mbaya sana jana ilitokea kidogo mvutano hapa wa kikanuni kwa sababu kwa mujibu wa kanuni Mjumbe ambae anachangia anaweza akaashiria katika mchango wake akasema kwamba nakusudia kuzuia kifungu na akakitaja kifungu chenyewe na hayo yalifanyika bahati kwa bahati mbaya sana Mhe. Mohammed Said Mohammed alifanya hayo lakini kiti ni mwanadamu, tunaita kiti lakini wanaokaa hapa ni watu.

Kwa hiyo, imo kupitikiwa mimi nadhani tuendelee kukumbushana kuhusiana na masuala ya kanuni. Hata, sisi tunaokaa hapa siyo mabingwa wa kanuni hizi kuna mambo mengi sana mpaka turudi tena ndani ya kanuni tuangalie, kwa hivyo wakati mwingine kupitikiwa kunakuwepo lakini ninachoahidi Waheshimiwa Wajumbe kwamba haya tutayarekebisha na tutaangalia mwenendo mzuri tutaendelea kuendesha kwa uangalifu kama vile ambavyo inahitajika kwa mujibu wa kanuni. *(Makofi)*

Baada ya maelezo hayo, naomba nimwite sasa Mwenyekiti ili aje achukue kiti na tuweze kuendelea na shughuli nyingine. Mhe. Mwenyekiti karibu sana.

(Mwenyekiti, Mhe. Shehe Hamad Mattar Alikalia kiti)

Mhe. Mwenyekiti: Katibu kwa shughuli inayoendelea.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Katibu, naomba nimwite Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, karibu sana.

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha

2018/19 - Wizara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa,
Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kuwasilisha hotuba ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa mwaka 2018/19, na kabla sijaanza kusoma muhtasari Mhe. Mwenyekiti naomba Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waelewe kwamba hotuba nitayoisoma ni muhtasari, lakini naomba pia kitabu hiki cha hotuba yetu kuanzia ukurasa wa kwanza hadi wa 175 uingie katika *Hansard* wa bajeti ya mwaka 2018/19.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu likae kama kamati kwa madhumuni ya kupokea kujadili na hatimae kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa mwaka 2018/19.

Mhe.Mwenyekiti, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, Mwingi wa Rehema, kwa kutujaalia kukutana tena hapa leo tukiwa na afya njema na kutuwezesha kuendelea katika Baraza hili la tisa, mkutano wa kumi wa bajeti kwa maendeleo ya wananchi wa Zanzibar.

Mhe.Mwenyekiti, nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kuiongoza nchi yetu katika hali ya utulivu, amani na siasa safi. Aidha, nampongeza kwa kusimamia vyema utekelezaji wa ILANI ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015-2020 inayotekelezwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Uongozi wake mahiri ni nguzo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kufikia uchumi wa kati ifikapo mwaka 2020. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nachukua nafasi hii pia kumpongeza Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, Balozi Seif Ali Iddi kwa utendaji wake mahiri. Miongozo na michango anayotupatia ina lengo la kuleta maendeleo katika ufanikishaji wa utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ.

Aidha, nikupongeze wewe Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Spika, Mhe. Naibu Spika, na Wenyeviti wa Baraza, kwa kuliongoza vyema na kwa umahiri mkubwa Baraza letu la Wawakilishi. Vile vile, nawapongeza Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati mbalimbali za Baraza la Wawakilishi, kwa ushirikiano na miongozo inayopelekea kupata ufanisi katika utendaji wa majukumu yetu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nitumie fursa hii kuipongeza Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum chini ya Mwenyekiti wake Mhe. Machano Othman Said, Mwakilishi wa Wananchi Jimbo la Mfenesini kwa maoni na ushauri wanayotupatia katika kipindi chote cha uhudumu wa kamati.

Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima kubwa naomba niwashukuru wananchi wa Jimbo la Tumbatu kwa mashirikiano wanayonipatia katika kuliendeleza jimbo letu. Ninawaahidi kuzidi kushirikiana nao kwa kipindi chote ili kufikia malengo tuliyojipangia. Aidha, natumia fursa hii kuwapa pole waathirika wa mvua za masika zinazonyesha na kupelekea watu kupoteza mali na

makaazi. Nachukua fursa hii kutoa wito kwa wananchi kuchukua tahadhari ili kuepukana na athari zinazoweza kutokea ikiwa ni pamoja na maradhi ya mripuko.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo, naomba sasa niwasilishe utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA WAKA WA FEDHA 2017/2018

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Ofisi iliidhinishiwa kiasi cha shilingi 122,322,500,000.00 zikiwemo shillingi 14,434,800,000.00 kwa matumizi mengineyo, shilingi 68,463,100,000.00 mishahara, shilingi 28,320,000,000.00 kwa kazi za maendeleo na shilingi 11,104,600,000.00 kwa ajili ya ruzuku kwa Wakala wa JKU, Tume ya Utumishi ya Idara Maalum na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, iliidhinishiwa kukusanya shilingi 629,090,000.00 ikiwa ni mapato yatakayoingizwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

Hadi kufikia Machi 2018, Ofisi iliingiziwa shilingi 97,237,361,078.00 sawa na asilimia 79. Kati ya hizo, shilingi 55,761,624,394.00 kwa ajili ya mishahara sawa na asilimia 81, shilingi 10,886,412,282.00 matumizi mengineyo sawa na asilimia 75, shilingi 21,932,887,016.00 kwa ajili ya kazi za maendeleo sawa na asilimia 77 na shilingi 8,656,437,386.00 sawa na asilimia 78 kwa ajili ya ruzuku.

Aidha, imekusanya shilingi 397,431,800.00 sawa na asilimia 63. Kwa upande wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, zilikadiriwa kukusanya shilingi 8,712,306,560.00 hadi Machi, 2018 zilikusanya shilingi 7,642,590,539.00 sawa na asilimia 88.*(Angalia kiambatanisho namba 1, 2 na4).*

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ imetekeleza majukumu yake kupitia Programu kubwa 30. Programu hizo zimegawika katika mafungu D01 hadi D12. Fungu D01 ni Programu zinazotekelezwa na Idara za Ofisi Kuu, Fungu D02 hadi D06 ni Programu zinazotekelezwa na Idara Maalum za SMZ, Fungu D07 hadi D11 ni Programu za Mikoa na Fungu D12 ni Programu ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii.

Mhe. Mwenyekiti, kupitia Programu zote 30, jumla ya watendaji 166 wamejengewa uwezo kupitia mafunzo ya muda mrefu katika ngazi na fani mbali mbali ambapo wanawake ni 79 na wanaume 87 *(Angalia kiambatanisho namba 5).*

Aidha, mazingira ya utendaji kazi ya ofisi yameendelea kuimarishwa kwa kufanya ukarabati wa ofisi, kuzipatia ofisi vitendea kazi na kuwapatia wafanyakazi stahiki zao. Ziara na safari za kikazi kwa Viongozi na Watendaji wa ofisi zimefanyika kwa lengo la kuongeza ufanisi.

Mhe. Mwenyekiti, kupitia mikoa yote, jumla ya wanafunzi 56,537 wameandikishwa na kuanza darasa la kwanza kwa mwaka 2018 Unguja na Pemba. *(Angalia kiambatanisho namba 9).*

Kwa upande wa msaada wa shilingi 5,000 kwa wazee wasiojiweza, jumla ya shilingi 412,560,000.00 zimetumika kwa wazee 9,168. *(Angalia kiambatanisho namba 10).*

Aidha, jumla ya matukio 713 ya udhalilishaji yameripotiwa yakihusisha wanawake 600 na wanaume 113 *(Angalia kiambatanisho namba11).*

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo ya jumla, naomba sasa kuwasilisha utekelezaji kwa kila fungu kuanzia D01 hadi D12.

PROGRAMU ZA OFISI KUU

Mhe. Mwenyekiti, Programu za Ofisi Kuu zinahusisha Programu kuu tatu ambazo ni Programu ya Usimamizi na Uendeshaji wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ ambayo inazo Programu Ndogo za Utumishi na Uendeshaji, Uratibu wa Kazi za Mipango, Sera na Utafiti na Program ndogo ya Uratibu wa Kazi za Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ Pemba; Programu ya Pili ni; Uratibu wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa inahusisha Programu ndogo mbili ambazo ni; Uratibu wa Tawala za Mikoa na Uratibu wa Serikali za Mitaa na Programu ya Tatu ni; Usimamizi wa Utumishi na Uratibu wa Idara Maalum za SMZ.

IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Idara ya Uendeshaji na Utumishi kupitia Programu ndogo ya Utumishi na Uendeshaji, ilipanga kutekeleza majukumu ya usimamizi wa masuala ya kiutumishi na huduma za Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ pamoja na kazi za Ukaguzi wa Ndani, Uhasibu, Ununuzi, na Utoaji wa Habari zinazohusu Ofisi. Kwa kipindi cha Julai hadi Machi 2018, shughuli zifuatazo zimetekelezwa:-

Mhe. Mwenyekiti, watendaji wa Ofisi wamejengewa uwezo kwa kupatiwa mafunzo ya muda mrefu katika ngazi na kada tofauti ikiwemo Shahada ya Manunuzi na Ugavi, Ukatibu Muhtasi, Stashahada na Shahada ya Kwanza ya Mahusiano ya Kimataifa na Stashahada ya Usimamizi na Utunzaji Kumbukumbu. Aidha, imetoa mafunzo ya ndani juu ya Sheria ya Utumishi wa Umma, Sheria ya Manunuzi na Uondoshaji wa mali chakavu, Sheria ya Fedha na Sheria ya Kazi Nambari 11 ya mwaka 2005 kwa watendaji wa Idara na Taasisi za Ofisi. Vile vile, imeendelea kuwapatia wafanyakazi stahiki zao.

Mhe. Mwenyekiti**,** vikao vinne vya Kamati ya Uongozi vimefanyika kujadili taarifa na nyaraka mbali mbali za Kisera na Sheria kwa ajili ya maamuzi ya vikao vya ngazi za juu Serikalini. Aidha, vikao vitano vya Bodi ya Zabuni na vitano vya Bodi ya Tathmini vimefanyika kujadili na kupitisha ununuzi wa huduma na vitendea kazi mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa upashaji habari jamii, Kitengo cha habari na Mawasiliano kimeendelea na kazi zake za kutoa taarifa mbali mbali kwa umma kupitia televisheni na redio za ZBC ambapo jumla ya vipindi 13 vinavyohusu ugatuzi na taarifa mbali mbali za Viongozi vimerushwa hewani na kuwafanya Wananchi kupata uelewa wa suala la Ugatuzi na faida zake Aidha, Kitengo kimetayarisha na kusambaza vipeperushi vyenye taarifa za utekelezaji wa kazi mbali mbali za Ofisi.

IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

Mhe. Mwenyekiti, kupitia Programu ndogo ya Uratibu wa Kazi za Mipango, Sera na Utafiti,kwa mwaka wa fedha 2017/2018, idara ilipanga kuratibu utayarishaji wa nyaraka, mipango, taarifa za utekelezaji, shughuli za utafiti na kutayarisha mfumo wa ufuatiliaji na tathmini. Kupitia Programu hii, shughuli zifuatazo zimetekelezwa:-

Mhe. Mwenyekiti, nyaraka mbali mbali zimetayarishwa na kuwasilishwa Serikalini kwa maamuzi na maelekezo. Nyaraka hizo ni pamoja na Waraka wa Mfumo wa Usajili wa Matukio ya Kijamii, Waraka wa Mradi wa Mji Salama na Zanzibar Salama na Waraka wa Shamba la Pamoja Kati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Misri liliopo Bambi. Pia taarifa za utekelezaji zimetayarishwa na kuwasilishwa katika Mamlaka husika ikiwemo Baraza la Wawakilishi. Aidha, kikundi kazi cha utayarishaji wa mfumo wa ufuatiliaji na tathmini kinaendelea kukamilisha mfumo huo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kushirikiana na taasisi ya sayansi na teknolojia ya Tanzania *(COSTECH)*, maeneo ya utafiti kwa taasisi zote zilizo chini ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ yamebainishwa ambapo jumla ya maeneo 14 yamebainishwa kuwa yanahitaji kufanyiwa utafiti.

Miongoni mwa maeneo hayo ni ucheleweshaji wa wananchi kufanya usajili wa matukio ya kijamii, sababu zinazosababisha kurejea kwa wanafunzi wa Chuo cha Mafunzo kutiwa hatiani, Utekelezaji wa haki za binaadamu kwenye Chuo Cha Mafunzo na Muamko wa vijana kujiunga na mafunzo ya uzalendo na uzalishaji mali JKU, Aidha, tafiti mbili zimeratibiwa ambazo ni Uwezo wa Serikali za Mitaa katika utekelezaji wa majukumu yake na Tathmini ya utekelezaji wa ugatuzi kwa kushirikiana na Shirika la Msaada la Marekani *(USAID).*

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ imetekeleza miradi 10 ya Maendeleo iliyoratibiwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti. Miradi hiyo ni: Mradi wa Mji Salama, Mradi wa Mageuzi ya Serikali za Mitaa, Mradi wa Ujenzi wa Skuli ya Sekondari ya JKU, Mradi wa Ujenzi wa Chuo cha Kurekebisha Wanafunzi Watoto Hanyegwa Mchana, Mradi wa Ujenzi wa Nyumba za Makaazi na Mahanga wa Chuo cha Mafunzo, Mradi wa Ujenzi wa Vituo vya Uokozi na Uzamiaji, Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Mama Wajawazito na Watoto,Mradi wa Kuimarisha Majengo ya KMKM, Mradi wa Kuimarisha Kiwanda cha Viatu *(KVZ)* na Mradi wa Kuimarisha Mfumo wa Usajili.

Mhe. Mwenyekiti, kupitia mradi wa Mji Salama, jumla ya kamera 786 zimewekwa katika maeneo ya Mji Mkongwe, Bandarini, Barabara ya Uwanja wa Ndege, Mnazi Mmoja na barabara ya Mkapa – Mtoni hadi Bububu. Antena za mawasiliano zimefungwa katika majengo ya Hospitali ya Mnazi Mmoja na Uwanja wa Malindi. Ufungaji wa vifaa katika kituo cha kupokea mawasiliano umekamilika na hivi karibuni tunatarajia shughuli hiyo itaanza rasmin.

Mhe. Mwenyekiti, Mradi wa Kupeleka Madaraka kwa Wananchi *(ugatuzi)* una lengo la kuimarisha utendaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa na kusogeza huduma karibu na wananchi. Katika kutekeleza mradi huu, miongozo ya uendeshaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa

imetayarishwa ambayo ni miongozo ya mipango na bajeti, ukusanyaji wa mapato, uhamishaji wa Rasilimali Watu kutoka Serikali Kuu kwenda Serikali za Mitaa na Miundo ya Kitaasisi ya Sekta zilizogatuliwa. Mkakati wa Mawasiliano kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa uko katika hatua ya kuchapishwa ili uanze utekelezaji.

Mamlaka za Serikali za Mitaa na kusogeza huduma karibu na wananchi. Katika kutekeleza mradi huu, miongozo ya uendeshaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa imetayarishwa ambayo ni miongozo ya mipango na bajeti, ukusanyaji wa mapato, uhamishaji wa Rasilimali Watu kutoka Serikali Kuu kwenda Serikali za Mitaa na Miundo ya Kitaasisi ya Sekta zilizogatuliwa. Mkakati wa Mawasiliano kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa uko katika hatua ya kuchapishwa ili uanze utekelezaji.

Mhe. Mwenyekiti, katika kutekeleza Mradi wa Ujenzi wa Skuli ya Sekondari ya Jeshi la Kujenga Uchumi Mtoni, ujenzi umefikia hatua ya uezekaji wa paa ambapo jengo hilo linatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwaka wa fedha 2017/2018. Mradi wa ujenzi wa Chuo cha Urekebishaji Wanafunzi Watoto Hanyegwa Mchana umeendelea na kufikia hatua ya kuinua ghorofa. Kwa upande wa Mradi wa Ujenzi wa Nyumba za Askari na Mahanga wa Chuo Cha Mafunzo, jumla ya majengo matano yamekamilika kujengwa Tungamaa na kufikia hatua ya kuezeka paa. Aidha, kwa Kambi ya Kengeja jumla ya majengo saba yamekamilika na hatua inayofuata ni kuezekwa.

Mhe. Mwenyekiti, Mradi wa ujenzi wa Jengo la Mama Wajawazito na Watoto liliopo hospitali ya Kibweni umekamilika na hatua inayofuata ni ya ununuzi wa vifaa tiba. Aidha, ujenzi wa nyumba za askari Kojani umekamilika pia fidia ya shilingi 55,000,000.00 zimelipwa kwa wananchi kwa ajili ya kuanza ujenzi Makombeni. Vile vile, hatua za awali za malipo ya ununuzi wa boti za uokozi zimeanza kwa upande wa Mradi wa Vituo vya Uokozi na Uzamiaji.

Mhe. Mwenyekiti, maandalizi ya Mradi wa Kiwanda cha Ushoni yameanza kwa kufanya kikao cha kumtafuta mzabuni wa vifaa vya ujenzi. Aidha, matayarisho ya kuunganisha Ofisi za Wilaya zote za Unguja na Pemba na Mkonga wa Taifa yameanza kupitia Mradi wa Usajili wa Matukio ya Kijamii ili kuweka mfumo wa Usajili wa Kielektroniki.

Mhe. Mwenyekiti, katika utekelezaji wa miradi hiyo ya maendeleo, jumla ya Shilingi 21,932,887,016.00 zimetumika. *(Angalia kiambatanisho namba 3).*

AFISI KUU PEMBA

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Programu Ndogo ya Uratibu wa Kazi za Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ Pemba ilipanga kufanya Ufuatiliaji wa shughuli za Ofisi, Kuratibu shughuli za Utumishi na kuratibu shughuli za Mipango kwa Taasisi za Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa upande wa Pemba. Kupitia Programu hii, shughuli zifuatazo zimetekelezwa:-

Ufuatiliaji wa sekta zilizogatuliwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa umefanyika kwa lengo la kuangalia maendeleo ya utekelezaji. (2) Vikao vya kujadili utekelezaji wa majukumu ya taasisi vimefanyika ili kuongeza ufanisi. Aidha, Ofisi imewapatia mafunzo wafanyakazi wanne

kati ya hao wanawake watatu na mwanamme mmoja. (3) Ofisi pia imeratibu mafunzo kwa Waheshimiwa Madiwani na Masheha juu ya Sheria namba 7 na 8 ya mwaka 2014 pamoja na mwelekeo wa majukumu mapya ya ugatuzi.

IDARA YA URATIBU WA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Idara ya Uratibu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kupitia Programu ya Uratibu wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ilipanga kusimamia Utekelezaji wa Mpango wa Ugatuzi, kufanya Mapitio ya Mipaka ya Kiutawala na Kusimamia Matengenezo ya Barabara za Ndani katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Shughuli hizo zimetekelezwa kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, utekelezaji wa mpango wa ugatuzi umeanza kwa matayarisho ya msingi ya kuelekea utekelezaji halisi. Mkakati wa Utekelezaji wa Ugatuzi *(Decentralization by Devoluation Strategy and the Road Map),* umeweka utaratibu wa kutekeleza ugatuzi hatua kwa hatua ambapo maeneo makuu matano ya kimkakati yalipangwa kufanyiwa kazi. Hadi kufikia Mwezi Machi, 2018 maeneo yote matano yamefanyiwa kazi na kutolewa mapendekezo Serikalini juu ya namna bora ya kutekeleza Ugatuzi.

Mhe. Mwenyekiti, Nina furaha kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba mapendekezo takriban yote yamekubaliwa na Serikali, ambapo Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta zilizogatuliwa zimetakiwa ziyatekeleze.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa eneo la Rasilimali watu, jumla ya watumishi 9,710 kutoka Wizara za Kisekta wanatarajiwa kuhamishiwa katika Serikali za Mitaa ifikapo tarehe 1 Julai, 2018. Uhamisho wa watumishi hao unaokwenda sambamba na kuhamishwa kwa mishahara pamoja na kumbukumbu za kiutumishi ambapo wafanyakazi hao sasa watawajibika kwa Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, idara imeratibu uhamishaji wa rasilimali nyengine ikiwemo vitendea kazi pamoja na kusimamia mipango ya kibajeti kutoka sekta zilizogatuliwa na kupelekwa kwenye Serikali za Mitaa.

Mhe. Mwenyekiti, hatua iliyofikiwa kwa pamoja baina ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ na sekta zilizogatuliwa hadi sasa zinaendelea kuonesha mwelekeo wa kuridhisha. Hatua hizo ni pamoja na kuimarika kwa upatikanaji wa huduma za afya ya msingi, matengenezo ya vituo vya afya na madarasa ya skuli pamoja na huduma za ugani. Washirika wa Maendeleo mbali mbali wameanza kuziunga mkono juhudi hizi za serikali wakiamini kwamba uamuzi huu ni fursa nyengine kwa wananchi kushiriki katika kupanga na kutekeleza mipango yao ya kujiletea maendeleo na pia kupata huduma zinazostahiki.

Mhe. Mwenyekiti, idara imeraatibu uanzishwaji wa Mabaraza ya Wadi na Kamati za Mashauriano za Shehia umeratibiwa ambapo jumla ya Kamati za Mashauriano za Shehia 268 na Mabaraza ya Wadi 59 kati ya 111 yameundwa. Aidha, miundo, miongozo na majukumu ya Idara za ndani, Mikoa na Halmashauri imetayarishwa na inatarajiwa kuanza utekelezaji wake mwanzoni mwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mhe. Mwenyekiti, kazi ya kuweka mipaka ya kiutawala inaendelea na inatarajiwa kukamilika mwishoni mwa robo ya pili ya mwaka 2018/2019. Katika kufanikisha kazi hii ushirikishwaji mkubwa umefanyika pamoja na kutoa mafunzo katika ngazi ya shehia. Jumla ya alama za kudumu "*beacon*" 4,000 zinaendelea kutengenezwa. Alama ambazo zitawekwa katika shehia zote za Unguja na Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, kukamilika kwa kazi ya uwekaji mipaka, kutaiwezesha serikali kuwa na maelezo sahihi ya mipaka ya kila shehia, ramani za kila shehia, wilaya na mikoa. Aidha, kazi hii inajumuisha pia kutayarishwa kwa *"data base"* ya taarifa zote za mipaka ya kiutawala pamoja na mfumo wa mawasiliano utakaowaruhusu wahusika wengine kupata taarifa hizo.

Mhe. Mwenyekiti, matengenezo ya barabara za ndani yanayofanywa na Ofisi ni miongoni mwa majukumu ya kisheria yanayoendelea kutekelezwa. Katika mwaka huu wa fedha, idara ilipanga kuzifanyia matengenezo barabara ndogo mbili za Msingini Chake Chake yenye urefu wa kilomita 0.65 na ile ya Soko Kongwe hadi Skuli ya Ng'ombeni Mkoani yenye urefu wa kilomita 0.21 kwa upande wa Pemba. Kwa upande wa Unguja barabara inayounganisha Nyarugusu hadi Kijitoupele yenye urefu wa kilomita 1.65 matengenezo yake yamekamilika na kwa zile za Pemba hatua iliyofikiwa ni ya kuwasilisha Mkataba wa Ujenzi kwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Mwenyekiti, mahitaji ya matengenezo ya barabara zilizo chini ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ ni makubwa ukilinganisha na uwezo halisi wa kifedha uliopo kwa hivi sasa. Kwa kipindi cha miaka mitatu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ imepokea shillingi 4,600,000,000.00 kutoka Mfuko wa Barabara kwa matengenezo ya barabara za ndani. Kiasi hichi cha fedha ni kidogo mno kukidhi mahitaji ya matengenezo ya barabara zenye urefu wa kilomita 50 zilizokwishafanyiwa upembuzi yakinifu na zile zinazojitokeza kwa mahitaji maalum.

Mhe. Mwenyekiti**,** mahitaji ya fedha za matengenezo ya barabara kwa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ yameongezeka pia baada ya kukabidhiwa barabara zilizojengwa kupitia Mradi wa *MIVARF* kutoka Wizara ya Kilimo. barabara hizo zilizojengwa kwa kiwango cha kifusi Unguja na Pemba kwa ujumla wake zina urefu wa kilomita 146. Kwa kuwa barabara hizi ni za kiwango cha kifusi, ni dhahiri kuwa muda wake wa kudumu ni mfupi. Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ inafikiria kuzifanyia matengenezo barabara hizi kwa kiwango cha lami, ili kuepuka gharama za matengenezo ya kila baada ya kipindi kifupi.

Mhe. Mwenyekiti, dhamira ya kujengwa kwa barabara hizi za *MIVARF* ni njema na naomba kuchukuwa fursa hii kuwapongeza na kuwashukuru wenzetu wa Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwa kusimamia ujenzi wa barabara hizi. Lengo kuu lilikuwa ni kuwasaidia wakulima wa vijijini kuongeza thamani ya mazao na kuwasilisha sokoni mapema na kwa gharama nafuu. Hata hivyo, wakati Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ inakabidhiwa barabara hizi, tayari zimeanza kuharibika na haja ya kufanyiwa matengenezo makubwa imejitokeza. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tayari imeshatoa muongozo na mkakati wa matengenezo ya barabara hizo.

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ iliahidi kuanza kutumia mfumo wa Kielektroniki katika ukushanyaji wa mapato katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kabla ya kumalizika kwa mwaka huu wa fedha.

Naomba kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba utekelezaji wa jambo hili umefikia hatua nzuri kwa kukamilika uwekaji wa miundombinu ya kupokea mfumo wa ukusanyaji wa mapato kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa zote. Hata hivyo, wakati Ofisi inajiandaa kupata kampuni ya kuweka mfumo huo, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ ilishauriwa kwamba kwa kuwa Serikali inakamilisha Mradi wa mfumo mmoja wa ukushanyaji mapato ya aina zote kupitia Bodi ya Mapato Zanzibar (*ZRB*) ambapo Serikali za Mitaa zitakuwa ni sehemu ya mfumo huo, ni vyema ikasubiriwa kuanza kwa mfumo huo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kufanya hivyo imeonekana ni dhahiri kwamba kutakuwa na unafuu mkubwa wa gharama za Mfumo pamoja na usimamizi wake. Hata hivyo, Halmashauri mbili za Wilaya ya Kati na Wilaya ya Kaskazini "A" tayari zimeanza kukushanya mapato yake kwa njia hiyo ya Kielektroniki ambapo mifumo yake itaunganishwa na Mfumo Mkuu wa Serikali mara tu utakapoanza kufanya kazi zake.

Mhe. Mwenyekiti, naomba Waheshimiwa Wajumbe waangalie ukurasa wa 11 hadi 16 kwa maelezo zaidi ya utekelezaji wa Programu ya Uratibu wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

IDARA YA URATIBU WA IDARA MAALUM ZA SMZ

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Idara ya Uratibu wa Idara Maalum za SMZ, kupitia Programu ya Uratibu na Usimamizi wa Idara Maalum za SMZ ilipanga kufuatilia utekelezaji na kutoa miongozo ya kazi kwa Idara Maalum za SMZ, kuandaa vikao vya Mahakama ya Rufaa na kufanya semina kwa kukuza uelewa wa shughuli za ulinzi na usalama kwa watumishi wa Idara Maalum za SMZ. Aidha, idara imepanga kuwajengea uwezo watumishi katika fani na ngazi mbalimbali.

Mhe. Mwenyekiti, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe waangalie ukurasa wa 16 hadi 17 kwa maelezo ya utekelezaji wa Programu ya Uratibu wa Usimamizi wa Idara Maalum za SMZ.

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Uratibu wa Idara Maalum za SMZ imefuatilia na kukagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya Idara Maalum za SMZ Unguja na Pemba, vile vile imesimamia na kukamilisha zoezi la uandikishaji wa vijana wa kujitolea wa JKU na JKT. Imeratibu na kusimamia vikao vitatu vya mahakama ya rufaa ya Idara Maalum za SMZ na kusikiliza maombi manne ya rufaa, kati ya hayo maombi matatu yameshatolewa maamuzi na ombi moja linasubiri maamuzi. Aidha, imefanya semina mbili za kukuza uelewa wa shughuli za ulinzi na usalama kwa watumishi wa Idara Maalum za SMZ.

TUME YA UTUMISHI IDARA MAALUM ZA SMZ

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Tume ya Utumishi ya Idara Maalum ilipanga kusimamia na kuendesha zoezi la uajiri, kutoa mafunzo ya Sheria za Utumishi kwa Maafisa na wapiganaji wa Idara Maalum za SMZ, kuwapandisha vyeo maafisa wa Idara

Maalum, Kusikiliza na kuyatolea maamuzi malalamiko ya watumishi na kuidhinisha nyongeza ya muda wa utumishi na ajira za mikataba.

Mhe. Mwenyekiti, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe waangalie ukurasa wa 17 kwa maelezo zaidi ya utekelezaji wa Programu ya Uratibu wa Usimamizi wa Idara Maalum za SMZ.

Mhe. Mwenyekiti, kupitia vikao vya Tume ya Utumishi ya Idara Maalum, jumla ya Maafisa 66 wa Idara maalum za SMZ wamepandishwa vyeo, malalamiko matatu yamesikilizwa na kutolewa maamuzi pamoja na kuidhinisha ombi la ajira ya mkataba na kuongeza muda wa utumishi kwa Maafisa saba. Aidha, kikao cha kujadili rasimu ya Sheria ya Tume ya Utumishi ya Idara Maalum za SMZ namba 6 ya mwaka 2007 kimefanyika, pia Semina mbili kwa Maafisa na Wapiganaji 125 kuhusu Sheria ya Utumishi ya Idara Maalum zimefanyika.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, fungu D01 liliidhinishiwa shilingi 25,720,200,000.00. Kati ya hizo, shilingi 2,465,000,000.00 kwa ajili ya mishahara, shilingi 2,060,200,000.00 kwa ajili ya matumizi mengineyo, shilingi 20,500,000,000.00 kwa kazi za maendeleo na shilingi 695,000,000.00 kwa ajili ya ruzuku ya Wakala wa JKU na Tume ya Utumishi ya Idara Maalum. Hadi kufikia Machi 2018, jumla ya shilingi 18,663,924,622.00 sawa na asilimia 73 zilipatikana. Kati ya hizo, shilingi 1,566,864,890.00 sawa na asilimia 64 kwa ajili ya mishahara, shilingi 1,293,476,452.00 sawa na asilimia 63 kwa matumizi mengineyo, shilingi 15,340,250,000.00 sawa na asilimia 75 kwa kazi za maendeleo na shilingi 463,333,280.00 sawa na asilimia 67 kwa ajili ya ruzuku. *(Tafadhali Angalia Kiambatanisho namba 1 na 2)*

PROGRAMU ZA IDARA MAALUM ZA SMZ (D02 – D06)

Mhe. Mwenyekiti, Idara Maalum za SMZ zinayo mafungu D02 hadi D06 ambapo kupitia mafungu hayo, jumla ya Programu 10 zimetekelezwa. Programu hizo ni Mafunzo kwa Vijana, Uzalishaji Mali na Ulinzi na Programu ya Utawala wa Jeshi la Kujenga Uchumi, Programu ya Huduma za Urekebishaji Wanafunzi na Programu ya Uongozi na Utawala wa Chuo Cha Mafunzo, Programu ya Ulinzi na Uzuiaji wa Magendo na Programu ya Utawala na Uendeshaji wa Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo, Programu ya Uzimaji Moto na Uokozi na Programu ya Utawala na Uendeshaji na Programu ya Ulinzi wa Nchi, Raia na Mali zao na Programu ya Utawala na Uendeshaji wa Kikosi cha Valantia.

Mhe. Mwenyekiti, maelezo yafuatayo yanahusu utekelezaji wa Programu hizo kwa Idara Maalum za SMZ.

JESHI LA KUJENGA UCHUMI (D02)

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Jeshi la Kujenga Uchumi kupitia Programu ya Mafunzo kwa Vijana na Uzalishaji Mali na Programu ya Ulinzi na Utawala lilipanga kuimarisha mafunzo ya amali na uzalendo kwa vijana, kuimarisha shughuli za uzalishaji mali, kuimarisha shughuli za Utawala na Uendeshaji na kuanzisha Wakala wa Ulinzi wa JKU.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nitoe maelezo mafupi kuhusiana na Ofisi ya Wakala wa Ulinzi wa JKU.

Mhe. Mwenyekiti, Wakala wa Ulinzi wa JKU ni Wakala wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mujibu wa Sheria namba 2 ya mwaka 2015. Wakala umeanza kufanya kazi zake baada ya kuteuliwa Mkurugenzi Mtendaji mwezi Agosti, 2017 na kufuatiwa kuteuliwa kwa Bodi ya Wakala wa Ulinzi mwezi Disemba, 2017. Wakala wa Ulinzi unafanya kazi zake chini ya mwamvuli wa Jeshi la Kujenga Uchumi na umepewa majukumu yafuatayo:-

1. Kutoa ulinzi kwa maeneo ya uwekezaji na shughuli zote za kitalii;

2. Kuhakikisha usalama wa wawekezaji; na

3. Kutoa miongozo ya kiusalama kwa wawekezaji.

Mhe. Mwenyekiti, Wakala wa Ulinzi umeanza kutoa huduma za ulinzi katika sehemu za kitalii na kibiashara. Hadi sasa unatoa huduma hizo kwa Hoteli 16 na Taasisi za Serikali nne.

Mhe. Mwenyekiti, naomba Waheshimiwa Wajumbe waangalie ukurasa wa 19 hadi 21 kwa maelezo ya utekelezaji ya Programu Jeshi la Kujenga Uchumi.

Mhe. Mwenyekiti, Jeshi la Kujenga Uchumi kupitia Programu ya mafunzo kwa vijana, limeendelea kutoa mafunzo ya uzalendo na amali kwa vijana 2,848. Kati ya hao, vijana 848 wanaendelea na mafunzo ya amali katika fani za Useremala, Umeme, Ufundi uwashi, Ufundi Bomba, Magari na Ufundi Mchundo katika skuli ya Ufundi ya JKU Mtoni. Vijana 2,000 wanaendelea na mafunzo ya uzalendo na uzalishaji mali katika kambi za JKU Unguja na Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, kupitia shughuli za uzalishaji mali za kilimo, mifugo, uvuvi, na viwanda vidogo vidogo, Jeshi la Kujenga Uchumi limezalisha tani 220 za mpunga, kunde tani 2 na mahindi na mtama tani 2. Kwa upande wa mifugo ya kuku na ng`ombe, JKU inafuga kuku 12,000 wa nyama na mayai pamoja na ng`ombe 54. Kwa upande wa Uvuvi JKU ina boti tatu za uvuvi ambazo zimeendelea kuvua samaki kwa wastani wa tani 1.5 kwa mwezi. Aidha, kupitia viwanda vidogo vidogo JKU imeendelea na uzalishaji wa fanicha mbali mbali na matofali.

Mhe. Mwenyekiti, katika Programu ya Utawala na Uendeshaji, watumishi tisa walijengewa uwezo katika fani za Afya, Uhasibu, Ugavi, Kilimo, Mifugo na Masoko. Aidha, jumla ya askari 184 walipatiwa mafunzo ya Uongozi mkubwa na mdogo wa kijeshi katika Vyuo vya Jeshi la Kujenga Uchumi, Kikosi cha Valantia Zanzibar na Jeshi la Wananchi Tanzania. Vile vile, watumishi walipatiwa stahiki zao na huduma ya chakula kwa walinzi imetolewa.

Huduma za Afya Zimeendelea Kutolewa kwa Maafisa,

Wapiganaji na Wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa miradi ya maendeleo, Jeshi la Kujenga Uchumi linatekeleza mradi wa Ujenzi wa Skuli ya Sekondari ya JKU ambayo imefikia hatua ya uwezekaji.Jengo hilo la ghorofa tatu linatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Jeshi la Kujenga Uchumi liliidhinishiwa shilingi 16,123,700,000.00 kwa kazi za kawaida hadi kufikia Machi 2018, liliingiziwa shilingi 14,711,743,542.00 sawa na asilimia 91. Kwa upande wa miradi ya maendeleo liliidhinishiwa shilingi 1,200,000,000.00 na limeingiziwa shilingi 940,000,000.00 sawa na asilimia 78. Aidha, Jeshi lilipangiwa kukusanya shilingi 84,555,000.00 na kukusanya shilingi 50,725,000.00 sawa na asilimia 60.

CHUO CHA MAFUNZO (D03)

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Idara ya Chuo cha Mafunzo ilipanga kutekeleza Programu ya Urekebishaji wa Wanafunzi wa Chuo cha Mafunzo na Programu ya Utawala na Uendeshaji.

Mhe. Mwenyekiti, naomba Waheshimiwa Wajumbe waangalie ukurasa wa 21 hadi 23 kwa maelezo ya utekelezaji wa Programu za Chuo cha Mafunzo.

Mhe. Mwenyekiti, kupitia Programu ya Urekebishaji wa Wanafunzi wa Chuo cha Mafunzo, Idara imetoa mafunzo ya elimu za amali kwa wanafunzi 144 katika fani za ufundi ushoni, uchongaji, uwashi, kilimo na kazi za mikono. Aidha, jumla ya wanafunzi 138 wamepatiwa huduma ya ushauri nasaha. Pia, imekamilisha ujenzi wa darasa la kufundishia wanafunzi Kiinua Miguu.

Mhe. Mwenyekiti, kupitia Programu ya Utawala na Uendeshaji, Idara imeendelea kuvipatia vifaa tiba vituo vyote vya afya vya Chuo cha Mafunzo. Imefanya kampeni ya kupima kifua kikuu na kufanya semina ya maradhi ya kuambukiza kwa Wanafunzi wote wa Chuo cha Mafunzo. Ujenzi wa ukuta wa Makao Makuu unaendelea. Vile vile, Idara imewapatia mafunzo watendaji tisa katika fani za Ufuatiliaji na Tathmini, Ushauri nasaha, Sheria, manunuzi, Rasilimali Watu, Uhasibu, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano na fani ya Kutunza Kumbukumbu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa shughuli za uzalishaji, Idara ya Chuo cha Mafunzo imenunua mashine mbili na kutengeneza miundombinu ya umwagiliaji maji katika shamba la Langoni. Aidha, imenunua pembejeo na kusambaza katika kambi za Unguja na Pemba. Katika kutekeleza Miradi ya Maendeleo, ujenzi wa Chuo cha Urekebishaji Wanafunzi Watoto huko Hanyegwa Mchana umeendelea na kufikia hatua ya uwekaji wa zege na kuinua matofali ya ghorofa. Kupitia Mradi wa Ujenzi wa Nyumba za Askari na Mahanga, jumla ya majengo matano kwa kambi ya Tungamaa yamekamilishwa kuezekwa na kazi za kuweka mifumo ya maji na umeme zinaendelea. Aidha, kwa upande wa Kambi ya Kengeja, majengo saba yamekamilika na maandalizi ya kuyaezeka majengo hayo yanaendelea.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Idara ya Chuo cha Mafunzo iliidhinishiwa shilingi 12,528,600,000.00 kwa ajili ya kazi za kawaida na shilingi 1,600,000,000.00 kwa miradi ya maendeleo. Hadi kufikia Machi 2018, jumla ya shilingi 10,250,412,136.00 zimeingizwa sawa na asilimia 81 kwa kazi za kawaida na shilingi 1,531,000,000.00 sawa na asilimia 96 kwa kazi za maendeleo. Aidha, ilipangiwa kukusanya shilingi 78,051,000.00 na kukusanya shilingi 34,000,000.00 sawa na asilimia 44.

KIKOSI MAALUM CHA KUZUIA MAGENDO (D04)

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo kilijipangia kutekeleza Programu kuu mbili ambazo ni Programu ya Ulinzi na Uzuiaji wa Magendo na Programu ya Utawala na Uendeshaji wa huduma za KMKM.

Mhe. Mwenyekiti, naomba Waheshimiwa Wajumbe waangalie ukurasa wa 23 hadi 24 kwa maelezo ya utekelezaji ya Programu za Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo.

Mhe. Mwenyekiti, kupitia Programu ya Ulinzi na Uzuiaji wa Magendo, doria katika ukanda wa bahari na nchi kavu zimefanyika kwa Unguja na Pemba ili kudhibiti hali ya usalama, magendo na uchafuzi wa mazingira baharini. Katika doria hizo, matukio ya utoroshaji wa rasilimali za nchi yaliweza kudhibitiwa ambapo jumla ya shilling 118,530,000.00 zimeokolewa kupitia doria hizo.

Mhe. Mwenyekiti, kupitia Programu ya Utawala na Uendeshaji wa huduma za KMKM, jumla ya wafanyakazi 53 wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu katika ngazi na fani mbali mbali zikiwemo Afya, Ubaharia, Utawala na Manunuzi. Huduma za chakula kwa Maafisa na Wapiganaji zimetolewa. Aidha, huduma za matibabu zimeendelea kutolewa kwa Maafisa, Wapiganaji na raia sambamba na kushiriki kuwapatia huduma za afya bure wananchi katika sherehe za miaka 54 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, katika kutekeleza miradi ya maendeleo, ujenzi wa Jengo la Mama Wajawazito na Watoto liliopo Hospitali ya Kibweni limekalizika na hatua inayofuata ni ununuzi wa vifaa tiba. Aidha, ujenzi wa nyumba mbili za Askari Kojani umekamilika na fidia kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Makombeni zimelipwa ambapo jumla ya shilingi 55,000,000.000 zimelipwa kwa wamiliki wa eneo ili kuanza kwa ujenzi wa nyumba hizo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo kiliidhinishiwa shilingi 20,695,400,000.00 kwa matumizi ya kawaida na shilingi 4,120,000,000.00 kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia Machi 2018, Kikosi kiliingiziwa shilingi 16,675,091,000.00 sawa na asilimia 81 kwa matumizi ya kawaida na shilingi 3,470,000,000.00 sawa na asilimia 84 kwa kazi za maendeleo. Aidha, Kikosi kilipangiwa kukushanya shilingi 39,025,000.00 na kukushanya shilingi 25,000,000.00 sawa na asilimia 64.

KIKOSI CHA ZIMAMOTO NA UOKOZI (D05)

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Kikosi kilipanga kutekeleza Programu kuu mbili ambazo ni Programu ya Utoaji wa Huduma za Zimamoto na Uokozi na Programu ya Utawala na Uendeshaji.

Mhe. Mwenyekiti, naomba Waheshimiwa Wajumbe waangalie ukurasa wa 24 hadi 26 kwa maelezo ya utekelezaji ya Programu za Zima Moto na Uokozi.

Mhe. Mwenyekiti, kupitia Programu ya utoaji wa huduma za Zimamoto na Uokozi, jumla ya matukio 341 yameripotiwa na kupatiwa huduma katika vituo vyote vya Unguja na Pemba. Jumla

ya watu 32 wameokolewa wakiwa hai na 16 wakiwa wamefariki. (Angalia kiambatanisho namba 7). Aidha, matukio yaliyoripotiwa yamesababisha hasara ya shilingi 3,170,000,000.00 na shilingi 12,900,000,000.00 zimeokolewa.

Mhe. Mwenyekiti, Kikosi kimefanya matengenezo madogo ya Makao Makuu ya Kikosi, Kituo cha Zimamoto Mwanakwerekwe, Kituo cha Zimamoto Kitogani, Kituo cha Zimamoto Marumbi, Ofisi Kuu ya Zimamoto-Pemba na Kituo cha Zimamoto Mkoani. Vilevile, matengenezo makubwa na madogo ya gari 20 yamefanyika. Aidha, gari mbili za kusafirishia Askari zimenunuliwa.

Mhe. Mwenyekiti, Kikosi kimeendelea kuimarisha usalama katika viwanja vya ndege kwa kuhudumia ndege kubwa 3,640 na ndege ndogo 5,202 wakati wa kutua, kuruka na kutia mafuta pia huduma kama hizo zimetolewa katika utiaji wa mafuta kwenye meli 704 na boti 1,493 na kuendelea kukuza usalama wa mizigo na abiria wanaotumia bandari. Katika kuelimisha jamii kuhusu kuchukua tahadhari juu ya majanga ya moto, vipindi 30 vya redio na 17 vya television ya ZBC vimerushwa hewani, vipeperushi 113 na elimu kwa Taasisi 37 za Serikali na 86 za watu binafsi vimetolewa. *(Angalia kiambatanisho namba 8).*

Mhe. Mwenyekiti, katika kutekeleza Programu ya Utawala na Uendeshaji. Maafisa 108 na Wapiganaji 220 wamelipwa posho za likizo, sare na kupatiwa huduma mbali mbali. Maafisa na Wapiganaji wamepatiwa mafunzo ya fani na kada tofauti zikiwemo Sheria, Manunuzi, Uchumi, Fedha, Afya, Katibu Muhutasi, Habari, Uzimaji moto viwanja vya ndege, Ufundi na Ugunduzi wa moto. Aidha, mafunzo ya uzamiaji kwa wapiganaji 20 na ya udereva kwa wapiganaji 31 yametolewa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Kikosi cha Zima Moto kiliidhinishiwa jumla ya shilingi 7,660,500,000.00 kati ya hizo, shilingi 6,810,500,000.00 kwa ajili ya mishahara na shilingi 850,000,000.00 kwa ajili ya matumizi mengineyo. Hadi kufikia Machi 2018, Kikosi kimeingiziwa shilingi 5,817,311,830.00 sawa na asilimia 74, kati ya fedha hizo, shilingi 5,053,425,900.00 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi 763,885,930.00 kwa matumizi mengineyo. Aidha, Kikosi kilikadiriwa kukusanya shilingi 52,034,000.00 na kukushanya shilingi 36,630,000.00 sawa na asilimia 70.

KIKOSI CHA VALANTIA (D06)

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Kikosi cha Valantia kilipanga kutekeleza Programu ya Ulinzi wa Nchi, Raia na Mali zao na Programu ya Uendeshaji na Utawala ambapo kupitia Programu hizo Kikosi kilipanga kuendelea kuimarisha amani na utulivu kwa nchi, raia na mali zao, kuwajengea uwezo wa kiutendaji kwa kuwapatia elimu Maofisa na Wapiganaji, kuimarisha makaazi ya Wapiganaji na kuendelea kutekeleza mradi wa Kiwanda cha Viatu cha Idara Maalum za SMZ.

Mhe. Mwenyekiti, naomba Waheshimiwa Wajumbe waangalie ukurasa wa 26 hadi 27 kwa maelezo ya utekelezaji wa Programu za Kikosi cha Valantia.

Mhe. Mwenyekiti, kupitia Programu ya Ulinzi wa Nchi, Raia na Mali zao, Kikosi kimefanya doria na pia kuwafikisha wapiganaji katika vituo vya ulinzi kwa wakati. Vile vile, kimeimarisha ulinzi katika vituo ikiwa ni pamoja na Ofisi za Serikali, Taasisi binafsi na nyumba za Viongozi Wakuu wa Serikali. Aidha, Kikosi kimetoa huduma za chakula kwa wapiganaji wote waliokuwa katika shughuli za ulinzi vituoni.

Mhe. Mwenyekiti, kupitia Programu ya Utawala na Uendeshaji, Kikosi kimesambaza dawa za matibabu katika vituo vinne vya afya vya Kikosi. Vile vile, Kikosi kimewapatia mafunzo ya kijeshi ngazi ya uongozi mdogo wapiganaji wake katika Chuo cha JWTZ kilichopo Lugalo. Aidha, kimeandaa Kanuni za Kikosi cha Valantia na kuzisambaza kwa wahusika wengine kwa ajili ya kupata maoni na michango. Ujenzi wa jengo la Ofisi Kambi ya KVZ Micheweni umefikia hatua ya uezekaji na gari moja kwa ajili ya shughuli za kiutawala imenunuliwa. Kwa upande wa mradi wa maendeleo, Kikosi kwa kushirikiana na vikosi vyote vya SMZ vimeanza maandalizi ya Kiwanda cha Ushoni na hatua iliyofikiwa ni kuandaa ramani za jengo la kiwanda na hatua za ununuzi wa vifaa vya ujenzi zitafanyika hivi karibuni.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Kikosi cha Valantia kiliidhinishiwa kutumia shilingi 9,788,400,000.00 kwa matumizi ya kawaida na shilingi 400,000,000.00 kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia Machi 2018, jumla ya shilingi 8,086,595,018.00 zimepatikana kwa matumizi ya kawaida sawa na asilimia 83 na shilingi 248,700,000.00 sawa na asilimia 62 kwa kazi za maendeleo. Aidha, kikosi kilipangiwa kukushanya shilingi 45,530,000.00 na kukushanya shilingi 32,400,000.00 sawa na asilimia 71.

PROGRAMU ZA MAMLAKA ZA MIKOA (D07-D11)

Mhe. Mwenyekiti, programu zinazotolewa za Mamlaka za Mikoa zimetekelezwa kupitia mafungu matano yaliyoanzia fungu D07 hadi 11, fungu D07 ambao ni Mkoa wa Mjini Magharibi, D08- Mkoa wa Kusini Unguja, D09- Mkoa wa Kaskazini Unguja, D10 - Mkoa wa Kusini Pemba na D11- Mkoa wa Kaskazini Pemba. Mikoa yote imetekeleza majukumu yake kupitia programu kuu tatu ambazo ni; Programu ya Kusimamia Shughuli za Serikali katika Mkoa, Programu ya Uratibu na Uendeshaji wa Tawala za Mikoa na Programu ya Usimamizi na Uendeshaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sasa nielezee utekelezaji kwa Mamlaka za Mikoa kuanzia fungu D07 hadi D11.

MKOA WA MJINI MAGHARIBI (D07)

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Mkoa wa Mjini Magharibi ulipanga kuimarisha ulinzi na usalama, kusimamia mpango wa matumizi bora ya ardhi, usafi wa kuufanya mji upendeze na kutoa huduma kwa wananchi ikiwa ni pamoja na kuwaendeleza vijana na kusimamia na kuwezesha utekelezaji wa dhana ya upelekaji madaraka kwa wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba Waheshimiwa Wajumbe waangalie ukurasa wa 28 hadi 36 kwa maelezo ya utekelezaji wa Programu za Mkoa Mjini Magharibi zikiwemo Manispaa ya

Magharibi, zikiwemo Manispaa ya Mjini, Manispaa ya Magharibi A na Manispaa ya Magharibi B.

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia Machi 2018, Programu ya kusimamia shughuli za Serikali katika Mkoa, imesimamia lengo la Serikali la kuwapatia elimu watoto wote waliotimia umri wa kuandikishwa skuli. Kupitia Kampeni ya MIMI na WEWE, Mkoa umeshirikiana na wananchi na viongozi wa Majimbo kukamilisha ujenzi wa madarasa matatu na maktaba moja Skuli ya Kijitoupele, madarasa manane na vyoo viwili Skuli ya kwa Sharifu Msa na madarasa manne katika Skuli ya Fuoni yenye vyumba vinne. Aidha, Mkoa umeshajihisha upatikanaji wa madawati 250 ili kupunguza tatizo la madawati mashuleni.

Mhe. Mwenyekiti, Mkoa umefanikiwa kukimbiza na kuadhimisha Kilele cha Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa kwa mwaka 2017 ambapo jumla ya miradi 15 ya maji, afya, elimu na umeme yenye thamani ya shilingi 6,584,991,587.00 imewekewa mawe ya msingi na kuzinduliwa.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuimarisha ustawi wa jamii, Mkoa umeratibu ulipaji wa pencheni jamii ya shilingi 20,000 ambapo jumla ya wazee 7,881 wamelipwa wakiwemo wazee wa Wilaya ya Mjini 4,684, Wilaya ya Magharibi "A" 1,473 na Wilaya ya Magharibi" B" 1,724. Mkoa umesaidia kaya masikini 2,000 kwa kuzipatia mahitaji muhimu ikiwemo chakula na nguo. Vilevile, Mkoa umeandaa matamasha maalum ya kuchangia damu kwa lengo la kusaidia mahitaji ya wananchi katika hospitali zetu ambapo jumla ya "packets" 1,132 za damu zilipatikana.Mkoa umeshirikiana na Jumuiya ya ZARDEFO kuchimba visima katika maeneo ya Mwera, Masingini, Dole, Nyamanzi na Chumbuni na taratibu za uchimbaji wa visima vyengine 21 zinaendelea.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuimarisha hali ya usalama, jumla ya vikao 33 vya kawaida na 46 vya dharura vya Kamati za usalama vimefanyika pamoja na kufanya ziara za ufuatiliaji wa masuala ya kiusalama yakiwemo udhibiti wa dawa za kulevya ambapo wauzaji wakubwa 25 wa dawa za kulevya walikamatwa na kufikishwa Mahakamani.

Mhe. Mwenyekiti, Mkoa wa Mjini Magharibi unaendelea kusimamia utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Kupambana na Vitendo vya Udhalilishaji wa wanawake na watoto kwa kubainisha viashiria vya udhalilishaji na kuwachukulia hatua wanaohusika pamoja na maeneo yanayohusishwa na vitendo hivyo. Aidha, Mkoa umezifungia nyumba za kulaza wageni zinazojihusisha na huduma za madanguro tisa na kumbi za muziki 10 zisizofuata utaratibu uliowekwa.

Mhe. Mwenyekiti, Programu ya Utawala na Uendeshaji wa Mkoa imeimarisha mazingira ya utendaji kazi kwa kufanya matengenezo madogo madogo na kuipatia Ofisi vifaa vikiwemo vya usafi, huduma za umeme na mawasiliano. Aidha, wafanyakazi wamepatiwa stahiki zao ikiwemo mishahara na maposho mbali mbali. Watumishi saba wamelipiwa sehemu ya ada zao ya mafunzo ya muda mrefu katika ngazi ya Uzamili, Shahada, Stashahada na Cheti katika fani ya Utawala wa Umma, Katibu Muhtasi, Sayansi ya Habari, na Uwekaji Kumbukumbu. Vile vile, mafunzo ya ndani yametolewa kwa wafanyakazi na Masheha 95. Aidha, vikao vya kamati za kisekta na uongozi vimefanyika kutathmini utekelezaji wa shughuli mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Mkoa wa Mjini Magharibi uliidhinishiwa shilingi 6,921,000,000.00 kwa matumizi ya kawaida. Hadi kufikia Machi 2018, shilingi 5,773,511,921.00 zimepatikana sawa na asilimia 83. Aidha, Mkoa ulipangiwa kukushanya mapato ya shilingi 45,530,000.00 na kukushanya shilingi 34,652,000.00 sawa na asilimia 76.

Mhe. Mwenyekiti, Programu ya Usimamizi na Uendeshaji wa Serikali za Mitaa katika Mkoa wa Mjini Magharibi inatekelezwa na Manispaa tatu ambazo ni Manispaa ya Mjini, Manispaa ya Magharibi "A" na Manispaa ya Magharibi "B". Maelezo yafuatayo yanaelezea utekelezaji wa shughuli zinazofanywa na Serikali za Mitaa;

BARAZA LA MANISPAA YA MJINI

Mhe. Mwenyekiti, katika kutekeleza shughuli za uendeshaji wa Ofisi, Baraza la Manispaa Mjini limeimarisha usafi wa mji kwa kusafisha, kuzoa na kuondosha taka zenye wastani wa ujazo wa 145,200m3, kusafisha misingi ya maji yenye urefu wa kilomita 21 katika maeneo ya Kwa Abasi Husein, Kwaalinatu, Miembeni, Begamoja, Gulioni na Mwembenjugu. Vile vile Baraza limesimamia ujenzi wa misingi mipya yenye urefu wa kilomita 19 unaofanyika kupitia mradi wa ZUSP katika maeneo ya Magogoni-Lumumba, Kijangwani, Magomeni-Migombani, Mnazi Mmoja, Karakana-Mtopepo na Kwamtipura-Saateni. Aidha, zoezi la kukusanya taarifa na kuzitambua nyumba zote zisizokuwa na karo na vyoo ndani ya Manispaa ya Mjini limefanyika pamoja na kufanya ukaguzi wa maeneo ya biashara za vyakula.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuimarisha usalama wa barabarani, Baraza limefunga mkataba na Serikali ya watu wa China kwa ajili ya uwekaji wa taa katika barabara zenye urefu wa kilomita 15. Mkataba huo utahusisha barabara ya Malawi (Malindi -Kwanyanya) na barabara ya Mkapa (Amani - Mtoni). Aidha, Baraza kwa hatua ya awali limeweka kifusi na kujenga vyoo katika kituo kipya cha daladala Kijangwani ili kiweze kutumika kwa muda na kuhamisha kituo cha daladala cha Kiswandui. Hatua inayofuata ni uwekaji wa lami ambao utafanyika mwishoni mwa mwaka 2017/2018. Kwa upande wa huduma za kiutumishi Baraza limewapatia mafunzo ya muda mrefu wafanyakazi wanane katika kada za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, Uhasibu, Ununuzi na Biashara.

Mhe. Mwenyekiti, katika utekelezaji wa shughuli za sekta zilizogatuliwa, Baraza la Manispaa Mjini limeimarisha utoaji wa huduma za afya kwa jamii kwa kuanzisha huduma za mama na mtoto katika kituo cha afya cha Chumbuni. Kadhalika Baraza lilitoa elimu kwa wakunga wa jadi juu ya umuhimu wa mama kujifungulia Hospitali, kupima afya kwa wananchi kupitia siku ya afya ya kijiji pamoja na kununua na kusambaza vifaa tiba na vitendanishi katika vituo vya afya 12 viliopo mjini.

Mhe. Mwenyekiti, Baraza la Manispaa la Mjini limeidhinishiwa kutumia shilingi 2,933,642,843 hadi kufikia Machi 2018, shilingi 2,622,070,606 zimepatikana sawa na asilimia 89. Kwa upande wa mapato Bazara lilipanga kukusanya shilingi 3,535,518,000 na kukusanya shilingi 2,723,964,746 sawa na asilimia 77.

BARAZA LA MANISPAA MAGHARIBI "A":

Mhe. Mwenyekiti, katika utekelezaji wa shughuli za uendeshaji wa Ofisi, Manispaa ya Magharibi "A" imeendelea na jitihada za kuimarisha usafi wa maeneo kwa kuondosha taka tani 5,760, kusafisha misingi ya maji na kupunguza majaa yasio rasmi 14. Zoezi la ukaguzi wa nyumba za makaazi 2,935 limefanyika, na matokeo yameonesha nyumba 2,053 hazikidhi vigezo vya afya na mazingira ambapo hatua za kisheria zimechukuliwa. Vile vile ukaguzi wa nyumba za biashara za vileo 25 umefanyika na matokeo yameonesha kutokidhi vigezo kwa nyumba hizo, hivyo hatua za kisheria zimechukuliwa ikiwa ni pamoja na kufutiwa leseni. Aidha, elimu ya afya na usafi imetolewa kwa jamii kupitia vipindi tisa vilivyorushwa na Shirika la Utangazaji la Zanzibar na pia kufanya mikutano 18 ya hadhara kwa wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, katika utekelezaji wa miradi ya wananchi, Baraza limeweka uzio Hospitali ya Selem Mfenesini; limefanya matengenezo katika Skuli za Kizimbani; Kianga na Mtopepo. Aidha, matengenezo ya vituo vya Afya Kizimbani, Selemu na Chuini yamefanyika yaliyohusisha uchimbaji wa kisima cha maji na uwekaji wa tenki kwenye kituo cha afya Chuini. Baraza limefanya matengenezo kwa uwekaji kifusi kwenye baadhi ya njia za ndani huko Mwera, Kihinani, Kijichi, Mtufaani, Masingini, Welezo na Mtoni. Vile vile, kwa kushirikiana na Viongozi wa Jimbo, Baraza limejenga darasa moja katika skuli ya Chuini na madaraja mawili katika Shehia ya Dole na Chunga.

Mhe. Mwenyekiti, katika utekelezaji wa sekta zilizogatuliwa, huduma za afya ya msingi imeimarishwa kwa kununua na kusambaza vifaa tiba katika vituo vya afya, kutoa huduma za mkoba, kutoa mafunzo juu ya huduma za mama na kununua na kusambaza vifaa vya usafi katika vituo vyote. Katika kuimarisha sekta ya Elimu, wahamasishaji wa elimu wa jamii 44, Walimu Wakuu na Wakuu wa Seksheni wamejengewa uwezo juu ya usimamizi wa Elimu, Uongozi na Utawala. Kwa upande wa sekta ya Kilimo; elimu na huduma za mifugo kwa wafugaji 67 imetolewa; wanyama 3,179 wametibiwa na wanyama 9,360 wamepatiwa chanjo dhidi ya magonjwa mbalimbali. Vile vile, elimu ya uvuvi bora imetolewa kwa vikundi vya uvuvi na mazao ya baharini.

Aidha, mafunzo kwa mabibi na mabwana shamba yametolewa kwa lengo la kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula.

Mhe. Mwenyekiti, Baraza la Manispaa Magharibi 'A' limeidhinishiwa kutumia shilingi 823,119,173.00 hadi kufikia Machi, 2018 shilingi 809,275,881.00 zimepatikana sawa na asilimia 98. Kwa upande wa mapato Bazara lilipanga kukusanya shilingi 650,000,000.00 na kukusanya shilingi 617,496,888.00 sawa na asilimia 95.

BARAZA LA MANISPAA MAGHARIBI "B"

Mhe. Mwenyekiti, katika kutekeleza shughuli za uendeshaji wa Ofisi, Manispaa ya Magharibi "B" imeimarisha usafi wa mazingira katika maeneo na kuondoa taka ambapo jumla ya tani 7,909 zimeondolewa. Operesheni maalum za kuzoa taka katika majaa yasiyo rasmi katika maeneo ya Kwa Mzungu, Magereza, Pangawe na Taveta zimefanyika. Manispaa imesafisha misingi ya maji ya Kiembesamaki, Uwanja wa Ndege na Mombasa hadi Kisauni. Katika kuimarisha afya za wananchi, Manispaa imefanya ukaguzi wa wafanyabiashara wa vyakula 478, kati yao 409 wamepewa vibali vya kuendelea na biashara.

Aidha, Manispaa imetayarisha na kurusha hewani vipindi 39 vya redio na televisheni ya ZBC vilivyoelimisha wananchi kuhusiana na masuala ya afya na mazingira.

Mhe. Mwenyekiti, katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa wananchi, Manispaa imekamilisha Ujenzi wa Skuli ya Abdalla Sharia Tomondo, imefanya matengenezo makubwa ya kituo cha Afya cha Mama na Mtoto Shehia ya Kombeni, kituo cha Afya Shakani, uwekaji wa nishati ya umeme wa Jua kituo cha afya Kombeni na Chukwani na kuunganisha huduma ya maji kituo cha Afya Kombeni. Aidha, imefanya matengenezo ya njia za ndani kwa kuweka kifusi katika njia ya Jumbi bonde la mpunga na Chukwani – Buyu.

Mhe. Mwenyekiti, katika utekelezaji wa shughuli za sekta zilizogatuliwa, Manispaa imeendelea kuimarisha utoaji wa huduma katika vituo vya afya kwa ununuzi wa samani katika vituo 10 vya Wilaya ya Magharibi "B",ununuzi wa vifaa tiba na vitendanishi kwa vituo vyote pamoja na kuendeleza huduma za mama na mtoto. Kwa upande wa sekta ya elimu, uhamasishaji wa uandikishaji wa wanafunzi umefanyika ambapo jumla ya wanafunzi 5,662 wameandikishwa kwa darasa la kwanza na wanafunzi 1,628 wameandikishwa kwa ngazi ya maandalizi. Katika sekta ya Kilimo, Manispaa imesambaza mbegu ya mpunga tani moja na mbolea kilo 3,050 kwa wakulima. Jumla ya mifugo 7,843 imepatiwa chanjo aina ya Mahepe, Gumboro na Chambavu katika Shehia zote 18 za kiufugaji na kutibiwa magonjwa yaliyojitokeza. Katika kuendeleza uhifadhi wa Misitu, Manispaa imeotesha zaidi ya miche 170,000 ya miti ya kudumu katika vitalu vya Shakani, Kombeni na Dimani.

Mhe. Mwenyekiti**,** Baraza la Manispaa Magharibi 'B' limeidhinishiwa kutumia shilingi 812,459,732.00 hadi kufikia Machi shilingi 551,958,421.00 zimepatikana sawa na asilimia 68. Kwa upande wa ukusanyaji wa mapato ya ndani, Baraza lilipanga kukusanya shilingi 1,480,000,000.00 na kukusanya shilingi 1,125,989,621.00 sawa na asilimia 76.

MKOA WA KUSINI UNGUJA – (D08)

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Mkoa umetekeleza programu kuu tatu ambazo ni; Kusimamia Shughuli za Serikali katika Mkoa, Uendeshaji na Utawala wa Mkoa, Wilaya na Shehia na Usimamizi na Uendeshaji wa Serikali za Mitaa.

Mhe. Mwenyekiti, naomba Waheshimiwa Wajumbe waangalie ukurasa 36 hadi 42 kwa maelezo ya utekelezaji wa Programu za Mkoa wa Kusini Unguja zikiwemo Halmashauri Wilaya ya Kusini na Halmashauri ya Wilaya ya Kati.

Mhe. Mwenyekiti, Mkoa wa Kusini Unguja umefanya ufuatiliaji wa shughuli za maendeleo na kusikiliza kero za wananchi katika Shehia 21 na kubaini changamoto mbali mbali zikiwemo za upungufu wa elimu ya ufugaji wa kisasa, upungufu wa wataalamu wa huduma za ugani, kuwepo uvuvi haramu, upungufu wa wafanyakazi katika vituo vya Afya na uhaba wa upatikanaji wa maji safi na salama kwa lengo la kuzipatia ufumbuzi. Mkoa umeshirikiana na Mamlaka ya Maji Zanzibar ambapo umeweza kuitafutia ufumbuzi changamoto ya ukosefu wa maji katika Shehia 30. Miongoni mwa changamoto hizo ni kuchakaa kwa visima na matangi ya kuhifadhia maji, uwezo mdogo wa matangi ya kuhifadhia maji kulinganisha na matumizi na kukosekana kwa

huduma za maji safi na salama katika baadhi ya maeneo. Hata hivyo, baadhi ya changamoto zimeanza kutatuliwa ikiwemo kuchimbwa visima katika vijiji vya Cheju na Kijibwemtu. Aidha, ujenzi wa Kituo kipya cha maji Mitakawani umesimamiwa.

Mhe. Mwenyekiti, Mkoa umesimamia Ulinzi na Usalama kwa kuhakikisha amani na utulivu inapatikana katika kuwaletea maendeleo Wananchi ambapo jumla ya vikao 30 vya Kamati za Usalama vimefanyika na kujadili mambo muhimu yakiwemo kupunguza vitendo vya udhalilishaji, kupambana na dawa za kulevya, magendo, matukio ya uhalifu, uvunjifu wa amani, usalama wa raia na mali zao na kuimarisha doria za ulinzi katika Shehia zote za Mkoa.

Mhe. Mwenyekiti, umefanya ukaguzi wa Walimu na wanafunzi na kukutana na Kamati za Wazee za Skuli na Bodi za Elimu katika Skuli 16 za Mkoa. Shughuli za uratibu wa mitihani ya Taifa katika ngazi ya darasa la nne, la sita, kidato cha pili na kidati cha nne kwa mwaka 2017 zimesimamiwa na matokeo yameonesha kiwango kidogo cha ufaulu Kitaifa kulinganisha na mwaka 2016 ambapo kwa darasa la sita ongezeko la ufaulu ni asilimia 42, kidato cha pili ni asilimia 9 na kidato cha nne ni asilimia 13. Hivyo, mpango mkakati wa kuinua kiwango cha ufaulu umeandaliwa na hatua za utekelezaji zimeanza. Aidha, uhamasishaji wa uandikishaji watoto katika elimu ya Maandalizi na Msingi umefanyika.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuimarisha huduma za Afya, Mkoa umeratibu upatikanaji wa huduma za mama na mtoto na utoaji wa chanjo (Penta 3), utoaji wa elimu ya magonjwa yanayoambukiza na yasiyoambukiza na ugawaji wa dawa na vifaa tiba na kusambaza chanjo katika vituo 37 vya Afya. Vituo saba vipya vya Mama na Mtoto vimejengwa, kati ya hivyo vinne vimefunguliwa ambavyo ni kituo cha Afya Bambi, Umbuji, Ukongoroni na kituo cha Afya cha mkono kwa mkono Makunduchi na vitatu vipo katika hatua ya umaliziaji navyo ni kituo cha Afya Uroa, Kiboje na Tunguu.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuimarisha kilimo, Mkoa umeratibu matayarisho ya kilimo cha mpunga ambapo ekari 2,588 kati ya ekari 3,949.75 sawa na asilimia 65 zimechimbwa na kuburugwa, ambapo matarajio ya Mkoa ni kuvuna wastani wa tani 1.33 kwa ekari. Mradi wa Ng'ombe na Mbuzi wa maziwa katika Shehia ya Ndijani Mseweni na Mpapa umefuatiliwa. Matokeo ya ufuatiliaji huo ni kuongezeka kwa taaluma ya ufugaji wa kisasa na kupelekea kuongezeka kwa kipato. Aidha juhudi za kusaidia wakulima wa kilimo cha mboga zimefanyika ambapo wastani wa eka 200 zimelimwa. Mkoa kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi ulifanya mkutano na wananchi wa Shehia ya Charawe kuzungumzia umuhimu wa uhifadhi wa mazingira na kuzuia ukataji wa Mikoko sambamba na kuhamasisha upandaji wa miti ambapo jumla ya miti 2,572,959 imepandwa.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuweka mazingira bora ya kazi, Mkoa umefanya matengenezo ya Ofisi na kuipatia vitendea kazi. Aidha, wafanyakazi wawili wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu ngazi ya Shahada ya kwanza katika fani ya utunzaji kumbukumbu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Mkoa wa Kusini Unguja uliidhinishiwa shilingi 2,817,900.000.00 kwa matumizi ya kawaida. Hadi kufikia Machi 2018, shilingi 2,004,202,480.00 zimepatikana sawa na asilimia 71. Aidha, ulipangiwa kukushanya shilingi 13,008,000.00 na kukushanya shilingi 13,500,000.00 sawa na asilimia 104.

HALMASHAURI YA WILAYA YA KUSINI

Mhe. Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Kusini imesimamia shughuli za kuzoa taka katika mahoteli kupitia kampuni ya ZAN REK ambapo jumla ya shehena 252 sawa na wastani wa tani 502 zimezolewa. Vile vile, imeendelea kuimarisha mazingira ya kazi kwa kufanya utanuzi wa jengo la Ofisi na ununuzi wa samani pamoja na kuwapatia mafunzo ya muda mrefu watumishi wawili katika fani ya fedha na ustawi wa jamii ngazi ya Stashahada. Kwa upande wa miradi ya wananchi, Halmashauri imeendelea kuimarisha miundombinu ya utoaji wa huduma kwa kujenga vyoo Skuli ya Michamvi na Mtende na uezekaji paa Skuli ya Kijigoni. Aidha, banda la wanaotembelea wagonjwa Hospitali ya *'Cottage'* Makunduchi limejengwa.

Mhe. Mwenyekiti, katika utekelezaji wa shughuli za sekta zilizogatuliwa, Halmashauri imetoa huduma za afya ya msingi kwa mama na mtoto, ununuzi wa vitenganishi na vifaa tiba pamoja na kugharamia huduma za maji na umeme katika vituo vya Afya 11. Kwa upande wa sekta ya elimu, ukaguzi wa Skuli nne za maandalizi na tisa za msingi umefanyika na huduma ya lishe kwa watoto 1,264 katika skuli 10 imetolewa.Aidha, katika sekta ya kilimo, huduma za utibabu wa mifugo zimetolewa kwa kuwapatia chanjo Ng'ombe 850. Mafunzo ya ujasiri amali kwa vikundi 31 ambavyo vimejifunza njia ya utengenezaji wa dawa za asili za kuulia wadudu waharibifu yametolewa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Halmashauri ya Wilaya ya Kusini Unguja ilikadiriwa kukusanya shilingi 369,198,560 hadi kufikia Machi, 2018 imekusanya shilingi 442,894,240 sawa na asilimia 120. Halmashauri iliidhinishiwa shilingi 232,172,845 kwa shughuli za sekta zilizogatuliwa hadi kufikia Machi, 2018 imeingiziwa shilingi 192,583,062 sawa na asilimia 83. Ruzuku ya matumizi mengineyo iliyoidhinishiwa ni shilingi 230,000,000 hadi kufikia Machi, 2018 zimeingiziwa ya shilingi 192,410,000 sawa na asilimia 84.

HALMASHAURI YA WILAYA YA KATI

Mhe. Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Kati imetekeleza mradi wa ujenzi wa Skuli ya Maandalizi Bambi Matora na Pagali pamoja na kutoa huduma ya lishe kwa skuli 35 za maandalizi. Halmashauri pia imesimamia upatikanaji wa vifaa tiba, vitenganishi, huduma ya maji na umeme katika vituo vyote vya Afya 25. Ofisi imevipatia vitendea kazi vituo vya kilimo Dunga na Mchangani pamoja na kuimarisha huduma za kilimo kwa kuanzisha mashamba darasa mawili. Mabaraza matano ya vijana yamesaidiwa jumla ya Shilingi 3,080,125.00 pamoja na vifaa ili kujiajiri na kupunguza utegemezi wa ajira kutoka Serikalini.

Mhe. Mwenyekiti, shughuli za uendeshaji wa Ofisi ikiwemo ununuzi wa vitendea kazi, ukaguzi wa maduka ya biashara na usafi wa mazingira katika Shehia nane umefanyika. Wafanyakazi saba wamepatiwa mafunzo katika fani na ngazi mbali mbali. Semina tatu zilizohusiana na masuala ya Ugatuzi, ulipaji kodi na matumizi ya Sheria zimetolewa kwa Waheshimiwa Madiwani 12 na Watendaji.

Aidha, ujenzi na upanuzi wa jengo la Ofisi Dunga umefanyika.

Mhe. Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Kati kwa mwaka wa fedha 2017/2018, ilikadiriwa kukusanya shilingi 500,000,000 hadi Machi, 2018 imekusanya jumla ya shilingi 495,542,157 sawa na asilimia 99. Halmashauri iliidhinishiwa shilingi 381,227,156 kwa shughuli za sekta zilizogatuliwa hadi kufikia Machi, 2018 fedha zilizopatikana ni shilingi 260,477,199 sawa na asilimia Ruzuku ya matumizi mengineyo iliyoidhinishiwa ni shilingi 230,000,000 na hadi kufikia Machi 2018, fedha zilizopatikana ni shilingi 190,000,000 sawa na asilimia 83.

MKOA WA KASKAZINI UNGUJA (D09)

Mhe. Mwenyekiti, Mkoa wa Kaskazini Unguja umetekeleza Programu kuu tatu ambazo ni kusimamia shughuli za Serikali katika Mkoa, Utawala na uendeshaji katika Mkoa na Usimamizi na Uendeshaji wa Serikali za Mitaa. Kwa mwaka wa fedha 2017/2018, ulipanga kuendelea kusimamia shughuli za Serikali katika Mkoa, kuimarisha ulinzi na usalama, kusimamia na kuwezesha utekelezaji wa dhana ya upelekaji wa madaraka kwa wananchi na kuhamasisha jamii kupinga udhalilishaji.

Mhe. Mwenyekiti, naomba Waheshimiwa Wajumbe waangalie ukurasa 42 hadi 47 kwa maelezo ya utekelezaji ya Programu za Mkoa wa Kaskazini Unguja zikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini A na Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini B.

Mhe. Mwenyekiti, hadi Machi 2018, Mkoa wa Kaskazini Unguja umefanya vikao vya sekta ya elimu, kilimo na maji kwa lengo la kujadili utendaji wa sekta hizo. Aidha, Mkoa umefanya maandalizi na ukimbizaji Mwenge wa uhuru ambapo jumla ya miradi 14 yenye thamani ya shilingi 5,219,700,880 imetembelewa.

Mhe. Mwenyekiti, Mkoa umefanya ziara katika sekta ya Utalii ambapo umefanya uhamasishaji kwa wawekezaji wa mahoteli ya Kiwengwa juu ya umuhimu wa kuchangia miradi ya kijamii ambapo wawekezaji wamekubali kusaidia mradi wa maji Kiwengwa pamoja na kuongeza nafasi za ajira kwa wazawa. Vilevile, Mkoa umetoa mafunzo juu ya dhana ya "Utalii kwa Wote'' kwa wanafunzi wa skuli nne za Pwani Mchangani, Kinyasini, Donge na Mahonda kwa lengo la kuwafahamisha umuhimu wa sekta ya utalii na mchango wake kwa uchumi na maendeleo ya Taifa.

Mhe. Mwenyekiti, vikao 21 vya Kamati ya Uongozi vya Mkoa na Wilaya, vikao 31 vya Kamati za Usalama na vikao 13 vya Masheha vimefanyika ambavyo vilijadili na kuweka mikakati juu ya masuala ya kupinga udhalilishaji, ulinzi na usalama wa wananchi, magendo, uharibifu wa mazingira na kuangalia mwenendo mzima wa uwajibikaji kwa wafanyakazi. Aidha, vikao 19 vya Kamati ya Kupinga Udhalilishaji vya Mkoa na Wilaya vimefanyika. Mkoa umewafikia jumla ya wananchi 3,030 kupitia mikutano ya kupinga udhalilishaji katika Shehia 32 pamoja na kuendesha kongamano la wazi katika Wilaya Ndogo Tumbatu.

Mhe. Mwenyekiti, katika utekelezaji wa uendeshaji wa Ofisi, wafanyakazi sita wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu katika fani ya uchumi, usimamizi wa miradi ya maendeleo, Usimamizi wa Rasilimali watu, Katibu Muhtasi na Habari. Mkoa umewapatia wafanyakazi stahiki zao kwa wakati na kutoa huduma za Ofisi ikiwemo ununuzi wa vitendea kazi na kufanya matengenezo madogo madogo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Mkoa wa Kaskazini Unguja uliidhinishiwa shilingi 3,062,500,000.00 kwa matumizi ya kawaida. Hadi kufikia Machi 2018, shilingi 2,150,003,155.00 zimepatikana sawa na asilimia 70. Aidha, Mkoa ulipangiwa kukushanya mapato ya shilingi 13,008,000.00 na kukushanya shilingi 4,837,000.00 sawa na asilimia 37.

HALMASHAURI YA WILAYA YA KASKAZINI 'A'

Mhe. Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini 'A' iliendesha Tamasha la biashara la wajasiriamali Nungwi kwa lengo la kutambua fursa za biashara na masoko zilizopo. Halmashauri imesimamia usafi wa mazingira ikiwemo kufanya operesheni za usafi katika maeneo ya Nungwi, Mkokotoni, Pwani Mchangani, Kinyasini na Hospitali ya Kivunge ambapo jumla ya tani 1,922 za taka ziliondolewa kupitia vituo 21 vya kutupia taka vilivyojengwa. Ili kuhakikisha usafi wa mazingira unakuwepo katika maeneo mbali mbali ndani ya Wilaya, vifaa mbali mbali vya usafi vimenunuliwa na kukabidhiwa kwa skuli 33 za msingi.

Katika kuimarisha ukusanyaji wa mapato, Halmashauri imeanza kutumia mfumo mpya wa ukusanyaji wa mapato kwa njia ya kielektroniki kuanzia tarehe 15 Aprili 2018.

Mhe. Mwenyekiti, Halmashauri imetoa huduma za lishe, umeme na maji safi kwa skuli 37 za maandalizi na msingi na kufanya mikutano miwili ya uhamasishaji juu ya uandikishaji wa watoto skuli. Aidha, skuli za Potoa na Pwani Mchangani zimepatiwa huduma za maji safi kwa kuchimbiwa visima viwili na kufanya matengenezo ya vyoo vya skuli tatu za Pwani Mchangani, Mkokotoni na Kibeni. Madarasa manane pia yamefanyiwa matengenezo katika skuli za Nungwi na Kinyasini.

Mhe. Mwenyekiti, Halmashauri imefanya matengenezo makubwa ya kituo cha Afya Tazari na kujenga nyumba ya Daktari sambamba na kuweka mfumo wa maji katika kituo cha afya Tumbatu Jongowe. Vilevile, huduma za Mkoba kwa watoto 183 na watu wazima 23 zimetolewa. Aidha, huduma ya chanjo kwa watoto 8,096 na elimu ya Afya mashuleni kwa wanafunzi 1,469 katika skuli 16 zimetolewa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa mifugo, Halmashauri imekifanyia matengenezo kituo cha Potoa, imefanya ununuzi wa baiskeli kwa ajili ya mabwana na mabibi shamba na kutoa mafunzo ya ugani kwa wakulima 309. Aidha, imeotesha miche ya Mikarafuu 15,460, miche ya misitu 25,638 na miche ya matunda na viungo 23,397 katika kitalu cha Kivunge. Mikutano mitano ya uhamasishaji wa namna bora ya ufugaji samaki na ukulima wa mwani kwa wakulima 238 imefanyika sambamba na kutoa elimu kwa wafugaji 74 na kuwapatia chanjo wanyama 224. Matokeo ya uhamasishaji huo ni kupungua kwa maradhi ya mifugo na kuongezeka kwa uzalishaji. Aidha wafugaji wa samaki wamehamasika kwa kutafuta maeneo zaidi kwa ajili ya kutumia teknolojia ya kisasa ya ufugaji.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Halmashauri ilikadiria kukusanya jumla ya Shilingi 555,000,000.00 hadi kufikia Machi, 2018 imekusanya Shilingi 559,314,109.00 sawa na asilimia 101. Ongezeko hilo limetokana na kuongezeka kwa chanzo kipya cha mapato kupitia

ukusanyaji wa taka. Halmashauri ilipanga kupokea ruzuku ya Shilingi 758,827,000.00 ambapo hadi kufikia Machi 2018 imepokea Shilingi 539,551,000.00 sawa na asilimia 71.

HALMASHAURI YA WILAYA YA KASKAZINI "B"

Mhe. Mwenyekiti, Halmashauri imetoa huduma ya lishe kwa skuli 22 na kuhamasisha uandikishaji wa wanafunzi. Pia, Halmashauri imesambaza vifaa vya ujenzi kwa skuli ya msingi Donge Karange pamoja na kuendeleza ujenzi wa vituo sita vya TUTU. Aidha, matengenezo ya mfumo wa maji kwa skuli ya Mahonda msingi na ununuzi wa Vifaa vya maabara katika Skuli ya Mahonda Sekondari yamefanyika.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa huduma za afya, Halmashauri imefanya matengenezo ya Kituo cha Afya Bumbwini Makoba, ununuzi wa vifaa vya umeme Kituo cha Afya cha Kiongwe na Mahonda na ununuzi wa vifaa vya huduma za meno kituo cha afya Bumbwini Misufini umefanyika. Aidha, uwekaji wa samani Kituo cha Afya Mgonjoni, usambazaji wa dawa na vifaa tiba kwa Vituo 13 vya Afya umefanyika. Halmashauri pia imetoa elimu ya afya mashuleni na kufanya uchunguzi wa afya kwa wanafunzi 1,362 (wanawake 711, wanaume 651). Vilevile, Halmashauri imetoa huduma ya mkoba kwa watoto 252.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuimarisha huduma za ugani, Halmashauri imetengeneza Ofisi ya kilimo na ghala la kuhifadhia pembejeo katika kituo cha kilimo Mahonda Sakafuni lenye uwezo wa kuhifadhi zaidi ya tani 22,000 za mbolea, imefanya matengenezo ya matrekta sita yaliyotolewa na mradi wa PADEP ambayo yametumika kuchimbua na kuburuga kiasi cha ekari 1,832 za mashamba ya mpunga na kusaidia wakulima 4,640. Halmashauri imenunua vitendeakazi kwa wafanyakazi wa sekta ya kilimo pamoja na kuandaa shamba tano za mfano kwa mazao ya mpunga, muhogo, migomba, viazi vikuu na mahindi.

Mhe. Mwenyekiti, Halmashauri imechimba visima viwili vya maji safi katika vijiji vya Pangatupu na Kichungwani na kusambaza maji safi katika vijiji vya Mafufuni na Fujoni. Kupatikana kwa visima hivyo kumewapunguzia wananchi changamoto ya upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama. Aidha, Halmashauri imeliwezesha Baraza la Vijana la Wilaya kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, Halmashauri imejenga kituo kipya cha kitalu cha Mwanakombo na kukipatia huduma ya maji na umeme. Jumla ya miche ya mikarafuu 14,500, imeoteshwa na kusambazwa kwa wananchi, miche ya misitu 200 imoteshwa na kupandwa katika maeneo yaliyochimbwa mchanga na jumla ya miche 300 ya matunda imeoteshwa katika kitalu hicho na kuuzwa kwa wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini 'B' ilikadiria kukusanya jumla ya Shilingi 582,590,000.00 hadi kufikia Machi, 2018 imefanikiwa kukusanya Shilingi 703,270,277.00 sawa na asilimia 121. Ongezeko hilo ni kutokana na ongezeko la mapato yatokanayo na rasilimali ya mchanga. Halmashauri ilipanga kupokea ruzuku ya Shilingi 599,273,000.00 hadi kufikia Machi 2018 imepokea Shilingi 408,460,000.00 sawa na asilimia 68.

MKOA WA KUSINI PEMBA (D10)

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Mkoa wa Kusini Pemba kupitia Programu kuu tatu ulipanga kusimamia shughuli za Serikali katika Mkoa, kusimamia Ulinzi na Usalama, Kuwezesha utekelezaji wa dhamira ya upelekaji wa madaraka kwa wananchi na kusimamia upatikanaji wa huduma za kijamii katika Mkoa.

Mhe. Mwenyekiti, naomba Waheshimiwa Wajumbe waangalie ukurasa wa 48 hadi 52 kwa maelezo ya utekelezaji wa Programu za Mkoa wa Kusini Pemba ikiwemo Baraza la Mji Chake Chake, Baraza la Mji Mkoani.

Mhe. Mwenyekiti, Mkoa umefuatilia na kusimamia ujenzi wa madarasa mapya 17 katika Skuli ya Msingi Mizingani, Mgelema,Vitongoji na Furaha na ujenzi wa vyoo 12 katika Skuli ya Msingi Ngwachani na Mjini Ole. Mkoa umefuatilia na kusimamia utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa barabara zinazoendelea kujengwa katika Mkoa zikiwemo za Ole – Kengeja, Kipapo – Mgelema na Kuyuni – Ngomeni. Katika kuimarisha shughuli za kilimo na ufugaji, Mkoa umefanya ukaguzi wa miradi ya kilimo cha mboga pamoja na ufugaji wa ng'ombe wa kisasa na kuvijengea uwezo vikundi vya ushirika na ujasiriamali. Jumla ya ekari 8,950.25 zimelimwa sawa na asilimia 84 ya lengo, kati ya hizo ekari 7,101 zimelimwa kwa trekta na ekari 1,849.25 zimelimwa kwa kutumia jembe la mkono ambapo lengo la Mkoa ni kulima ekari 10,600.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuimarisha mazingira ya Ofisi, Mkoa umeendelea kuzifanyia matengenezo madogo madogo Ofisi za Mkoa na Wilaya ikiwemo uezekaji wa paa jipya katika Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Mkoani na kununua gari moja kwa ajili ya matumizi ya Ofisi na Viongozi wa Mkoa.

Mhe. Mwenyekiti, ili kuhakikisha amani, utulivu na Usalama wa raia na mali zao unaimarika, jumla ya vikao 41 vya Kamati ya Ulinzi na Usalama vilifanyika kujadili masuala ya amani na utulivu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Mkoa wa Kusini Pemba uliidhinishiwa shilingi 3,234,400,000.00 kwa matumizi ya kawaida. Hadi kufikia Machi 2018, shilingi 2,207,351,295.00 zimepatikana sawa na asilimia 70. Aidha, Mkoa ulipangiwa kukushanya mapato ya shilingi 11,708,000.00 na kukushanya shilingi 7,500,500.00 sawa na asilimia 64.

BARAZA LA MJI CHAKE CHAKE

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, katika utekelezaji wa miradi ya wananchi, Baraza la Mji Chake Chake limetekeleza miradi mbali mbali ya maendeleo ikiwemo ujenzi wa madarasamatano Skuli ya Mgelema, madarasa matano skuli ya Furaha, ujenzi wa vyoo vya umma sita Mjini Ole na ujenzi wa ukuta wa bwawa la maji machafu Kichungwani. Pia, matengenezo ya kituo cha Afya Tundauwa yamefanyikana kuweka mfumo wa maji safi na salama katika Vituo vya Afya Pujini, Shungi na Ndagoni.

Mhe. Mwenyekiti, katika uendeshaji wa Ofisi, Baraza limeendelea kupata huduma mbali mbali za uendeshaji wa Ofisi, ununuzi wa vitendea kazi, kufanya matengenezo ya vyombo vya usafiri

na limetoa huduma za uendeshaji wa Ofisi. Aidha, Baraza limefanya usafi wa mazingira katika maeneo yote ya Mji, misingi ya maji, uzoaji wa taka na kutoa elimu ya usafi katika Shehia.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa Sekta zilizogatuliwa, katika utekelezaji wa Sekta ya afya, Barazalimetoa huduma za mkoba, limewapatia chanjo watoto 6,033 na kuvipatia vituo vya afya 13 vifaa tiba na vifaa vya Ofisi. Kwa upande wa sekta ya elimu, Baraza limewapatia huduma ya lishe wanafunzi 1,338 wa skuli za maandalizina kufanya mikutano ya uhamasishaji wa uandikishaji wa wanafunzi katika skuli za maandalizi na msingi. Kwa upande wa sekta ya kilimo, jumla ya miche ya mikarafuu 8,000 na miti ya matunda 4,791 imeoteshwa katika vitalu vya Mkatamaini na Dodeani na kutoa vifaa vya kuendeleza ufugaji wa samaki kwa vikundi vitatu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Baraza la Mji la Chake Chake lilikadiria kukusanya shilingi 390,000,000.00. Hadi kufikia Machi 2018, limekusanya shilingi 346,258,505.00 sawa na asilimia 89. Baraza limeidhinishiwa shilingi 438,438,617.00 kwa shughuli za sekta zilizogatuliwa na kuingiziwa shilingi 305,855,110.00 sawa na asilimia 70. Ruzuku ya matumizi mengineyo liliidhinishiwa shilingi 158,500,000.00 na kupatiwa shilingi 106,152,157.00 sawa na asilimia 67 na ruzuku ya mishahara liliidhinishiwa shilingi 509,531,600.00 na kupatiwa shilingi 364,336,970.00 sawa na asilimia 72.

BARAZA LA MJI MKOANI

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Baraza la Mji Mkoani limeendeleza usafi katika maeneo yote ya Mji na kutoa elimu ya usafi katika Shehia saba, limepanda bustani kutoka barabara ya Ikulu hadi Bandarini na kujenga misingi ya maji ya mvua. Aidha, Baraza limeendelea kupata huduma za uendeshaji wa Ofisi pamoja na ununuzi wa vitendea kazi.

Mhe. Mwenyekiti, katika utekelezaji wa miradi ya wananchi, hatua mbali mbali zimefikiwa ikiwemo ujenzi wa barabara ya Mbuyuni- Chokaani na barabara ya Bububu – Shangini Michenzani kwa kiwango cha kifusi. Baraza limekamilisha ujenzi wa vyoo 12 vya Skuli ya Makombeni na vyoo sita katika Skuli ya Msingi Ngwachani,Soko la samaki na matunda Kangani na ujenzi wa madarasa mawili skuli ya msingi Mizingani. Pia, Baraza limefanya matengenezo makubwa ya Kituo cha Afya Makombeni.

Aidha, matayarisho ya ujenzi wa Ofisi ya Elimu Wilaya ya Mkoani yameanza kwa kuandaa michoro na kusafisha eneo la kiwanja.

Mhe. Mwenyekiti, katika utekelezaji wa Sekta zilizogatuliwa, Baraza limewapatia huduma ya lishe wanafunzi 2,522 wa skuli za maandalizi. Baraza limeendelea kutoa huduma ya chanjo ya kuzuia kifua kikuu kwa wananchi 1,493 pamoja na kufanya mikutano ya huduma ya mama baada ya kujifungua na pia kutayarisha mfumo wa ukusanyaji wa taarifa za afya.Baraza limesimamia shamba darasa kwa wakulima1,800 na kutayarisha ekari 100 za kuvuna maji ya mvua kwa kilimo cha mpunga Chambani. Uhamasishaji wa wafugaji kuogesha mifugo umefanyika katika Shehia 20 na kusaidia vifaa kwa vikundi tisa vya ufugaji wa samaki.

Mhe. Mwenyekiti, Baraza la Mji Mkoani kwa mwaka wa fedha 2017/2018, lilikadiriwa kukusanya shilingi 230,000,000.00 hadi kufikia Machi, 2018 limekusanya shilingi 259,959,485.00 sawa na asilimia 113. Baraza liliidhinishiwa shilingi 463,622,158.00 kwa shughuli za sekta zilizogatuliwa hadi kufikia Machi, 2018 Baraza fedha zilizopatikana ni shilingi 343,737,100.00 sawa na asilimia 75 Ruzuku ya matumizi mengineyo liliidhinishiwa shilingi 201,650,000.00 hadi kufikia Machi, 2018 fedha zilizopatikana ni shilingi 157,564,250.00 sawa na asilimia 78 Aidha, ruzuku ya mishahara iliidhinishwa shilingi 408,243,960.00 na fedha zilizopatikana ni shilingi 304,837,140.00 sawa na asilimia 75.

MKOA WA KASKAZINI PEMBA (D11)

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Mkoa wa Kaskazini Pemba ulipanga kusimamia shughuli za serikali katika mkoa, ulinzi na usalama, kuwezesha utekelezaji wa dhana ya upelekaji wa madaraka kwa wananchi na kusimamia masuala mtambuka katika Mkoa.

Mhe. Mwenyekiti, katika utekelezaji wa usimamizi wa shughuli za Serikali, Mkoa umesimamia na kufuatilia miradi 23 ya wananchi. Umesimamia kilimo cha mazao ya juu ekari 17,880.25 nakilimo cha mpunga ekari 8,059.75 ambapo jumla yatani 4,285 za mpunga zimevunwa. Aidha, ekari 193 zimelimwa kwa kilimo cha umwagiliaji maji. Mkoa pia umesimamia upatikanaji wa pembejeo za kilimokwa wakulima na kufuatilia shughuli za kilimo ili kuona juhudi zinazochukuliwa na wakulima katika kuimarisha kilimo nchini. Aidha, ziara katika sekta ya elimu zimefanyika katika Skuli za Maandalizi, Msingi na Sekondari ili kuangalia utendaji wa walimu katika Skuli.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuimarisha ulinzi na usalama, Mkoa umefanya vikao 20 vya Kamati ya Usalama vikiwemovikao 12 vya kawaida na vinane vya dharura. Vikao hivyo vilijadili masuala mbali mbali ya kuimarisha hali ya usalama ndani ya Mkoa. Aidha, operesheni maalum zilifanyika kudhibiti matumizi ya misumeno ya moto ambapo ya misumeno 38 ilikamatwa na matukio 44 ya dawa za kulevya yameripotiwa kituo cha Polisi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Mkoa wa Kaskazini Pemba uliidhinishiwa shilingi 3,289,100,000.00 kwa matumizi ya kawaida. Hadi kufikia Machi 2018, shilingi 2,605,137,886.00 zimepatikana sawa na asilimia 79. Aidha, Mkoa ulipangiwa kukusanya mapato ya shilingi 11,708,000.00 na kukusanya shilingi 6,011,000.00 sawa na asilimia 51 ya lengo.

BARAZA LA MJI WETE

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Baraza la Mji Wete limetekeleza miradi ya wananchi kwa kufanya matengenezo makubwa ya kituo cha afya Kiungoni, Ofisi ya afya Wete na vyoo saba Skuli ya Jadida. Ujenzi wamsingi wa maji ya mvua Bubujiko, ujenzi wa barabara ya Bubujiko-Uchozini kwa kiwango cha kifusi na ujenzi wa vidaraja katika eneo la kushukia pwani Ukunjwi umefanyika.

Mhe. Mwenyekiti, katika uendeshaji wa Ofisi, Baraza limenunua vitendea kazi na vyombo vya usafiri na kuwasomesha watumishi watatu katika ngazi ya Stashahada. Aidha, limeendelea

kusimamia usafi wa mji katika maeneo ya Wilaya ya Wete na kutoa elimu kwa wananchi juu ya umuhimu wa usafi na mazingira.

Mhe. Mwenyekiti, katika utekelezaji wa Sekta zilizogatuliwa, Baraza limewapatia huduma ya lishe wanafunzi 2,927 wa skuli za maandalizi. Baraza limenunua na kusambaza vifaa tiba kwa vituo vya afya 19, limetoa chanjo kwa watoto 5,368 na kuendeleza huduma za Mkoba katika vijiji 16 na visiwa viwili vya Uvinje na Kokota. Baraza pia limeanzisha mashamba darasa matatu kwa wakulima 60, limenunua vifaa vya kuulia wadudu waharibifu wa mazao, chanjo kwa mifugo na kutoa ushauri kwa wafugaji 620 kuhusiana na ufugaji bora. Aidha, tathmini ya uhifadhi wa pweza katika vijiji vya Uvinje, Mabaoni Fundo, Ngagu na Ndooni imefanyika ambapo wavuvi wamehamasika juu ya uhifadhi wa pweza ili kuongeza kipato chao.

Mhe. Mwenyekiti, Baraza la Mji Wete kwa mwaka wa fedha 2017/2018, lilikadiriwa kukusanya shilingi 250,000,000.00. Hadi kufikia Machi 2018, limekusanya shilingi 214,702,787.00 sawa na asilimia 86. Baraza liliidhinishiwa shilingi 439,412,000.00 kwa shughuli za sekta zilizogatuliwa hadi Machi, 2018 Baraza liliingiziwa shilingi 290,280,000.00 sawa na asilimia 66. Ruzuku ya matumizi mengineyo iliidhinishiwa shilingi 203,102,000.00 na kupata shilingi 132,200,000.00 sawa na asilimia Aidha, ruzuku ya mishahara iliidhinishwa shilingi 505,654,240.00 na kuingiziwa shilingi 375,522,420.00 sawa na asilimia 74.

HALMASHAURI YA WILAYA MICHEWENI

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni imetekeleza miradi ya wananchi kwa kukamilisha ujenzi wa soko la samaki Njuguni, kuendeleza ujenzi wa skuli ya msingi ya Chimba na ujenzi wa skuli ya Mjini Wingwi. Pia, matengenezo ya barabara ya Tumbe Magharibi na Kiuyu Kwamanda hadi Msitu wa Ngezi yamefanyika kwa kiwango cha kifusi. Matengenezo ya kituo cha afya Mkia wa Ng'ombe na uwekaji wa nishati ya umeme wa jua katika kituo hicho yamefanyika. Aidha, ujenzi wa nyumba ya daktari kituo cha Afya Maziwa Ng'ombe, matengenezo ya vituo vya afya vinane na ujenzi wa choo cha kituo cha afya Msuka yamefanyika. Vile vile, imeweka matangi ya kuhifadhia maji katika skuli ya Mtemani Wingwi, Kwale na Chamboni.

Mhe. Mwenyekiti, katika uendeshaji wa Ofisi, Halmashauri imenunua vitendea kazi, vyombo vya usafiri ikiwemo gari pamoja na kuwapatia mafunzo ya muda mrefu wafanyakazi watatu. Aidha, imeendelea kusimamia usafi katika maeneo yote ya Halmashauri na kuhamasisha wananchi juu ya umuhimu wa usafi na mazingira.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa utekelezaji wa Sekta zilizogatuliwa, Halmashauri imevipatia vituo vya afya 16 vifaa tiba, kulipia gharama za maji na umeme kwa vituo vya afya na kutoa huduma ya chanjo kwa watoto 4,313.

Imefanya Programu ya siku ya afya vijijini kwa Shehia nane. Katika Sekta ya elimu ya msingi na maandalizi, Halmashauri imewapatia huduma ya lishe wanafunzi 1,578 wa skuli za maandalizi na huduma nyengine kwa walimu. Elimu kwa wafugaji na chanjo kwa wanyama 11,747 imetolewa. Aidha, miche ya matunda 6,696 na mikarafuu 5,900 imeoteshwa.

Mhe. Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni kwa mwaka wa fedha 2017/2018, ilikadiriwa kukusanya shilingi 170,000,000.00. Hadi kufikia Machi 2018, imekusanya shilingi 153,197,722.89 sawa na asilimia 90. Halmashauri iliidhinishiwa shilingi 429,188,000.00 kwa shughuli za sekta zilizogatuliwa na kuingiziwa shilingi 346,109,200.00 sawa na asilimia 81. Ruzuku ya matumizi mengineyo iliidhinishiwa shilingi 250,000,000.00 na kupata shilingi 190,500,000.00 sawa na asilimia 76.

WAKALA WA USAJILI WA MATUKIO YA KIJAMII (D12)

Mhe. Mwenyekiti, Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii imeanzishwa kwa sheria namba 3 ya mwaka 2018 iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi Zanzibar na kutiwa saini na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi tarehe 2/01/2018.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Ofisi ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii imetekeleza majukumu yake kupitia Programu kuu mbili ambazo ni Programu ya Usajili wa Matukio ya kijamii na Programu ya Utumishi na Uendeshaji. Kupitia Programu ya Usajili wa Matukio ya Kijamii, Ofisi imesajili Wazanzibari wakaazi 10,130, waliofanyiwa maombi ya pili 3,417, na kupatiwa vitambulisho vyao. Aidha, imesajili vizazi 30,643 ikiwemo wanaume 15,446, na wanawake 15,197, vifo 1,671 ikiwemo wanaume 922, na wanawake 749, ndoa 120 na talaka 7.

Mhe. Mwenyekiti, kupitia Programu ya Utumishi na Uendeshaji, Ofisi ya Wakala wa Usajili imewapatia mafunzo ya muda mrefu wafanyakazi wake katika ngazi tofauti, ikiwemo Shahada ya Uzamili wafanyakazi watano, Shahada ya Kwanza wafanyakazi watatu na Stashahada wafanyakazi watatu.

Mhe. Mwenyekiti, katika utekelezaji wa mradi wa Usajili wa Matukio ya Kijamii, Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii imeanza matayarisho ya kupeleka mkonga wa Taifa katika Ofisi za Wilaya zote Unguja na Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Ofisi ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii imeidhinishiwa shilingi 3,768,600,000.00 kwa kazi za kawaida. Hadi kufikia Machi 2018, jumla ya shilingi 1,699,439,313.00 zimepatikana sawa na asilimia 45. Aidha, ilipangiwa kukusanya shilingi 234,152,000.00 na kukusanya shilingi 150,576,300.00 sawa na asilimia 64. Kwa upande wa kazi za maendeleo ilipangiwa shilingi 500,000,000.00 na kuingiziwa shilingi 403,337,016.00 sawa na asilimia 81.

MWELEKEO KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2018/2019, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, taendelea kutekeleza majukumu yake katika mafungu 12 yaliyoanzia D01 hadi D12. Kupitia mafungu hayo, jumla ya Programu kuu 30 zitaendelea kutekelezwa.

PROGRAMU ZA OFISI KUU (FUNGU D01)

Mhe. Mwenyekiti, Programu za Ofisi Kuu zinahusisha Programu kuu tatu ambazo ni Programu ya Usimamizi na Uendeshaji wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ ambayo inazo Programu ndogo za Utumishi na Uendeshaji, Programu ndogo ya Uratibu wa Kazi za Mipango, Sera na Utafiti, na Programu ndogo ya Uratibu wa Kazi za Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ Pemba; Programu ya Pili ni Uratibu wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ambayo inahusisha Programu ndogo mbili za Uratibu wa Tawala za Mikoa na Uratibu wa Serikali za Mitaa na Programu ya Tatu ni Usimamizi wa Utumishi na Uratibu wa Idara Maalum za SMZ.

Mhe. Mwenyekiti, Programu ndogo ya Utumishi na Uendeshaji imepanga kutekeleza majukumu ya usimamizi na masuala ya kiutumishi, kutekeleza kazi za ukaguzi wa ndani, uhasibu, ununuzi wa vitendea kazi na utoaji wa habari zinazohusu Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, matengenezo ya jengo na ununuzi wa samani.

Mhe. Mwenyekiti, Programu ndogo ya Mipango Sera na Utafiti imepanga kuratibu utayarishaji wa nyaraka, mipango na taarifa za utekelezaji. Kuandaa mpango mkakati wa maendeleo ya takwimu wa Ofisi, kuratibu na kusimamia maendeleo ya Sera za Ofisi na masuala mtambuka, kuandaa maandiko ya miradi, kuimarisha shughuli za ufuatiliaji na tathmini na kuratibu, kusimamia na kufanya tafiti kubwa na ndogo. Aidha imepanga kufanya tafiti mbili kubwa ambazo ni utafiti kuhusu kuchelewa kwa wananchi kusajili matukio ya kijamii na utafiti kuhusu ustawi wa maisha ya wanafunzi Chuo Cha Mafunzo.

Mhe. Mwenyekiti, Programu Ndogo ya Uratibu wa Kazi za Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ Pemba imepanga kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa shughuli za Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum kwa upande wa Pemba, kuratibu uandaaji na utekelezaji wa Mipango ya Taasisi za Ofisi na kutoa mafunzo kwa watendaji na Viongozi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mhe. Mwenyekiti, Programu ya Uratibu wa Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa imepanga kuendelea na kazi ya uwekaji wa Mipaka ya Kiutawala, kutekeleza Mkakati wa Ugatuzi, kuratibu kazi ya mapitio ya Sera na Sheria, kuendeleza mpango wa utekelezaji wa anuani za makaazi na postikodi na kukamilisha ujenzi wa barabara ya Kijitoupele hadi Fuoni Mambosasa.

Mhe. Mwenyekiti, Programu ya Usimamizi wa Utumishi na Uratibu wa Idara Maalum za SMZ imepanga kufanya vikao vya mashirikiano na Taasisi za Ulinzi za Muungano, Mahakama ya Rufaa ya Idara Maalum za SMZ, kufanya ziara za kikazi Unguja na Pemba, kufanya marekebisho ya Sheria ya Tume ya Utumishi ya Idara Maalum namba 6 ya 2007 pamoja na kusimamia na kuendesha zoezi la uajiri katika Idara Maalum. Aidha, imepanga kusimamia na kutoa miongozo ya kazi, tafiti na miradi ya maendeleo na kuvijengea uwezo viwanda na vyuo vya Idara Maalum za SMZ.

Mhe. Mwenyekiti, Programu imepanga kuandaa mafunzo msasa *(Refresher course)* kwa maafisa na wapiganaji wa Idara Maalum kwenye vyuo vya ndani na nje ya nchi, kuandaa mafunzo kwa

wakufunzi na kuandaa mitaala ya mafunzo na kusimamia mafunzo ya maafisa *(crash program)* ili iwe sehemu ya sifa za upandishwaji wa vyeo. Aidha, imepanga kusimamia mafunzo ya awali kwa vijana wanaotegemea kuajiriwa katika Idara Maalum za SMZ, kusimamia utekelezaji wa ujenzi wa Kiwanda cha Nguo *ZQTL* na ufungaji wa mashine za Kiwanda cha Viatu cha KVZ, kusimamia ununuzi wa sare na ununuzi wa gari maalum za operesheni.

Mhe. Mwenyekiti, ili programu zilizo chini ya Fungu D01 ziweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, kwa mwaka fedha 2018/2019, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 34,666,600,000.00 kati ya fedha hizo shilingi 9,068,400,000.00 kwa matumizi mengineyo, shilingi 1,473,200,000.00 kwa ajili ya mishahara, shilingi 615,000,000.00 kwa ajili ya ruzuku na shilingi 23,510,000,000.00 kwa kazi za maendeleo.

PROGRAMU ZA IDARA MAALUM ZA SMZ KWA MWAKA 2018/2019

Mhe. Mwenyekiti, Idara Maalum za SMZ zinayo mafungu D02 hadi D06 ambapo kupitia mafungu hayo jumla ya Programu 10 zitatekelezwa kupitia Jeshi la Kujenga Uchumi, Chuo Cha Mafunzo, Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo, Kikosi cha Zimamoto na Uokozi na Kikosi cha Valantia Zanzibar.

JESHI LA KUJENGA UCHUMI – D02

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2018/2019, Jeshi la Kujenga Uchumi litatekeleza majukumu yake katika Programu ya Mafunzo kwa Vijana na Uzalishaji Mali na Programu ya Utawala na Uendeshaji. Kupitia Programu hizo, Jeshi limepanga kuendelea kuimarisha mafunzo ya Uzalendo na Uzalishaji kwa vijana, kuimarisha mfumo wa Uzalishaji mali katika mashamba ya Unguja na Pemba, kuimarisha huduma za kiutawala, kuwajengea uwezo wa kiutendaji watumishi na kuanza maandalizi ya ujenzi wa kiwanda cha chakula cha Mifugo. Aidha, Wakala wa Ulinzi wa JKU, umepanga kuimarisha huduma kwa Wawekezaji wazalendo na wageni, kutoa mafunzo ya Ulinzi ya teknolojia za kisasa na kutoa Semina Elekezi kwa Askari wa Wakala wa Ulinzi

Mhe. Mwenyekiti, ili Jeshi la Kujenga Uchumi liweze kutekeleza majumu yake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2018/2019, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 22,674,500,000.00 kati ya fedha hizo, shilingi 1,902,000,000.00 kwa matumizi mengineyo, shilingi 18,622,500,000.00 kwa ajili ya mishahara na shilingi 2,150,000,000.00 kwa kazi za maendeleo. Aidha, naliomba Baraza lako Tukufu liridhie makusanyo ya shilingi 79,469,000.00 yatakayoingizwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

CHUO CHA MAFUNZO – D03

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2018/2019, Chuo cha Mafunzo kitatekeleza Programu ya Huduma za Urekebishaji Wanafunzi na Programu ya Uongozi na Utawala wa Chuo cha Mafunzo. Kupitia programu hizo, idara imepanga kuendelea kutoa huduma ya urekebishaji tabia kwa wanafunzi wa Chuo cha Mafunzo, kuwapatia wanafunzi huduma za msingi zikiwemo chakula, sare na huduma za usafi, kuboresha huduma za kiutawala, kuongeza uzalishaji mali na

kuendelea na Mradi wa Ujenzi wa Nyumba za Askari na Mahanga kwa kambi ya Wete na Kangagani kwa awamu ya pili.

Mhe. Mwenyekiti, ili Chuo cha Mafunzo kiweze kutekeleza Programu zake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe shilingi 16,059,700,000.00, kati ya fedha hizo, shilingi 11,701,400,000.00 kwa ajili ya mishahara na maposho, shilingi 2,258,300,000.00 kwa matumizi mengineyo na shilingi 2,100,000,000.00 kwa kazi za maendeleo. Aidha, naliomba Baraza lako Tukufu liridhie makusanyo ya shilingi 70,991,000.00 ili kuchangia Mfuko Mkuu wa Serikali.

KIKOSI MAALUM CHA KUZUIA MAGENDO – D04

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2018/2019, Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo kimekusudia kutekeleza Programu ya Ulinzi na Uzuiaji wa Magendo na Programu ya Utawala na Uendeshaji wa huduma za KMKM. Kupitia programu hizo, kikosi kimepanga kuimarisha ulinzi wa doria, Uokozi na Udhibiti wa magendo, kutekeleza Miradi inayosimamiwa na KMKM ya Vituo vya Uzamiaji na Uokozi, kufanya ununuzi wa vifaa vya Jengo la Mama na Watoto na uimarishaji wa Majengo ya KMKM, kuweka mazingira mazuri ya kazi na Ustawi wa Wapiganaji na kutoa huduma za Afya kwa wapiganaji na raia.

Mhe. Mwenyekiti, ili Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo kiweze kutekeleza Programu zake kwa mwaka wa fedha 2018/2019, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 28,552,100,000.00 kati ya fedha hizo shilingi 19,606,100,000.00 kwa ajili ya Mishahara, shilingi 3,946,000,000.00 kwa matumizi mengineyo na shilingi 5,000,000,000.00 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Aidha, naliomba Baraza lako Tukufu liridhie ukusanyaji wa mapato ya shilingi 33,505,000.00 na kuchangia Mfuko Mkuu wa Serikali.

KIKOSI CHA ZIMAMOTO NA UOKOZI – D05

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2018/2019, kikosi kimepanga kutekeleza Programu ya Utoaji wa huduma za Zimamoto na Uokozi na Programu ya utawala na uendeshaji wa Zimamoto na Uokozi. Kupitia Programu hizo, Kikosi kimepanga kuimarisha huduma za Zimamoto na Uokozi, kuimarisha majengo na makaazi ya Wapiganaji, kuwapatia sare, mafunzo na maslahi wapiganaji, kuwajengea uwezo Maafisa na Wapiganaji na kutoa huduma katika vituo maalum vya bandarini na viwanja vya ndege.

Mhe. Mwenyekiti, ili Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kwa mwaka wa fedha 2018/2019 kiweze kutekeleza Programu zake kwa ufanisi, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 8,740,800,000.00, kati ya fedha hizo shilingi 1,351,000,000.00 kwa ajili kwa matumizi mengineyo, shillingi 6,889,800,000.00 mishahara na shilingi 500,000,000.00 kwa kazi za maendeleo. Aidha, naliomba Baraza lako Tukufu liridhie makusanyo ya shilingi 74,184,000.00 yatakayochangia Mfuko Mkuu wa Serikali.

KIKOSI CHA VALANTIA ZANZIBAR – D06

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2018/2019, Kikosi cha Valantia kimepanga kutekeleza Programu ya Ulinzi wa Nchi, Raia na Mali zao na Programu ya Uendeshaji na Utawala wa Kikosi cha Valantia. Katika kutekeleza programu hizo kikosi kimepanga kuhakikisha amani na utulivu kwa raia na mali zao, kuimarisha mazingira mazuri ya kufanyia kazi na kuimarisha makaazi ya Wapiganaji.

Mhe. Mwenyekiti, ili Kikosi cha Valantia kiweze kutekeleza programu zake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2018/2019, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe shillingi 12,165,600,000.00 kati ya fedha hizo, shilingi 1,416,300,000.00 kwa matumizi mengineyo, shilingi 10,249,300,000.00 ni mishahara na shilingi 500,000,000.00 kwa kazi za maendeleo. Aidha, naliomba Baraza lako Tukufu liridhie makusanyo ya shilingi 60,259,000.00 ili kuchangia Mfuko wa Serikali.

PROGRAMU ZA MAMLAKA ZA MIKOA (D07-D11)

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2018/2019, Mamlaka za Mikoa zitatekeleza jumla ya programu 15 kupitia mafungu matano yaliyoanzia fungu D07 ambao ni Mkoa wa Mjini Magharibi, D08- Mkoa wa Kusini Unguja, D09- Mkoa wa Kaskazini Unguja, D10 - Mkoa wa Kusini Pemba na D11 - Mkoa wa Kaskazini Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, kulingana na kufanana kwa majukumu ya Mikoa, Wilaya na Mamlaka za Serikali za Mitaa, mikoa yote itatekeleza majukumu yake kupitia programu kuu tatu ambazo ni Programu ya Kusimamia Shughuli za Serikali katika Mkoa, Programu ya Uratibu na Uendeshaji wa Tawala za Mikoa na Programu ya Usimamizi na Uendeshaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa.

MKOA WA MJINI MAGHARIBI – D07

Mhe. Mwenyekiti, Mkoa wa Mjini Magharibi katika Mwaka wa Fedha wa 2018/2019 umepanga kuimarisha ulinzi na usalama katika Mkoa, kusimamia mpango wa matumizi bora ya ardhi, usafi, na upendezeshaji wa mji, kuimarisha huduma kwa wananchi na kusimamia na kuwezesha utekelezaji wa dhana ya upelekaji madaraka kwa wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, ili Mkoa wa Mjini Magharibi uweze kutekeleza programu zake kwa ufanisi, kwa mwaka wa Fedha 2018/2019, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 33,396,000,000.00 kati ya fedha hizo shilingi 1,136,800,000.00 kwa ajili ya matumizi mengineyo, shilingi 1,417,500,000 ni mishahara, shilingi 30,071,700,000.00 ni ruzuku kwa Mabaraza ya Manispaa Mjini, Magharibi ‘A’ na ‘B’ na shilingi 770,000,000.00 kwa kazi za maendeleo. Aidha, naliomba Baraza lako Tukufu liridhie makusanyo ya shilingi 80,585,000.00 na kuchangia Mfuko Mkuu wa Serikali. Mhe. Mwenyekiti, naomba Waheshimiwa Wajumbe waangalie kiambatanisho 12B

MKOA WA KUSINI UNGUJA – D8

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2018/2019, Mkoa wa Kusini Unguja umepanga kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa shughuli za serikali katika mkoa, kuratibu shughuli za usalama katika mkoa, kusimamia shughuli za Serikali za Mitaa, kutoa huduma za utumishi na utawala na kuimarisha huduma za Ofisi.

Mhe. Mwenyekiti, ili Mkoa wa Kusini Unguja kwa mwaka wa Fedha 2018/2019, uweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya shilingi 12,878,300,000.00 kati ya fedha hizo shilingi 550,600,000.00 kwa matumizi mengineyo, shilingi 1,082,700,000.00 kwa ajili ya mishahara na shilingi 11,245,000,000.00 kwa ajili ya ruzuku kwa Halmashauri ya Wilaya ya Kusini na Halmashauri ya Wilaya ya Kati. Aidha, naliomba Baraza lako Tukufu liridhie makusanyo ya shilingi 35,000,000.00 kuchangia Mfuko Mkuu wa Serikali.

MKOA WA KASKAZINI UNGUJA – D9

Mhe. Mwenyekiti, Mkoa wa Kaskazini Unguja kwa mwaka wa fedha 2018/2019, umepanga kusimamia shughuli za Serikali katika Mkoa, kusimamia ulinzi na usalama katika Mkoa, kusimamia na kuwezesha utekelezaji wa dhana ya upelekaji madaraka kwa wananchi na kuhamasisha jamii kupinga udhalilishaji.

Mhe. Mwenyekiti, ili Mkoa wa Kaskazini Unguja kwa mwaka wa fedha 2018/2019, uweze kutekeleza programu zake kwa ufanisi, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 14,358,800,000.00, Kati ya fedha hizo, shilingi 560,100,000.00 ni matumizi mengineyo, shilingi 1,188,000,000.00 ni mishahara, na shilingi 12,610,700,000.00 ni kwa ajili ya Ruzuku za Halmashauri za Wilaya ya Kaskazini ‘A’ na ‘B’. Aidha, naliomba Baraza lako Tukufu liridhie makusanyo ya shilingi 20,848,000.00 na kuchangia Mfuko Mkuu wa Serikali.

MKOA WA KUSINI PEMBA (D10)

Mhe. Mwenyekiti, Mkoa wa Kusini Pemba kwa mwaka wa fedha 2018/2019, umepanga kusimamia upatikanaji wa huduma za jamii katika Mkoa, kusimamia Ulinzi na Usalama katika Mkoa, kuanzishwa na kusimamia kazi za Sekretarieti ya Mkoa, kusimamia na kushauri Mamlaka za Serikali za Mitaa katika utekelezaji wa shughuli za sekta zilizogatuliwa na kusimamia na kutekeleza mikakati ya kupiga vita udhalilishaji wa kijinsia na mapambano dhidi ya dawa za kulevya.

Mhe. Mwenyekiti, ili Mkoa wa Kusini Pemba kwa mwaka wa fedha 2018/2019, uweze kutekeleza programu zake kwa ufanisi, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 12,038,500,000.00 kati ya fedha hizo, shilingi 925,400,000.00 ni mishahara, shilingi 515,500,000.00 matumizi mengineyo na shilingi 10,597,600,000.00 ni Ruzuku kwa Mabaraza ya Mji ya Chake-Chake na Mkoani. Aidha, naliomba Baraza lako Tukufu liridhie makusanyo ya shilingi 12,663,000.00 na kuchangia Mfuko Mkuu wa Serikali.

MKOA WA KASKAZINI PEMBA (D11)

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2018/2019, Mkoa wa Kaskazini Pemba umepanga kusimamia Shughuli za Serikali katika Mkoa, kufanya Vikao vya Kamati ya Ulinzi na Usalama, kuratibu ziara za viongozi na Sherehe za kitaifa na kuimarisha mazingira bora ya kufanyia kazi na ustawi wa watumishi.

Mhe. Mwenyekiti, ili Mkoa wa Kaskazini Pemba kwa mwaka wa fedha 2018/2019, uweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe shilingi 11,379,500,000.00 kati ya fedha hizo, shilingi 1,081,000,000.00 ni mshahara, shilingi 684,300,000 matumizi mengineyo na shilingi 9,614,200,000.00 ni Ruzuku kwa Baraza la Mji Wete na Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni. Aidha, naliomba Baraza lako Tukufu liridhie makusanyo ya shilingi 15,793,000.00 ili kuchangia Mfuko Mkuu wa Serikali.

WAKALA WA USAJILI WA MATUKIO YA KIJAMII(D12)

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2018/2019, Ofisi ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii itatekeleza Programu kuu mbili ambazo ni Programu ya Usajili wa Matukio ya Kijamii na Programu ya Utumishi na Uendeshaji. Kupitia programu hizo, Ofisi ina kusudia kuimarisha mfumo wa Usajili wa matukio ya kijamii, kuimarisha mazingira ya Ofisi na Utawala na kujenga uwezo wa wafanyakazi kitaaluma.

Mhe. Mwenyekiti, ili Ofisi ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, kwa mwaka wa fedha 2018/2019, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 3,315,200,000.00 kati ya hizo shilingi 1,646,200,000.00 kwa matumizi ya kazi za kawaida, shilingi 1,169,000,000.00 mishahara na shilingi 500,000,000.00 kwa kazi za maendeleo. Aidha, naliomba Baraza lako Tukufu liridhie makusanyo ya shilingi 350,000,000.00 kuchangia Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, kwa makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2018/2019, naomba Waheshimiwa Wajumbe waangalie kiambatanisho namba 12 na 13.

SHUKURANI

Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kuweza kuiwasilisha hotuba hii mbele ya Baraza lako Tukufu. Aidha, naomba kutoa shukurani za kipekee kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein, ambaye ndiye Kamanda Mkuu wa Idara Maalum za SMZ, kwa kuendelea kuniamini na kumsaidia katika kazi za kusimamia ofisi yake inayohusikana na Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idaa Maalum. *(Makofi)*

Vile vile, niwashukuru kwa dhati wasaidizi wangu wakiwemo Naibu Waziri Mhe. Shamata Shaame Khamis Mwakilishi wa Wananchi Jimbo la Micheweni, Katibu Mkuu ndugu Radhiya Rashid Haroub, Naibu Katibu Mkuu anaeshughulikia masuala ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ndugu Kai Bashir Mbaruk na Naibu Katibu Mkuu anaeshughulikia masuala ya Idara

Maalum za SMZ ndugu Sida Himid Mohamed kwa ushirikiano wa hali ya juu wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu na kufikia malengo tuliyojipangia. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nichukue fursa hii kuwashukuru Makamanda wa Idara Maalum za SMZ wakiongozwa na *Commodore* Hassan Mussa Mzee, Wakuu wa Mikoa, Wilaya, Wenyeviti wa Bodi ya Ushauri ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii na Wakala wa Ulinzi wa JKU, Mwenyekiti wa Utumishi Idara Maalum za SMZ, Makatibu Tawala wa Mikoa na Wilaya, Wakurugenzi, Madiwani, Masheha na watendaji wote wa Ofisi ya Rais,Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa utendaji wao, uzalendo na mashirikiano katika kutekeleza majukumu ya ofisi. *(Makofi)*

Aidha, natoa shukrani kwa Taasisi wenza za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiwemo Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Wizara ya Mambo ya Ndani, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na vyombo vya Ulinzi na Usalama vya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee naishukuru familia yangu kwa uvumilivu wao kwa muda wote niliokuwa mbali nao wakati nikitekeleza majukumu ya kitaifa. Aidha, navishukuru vyombo vya habari ambavyo vimetoa mchango mkubwa katika kuhamasisha, kutangaza na kuelimisha jamii juu ya matukio na taarifa mbali mbali zinazohusu Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nawashuru Washirika wetu wa Maendeleo na nchi marafiki kwa misaada na michango yao ambayo imechangia mafanikio ya Ofisi yangu. Miongoni mwao ni Shirika la Kuhudumia Watoto (*UNICEF*), Shirika la Mpango wa Maendeleo la Umoja wa Mataifa (*UNDP*), Shirika la Msaada la Marekani (*USAID*), Shirika la Msalaba Mwekundu, Benki ya Dunia (*WB*), Jamhuri ya Watu wa China, Jamhuri ya Kiarabu ya Misri na wengine wote waliofanikisha kuchangia maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

HITIMISHO

Mhe. Mwenyekiti, naomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu wachangie hotuba hii na hatimae waiidhinishie Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, makadirio ya shilingi 210,225,600,000.00 zikiwemo shilingi 25,035,500,000.00 kwa matumizi mengineyo, shilingi 75,405,900,000.00 mishahara na maposho, shilingi 35,030,000,000.00 matumizi ya kazi za maendeleo na shilingi 74,754,200,000.00 ni ruzuku kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wakala wa Ulinzi wa JKU na Tume ya Utumishi ya Idara Maalum za SMZ. Aidha, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe waridhie mchango wa shilingi 834,030,000.00 ikiwa ni mapato yatakayoingizwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali.
Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

TABLES

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, kwa uwasilishaji wako na kujali muda na kwa vile imeungwa mkono. Sasa naomba nimwite Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum, ili na yeye aweze kuleta maoni yake,

Mhe. Machano Othman Said (Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum): Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kutoa hotuba ya maoni ya Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote naomba kutumia nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, Mwenye wingi wa Rehma, Muumba wa mbingu na ardhi na vyote vilivyomo, kwa kutujaalia kukutana kwa mara nyengine tena, asubuhi hii ya leo, katika Mkutano huu wa Kumi wa Baraza la Tisa kwa dhamira ya kujadili Bajeti kuu ya Serikali na Taasisi zake, chini ya Baraza lako Tukufu. Kwani hii ni rehma yake Muumba kwa kutupa pumzi na afya njema ambayo wenzetu wengine amewanyima fursa hii.

Mhe. Mwenyekiti, pia napenda kutumia fursa hii adhim kushukuru na kukupongeza wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kusimama mbele ya Baraza lako Tukufu, kwa lengo la kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum ya SMZ kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Wizara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa mwaka wa fedha 2018/2019 kama sheria na Kanuni za Baraza hili zinavyoelekeza.

Aidha, nawapongeza na kuwashukuru kwa dhati viongozi wa Wizara hii wakiongozwa na Waziri wao makini Mhe. Haji Omar Kheir, Naibu Waziri, Mhe. Shamata Shaame Khamis, Nd. Katibu Mkuu, Wakuu wa Mikoa pamoja Afisa Mdhamini Pemba, na watendaji wote kwa mashirikiano yao makubwa waliyotuonesha katika Kamati yetu kwa kutekeleza majukumu yetu ipasavyo. Vile vile, shukurani za pekee ziende kwa Wakuu, Maafisa na Wapiganaji wote wa Idara Maalum za SMZ kwa mashirikiano yao waliyotupatia kwa kipindi chote cha utekelezaji wa shughuli za Kamati. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, **s**ambamba na hayo, natumia nafasi hii kuishukuru Wizara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa kutumia na kutekeleza vyema ushauri na maagizo ya kamati pamoja kuisimamia kikamilifu bajeti yao ya mwaka 2017/2018. Jambo hili limewawezesha kujenga ari ya kuwasilisha mbele ya kamati yetu, pamoja na Baraza lako Tukufu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha, kwa mwaka wa Fedha 2018/2019 ili ipate baraka za Wajumbe wako na kwa mnasaba huo, tunaomba Baraza lako tukufu liiridhie na liipitishwe Bajeti hii kwa maslahi ya wananchi wa Zanzibar pamoja na serikali.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa shukrani na pongezi za dhati na pekee kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya uongozi imara wa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein, kwa kusimama vyema katika uongozi wake na kuhakikisha maendeleo ya watu na ustawi wa jamii nchini yameimarika pamoja na kusimamia maendeleo ya uchumi kufuatana na misingi na madhumuni yaliyowekwa na Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, kwa kuhakikisha upatikanaji wa huduma muhimu kwa jamii. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, Ni matumaini ya Kamati yangu kuwa mafanikio yanayopatikana katika utekelezaji uimarikaji wa uchumi wetu na huduma za kijamii yanatokana na Utekelezaji mzuri wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2015/2020, ambapo utekelezaji wake utaendelea kwa kipindi chote cha bajeti ya mwaka 2018/2019 na kuhakikisha kuwa hatua kubwa ya maendeleo inafikiwa chini ya misingi bora iliyoainishwa ndani ya Ilani hii ili kuakisi na kuiwezesha jamii kiuchumi na kujikwamua na hali ngumu ya umasikini.

Mhe. Mwenyekiti, bajeti hii imekadiriwa kufanya kazi kwa kuzingatia malengo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na inaakisi hali halisi ya uchumi wetu na harakati za kupunguza umasikini ifikapo mwaka 2020, lakini pia kwa kuzingatia malengo ya Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Zanzibar (MKUZA III).

Mhe. Mwenyekiti, pia nachukua nafasi hii kuwashukuru kwa kazi kubwa walioifanya Wajumbe wa Kamati yangu wakati tukiwa tunapitia bajeti hii, kwa kuonesha mashirikiano yao makubwa katika kutekeleza majukumu ya Kamati hii.

Hivyo, kwa ridhaa yako naomba sasa uwatambue Wajumbe wa Kamati hii kama ifuatavyo:-

1.	Mhe. Machano Othman Said	Mwenyekiti
2.	Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis	Makamu Mwenyekiti
3.	Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa	Mjumbe
4.	Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Mjumbe
5.	Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf	Mjumbe
6.	Mhe. Ali Khamis Bakar	Mjumbe
7.	Mhe. Suleiman Makame Ali	Mjumbe
8.	Ndg. Ali Alawy Ali	Katibu, na
9.	Ndg. Haji Jecha Salim	Katibu.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum imetumia uweledi wake wa hali ya juu katika kupitia, kuchambua na kujiridhisha katika programu zote zilizokusudiwa kufanyiwa kazi kupitia Fungu la Bajeti la wizara hii kama ilivyoelezwa katika Kanuni ya 96(1) na 106(3) katika jadweli la kwanza la Kanuni za Baraza la Wawakilishi, 2016.

Mhe. Mwenyekiti, ni imani ya kamati hii kwamba kupatikana kwa fedha zilizopangwa katika wizara hii kutasaidia kwa kiasi kikubwa utekelezaji na ukamilishaji wa malengo yaliyokusudiwa kutekelezwa ikiwa ni pamoja na kukamilisha miradi iliyotengwa kwa mwaka huu wa 2018/2019, na vile vile kuendeleza mradi mkubwa wa Mahanga na nyumba za Askari wa Idara Maalum kisiwani Pemba.

IDARA ZA MAKAO MAKUU (FUNGU D 01)

Mhe. Mwenyekiti, katika kutekeleza kazi zake kwa mwaka wa fedha 2017/2018, kamati yangu imefanikiwa kutembelea na kujionea shughuli mbali mbali za kawaida na zile za miradi ya maendeleo ambazo zinasimamiwa na kuratibiwa na wizara hii katika utekelezaji wake, ikiwa zinakabiliwa na changamoto kadhaa, kama vile uchache wa vitendea kazi na visivyokidhi wakati tulionao, uhaba wa vyombo vya usafiri pamoja na upungufu mkubwa wa watendaji katika sekta zilizogatuliwa, ubovu wa barabara za ndani pamoja na uchakavu wa baadhi ya Mahanga na nyumba za Askari wetu wa Idara Maalum. Hata hivyo, kamati inaipongeza sana serikali kwa kuanza ujenzi wa Mahanga ya Wapiganaji wa Vikosi vyetu kupitia mradi maalum.

Mhe. Mwenyekiti, kamati inashauri kwa mwaka wa fedha 2018/2019 idara hizi kupatiwa fedha za kutosha na kwa wakati, ili kuweza kutatua changamoto ambazo zinawakwaza katika uendeshaji wa shughuli zao, kwa lengo la kuleta ufanisi na kuimarisha sekta zote za maendeleo katika taasisi hizo.

Mhe. Mwenyekiti, kamati inapongeza sana kazi nzuri zinazofanywa na afisi kuu kwa kupitia na kuandaa miradi mbali mbali ya maendeleo ambayo msingi wake ni kuongeza kasi ya maendeleo ya kiuchumi katika nchi yetu. Hata hivyo, kamati imebaini, katika bajeti hii wizara imekusudia kujenga barabara za ndani kupitia Halmashauri zake mbali mbali za Unguja na Pemba lakini fedha zilizokusudiwa kujengewa barabara hizo hazionekani katika bajeti hii, jambo ambalo linatia shaka utekelezaji wake. Kamati, inashauri serikali kupitia Mfuko wa Barabara kuwapataia fedha walau asilimia 30% ya makusanyo yao ili wizara iweze kujenga barabara ra ndani.

Mhe. Mwenyekiti, kamati inashauri, wizara inapoweka mipango ya ujenzi wa barabara au mradi wowote uliokusudiwa kutekelezwa na Halmashauri au Manispaa fedha zake zioneshwe mapema katika bajeti ya Wizara katika mwaka husika ili wajumbe wa Baraza hili tukufu watambue mapema kiasi cha fedha zilizotengwa kwa kuendeleza ujenzi huo kama zinakidhi mahitaji au hazikidhi kwa mujibu wa umuhimu wa barabara hizo.

Aidha, kamati inashauri barabara ambazo zilikusudiwa kujengwa na Halmashauri katika bajeti ya mwaka 2017/2018 na kushindwa kujengwa kwa ukosefu wa fedha, barabara hizo zijengwe katika bajeti hii inayokuja kwa mwaka 2018/2019.

IDARA YA URATIBU WA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (Fungu D 07 – D 11)

Mhe. Mwenyekiti, Katika programu ya Uratibu wa Tawala za Mikoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa, kwa ujumla Kamati yangu ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum imeridhishwa na utekelezaji wa programu mbali mbali zinazosimamiwa na Tawala za Mikoa pamoja Mamlaka ya Serikali za Mitaa zaidi katika ukusanyaji wa mapato kutokana na baadhi ya Halmashauri, Mabaraza na Manispaa kuvuka malengo waliyokusudia. Hii inaonesha wazi kuwa endapo vyanzo vya mapato vitasimamiwa ipasavyo, basi hali ya uchumi katika nchi yetu itaimarika na hivyo kuweza kutekeleza vyema Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2015/2020.

Mhe. Mwenyekiti, kamati imebaini kuwepo kwa changamoto katika utekelezaji wa Sheria ya Tawala za Mikoa, Namba 8 ya mwaka 2014, kifungu cha 30(1) ambacho kinazitaka Kamati za Maendeleo za Mikoa kukutana mara mbili kwa mwaka. Hata hivyo, vikao hivyo havifanyiki na kupelekea mikoa kushindwa kufanya tathmini nzuri juu ya utekelezaji wa shughuli zake hivyo kupelekea kukosekana kwa maendeleo ya nchi.

Mhe. Mwenyekiti, kukosekana kufanyika kwa vikao hivi katika Kamati za Maendeleo ya Mkoa kunapelekea malalamiko mbali mbali kwa baadhi ya wajumbe wa kamati hizi wakiwemo Wabunge na Waheshimiwa Wawakilishi ambao huingiziwa fedha zao katika miradi iliyopangwa lakini pia hukosa marejesho ya matumizi ya fedha hizo kwa vile vikao hivi vimekosekana.

Mhe. Mwenyekiti, kamati inashauri katika bajeti hii tunayoijadili, serikali kupitia Wizara hii ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kuhakikisha kuwa vikao hivi vinafanyika na kwa wakati mahususi, ili kuendana sambamba na sheria hii pamoja kusaidia kuibua miradi mengine ya kimaendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, kamati inaipongeza sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kusimamia kikamilifu mradi wa Ugatuzi ambao kwa mwaka huu unaoishia Juni 30, 2018 mafanikio kadhaa yamepatikana ikiwa ni pamoja na uelewa wa wananchi juu ya dhana kamili ya Ugatuzi na faida zake kwa jamii. Kwa kuwa, hili ni jambo jema kwa nchi yetu na kwa kuwa lengo la serikali ni kuwashirikisha wananchi katika serikali yao kama ambavyo Katiba yetu inatuelekeza, hivyo ni vyema Ugatuzi ukaendelezwa na kusimamiwa. Aidha, kamati inaiomba serikali ifikirie kugatua pia sekta ya maji ili kupunguza changamoto ya upatikanaji wa maji safi na salama ambazo zinajitokeza katika Halmashauri mbali mbali hapa nchini.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa dhana ya Ugatuzi ni njema na inaleta ufanisi kwa watendaji, Kamati inapongeza sana juhudi za serikali katika kusimamia vyema Ugatuzi huo Taasisi zilizogatuliwa na kupelekwa Halmashauri. Aidha, kamati imeridhishwa na wizara ambazo zimegatua watumishi wao kikamilifu na kuwapeleka Mamlaka ya Serikali za Mitaa ikiwemo Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali hata hivyo, pamoja na Wizara ya Afya.

Hata hivyo, Kamati haikuridhika na mpango wa Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwa kucheleweshe kupeleka stahiki za watumishi wake walioko Halmashauri na hivyo kushindwa moja kwa moja kuonekana kwenye bajeti katika fedha za matumizi kutoka wizarani kwenda katika Halmashauri zao, hadi tunajadili na kupitisha bajeti hii kwenye Kamati, Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi imehamisha mishahara tu bado stahiki nyengine kama vile fedha za likizo, mchango wa *ZSSF* na matumizi mengine yaani (*OC*). Hivyo, kamati inaiomba Wizara ya Fedha na Mipango kuingilia kati ili fedha hizo zipelekwe Wizara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ katika mwaka wa fedha 2018/2019.

Aidha, kamati inashauri wizara kwa kushirikiana na Mamlaka ya Serikali za Mitaa kutoa uelewa juu ya matumizi ya fedha za miradi ya maendeleo kwa Waheshimiwa Madiwani juu ya namna ya kutumia fedha za miradi kama sheria zinavyoelekeza.

Mhe. Mwenyekiti, kamati imebaini katika mwaka huu wa fedha kuwepo kwa changamoto kubwa ya kukosekana kwa hatimiliki katika baadhi ya maeneo ya uzalishaji pamoja na majengo ya ofisi, jambo linalopelekea maeneo hayo kutotambulika kisheria kwa maeneo hayo na hivyo kupelekea baadhi ya mapato kupotea. Hata hivyo, kamati imeelezwa kuwepo kwa agizo la serikali la kupatiwa hati kwa maeneo yote yanayomilikiwa na Halmashauri za Unguja na Pemba pamoja na kupatiwa Hati za Madiko yaliyomo katika Halmashauri hizo na kuleta taswira njema kwa Serikali yetu ambayo kila siku ipo katika harakati za kuhakikisha suala la ukusanyaji mapato limeimarika.

Mhe. Mwenyekiti, kamati inashauri Baraza la Mji Wete pamoja na Halmashauri ya Micheweni kuhakikisha zinaongeza nguvu ya ukusanyaji wa mapato ikiwa ni pamoja na kutoa elimu kwa wananchi juu ya umuhimu wa ulipaji kodi na kuwachukulia hatua wale wote wanaokwenda kinyume na agizo la ulipaji kodi na hivyo, kupelekea mapato ya taasisi hizo kushuka ingawa katika kipindi hiki inaonekana Baraza la Mji Wete likipiga hatua ya ukusanyaji ila juhudi hizo zinahitaji kulindwa na kuimarishwa.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu inaliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha kiasi cha fedha zilizotengwa kwa ajili ya uendeshaji wa programu zote zilizopangwa katika Tawala za Mikoa pamoja na Mamlaka ya Serikali za Mitaa, ili kusaidia kufikia malengo yaliyokusudiwa.

PROGRAMU ZA IDARA MAALUM ZA SMZ (FUNGU D 02 – D 06)

Mhe. Mwenyekiti, kamati inapongeza sana juhudi zinazofanywa na wapiganaji wetu wa vikosi kwa kazi nzito wanazozifanya za kulinda, kusimamia na kudumisha usalama wa raia na mali zao pamoja na kuhakikisha kuwepo kwa amani na utulivu katika nchi yetu. Sambamba na hayo, Kamati imeridhika kwa kiasi kikubwa hatua iliyofikiwa ya ujenzi wa Mahanga ya Askari kisiwani Pemba. Juhudi hizo za serikali zinaonekana kutia moyo kwa kuona kwamba serikali inawajali na kuwathamini vijana wetu pia serikali kutekeleza kwa vitendo ahadi zake zilizotolewa katika Ripoti ya Kamati na Bajeti ya mwaka 2017/2018. Kamati pia, inaiomba Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ifikirie kuijenga kwa kiwango cha lami barabara ya kutoka Kama Meli Kumi hadi Makao Makuu ya Kambi ya KMKM Kama ambayo inatarajiwa kujengwa Chuo cha Mafunzo ya Kijeshi kwa Vikosi vyetu vya SMZ.

Mhe. Mwenyekiti, kamati imebaini kuwepo changamoto ya kuwekewa kiwango kikubwa cha Makadirio ya Mapato kwa vikosi vya Idara Maalum ambapo kila kikosi kimetakiwa kukusanya mapato kama inavyoonekana katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Hivyo, kamati inaitaka Wizara ya Fedha na Mipango wakati wanapofikiria upangaji na makadirio ya ukusanyaji wa Mapato kwa Idara Maalum wafikirie na vyanzo vyao vya mapato na vile vile wazingatie kazi za msingi zinazotekelezwa katika idara hizi, kwa mfano Kikosi cha Valantia Zanzibar kimekasimiwa kukusanya jumla ya shilingi 60,259,000.00 ambazo zitaenda katika Mfuko Mkuu wa Serikali, hali ambayo ni vigumu kukusanya fedha hizo kutokana na ukoksefu wa vyanzo vya mapato lakini pia uchache wa wataalamu na rasilimali ziliomo katika kikosi hiki zinachangia kutofikiwa kwa malengo.

Aidha, kamati inaishauri Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Fedha na Mipango kupunguza au kuondosha kabisa Makadirio ya Mapato ya shilingi 70,991,000.00/- kwa

mwaka wa fedha 2018/2019 kwa Idara ya Chuo cha Mafunzo ambao wakati wote nguvu zao zipo katika ujenzi wa Mahanga ya Askari na Nyumba za Maafisa na vile vile wanaendelea na ujenzi wa gereza la watoto – Hanyegwa Mchana. Hivyo, hakuna chanzo chengine chochote cha mapato ambacho kitatumika kukusanyia fedha hizo. Pia, Kikosi cha Valantia kimepangiwa kuchangia shilingi 60,259,000/- toka Fungu la Ada ya Ulinzi. Hata hivyo, kwa mujibu wa maelezo yao kazi hiyo sasa itafanywa na Wakala wa Ulinzi wa JKU.

Mhe. Mwenyekiti, kamati pia haikuridhika na kiwango cha mapato ambacho Kikosi cha Zimamoto na Uokozi wamepangiwa kukusanya ambacho ni jumla ya shilingi 74,184,000.00 kiwango hicho ni ikubwa na Kikosi hiki hakina uwezo wala vyanzo vya kupata mapato hayo. Kati ya fedha waliopangiwa Kikosi cha Zimamoto, shilingi 25,000,000/- ni ada ya ulinzi na shilingi milioni 3 ni ada ya ujenzi, shughuli ambazo hazipo kwa mwaka huu wa fedha kwenye kikosi hicho.

Mhe. Mwenyekiti, kamati kwa mara nyengine tena imesikitishwa na baadhi ya Taasisi za Serikali kukataa kutekeleza maagizo ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein la kuwaimarishia Kikosi cha Zimamoto huduma zao katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume, ikiwemo ujenzi wa Banda la kuhifadhia gari zaoza Zimamoto eneo la Uwanja wa Ndege wa zamani pamoja na kuwapatia maji katika hodhi lao liliopo katika kituo cha kipya uwanja huo wa ndege na kuifanyia matengenezo barabara ambayo inatumiwa na magari ya Zimamoto kiwanjani hapo.

Aidha, kamati inaishauri Wizara ya Tawala za Mikoa kukaa na Wizara nyengine kuangalia jinsi ambavyo Zimamoto watapata mgao wao kutokana na huduma wanazotoa katika Taasisi mbali mbali hasa uwanja wa Ndege wa Kimataifa, kama ilivyo kwa upande wa Tanzania Bara na nchi nyengine duniani.

Mhe. Mwenyekiti, kamati inapongeza juhudi za kuanzishwa kwa Ofisi ya Wakala wa Ulinzi wa JKU ambapo majukumu ya ofisi hii yameainishwa kwa mujibu wa Sheria Namba 2 ya mwaka 2015 na itafanya kazi za ulinzi katika sekta mbali mbali ikiwemo mashirika ya umma na watu binafsi, ni imani ya kamati yangu kuwa ofisi hii itaimarisha ulinzi na usalama wa mali za raia na wageni wanaowekeza katika nchi yetu. Hata hivyo, katika kufikia malengo yake, kamati inashauri serikali iangalie uwezekano wa kupatiwa fungu lao la fedha ambalo litawawezesha kujitegemea wenyewe kwa mujibu wa majukuu yao.

Aidha, kamati inashauri Wajumbe wa Baraza hili tukufu kuridhia na kuidhinisha fedha za ruzuku zilizopangwa kwa ajili ya ofisi hii ili ipate kwenda sambamba na malengo yaliyokusudiwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa nyakati tofauti kamati imeweza ikizungumzia suala la hatimiliki kwa maeneo yanayokaliwa au kutumiwa na Vikosi vya Idara Maalum za SMZ kwa shughuli mbali mbali ikiwemo ulinzi na usalama wa raia na mali zao. Kwa kuwa, suala hili limekuwa na ukakasi katika utekelezaji wake kwa bajeti iliyopita lakini pia bajeti hii tuliyonayo. Kamati, inashauri serikali kupitia Idara ya Ardhi kufuta baadhi ya viwanja ambavyo vimetolewa na serikali kwa makazi ya watu na vipo karibu na maeneo ya Kambi hususan katika Kambi ya Ndugukitu kisiwani Pemba ambapo kwa kiasi kikubwa hupelekea wakaazi wa maeneo hayo kukwaza shughuli mbali mbali za askari wetu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa kilimo ni uti wa mgongo na kwa kuwa kilimo ndio msingi mkuu wa maendeleo katika nchi yoyote. Kamati inashauri Wizara ya Fedha na Mipango na Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi itakapopata miradi ya kilimo pia iwashirikishe na kuviwezesha kitaalamu na kifedha Vikosi vya JKU na Mafunzo kuendesha miradi yao ya kilimo kwa mashamba yote yaliyochini ya vikosi hivyo yanatumika kwa ajili ya uzalishaji wa chakula na mboga mboga.

WAKALA WA USAJILI WA MATUKIO YA KIJAMII (FUNGU D 12)

Mhe. Mwenyekiti, Wakala wa Usajili na Matukio ya Kijamii inalo jukumu kubwa la kuimarisha mfumo wa Usajili wa Matukio ya Kijaamii katika nchi yetu na ni Taasisi pekee ambayo inategemea kwa ajili ya kutunza takwimu sahihi za jamii yetu. Katika ziara zilizopita, kamati imebaini kuwepo kwa changamoto kubwa ya ucheleweshwaji wa kutolewa vyeti vya kuzaliwa katika wilaya zote za Unguja na Pemba.

Kamati, inashauri serikali kwa bajeti ya mwaka wa fedha 2018/2019 serikali kupitia Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii kuhakikisha kwamba inaweka miundombinu rafiki na mazingira rahisi katika kutoa vyeti vya kuzaliwa katika ofisi za wilaya zote Unguja na Pemba kwa kuzingatia utaratibu unaofaa.

HITIMISHO

Mhe. Mwenyekiti, katika bajeti hii ambayo inatumia mfumo wa *PBB* yaani *(Program Based Budget)* ina utaratibu wake mzuri ambao tumeshauzoea Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu wale wazoefu wa siku nyingi humu Barazani lakini pia na wale wapya wameshauzoea mfumo huu. Kwa maana hiyo, lipo tatizo la kubadilisha vipengele vilivyomo ndani ya mfumo huu kwa kuzingatia programu kuu na programu ndogo jambo ambalo limewakwaza sana Waheshimiwa Wajumbe wakati wa upitiaji wa bajeti hii katika kamati. Kamati, inashauri wakati Wizara ya Fedha na Mipango wanapofanya mabadiliko ndani ya mfumo huu tuliouzoea katika kupitia bajeti, basi watoe mafunzo au elimu kwa Wajumbe ili kuzuia hoja zitakazojengwa dhidi ya mabadiliko hayo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia, nachukua fursa hii kuiomba jamii katika kipindi hiki cha mvua za masika zinazoendelea kunyesha kuzidi kuweka usafi katika mazingira yetu kwa kuitunza michirizi ya maji ya mvua na kuepuka kutupa takataka kiholela katika kila sehemu ndani ya miji yetu, kufanya hivyo kutasaidia kujikinga na maradhi ya mripuko na malaria ambayo ni hatari kwa nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nichukuwe fursa hii kuwashukuru Makamanda wa Idara Maalum za SMZ, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Makatibu Tawala wa Mikoa na Wilaya, Wakurugenzi, Madiwani, Masheha na watendaji wote wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa utendaji wao uliotukuka. Vile vile, naomba kumshukuru Katibu wa Baraza ala Wawakilishi na watendaji wake wote kwa kuisaidia kamati kuweza kutekeleza kazi zake kwa ufasaha na uweledi kabisa. *(Makofi)*

Aidha, kwa kumalizia kamati inawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu waichangie bajeti hii na hatimae waidhinishe Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, makadirio ya fedha zilizopangwa kutumiwa kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho kabisa naomba niwatakie kheri Wazanzibari wote hasa waislamu pamoja na wananchi wa Jimbo la Mfenesini wawe na funga nzuri katika Mwezi Mtukufu wa Ramadhani na Mwenyezi Mungu atujalie funga yetu ya Mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa uwasilishaji wako na kuanza kuunga mkono hotuba. Sasa tunaanza na mijadala kwa kuchangia Hotuba ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum ya SMZ, mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa Mhe. Ali Suleimain Ali akifuatiwa na Mhe. Jaku Hashim Ayoub na Mhe. Abdalla Maulid Diwani ajitayarishe ahsante.

Mhe. Ali Suleimain Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote nishukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa mbele ya Baraza lako tukufu na kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum ya SMZ kwa bajeti ya mwaka 2018/2019.

Mhe. Mwenyekiti, kwa dhati kabisa nampongeza Mhe. Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Manaibu Katibu Wakuu, Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa, Wilaya na Makatibu Tawala wote, Makamanda wetu wa vikosi pamoja na wapiganaji wote wa vikosi vyetu vya SMZ. Lakini na wafanyakazi wote wa wizara hii kwa kazi kubwa wanayoifanya kuhakikisha kwamba kwanza tuko salama katika maeneo yetu, lakini pili tunaishi salama katika mazingira yetu.

Mhe. Mwenyekiti, hotuba hii kama alivyosema Mhe. Waziri ni ndefu lakini ina mambo mengi na kuokoa muda mimi nitasema machache kama nilivyojipangia.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza navipongeza Vikosi vyetu vya SMZ kwa kazi zao nzuri wanazofanya, na kuhakikisha kwamba vinakaa imara katika shughuli zao na kulala sisi usingizi bila ya kuwa na matatizo bila ya wao Mhe. Mwenyekiti hatuna usalama mwema katika maeneo yetu. Lakini pamoja na hayo niseme tu nimuombe sana Mhe. Waziri hivi sasa hivi kuna vitendo vingi vya matatizo katika maeneo mbali mbali kunatokea unyang'aji, watu wanaporwa, kuna vikundi viovu vyingi katika baadhi ya maeneo. Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri tuongeze doria katika maeneo mbali mbali katika nchi yetu, mimi nitasemea zaidi katika Jimbo langu la Kijitoupele. Nitazungumzia zaidi maeneo ya Kwarara, Tomondo na kwengineko tuongeze bidii kuhakikisha kwamba wananchi wetu wanakuwa salama na amani katika maeneo yao.

Vile vile, nikipongeze Kikosi cha KMKM kwa kazi zao nzuri wanazofanya, lakini katika hili pia niseme tu kwamba shughuli zao hizi zinahitaji nyenzo za vyombo, niipongeze serikali yetu juzi nimeona tu kwamba tumepata boti moja nzuri mpya yenye mwendo wa kasi kwa upande wa KMKM lakini pili na kikosi chetu cha Zimamoto kwa hivyo naipongeza serikali kuona umuhimu wa majanga yanafatiliwa na tunafatilia kwa haraka na tunapata uamuzi wa mara kwa mara.

Lakini niko kwenye vikosi niseme jengine mheshimiwa katika ukurusa wa 99 katika kitabu chetu ukurasa wa 96 kiambatanisho namba 6 kidogo kimenipa mashaka sijakifahamu vizuri. Kwa hiyo, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja atupe ufafanuzi kamili ili tujuwe, magendo yaliyokamatwa kuanzia Julai 2017 hadi Machi 2018 karafuu gunia 14, thamani yake milioni kumi na tano, mafuta ya kupikia madumu 6,774 thamani yake arubaini milioni, mchele paketi 67 thamani yake milioni nne na ishirini alfu, dizeli pipa 81 thamani yake arubaini na saba milioni, mia saba na tisini alfu halafu petroli pipa 20, milioni kumi na moja, laki saba na ishirini alfu jumla yetu tunapata milioni 118,530,000/=.

Mhe. Mwenyekiti, hii hapa kidogo takwimu naona sijui alivyozipata, lakini si sahihi namuomba akija mheshimiwa afatilie uzuri takwimu zake, kwa sababu tunaisikia *ZRB* mara kwa mara wanatangaza tunauza mapipa ya mafuta, tunafanya nini au karafuu zimekamatwa wapi kwa hivyo mimi hizi gunia kumi na nne siamini vizuri labda kuna matatizo hapa na pale kutoka na mawasiliano yao, lakini pamoja na hivyo navipongeza chombo chetu hicho na vyenginevyo kwa kufanya kazi nzuri.

Mhe. Mwenyekiti, nakuja Mkoa wangu wa Mjini Magharibi nampongeza sana Mkuu wa Mkoa wangu Mhe. Ayoub Mohamed Mahmoud pamoja na Wakuu wake wa Wilaya, Katibu wake wa Mkoa na Wilaya lakini pia nakuja kwenye Manispaa zetu nawapongeza kwa kazi nzuri wanazofanya. Lakini niseme tu Mhe. Mwenyekiti bado nina kilio na ninasema leo labda Mhe. Waziri angetupa hasa suala zuri akajibu hili suala ninalotaka kumuuza.

Kwa kweli, kuna tatizo gani katika Mkoa wetu wa Mjini Magharibi kukosa afisi yenye hadhi mpaka leo na kama kuna fedha zinatoka wapi hata zisipatikane maana katika awamu nzuri ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kujenga ofisi za fahari tunampongeza kwa dhati kwamba Zanzibar imebadilika kutokana na ofisi zake. Sasa nalilia Mkoa wa Mjini Magharibi kwa sababu Mkoa wa Mjini Magharibi ni Mkoa mama una Manispaa tatu, pia ukija kwa Wakuu wa Wilaya wetu ofisi hazina hadhi. Ningemuomba sana Mhe. Waziri tumeingia katika awamu hii nzuri na inakwenda vizuri, kwa hiyo Ofisi ya Mkuu wa Mkoa pale Amani ijengwe na Wakuu wa Wilaya wa Magharibi ‘A’ na ‘B’ zijengwe wawe na ofisi zinazotambulika.

Mhe. Mwenyekiti, tunatembea sehemu mbali mbali unaweza kwenda kule utasikia Manispaa ukahangaika roho na ukashtuka, kwa hivyo hadhi yetu tunajishtukia katika maeneo yetu. Lakini hilo niombe Mhe. Waziri na kuomba kwa dhati kabisa lifanyiwe kazi.

Mhe. Mwenyekiti, ukija katika Wilaya ya Magharibi ‘A’ na ‘B’ tuna matatizo ya miundombinu ya barabara za ndani, tuna matatizo ya mitaro ya maji, tuna matatizo ya uzoaji wa taka. Namuomba sana Mhe. Waziri kwa kuwa yeye ndio baba wa Manispaa hizi hebu kidogo tufanye upendeleo wa makusudi, wenzetu walibahatika maana wakati wa Muungano tumepata Manispaa tatu, lakini Manispaa mama ipo na imebahatika kweli kweli na inanawiri na naipongeza, nampongeza Mkurugenzi pamoja na watendaji wake, hivyo angalau basi tufanye suluhu kidogo kuwasaidia gari japo moja moja Manispaa ya Magharibi ‘A’ na ‘B’ wakapunguza maeneo yenye kero za taka. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nakuthibitishia katika Mkoa wa Mjini wa Magharibi taka nyingi zinazalishwa katika Manispaa mbili hizo. Manispaa ya Magharibi 'B' na Manispaa ya Magharibi 'A' Wakuu wa Mikoa, Wakurugenzi, Wakuu wa Wilaya wetu wanahangaika kutafuta alau suluhisho la kuondoa taka mitaani. Mhe Mwenyekiti, nawapongeza hivi sasa taka zinaozolewa lakini bado kuchafu na hatari kwa mazingira yetu tuliyokuwa nayo na mvua hizi. Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri afanye ziara za makusudi ayaone ili tatizo hili liondoke katika maeneo yetu.

Mhe. Mwenyekiti, nasema hali halisi ilivyo na iko wazi kabisa. Katika jimbo langu ninayo majaa kama matatu yananiudhi sana. Lakini naipongeza Manispaa Mkurugenzi anajitahidi na watendaji wake lakini anazidiwa maana ana majimbo saba hayo majaa sijui yanafika 40 au 30 ya maeneo yake. Kwa kweli, eneo langu zuri sasa hivi kidogo hapa Taveta ndio nnapopasemea alhamdulilah kidogo, lakini pakikaa siku tatu au nne pameshajaa, akienda Tomondo Magereza akikaa siku mbili tatu pameshajaa, akienda Kwangulagwa Kwarara huko siku mbili tatu kumeshajaa. Kwa hivyo, nimuombe sana Mhe. Waziri wenzetu wa Manispaa wanajitahidi lakini nyenzo hawana, kwa hivyo magari ndio nyenzo zenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, nakuja hapo hapo namuomba sana Mhe. Waziri kutokana na ugatuzi tulioupata ninacho Kituo changu cha Afya cha Magirisi. Nimpongeze Mkurugenzi wangu wa Manispaa anakitambua lakini kwa hali halisi inavyoendelea pana kazi inataka imalizwe na wananchi katika kitu wanacholilia ni hicho. Kituo hicho kitakuwa salama kwa mama mjamzito na mtoto pamoja na watu wengine, tunaamini kikitengenea kituo hicho kikimalizika cha Magirisi-Taveta basi matatizo mengi yatapungua kule Fuoni. Mhe. Mwenyekiti, kituo cha Fuoni kinabeba watu wengi na adha, watu wanatoka mpaka Tunguu kuja hapo.

Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri kituo hiki kinataka milioni 59, lakini bahati nzuri nampongeza Mkurugenzi kwa juhudi yake anakwenda mbio na mimi nakwenda, maana mtu kweli yake mpe. Lakini na mimi mwenyewe nakwenda mbio kila pembe tuhakikishe kituo hiki kinamalizika katika sherehe za Mapinduzi kifunguliwe. Namuomba Mhe. Waziri kwamba hili tunapanga mimi, yeye pamoja na watendaji wake tukakitembelee akione baadae wananchi watamshukuru nafikiri watampokea kwa dufu akifika.

Tulikikabidhi Wizara ya Afya, lakini Wizara ya Afya wanakwambia sisi tuko kwenye ugatuzi hakimo. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri atusaidie watu wa Pangawe Mhe. Khamis Juma Mwalim yupo hapa, watu wa Tomondo, watu wa Kwarara, watu wa Kijitoupele, watu wa Melinne huko kote kitawasaidia na takwimu yake Mhe. Waziri kitachukua watu wasiopungua 50,000 watakaotegemea kituo hicho. Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri hicho atusaidie.

Mhe. Mwenyekiti, jengine niseme tu kwamba Wakuu wetu wa Mikoa wanafanya kazi nzuri, Wakuu wa Wilaya wanajitahidi, ombi langu tu kwamba mashirikiano ya hapa na pale tuzidishe ili kuendeleza kazi zetu katika maeneo yetu. Mhe. Mwenyekiti, tunaamini wanapambana na mambo mengi ulinzi na usalama ndio wenyeviti hao, lakini wanakwenda vizuri pamoja na wanaohusika nao tunashukuru kwa maendeleo hayo.

Mhe. Mwenyekiti, jengine tuseme suala la udhalilishaji na itabidi tulizungumze usiku na mchana, na ningewaomba Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na wananchi wenye kupenda nchi yao kila atapopata fursa mtu ya kusimama alani na tulaani kwa nguvu zetu zote vitendo hivi

viovu na havifai. Mhe. Mwenyekiti, juzi nilikwenda Tumbatu na Kamati yangu ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii. Kwanza nimpongeze sana Mhe. Waziri, nampongeza kwa sababu jamii ameiweka pamoja tumekwenda na mvua juzi hatujaamini Mhe. Mwenyekiti pakuweka mguu huna watu wameitikia wito kuanzia wanawake, wanaume na watoto uwanja umefurika.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri nasema ameshajihisha wananchi wake na wanampenda na wanamjali na wanamuamini. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti mimi la kweli nitasema na hakuna mtu mbaya katika maisha anayeliona zuri akasema baya, na lilokuwa baya akasema zuri huyo basi ni mgonjwa wa akili. Kwa hivyo, niseme tu Mhe. Waziri nampongeza na sisi tuigeni jamani Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tufanyeni mikutano kunusuru watoto wetu, watoto wetu ndio kizazi tunachokitegemea leo na kesho. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, tumepokea taarifa nzuri ngumu lakini ndio uongozi, tumepokea michezo mbali mbali ya kuigiza wametuthbitishia kwamba wananchi wanaelewa. Kwa hivyo, hili ni suala zuri na suala ambalo lisemewe na likemewe. Kwa upande wa jimbo langu kama kumetokea matukio nayasema hapa yasikikane japo niliwaambia wengine. Mhe. Mwenyekiti, kuna vitendo viovu vya kuibiwa watoto au kuitwa mtoto fulani, wewe fulani anaitikia naam, njoo nichukulie mzigo huu hapa nipelekee kwenye gari, kumbe ndio kwenye gari haionekani. Kuna mtoto mpaka leo hajaonekana inafika wiki ya pili sasa hivi, mtoto baleghe yuko *Form I* ameitwa na mwenzake twende tukapeleke mizigo kwenye gari, bahati mbaya mpaka leo nasimama hapa hajaonekana mtoto huyu sijui yuko wapi.

Kwa hivyo, bado naiomba serikali tuangalie usalama wa wananchi wetu na watoto wetu, pia wageni wanaokwenda katika maeneo tuhakikishe kwamba mgeni yule anafikia katika vyombo vya sheria, anaanzia kwa Katibu wa Sheha au msaidizi wa Sheha ama Sheha mwenyewe na wala tusikaribishe wageni tu katika nyumba zetu bila ya kuwatambua. Kwa mfano, mmoja kamuiba mtoto amekamatwa bandarini na mimi nimeshuhudia, huyu anatoka Fuoni Jitimai amepigiwa simu na Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma (Makamu wangu Mwenyekiti) nampongeza sana maana ninapopata taarifa tujuane, amenipigia yupo Makunduchi kwenye mkutano wa Mhe. Rais. Mhe. Ali Suleiman Ali nimepata taarifa nzito fuatilia bandarini, basi nikatoka mpaka bandarini.

Lakini lazima niitoe kauli njema. Mhe. Mwenyekiti, nalipongeza Jeshi la Polisi na kwa kazi yao nzuri Kituo cha Malindi kwa ushirikiano mzuri wa *OCD* mwenyewe pamoja na watendaji wake akafuatiliwa mtoto mpaka kwenye boti amekutikana ameshaingia kwenye boti, lakini bahati nzuri yule mtoto nashangaa mtoto mdogo mdogo tu ana umri wa miaka 19 huyo muibaji, alikuja kutafuta kazi, kufika pale akaambiwa kazi hapana akaambiwa pumzika mpaka kesho, alfajiri katoka nae mtoto kakata tiketi kenda bandarini. Kwa hivyo, mawasiliano ni jambo muhimu na lazima tuambizane ukweli tusiwe na aibu anapotokea mgeni lazima umuulize unatoka wapi.

Mhe. Mwenyekiti, jambo la mwisho mimi siku moja nipo Taveta-Magirisi uwanjani…

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, unazo dakika mbili.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Mwenyekiti, nakuomba dakika mbili tu, kwa sababu hii maana itatoa faida. Mhe. Mwenyekiti, nimesimama pale na vijana wangu wengi pana shughuli fulani kuna jamaa kasimama pale kama dakika 15 na gari yake vioo vya giza mchana. Nikawaambia

nyie jiandaeni twendeni pale kwenye gari, jamaa anakula *AC*, nikamwambia fungua vioo, nikapiga mimi kioo nalindwa na watu sina wasi wasi maana hata ulinzi shirikizi ni muhimu. Nikamwambia fungua kioo akaona zogo akafungua nikamuuliza unafanya nini hapa wewe mchana huu na watoto wa watu wanacheza hapa, akanimbiaa aah! Mimi nakaa mimi Mhe. Shihata wewe nakujua, sio mimi unanijua mimi Shihata utanijua na wengi wananijua, lakini wewe sikujui. Hivi vioo ulivyofunga fungua vyote tuone ndani maana watoto wetu mnawaiba nyinyi. Kwa hivyo, jamaa akaniambia naomba radhi kayayuka huyo kaenda zake.

Kwa hivyo, tunapokuta mazingira hayo tusimpe nafasi mtu, bahati nzuri Shihata nimepitia uaskari nilikuwa mwanajeshi, lakini tunaambiwa sote ulinzi shirikishi kwanza usiogope na uwe tayari kwa lolote lakini kulinda usalama wa watoto wetu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo narudia tena kuzipongeza Manispaa kwa makusanyo mazuri waliyoyapata, lakini pia walichoomba wapewe hususan katika kuendeleza mji wetu uwe safi na mazingira mengine. Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja sina matatizo. Ahsante mheshimiwa. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante, sasa anafuata Mhe. Jaku Hashim Ayoub na baadae Mhe. Abdalla Maulid Diwani.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, niendelee tena kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyeniwezesha kuwa hai na kuvuta pumzi zake hizi na nirudie tena huu si ujanja wangu wala akili yangu, wala uwezo wangu ni neema zake Mwenyezi Mungu kwa kusema *alhamdulillah*. Niendelee kumpa pole Mhe. Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu wa wizara hii kwa bajeti hii ambayo kuna sehemu haitumikii wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, bila ya kumsahau rafiki yangu Mkurugenzi wa Manispaa Aboud Hassan Serenge kwanza nimpongeze kwa dhati kwa kazi anayoifanya. Lakini, mara ya tatu mkuu wa kituo ndiye anayekamatwa kama watendaji wake wanafanya makosa "Anayekamatwa na Ngozi ndiye mwizi". Kama kuna mtu mwenye nidhamu kama Mkurugenzi huyu ndiyo yale yale moja, moja, mbili mbili, mbichi mbichi, kijani, kijani. Watendaji wa Manispaa ya Mjini hawako vizuri lakini tuache tutakuja mbele huko. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, niwapongeze Wakuu wa Mikoa hasa, hasa wa Kusini Unguja na Mkuu wa Wilaya ya Unguja, lakini nitakuwa sijamtendea haki Mkuu wa Mkoa Kusini Pemba bwana Hemed Suleiman Abdalla kazi anayoifanya. Kijana ametulia na makini kabisa hata katika maamuzi yake ametulia, nafikiri ndio kimemsababishia kumpandisha chati kuwa Mkuu wa Mkoa wa Kusini kutokana na utendaji wake. Lakini nirudie tu kuna methali inasema “mgema akisifiwa tembo hulitia maji”. Msije mkajisahau methali hazikukatazi kuzungumza ndani kwa mujibu wa kanuni zetu. Lakini nitakuwa mwingi wa fadhila kama sikumpongeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kusini, nitakuwa mtovu wa adabu wa mwisho kama sikumpongeza. Jamaa ukimuona saa 24 anacheka tu hajui kuhamaki hata kidogo yule kijana kwa umakini wake wa hali ya juu yeye ukimuona anacheka tu hata ukamkera vipi. Mkurugenzi endelea kufanya kazi kwa hali na mali. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, sasa mchango wangu itakuwa sehemu mbili mpaka tatu, nije kwenye masoko. Mhe. Mwenyekiti, tuko katika hali ya mvua masoko yote ya Unguja na Pemba ni uoza mtu na pesa zinazokusanywa pale anajua Mwenyezi Mungu. Lakini kukarabati hakuna hataki kufanya kazi, twende tukaangalie soko la Darajani ni aibu. Nimepiga kelele mwaka wangu wa saba huu zimetiwa bati kule utafikiri njia ya Makunduchi ya zamani ulipokuwa ukienda, unaziba kule mbele kiraka ukirudi tena nyuma kinarudi tena. Soko la Darajani pesa mnazokusanya hatari ya Mungu hapa ndio pakusema si pengine, mwaka wangu wa saba au wa nane kaitizame hali ya soko la Darajani shilingi ngapi zinakusanywa usiku na mchana saa 24 soko linafanya kazi, ni aibu, aibu haipendezi tuna wakati mgumu kwa kipindupindu mvua hizi tunakuja kutafuta mchawi, kinga bora kuliko tiba.

Mhe. Mwenyekiti, zinakwenda wapi pesa zile bati kule juu twende ukapite uangalie viraka vilivyotiwa kipande tena sio nzima, kipande kimekatwa au robo kinafunikwa. Hali ya soko la Darajani mwaka wa nane nimesema hamliwezi lipangisheni mtu achukue afanye kazi, lakini maradhi haya yanasababishwa na Manispaa, maradhi haya yanachangiwa kwa asilimia 60 au 50 na Manispaa. Leo atakuja kamatwa mtu muuza mikate kitu cha aibu ya mwisho na cha kuchekesha, muuza mikate kweli anachafua mazingira. Pale penye haja ya kutaka kufanywa hapafanywi jambo si kitu kizuri tena nikakwambieni wajumbe hapa msikilize kwa makini mtacheka mpaka mtaanguka.

Kitu kibaya kuliko chote Manispaa na Halmashauri hazina sheria, kakae Mhe. Waziri na watendaji wake na Wakurugenzi na Wanasheria ninayokwambia sasa hivi unisikilize kwa makini tumepitisha sheria hapa Nam.7 ya 2014 na Kanuni zake. Kanuni za huduma zinazotolewa na Mamlaka ya Manispaa zimefuta ukurasa wa 88 hii tumepitisha imekuja sheria na tumeipitisha. Kanuni zifuatazo zinafutwa, Kanuni ya Halmashauri za Wilaya na Mabaraza ya Mji ya 2006 Kanuni za Manispaa hazipo. Kwa hiyo, watu wameonewa mimi nilitaka kukamatwa nikatiwa ndani kwa kumtetea muuza mikate, lakini atanilipa Mwenyezi Mungu na shati langu la Italy likachanwa.

Mhe. Mwenyekiti, niendelee kumshukuru Mhe. Waziri ndiye aliyenipapatua na kama siko makini kukimbia mbio ningekaa ndani mahabusu, na sheria hawana Manispaa. Hapa Mhe. Waziri utakapokuja hili tuelezane njoo ukakae na wanasheria wako isijekuwa ile hadithi ya kukamata ng'ombe baadae ukatuletea kanuni humu ndani, aah! Mlikataa kuchangia. Ushakamata kitu baadae unatuletea sheria hivyo ni vichekesho, sisi ni wawakilishi tumechaguliwa na wananchi kuja kusema matatizo yao na cheo ni dhamana tutakwenda kuulizwa hapa tunapita tu walikuwepo wangapi, wapo hapa. Tunarudi kwenye uchaguzi pengine tukiwa hai tusirudi humu ndani lakini kila unachokipanda ukipanda nazi huwezi kuvuna chungwa, ukapanda papai huwezi kuvuna balungi ulichokipanda ndio utakachokivuna. Lakini sheria hamna kakae Mhe. Waziri uje unieleze, sheria mmezifuta mpaka leo hamjazitunga, mambo gani mnayofanya tunaonea watu wapiga kura hicho si kitu kizuri.

Mhe. Mwenyekiti, soko la Mombasa nenda kaliangalie ni aibu kitu kubwa kutoa milango ya maduka tu, kwa milango ya maduka mnaongoza Manispaa hilo nikupongezeni lakini japo uchochoro hili jambo kubwa. Kaliangalie Mwanakwerekwe likoje masoko yote ni uchafu mtupu, halitaki hata kumurikwa tochi pesa zinakusanywa sijui zinakwenda wapi, halafu unapiga kelele

kipindupindu, kipindupindu tunakichangia sisi, haielekei. Hapa nitakuja kuzuia fungu naanza ku-*declare* kabisa nisije nikasahau.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye kilio chengine cha *parking* ni hatari kweli kweli, ni hatari mno. Kwanza Mhe. Waziri kuna kijana anaitwa Pandu Ameir Pandu huyu unielezee huyu kijana mimi Mhe. Mwenyekiti sio aghlabu kutumia gari itokee mara moja moja tu nakwenda jimboni na kwa kuwa ni mbali. Niliweka gari dakika mbili tu kwenda kuchenjisha dola nakuja imeshapigwa mnyororo kuna gari nyengine hazikufungwa, huu ni ubaguzi wa rangi. Jengine namuuliza huyu Pandu Ameir Pandu risiti yake hii hapa naomba ichukue ukampa Mhe. Waziri aione na hizi risiti sijui kama ziko kweli hizi, shilingi 10,000/- kwa sekunde tu mpelekee Mhe. Waziri nidhamu mbovu kabisa na gari za SMZ hazifungwi, wewe ukaikataa Mhe. Waziri usikatae lakini ndio ukweli ulivyo. Haielekei dakika tano nimetoa shilingi 10,000/- pesa zinakwenda wapi, huku masoko yanauza pesa wanazipeleka wapi? Tusifike hapa tukataka kueleana si kitu dakika mbili shilingi 10,000/- halafu sheria huna ya kufunga gari. Kanuni hamjatengeneza mpaka leo huku huku mnalaumu wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, kuna kesi moja Pemba imetokea Mkurugenzi kama mpo na Halmashauri sikilizeni vizuri ni ushauri wa bure huo wala sijapata kumlipa. Jamaa kakamatwa na samaki wake Pemba wakampeleka mahakamani, ah! Juzi akasema, "Ukiujua huu na mimi naujua huu"; akapelekwa mahakamani jamaa akashusha samaki kufika pale akapandishwa juu akasema Mhe. Jaji mimi sikuwa nauza samaki nilikuwa nasafirisha samaki, kashinda kesi akawageuzia kibao Manispaa walilia, ndio maonevu mengine yanavuka mipaka yake wanatuchonganisha na viongozi wetu wakuu. Manisapaa hao sio Waziri wala Naibu Waziri, lakini mkamatwa na ngozi ndio mwinzi na humu ndimo tunamowajibika. Kwa hivyo, hali ndio kama hiyo kageuza kibao pale kasema alikuwa anateremsha samaki mahakama ikamuachia akawashitaki Manispaa.

Utaratibu wa kufunga magari Mkurugenzi huu utakuja ku-*cost* kuna siku mimi nasema kwa kuchukua gari. Mimi nimeshachukuliwa gari yangu ile ya kijani ikenda kutupwa Bwawani pale wiki nzima niko Dodoma wala sikujali, lakini baada ya kurudi nikenda nikaambiwa lugha nzuri kidogo Mkurugenzi namuheshimu lakini gari iko nyumbani kwangu ilitaka kuja kuchukuliwa.

Mhe. Mwenyekiti, leo kitu cha ajabu barabara ya Madema mpaka Mlandege wametoa vichochoro vyote Manispaa kwa ku-*charge* gari, duniani kote wanatembea viongozi wanakwenda barabara kubwa hakuna hata sheria moja ya kuweka *parking*.

Juzi niko Chake Chake pale nilicheka, kwenye *cross* mtu wa Manispaa anatoa zebra ili zi-*park* gari, nilikaa nikacheka kweli kweli, kwenye *cross PBZ* pale Chake Chake unapinda kwenda Tibirinzi ati anachora mchoro wa kufanya *parking* ni vitu vya vichekesho. Tunatafuta ajali na sheria hamna, kanuni hamna, akija Mhe. Waziri hapa atuelezee hizo kanuni. Kanuni zimefutwa huku watu tunaendelea kuwanyanyasa na hatuna kanuni mpaka leo hii hazijatungwa, sijui ziko njiani au zinaandikwa *spelling* moja, moja mpaka leo hazijesha, lakini haielekei.

Mhe. Mwenyekiti, halafu mtu ana duka lake unalipa *license,* unakwenda kununua umeme, duka la *hardware* kuna wengine walemavu kuweka gari mbele ya mlango wako kosa. Sioni kama ni utaratibu hapana kitu kama hicho hata sheria ya *traffic* ni mita 10. Wewe una duka unalipia,

kuzoa taka, umeme, *license* zaidi ya sita, *ZRB* kodi kwa mwezi halafu usiweke *parking* aa! Imezidi.

Sasa, jengine utacheka mpaka utaanguka Mhe. Mwenyekiti, unakwenda kununua mkate wa bofulo Darajani unaweka ile pikipiki yako wameshaacha magari wanakuja kwenye pikipiki kesho watakuja kwenye baskeli. Unanunua mkate wa bofulo shilingi 250 unalipa shilingi 300 vichekesho au vespa tunakwenda wapi? Huku mji kuutengeneza unawashinda pesa zinakwenda wapi. Hapa itabidi tuunde kamati teule nyengine sasa ata, hatuwezi tukaacha wananchi wakateseka wakati wenyewe mgumu huu, haiwezekani duka hilo unalipa kodi zote leo duka la *hardware* utanunuaje ndoo za rangi njia ya Mlandege yote wamechafua Manispaa na sheria hairuhusu wenye barabara wanapiga kelele, wenye mamlaka wao hawachangii chochote ugatuzi umekuja juzi na jana, kuna wengine walemavu halafu ubaya wenyewe kanuni hamna. Hapa nitakuwa mkali kweli kwenye kanuni maana yake nimekaa itakuwa ndio ile kadithi ya ng'ombe tumekamata ng'ombe wa watu baadae tukaleta kanuni ndani humu ni vichekesho.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye utaratibu wa kufungua mabaa. Maadili yetu kiasi kikubwa tusiwe na mabaa. Hii niiombe sana na nimpongeze Mkuu wa Mkoa wa Mjini kwa kazi aliayoifanya Bwana Ayoub Mohamed Mahmoud, amejitahidi na Mwenyezi Mungu atamlinda, lakini utaratibu huu wa baa uangaliwe.

Zimbabwe hata Uisilamu haupo lakini hufungui baa mtaani kabisa, wanaweza kuwa watu hata 40, kwanza wameridhika na kule watu wanalewa majumbani kwao na dini haipo kule. Kitu cha kuchekesha mabaa yamezidi. Hii njia ya Chukwani zaidi ya baa nane au kumi hata Mwezi wa Ramadhani wakati mwengine hujui, tunapoteza maadili ikisha utakuta tunalalamika. Lazima hapa sheria iangalie kuhusu haya mabaa.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye mchango katika kitabu sasa ukurasa wa 21 JKU. Hapa imesemwa JKU inavyo vianzio vingi vya kukusanya mapato lakini malengo yake iliyojiwekea kukusanya mapato yao ni kidogo kwa vile malengo hayo ya ukusanyaji hayajafika. Je, kwa nini, la kwanza.

La pili, naomba nitajiwe vyanzo vyake vya mapato JKU. Mhe. Waziri atapokuja kujumuisha. Hapa waliambiwa wakusanye shilingi 940 milioni sawa na asilimia 78, lakini walikusanya kama shilingi 50,725,000 na JKU wana vipato vingi sana Mwenyezi Mungu awajaalie. Hili haliko vizuri, kwa hili nitahitaji maelezo JKU wana vyanzo vingi lakini hawa wameambiwa shilingi 940 milioni wakusanye wamefika shilingi 50,725,000, lakini *still* wana vyanzo kwa nini wasifikie malengo hayo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia suala la uchapishaji wa risiti kukusanya mapato kwa Manispaa zote za Halmashauri. Hili ni agizo la serikali, inavyoonekana au kuna harufu Manispaa na Halmashauri risiti zao haziendi, baadhi sio zote kwenye kitengo chetu cha *press* kwenda kuchapishwa. Kwa hivyo, hili suala waliangalie wanapiga kelele watu. Kwa hili nitahitaji maelezo hapa napo liangaliwe baaghi yao hazipigwi *press* sijui wanakochapisha wanakujua wenyewe na kuna njia gani.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo nije suala la ugatuzi kuhusu Hospitali ...

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, dakika umemaliza.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, namalizia kuhusu Hospitali ya Michamvi. Tumeshazoea sisi tunaotoka shamba kule tukakaa kule tukaona ni hospitali tu hatujui kituo ni Kituo cha Afya. Nimpongeze sana Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kusini. Kituo kinaendelea vizuri naimuombe tu Mhe. Waziri wakimalize ili wananchi wapate matibabu hayo.

Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mjumbe. Lakini kabla sijamruhufu mchangiaji wetu wa mwisho kuna tangazo kutoka kwa Mwenyekiti wa UWAWAZA, mnaombwa mkutane baada ya kikao na Mwenyekjiti wa UWAWAZA, wajumbe mnajijua. Ahsante.

Mchangiaji wetu wa mwisho kwa muda huu atakuwa ni Mhe. Abdalla Maulid Diwani, karibu sana.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii kuweza kuchangia hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2018/2019 ya Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ.

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kunijaalia nguvu na uwezo wa kusimama hapa mbele ya Baraza lako hili tukufu kuweza kuchangia. Vile vile, nitoe shukurani zangu za pekee au pongezi katika wizara nzima hii kuanzia waziri na watendaji wake wote wa wizara hii, kwa ufanisi wa kazi zao wanazozifanya. Lakini shukurani za pekee nampongeza binafsi *DC* wa Kaskazini 'B' kwa vile ni mdau wangu katika rasi yangu ya *G1* kuweza kupata fursa kuchaguliwa kuwa Mkuu wa Wilaya ile. Namuamini na mchapa kazi najua tutafika namshukuru sana. *(Makofi)*

Naomba niende katika mchango wangu moja kwa moja bila ya kupoteza muda. Mhe. Mwenyekiti, mchango wangu nakwenda katika fungu la D01. Fungu hili nikipitia bajeti ya mwaka 2017/18 na bajeti ya mwaka 2018/19 naona kidogo kuna kama mvutano hivi, kwa vile katika miradi ya maendeleo ya miaka hii huku ilikuwa mitatu sawasawa sikatai na hata huku imekuja mitatu, lakini kuna mabadiliko katika hii iliyokuja huku. Sasa ningeomba waziri atapokuja ajaribu kutuweka sawa, kule walikuwa kuanzisha wakala wa ulinzi wa Zanzibar mradi wa *CCTV Camera* na Mradi wa Mageuzi ya Serikali za Mitaa.

Mhe. Mwenyekiti, lakini tukiangalia katika miradi ya maendeleo ya safari hii huku kuna kamera, kuna mageuzi katika Serikali za Mitaa na Kiwanda cha Ushoni JKU. Tunajua JKU tayari ina fungu lake kule, kwa sababu hata kwenye D06 kuna Mradi wa Kiwanda cha Viatu vile vile ni JKU. Kwa sababu E ni D hii kwa ajili ya utawala na mambo gani ya diwani lakini imeingia Mradi wa Ujenzi wa Skuli ya JKU. Ningeomba ufafanuzi hapa uko vipi ili tusipate shida katika hilo.

Tukiendelea mbele katika mchango huo hata nikienda katika masuala hayo hayo aya ya 38 katika D01 kulikuwa kuna mustakabali mzima walisema kwamba ujenzi wa barabara. Naomba kunuku uwalisema kwamba: " Mfuko wa Barabara kwa matengenezo ya barabara za ndani kiasi cha shilingi hizo zilizotajwa ni kidogo mno kukidhi mahitaji ya matengenezo ya barabara zenye urefu wa kilomita 50 zilishafanyiwa upembuzi yakinifu na zile zinazojitokeza kwa mahitaji maalum". Ningeomba sana Mhe. Waziri katufumba hajatuwekea wazi, alikuwa atueleze ni barabara gani zilizofanyiwa upembuzi yakinifu. Kwa sababu mimi toka niingie kwenye Baraza hili nina barabara yangu ya Jang'ombe *Danger*, niliambiwa inafanyiwa upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi lakini hakuna chochote mpaka leo.

Sio hilo tu, nina barabara yangu nyengine pia ambayo toka nimeingia humu naisemea na sitoweza kunyamaza mpaka nijue mwisho wake barabara ya Mpendae - Jang'ombe. Japo kwamba wenyewe wawili hao wanavutana wengine wanakwambia ile waijenge Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji lakini wenyewe wanasema ni ugatuzi barabara ile ijengwe na Halmashauri. Kwa hivyo, ningeomba jibu la msingi angalau wananchi wa Jang'ombe waweze kujua mustakabali mzima wa barabara ile, kutilia maanani kwamba barabara ile tayari hata kuna msamaria mwema mmoja alijitokeza alitoa kiwango cha fedha kwa ajili ya kutia chachu ya ujenzi wa barabara ile. Kipindi hicho Mhe. Issa Haji Ussi alikuwa Mhe. Naibu Waziri wa wizara ile ni miongoni mwa watu ambao walioshuhudia upokeaji wa fedha zile. Ni lini tutajua mustakabali wa barabara yetu ile ya Mpenda - Jang'ombe.

Mhe. Mwenyekiti, katika suala hilo nakwenda katika aya ya 41. Imekuwa nyimbo ya muda mrefu sasa kuhusu suala zima la mfumo wa *electronic* kukusanyika mapato. Tumezungumzwa mwaka 2015/16, 2016/17 na hivi leo tena imeletwa 2018/19 tumefikia wapi na tumekwamia wapi. Mara zote hizi tunakuwa tunazungumzia suala lile juu ya suala zima la ukusanyaji wa mapato kwa njia za *electronic* hizi Manispaa zetu na shughuli nyengine. Kwa kweli, imekuwa nyimbo ya muda mrefu lakini maitikio yake hayako vizuri, kwa sababu mpaka dakika hii tunayozungumza ni zaidi ya bajeti ya tatu tunazungumza suala hili lakini utekelezaji wake bado upo ule ule wa zamani, hatujaenda katika njia ya *electronics* tumekwama wapi, tatizo nini.

Sasa, hii inakuja na mafungu yale tunayapitisha hapa na fedha inatoka lakini tunakwamia wapi. Namuomba sana Mhe. Waziri hapa kidogo hiki kifungu nitakishika angalau nipate mwelekeo mzuri wa kuweza kujua, kwamba tumekwamia wapi na kwa nini tumekwama muda wote huo, kwa kuweza kutotekelezeka kwa suala hili la ukusanyaji wa mapato kwa njia za *electronics*.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea mbele nakwenda kwenye Tume ya Utumishi Idara Maalum. Kwanza nimpongeze sana Mhe. Waziri wa wizara hii kwa sababu tulipiga kelele nyuma huku lakini baadae ufanisi tukaona ni suala zima la wale vijana waliosimamishwa katika Idara ya KMKM kule. Ni kweli nashukuru zogo letu limesaidia wale vijana wamepelekwa katika Idara ya Ulinzi wa JKU napongeza sana na wameshaanza kupokea mishahara yao, lakini wana fedha zao ambazo waliposimamishwa mpaka leo mwaka mmoja hawajalipwa tatizo nini. Unapomtoa mtu akiwa na kesi ushamwambia kesi hiyo imemalizika, anaanza kazi pale ina maana tayari huyu mtu umeshamsafisha hana kosa kwa hivyo, yale mafao yake apatiwe.

Hivi sasa ni mwaka mmoja huu toka tumemaliza wale watu bado fedha zao hawajalipwa. Namuomba sana Mhe. Waziri katika hili tuone namna gani ya kuweza kuwasaidia wale vijana,

ili kupata yale mafao yao ambapo kipindi kile walichosimamishwa walikuwa hawapewi ili na wao wajihisi kwamba kweli wameweza kutatuka katika tatizo lile.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea kwa haraka haraka nizungumze suala la D7, Mkoa wa Mjini Magharibi. Kwanza nampongeza sana kaka yangu Mhe. Ayoub Mohamed Mahmuod, Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi namna anavyofanya kazi kwa ufanisi kabisa na kila mtu tusiwe wanafiki katika hicho tunapongeza utendaji wake wa kazi. Lakini penye mafanikio na changamoto hazikosekani au kasoro lazima ziwepo na ndio maisha yalivyo. Pamoja na kazi nzuri anazozifanya Mhe. Mkuu wa Mkoa huyu bado kuna matatizo ambayo wengi wao wananchi huku nyuma wakiwa wanaamini kwamba yanafanyika kupitia mkono wa Mhe. Mkuu wa Mkoa huyu.

Sasa Mhe. Waziri katika hili nalo vile vile sijui liko vipi sitaki kusema kitu ambacho sina uhakika nacho, lakini nina uhakika kwamba baadhi ya matendo yaliyofanyika wiki mbili zilizopita katika sehemu moja ya Chukwani *Coconut* wamedhalilishwa vijana wa kike kupita kiasi ni aibu kwa taifa hata na nje ya nchi yetu hii. Na ikachukuliwa azma nzima ya Mhe. Mkuu wa Mkoa huyu akathubutu kukutana na wale wahanga akawakataza hata kuzungumza na vyombo vya habari kwa nini awakataze kama ni haki yao ya msingi wameshafanyiwa matatizo yale wana haki kuulizwa na wakajibu ilikuwaje.

Wakati wanakwenda kuvamiwa katika suala lile pale inavyosemekana kwamba kulikuwa kuna ngoma ambazo zilikuwa haziendani na silka na mila na desturi yetu Wazanzibari, sawa hatukatai. Lakini je, adhabu yake ni ile waliyoipata? Nafikiri kuna adhabu na sheria, unapomkamata kavunja sheria kuna taratibu za kumpeleka katika vyombo vya sheria ili akaadhibiwe kisheria si yale ambayo wameadhibiwa. Ni aibu na maumivu ya hali ya juu wale miongoni mwao ni wapiga kura wetu wanatulalamikia, ningemuomba sana Mhe. Waziri katika hilo basi tatizo ni nini, kwa nini iwe hivyo?

Vile vile nikiendelea tena Mkoa wa Mjini huo huo, Mkuu wa Mkoa alikuwa na azma nzima juu ya suala la usafi. Suala la usafi katika Mkoa wa Mjini Magharibi lilikuwa na nia nzuri tu, lakini kwa kweli sasa hivi ile azma au lengo la yale mambo yamefifirika hayapo. Tuliona kwa nia safi kabisa Mkuu wa Mkoa alikutana na Madiwani, Wawakilishi akaleta azma ile kama ni maelekezo ya serikali lakini sasa hivi wale vijana wote waliotegemewa wafanye zile shughuli naoa wameacha. Kwenye mitaa yetu hususan Magharibi huko na hata mjini kumekuwa kazi hazifanyiki tena na masuala yale yalipitia kwenye Mabaraza ya Vijana, kwamba Mabaraza ya Vijana waunde Manispaa za Shehia sasa hivi naona hazipo.

Kwa kweli, pamoja na kujinasibu mbele ya Mhe. Rais tukazindua pale Sebleni sasa hivi naona hakuna kitu kinachoendelea. Sasa sijui tatizo gani lililopelekea hadi leo hii ikawa tunasuasua katika mazoezi yale. Sisi kwenye shehia au majimbo yetu wale vijana wengi wametupa mkono hawafanyi ile shughuli. Sasa ningeomba tu pamoja na sisi kushajihisha kwetu lakini na zile nguvu za kwake yeye Mhe. Mkuu wa Mkoa zinahitajika ili tuone namna gani tunaweza kukidhi yale mahitaji.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea mbele nakwenda katika Fungu D12. Hili ni fungu ambalo hata mwaka jana tulilipitisha na ikawa msimamizi wake kwa mujibu wa buku letu hili hapa

tuliambiwa kwamba, naomba ninukuu kidogo. "Pamoja na fungu hili matumizi yake yatasimaiwa na Mkurugenzi Afisi ya Usajili wa Vizazi na Vifo".

Mhe. Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa lile fungu huyu tuliyemthibitisha kwenye Baraza hili la Wawakilishi alinyang'anywa akawa halisimamii lile fungu, badala yake Katibu Mkuu wa wizara akawa analisimamia sijui imetokea nini. Sisi kama Baraza la Wawakilishi tulipitisha kamba fungu lile asimamie Mkurugenzi wa Vizazi na Vifo, lakini kwenda kule katika harakati zetu anasema hili fungu mimi nina zaidi ya miezi sita sasa hivi nimefungiwa, nafikiriwa tu *OC* kutoka kwa Katibu Mkuu wa wizara hii sijui taratibu ziko vipi hata imekuwa yale tuliopitisha hapa leo hii yamekwenda kubadilika.

Vile vile walipangiwa majukumu hawa ya D12 naomba ninukuu, walipangiwa majukumu mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, naomba umalizie haraka una dakika moja.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana, walipangiwa majukumu mbali mbali hawa ikiwa kuimarisha mfumo wa usajili wa vizazi na vifo na talaka, walipangiwa kuimarisha mazingira ya Afisi ya Utawala.

Mhe. Mwenyekiti, kama huyu mtu alinyang'anywa ule utekelezaji wake ilikuwa vipi. Haya mengine niliona kuna utekelezaji kuna watu wamekwenda kusoma wamepata fursa ile, lakini haya masuala ya mfumo wa usajili tumekwenda pale hata vifaa vya kutendea kazi imekuwa haviridhishi ni vifaa vibovu ambavyo vinakwenda kwa ujudi wa Mungu tu, pamoja na fungu lile lililokuwepo. Basi ningeomba Mhe. Waziri atapokuja anisaidie haya majibu mazuri ili tusipate shida, *unless*/*otherwise*, mimi hayo mafungu mawili itabidi niyazuwie kidogo natoa hadhari hiyo mpaka nitapopata maelezo mazuri kupitia Mhe. Waziri nitayaachia. Baada ya muda huo mchache naunga mkono hoja kwa asilimia 92 na asilimia 8 nasubiri majibu ya maelezo yangu. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mjumbe, kabla sijaakhirisha naomba niwasome wachangiaji wa jioni wafuatao. Kwanza Mhe. Omar Seif Abeid, akifuatiwa na Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf na Mhe. Abdalla Ali Kombo naye ajitayarishe.

Pia nakumbushia tangazo la Mwenyekiti wa UWAWAZA baada ya kikao mtaendelea kuwepo na mwenyekiti wenu. Baada ya hayo naakhirisha Baraza hili hadi saa 11:00 jioni ahsante sana.

(Saa 7:00 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Hotuba hii ya Bajeti ya Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ.

Awali ya yote sina budi kumshukuru *Allah Subhanah* wa Wataala alietujaalia kufika hapa leo jioni hii tukaweza kutekeleza jukumu letu kwa mara ya pili, hatuna budi kurejesha shukurani zetu kwake. Tunamuomba Mwenyezi Mungu mwenyewe atuzidishie uwezo huu wa afya aliotupa *Inshaallah.*

Pia nachukua fursa hii kumpongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dr. Ali Mohammed Shein kwa umahiri wake na bidii yake uzalendo na upendo wake wa nchi hii jambo ambalo limetufikisha hapa tulipo leo. Mimi binafsi nasema sisi Wazanzibari ni kama hidaya au tunu aliyotupa Mwenyezi Mungu kutupatia Rais huyu. Tunamuomba Mwenyezi Mungu ampe hekima amzidishie na afya njema amalize kazi yake ya kuliongoza taifa letu akiwa ni mzima ili tuendelee kupata busara na hekima kutoka kwake. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, mimi leo hapa nasimama kwa sababu ya muda na kwa sababu ya uzito wa wizara hii kawaida yangu nitaiacha kwa sababu kawaida yangu mie huwa napenda kupongeza sana serikali kwa mambo yale mazuri yote wanayoyafanya. Lakini kutokana na muda leo nitakuwa siendi hapo nitakwenda moja kwa moja. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, naomba kwanza nichangie wizara hii katika *page* ya 19 ya Wakala wa Serikali, Wakala wa Ulinzi wa JKU. Mhe. Mwenyekiti, ni jambo zuri naipongeza sana hii wizara kwa kuona hili na serikali kwa kuanzisha Uwakala. Lakini nilitaka nijituwe waziri atakapokuja kuna tafauti gani ya hao Wakala wa JKU na wale wa JKT SUMA kwa sababu wenzetu wa JKT SUMA wamejipanga vya kutosha wana mpaka miradi mikubwa ya maendeleo lakini wao wameeleza kama wanaendelea na mambo ya ulinzi kwa mahoteli tu.

Lakini wenzetu wale JKT SUMA wana mpaka makampuni makubwa ya ujenzi ambayo yanatumika kwa ujenzi wa majumba na mambo mengine. Sasa kama hivyo ndivyo, ningeomba waziri ukija uniambie umejipangaje kuiwezesha hii, huu Wakala wa Ulinzi ili kufikia angalau kama walivyo wenzao SUMA JKT. Lakini vijana wa Mafunzo ya Vijana 2848 pia mimi nilitaka kujua ambao tuliwapa mafunzo mpaka sasa tumeshawaajiri wangapi.

Lakini pia nilipenda tuendwe katika ukurasa wa 28D7 Mkoa wa Mjini Magharibi. Mimi sina budi kumpongeza sana Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi anafanyakazi kubwa kazi nzuri. Lakini mwenzangu Mhe. Abdalla Maulid Diwani kwamba kila "Penye zuri hapakosi kasoro". Tumeona kwamba matumizi bora ya ardhi wameeleza pale na usafi wa mji. Lakini mimi mara nyingi huwa napiga kelele juu wa uegeshaji ovyo wa magari kwenye barabara ya Fumba na maeneo mengine. Tatizo hili bado lipo wenye daladala wanasimamisha wanapotaka hakuna hatua yoyote inayochukuliwa ilimradi bila kujali usalama wa abira wanaowachukua.

Lakini pia Mhe. Waziri tulikuwa na mpango uliouanzisha wa kuweka ufasi wa mji kwa kuondoa wanyama tukakwambia isije kuwa nguvu wa soda na ukasema si nguvu ya soda ni nguvu wa kuendelea. Lakini leo pale Mbuyumnene ng'ombe wanafungwa hasa mbali ya kuwaondoa wapo wanafungwa. Sasa sijui ile nguvu yako uliyokuwa ukiisema imekwenda wapi. Lakini leo

wanyama wapo na wanaendelea kuwepo na hakuna linaloendelea. Kwa hiyo, nilikuwa naomba pia uje unambie kwamba ni hatua gani ulioichukua.

Mhe. Mwenyekiti, *page* ya 33 tuliona kwamba kulikuwa na ukaguzi wa nyumba katika *page* hiyo tuliona kuwa kuna ukaguzi wa nyumba zilizokaguliwa ili kuweza kuwabaini kwamba nyumba zenye vyoo na zilizokuwa hazina vyoo kwa watu Baraza la Manispaa. Lakini mimi nilitaka nijue hizi nyumba ambazo mmezikagua na mkaziainisha ni hatua gani zilichukuliwa na vipi mliwasaidia wale wananchi ili waweze kupata kujenga hivyo vyoo vya kujistiri wakaepukana na maradhi ya mripuko.

Mhe. Mwenyekiti, tukienda tena hapo katika ukurasa wa 32 nazungumzia suala la barabara, napenda kunukuu:

"Katika kuimarisha usalama barabarani Baraza limefunga mkataba na Serikali ya watu wa China kwa ajili ya uwekezaji wa taa katika barabara zenye urefu wa kilomita 15"

Lakini ukizitaja hizo barabara zenyewe. Aidha Baraza kwa hatua ya awali limeweka kifusi na kujenga vyoo katika vituo vipya ya daladala vya Kijangwani. Lakini Mhe. Waziri unasema kwamba utaweka lami katika bajeti inayoishia 2017-18 ambayo leo ni mwezi huu. Lakini pale naona mwezi unamaliza hatuoni dalili zozote. Je, vipi utekelezaji wake wa suala hili ambalo umelieleza wewe mwenyewe kwa upande wa huduma za kuweka lami. Nataka nijue pia utakapokuja.

Tukienda sasa katika Baraza la Manispaa la Magharibi "B" wanasema kwamba Manispaa imesafisha misingi ya maji ya Kiembesamaki, Uwanja wa Ndege, Mombasa hadi Kisauni. Jambo ambalo sisi wenyewe tunaliona tukipita pale kutoka Uwanja wa Ndege maji yanajaa yako vile vile na tumelizungumza. Lakini leo mimi nashangaa kuona kwamba hili limetajwa kama mmezibua misingi na mmesafisha hiyo misingi. Sijui ni misingi ipi iliyosafishwa Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, katika yote napenda kuchukua fursa hii adhimu niliyoipata kutoa shukurani zangu za dhati kwa viongozi. Narudi sasa kwa Mkoa wa Kaskazini Pemba. Napenda kuchukua fursa hii kumpongeza sana Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba kwa utaratibu wake aliouanzisha wa kujenga ule msingi wa kuondoa maji pale, ambayo ilikuwa ni kero kubwa mpaka kufikia Balozi mwenyewe na Rais kwenda kuiona. Kwa kweli wananchi wa Kaskazini Pemba hasa Mji wa Wete wamefarijika sana na ujenzi wa ule mtaro. Ule mtaro umesaidia kwa kiasi kikubwa na sisi tulitegemea mambo kama yale yafanywe na Wakuu wa Mikoa wengine kama lile kwa kadhia zinazotukuta kwa baadhi ya maeneo yetu.

Lakini pia napenda kuchukua fursa hii na kumpongeza sana mwanadada Mkuu wa Wilaya ya Micheweni. Mhe. Mwenyekiti, yule wanadada ni mtu wa kupigiwa mfano amejitolea kwa hali na mali, mimi mwenyewe katika Jimbo langu la Konde lilikuwa lile Jimbo limeoza. Limeoza kwa hali mbaya iliyokithiri ya uingizwaji wa dawa na mambo mengine. Nimshukuru sana msaada wake umechangia kwa kiasi kikubwa ameweza kumaliza lile tatizo lililokuwepo pale ambapo hapa wazee na wananchi wenyewe kwa ujumla sasa wengi wamefurahia ingawa mwanzo walikuwa hawakumuelewa dhamira yake. Lakini baada ya kuelewa dhamira yake ya kwamba

analolifanya ni jambo lilimo katika utekelezaji wa Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi na kulinda vijana wetu taifa letu la kesho, wameanza kuunga mkono kwa asilimia kubwa.

Lakini jambo la kushangaza la aina yake wizara kubwa kama hii leo Mkuu wa Wilaya ya Micheweni hana gari, gari anaazima kwa uhakika *ZSTC*, Mkuu wa Wilaya ya Wete hana gari anatumia gari yake na Wakuu wa Wilaya wengine. Mimi nataka utakapokuja unambie ni lini hawa Wakuu wa Wilaya watapatiwa magari kule Pemba, Mkuu wa Mkoa gari alilonalo ndio lile lile.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na uzito wa viongozi hawa na kazi ngumu wanazozifanya hawa wanatakiwa wawe na magari ya uhakika ya kufika kwenye maeneo yao ya kazi wakati wote. Mimi nilipata habari sikushuhudia lakini gari lile analopanda Mkuu wa Wilaya kuna siku moja kwenye msafara wa Kiongozi Mkubwa liliharibika njiani akashindwa kuunganisha msafara ule aibu. Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima naomba utakapokuja unambie lini Wakuu wa Wilaya tutawapa magari, Mkuu wangu wa Wilaya ya Micheweni lini atapata gari.

Mwisho naogopa kuchukua muda mwingi nataka niingie kwenye makusanyo nisije nikaja kumaliza na matumizi kwenye miradi ya maendeleo. Mhe. Mwenyekiti, kwenye miradi ya maendeleo mimi hapa kidogo nitakuwa siko pamoja na nyie kwa sababu nataka nipate ufafanuzi hasa wa mradi wa *CCTV Camera*. Huu naomba mnipatie maelezo ya kina. Kwa sababu tulipitisha shilingi bilioni ishirini kwa ajili ya Mradi wa *CCTV Camera* na kwa mujibu wa kitabu hichi shilingi bilioni kumi na tano milioni mia mia mbili na kumi na laki mbili na hamsini zilipatikana sawa sawa na asilimia sabini na sita. Lakini bado kunatakiwa na mara hii tuidhinishe tena shilingi bilioni ishirini. Suala langu na wasiwasi wangu nilionao kwamba hizo *CCTV Camera* sizioni, hizi pesa tunaambiwa tuingize tena bilioni ishirini. (*Makofi*)

Sasa mimi nataka kujua huu mradi halisi hasa gharama yake ni shilingi ngapi lini utaanza na lini utamaliza. Kwa sababu mimi maoni yangu kwamba pesa za *CCT Camera* Mhe. Mwenyekiti, iko haja ya kuzihamisha tukazipeleka kwenye barabara za wananchi hasa kule vijijini ambako zimeharibika kwa kiasi kikubwa. Wananchi vijijini wana matatizo makubwa ya barabara wizara hii imegatuliwa miradi yote imepelekwa kwao kupitia barabara, maji, elimu na mambo mengine. Sasa leo kuendelea kuweka bilioni ishirini tena kwa ajili ya *CCTV Camera* ambazo hatuzioni mimi naona si sahihi.

Kwa hiyo, kifungu hichi Mhe. Mwenyekiti, nina dhamira ya kukizuia mpaka pale nitakapopata maelezo ya kina vyenginevyo mie Mhe. Mwenyekiti, sitaunga mkono hii bajeti mpaka nitakapopewa maelezo ya kina kuhusiana na hizi pesa za *CCTV Camera* na hili nitawaomba na wenzangu waniunge mkono ili tuzihamishe pesa hizi tuwapelekee wananchi zikawasaidie vijijini. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, tumeshuhudia leo kutokana na mvua kubwa inayonyesha ukipita katika barabara pale kwa Mchina barabara ile haipitiki kwenye mataa watu wote pale juzi palikuwa na foleni watu hawapati kupita. Mimi napendekeza baada ya kutumia kwa jambo hili pesa hizi zipelekwe kwenye kitengo chengine sina maana kwamba wizara isichukuwe pesa, lakini ihamishwe kutoka Kitengo cha *CCTV Camera* kipelekwe kwenye maeneo mengine ili pesa hizi zikasaidie wananchi wengi. Mimi najua bilioni ishirini zikigaiwa kidogo kidogo wananchi wengi

pamoja na wangu mimi wa Konde pia zitawafika. Lakini zikienda kwenye *CCTV Camera* zitabakia hapa na hazitaleta matokeo yaliyo bora.

Mhe. Mwenyekiti, naona muda wangu umekamilika au kama utaniongeza dakika tano nina mengi ya kuyazungumza.

Mhe. Mwenyekiti: Muda umemaliza Mheshimiwa.

Mhe. Omar Seif Abeid: Haya ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Naunga mkono asilimia thamanini zilizobakia nitazizuia mpaka nitakapopata majibu. Ahsante. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante kwa mchango wako ambao umetoa. Naomba nimwite Mhe. Masoud Abdrahman na Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf, pamoja na Mhe. Mwanaasha Khamis Juma pia ajitayarishe.

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipatia nafasi hii ya kuchangia jioni hii.

Kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kukutana hapa jioni hii.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kwanza nimpongeze Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kazi nzuri ambayo anaifanya hasa suala la msingi ni suala zima la usalama katika nchi yetu.

Lakini pia nichukue nafasi hii kumpongeza Mhe. Waziri makini kabisa kaka yangu Haji Omar Kheir kwa kusimamia vizuri Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ. Lakini pia na Mhe. Naibu Waziri na watendaji wote wa wizara hii.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze moja kwa moja kumpongeza Mhe. Mkuu wa Mkoa wangu wa Mjini Magharibi kwa kazi nzuri ambazo anazifanya hasa suala zima la kusimamia usalama katika mkoa wetu. Kwa kweli Mkoa wetu ulikuwa na mambo mengi ya kuhatarisha amani lakini tokea Uchaguzi Mkuu wa 2015 mpaka sasa ni Mkoa wa kupigiwa mfano kwa amani na utulivu. Kazi kubwa ambayo anaifanya Mhe. Mkuu wa Mkoa. Lakini pia kwa kusimamia suala zima la madawa ya kulevya.

Kwa kweli mko wetu ulikuwa mkoa kidogo unatisha vijana wetu wengi walikuwa wameshaathirika na madawa ya kulevya, lakini kwa mkakati alionao yeye na Kamati yake ya Ulinzi na Usalama wamefanya kazi nzuri na sasa hivi maeneo mengi ambayo yalikuwa hatarishi wameondoka wale wauzaji unga wadogo wadogo na sasa Serikali Kuu tusimamie wauzaji wakubwa wasiingie nao huo unga ili kuwaharibu vijana wetu. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ambalo nilitaka nilizungumzie ni suala zima la ukurasa wa 62 wa Vyuo vya Mafunzo. Mhe. Mwenyekiti, katika jimbo langu kuna askari wa Chuo cha Mafunzo cha Langoni na Kinu Moshi. Mwaka jana wakati wa bajeti kama hii nilisimama na nikasema askari wale sasa hivi wana hali ngumu sana pamoja na wale wanafunzi wa Chuo cha

Mafunzo kwa muda mrefu sasa hivi wanakaa na nyumba zilizokuwa haziko katika hali nzuri. Nyumba zile zimejengwa toka Ukoloni lakini sasa hivi nyumba zile zinavuja, bahati mbaya sana nyumba zile zote wanatumia mita moja ya umeme pamoja na kinu chao cha kusagia nafaka. Niliomba bajeti iliyopita kuwa tuwasaidie wale watu hali haiko vizuri. Kwa sababu sasa hivi inafika wakati mvua kama hizi za masika zinaponyesha wafanyakazi wanaokaa pale na wanafunzi wanaweka mabeseni kwenye vyumba ili kukinga maji ambayo yanamwagika kwenye vyumba vyao.

Nimuombe Mhe. Waziri atakapokuja atuahidi labda kwenda kuwatengenezea wale askari wetu pamoja na wale wanafunzi walio kwenye chuo kile waweze kuishi na wao kwa amani na utulivu pale inaponyeshaa mvua.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, ukurasa wa 63 ni Idara Maalum ya Kikosi cha KMKM. Nataka nichukuwe tena nafasi hii na leo kuwapongeza askari wa KMKM kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya lakini pia kuonesha uaminifu mkubwa sana kwa serikali. Wenzangu waliopita au kitabu hichi kinaonesha vitu ambavyo wamekamata katika doria zao, vitu hivi kama wangekuwa askari wale si waaminifu visingelikuwa leo vinasomeka hapa na fedha nyingi ambazo wameziokoa. Kwa hivyo, niwapongeze sana na nimtake tu Komodoo aongeze jitihada kuwafanya askari wake wawe watiifu ili wahakikishe wanaitendea haki Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, nichukuwe nafasi hii tena kumpongeza Kamanda kwa kazi nzuri ambayo anaifanya, kwenye madaktari wake wa kituo cha afya cha KMKM, kituo kile kinafanya kazi muda wote hata ukienda saa saba usiku saa nane za usiku unahudumiwa kwa wakati mzuri sana. Sasa niombe tu serikali tuliomba kuwa kituo kile wananchi hawapati dawa za bure, muda wote dawa wakienda pale lazima wanunue kituo cha KMKM na kituoa cha jeshi Bububu. Lakini nasikia tetesi tetesi sina uhakika kwa sasa hivi wataanza kupata mgao wa dawa kwenye vituo vile viwili. Kwa hivyo niombe Mhe. Waziri watakapokuja hapa atwambie kama kuanzia mwezi huu na wenzetu wa KMKM na wanajeshi wa JWTZ na wao watapata nafasi ya kupata dawa kwa ajili ya kuwapa wananchi wakwezi na wakulima bure na wao wapate.

Mhe Mwenyekiti, nikitoka hapo niende kuwapongeza Mhe. Mkuu wa Wilaya ya Magharibi A na Mhe. Meya wa Magharibi A na Mkurugezi pamoja na madiwani wote kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya katika manispaa yetu ya Magharibi A. Kwa kweli wanastahiki kupewa pongezi suala la usafi katika manispaa yetu liko vizuri suala la barabarani wako vizuri na niseme tu kwamba hapa kuna changamoto katika usafishaji wa maeneo haya ya suala zima la magari ambayo asubuhi Mhe. Shihata kalizungumzia.

Kwa kweli suala la magari imekuwa ni tatizo niiombe serikali ikiwezekana wawape ruzuku wanunue magari mapya kwa sababu Halmashauri au Manispaa kama manispaa wanatakiwa wanunue magari wao na wao hawana uwezo wa kununua magari mapya. Kwa hivyo, niombe serikali kwa kupitia bajeti hii wawapatie fedha ili wanunue gari jipya la kuweza kusaidia kuokota taka. Wananchi ambao wanalazisha taka kila mwezi wafanyabiashara na wengine hutakiwa walipe elfu sita lakini wakati mwengine inaweza ikafika wiki nzima taka hazijenda kuchukuliwa katika eneo lake. Kwa hivyo, inakua zile pesa tukuenda kuchukua kama tunawadhulumu hivi.

Kwa hivyo, niombe sana serikali iandae utaratibu mzuri wa kuhakikisha tunapata magari mapya ili manispaa zetu na halmashauri wafanye kazi vizuri.

Lakini Mhe Mwenyekiti, niwapongeze tena Waheshimiwa hawa kwa kusimamia vizuri suala la ugatuzi ndani ya manispaa yetu toka kumeelekezwa suala la ugatuzi tumepata faida nyingi. Mhe. Mwenyekiti na Mhe. Waziri nikwambie tu tayari manispaa ya magharibi A imeshajenga skuli ya Mbuzini, lakini imesaidia na skuli na Skuli ya Chuini, imesaidia na skuli ya Kizimbani na imesaidia na Skuli ya Mfenesini.

Pia imetia kifusi katika maeneo yangu ya Bububu lakini imewahi kupata nafasi ya kuchimba visima na bado inaendelea na shughuli mbali mbali. Nimpongeze tena Mwenyekiti na Mstahiki Meya pale na Mkurugenzi na Mkuu wa Wilaya kwa kutekeleza kwa haraka sana ahadi ya Mhe Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Katika ziara yake Mhe. Rais wananchi walitoa changamoto kwenye Mkoa wa Magharibi kwamba wana tatizo la soko katika Wilaya ya Magharibi A na Mhe. Rais akaagiza kama anataka utekelezaji mara moja aliagizwa Mkuu wa Mkoa.

Mhe. Mwenyekiti, na Mhe. Waziri nataka niseme Mhe. Mkurugenzi pamoja na na Mstahiki meya na Madiwani wake tayari wameshapitisha bajeti ya kujenga soko la chuini. Kwa hivyo niombe tu wale watu wa mipango miji wafanye haraka ili zile fedha zisije zikarudi tena. Mwaka jana tayari kulikua na bajeti ya kufanya kazi pale lakini mpaka mwaka mpya wa fedha umeingia zile fedha hazikupata nafasi ya kutumika. Kwa hivyo, niombe tu serikali ifanye haraka hasa watu wa mipango miji waweze kutukabidhi hiyo *site* ili wapate kufanya kazi.

Mheshimiwa katika manispaa hii bahati na mimi nilikua diwani wa muda mrefu pale kuna changamoto ya suala zima la ajira. Kuna vijana ambao wamefanya kazi pale kutoka mwaka 2000 mpaka 2018 hawaajiriwa na wanafanya kazi ngumu ambazo wanahatarisha hata afya zao. Sasa niiombe tu serikali sasa hivi inapofika wakati wa ajira huwa Tume ya Utumishi inatangaza nafasi na watu wanajaza lakini wale kwa sababu wanafanya kazi ngumu ya ukusanyaji wa taka katika maeneo mbali mbali na wameshachukua karibu miaka 18 ya kazi hiyo ya kujitolea niombe wapewe upendeleo maalum ili waweze kuajiriwa katika maeneo yao na wao wapate kujisikia katika nchi yao.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo niende suala la Magharib B Mhe. Mwenyekiti, Mkurugenzi wa Magharib B na yeye anajitahidi kufanya kazi lakini tatizo lake ni lile lile tu la ukosefu wa magari katika manispaa yake. Kwa hivyo, niombe serikali tena tu iandae utaratibu wa kuhakikisha kwamba na sisi tunapata gari kwenye manispaa hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, jengine suala zima la barabara za ndani, katika taarifa hii haikuonesha mwaka jana kama manispaa yetu ya magharibi B kuna kifungu au kuna eneo wamefanya kazi ya ujenzi ya barabara na sasa hivi ukienda kwenye barabara unaambiwa shughuli zote za ujenzi ziko manispaa. Kwa hivyo, nimuombe tu Mhe. Waziri atakapokuja aniambie kwa manispaa yangu ya magharibi A kwa mwaka huu inategemea kujenga barabara gani angalau wananchi nao wapate kufaidika na ujenzi wa barabara hizo.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo nilitaka nilisema ni suala la hospitali ya Mbuzini kwa muda mrefu sana hospitali ya Mbuzini nilikua nazungumza sana na Mhe. Waziri aliyepita kwa bahati nzuri sasa limefikia kwako Mhe. Waziri Haji Omar Kheir nikuombe sana na kwa unyenyekevu mkubwa ile ilikuwa ni ahadi ya Mhe. Rais, Mhe Rais aliwaahidi wananchi kwenye mkutano wa hadhara, kwa hivyo, niombe ulifatilie kwa karibu ili hospitali ile iweze kumalizwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwenye ugatuzi kuna suala zima la kilimo, naomba sana nimpongeze naibu Katibu Mkuu wa CCM Zanzibar alifanya ziara ya uzinduzi wa ukulima katika bonde la Kizimbani alizungumza na wakulima wengi na akawaahidi kuwanunulia (power tiller) moja kwaajili ya uchimbaji wa konde zao. Lakini pia nimpongeze Mhe. Makamu wa Rais wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan na yeye alikuja kwenye upandaji wa mpunga katika bonde la mpunga la Kizimbani alishirikiana na wananchi na baadae akawaahidi kuwapa trekta moja la kuchimbia.

Mhe. Mwenyekiti, kwenye mafanikio hakukosi changamoto niwapongeze tena Mhe. Waziri wa Kilimo lakini kwa sababu lipo kwenye ugatuzo na Mhe. Haji Omar Kheir nimpongeze, mara hii tumepata pembejeo kwa wakati nzuri sana lakini pia tumepata mbegu kwa wakati lakini ninaloliomba kwa kupitia kikao hichi mututafutie mabibi shamba na mabwana shamba wengi, kwa sababu linapotokea tatizo wale watatuzi wanakuwa ni kidogo sana kwa sababu mabibi shamba na mabwana shamba ni kidogo sana katika Wilaya yetu ya Magharibi A.

Mhe. Mwenyekiti, pia nilizungumzie suala zima la ofisi ya manispaa baada ya ugatuzi wafanyakazi wamekuwa wengi ofisi moja unaweza ukawakuta wafanyakazi karibu kumi. Manispaa yetu ya Magharibi A sasa hivi haina ofisi ambayo inamiliki wenyewe kama manispaa. Niombe Mhe. Waziri awatafutie kiwanja penginejapo kwenye eneo hilo la Chuini ambalo litakuwa karibu na watu wengi ili na Ofisi ya Manispaa ya Magharibi A nao wapate kujenga ofisi nzuri ya kisasa ambayo wafanyakazi wote watapata maeneo ya kukaa kwa salama na amani na kutekeleza vizuri majukumu yao.

Mwisho Mhe. Mwenyekiti naunga mkono bajeti hii ya Tawala za Mikoa na Serikali za mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa asilima mia moja.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Masoud, ndugu wajumbe naomba maongezi yake kwa sauti ya chini ili mchangiaji nae asikiie na Waziri ajue kitu gani kinazungumza kutokana na mchangiaji. Anaefuta ni Mhe. Nadir Abdul-latif na baadae Mhe. Mwanaasha ajitayarishe.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Bisimilah rahmani rahim, Mhe. Mwenyekiti, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uzima na pia nipo hapa katika kuchangia hutuba ya Waziri Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa kwa mwaka wa fedha 2018/2019 na mimi nitazungumza yangu kwa sababu pia ni mjumbe wa kamati sitofata kitabu hichi kwa sababu kitabu ninacho mwenyewe kichwani mwangu na najua mwenyewe nataka kuzungumza nini.

Mhe. Mwenyekiti mimi ningeomba nianze na suala la ajira, ningemuomba Mhe. Waziri ni vyema kwenye ajira za vikosi akashirikisha Waheshimiwa Wawakilishi zinapotaka kutolewa. Kwa sababu tuna vijana wetu wengi sana ambao wametumikia kwa muda mrefu wanafanyakazi kwa muda mrefu lakini zikifika siku za ajira hawajui waende wapi na sijui nani hasa

anaekabidhiwa mamlaka haya ya kuwapa ajira vijana hawa. Kwa sababu sisi kama wawakilishi ambao wananchi wetu wamo ndani hatupewi hata taarifa haya mambo yanaenda tu watu wanavotaka wao wananchi wanaopelekwa kule inaonekana watu wanapeleka kwenye kazi zile kwa watu wanaowataka wao wenyewe.

Tungeomba sisi wawakilishi wenye majimbo tushirikishwe kwenye suala hili angalau tukapeana mawazo tukajua basi nani anachukuliwa nani hachukuliwi, kwa sababu siku ya siku wananchi wanakuja kwetu sisi waheshimiwa Wawakilishi wa Majimbo, hili tatizo lipo kubwa hasa katika jimbo langu la Chaani vijana wangu wengi wanalalamika ajira zinapokuja Wilayani zinapekwenda sehemu nyenginezo hazijulikani wananchi wale wanapelekwa nani anachukuliwa nani anaachwa nani kila siku wanapigwa *date*, sasa ningekuomba Mhe Waziri suala hili uje utueleze tunapokuja kwenye majumuisho haya mambo ya ajira yako vipi kwa sababu wananchi wanalalamika kwamba kila siku wanapokwenda wanaambiwa kesho mara safari hii wameitwa wameambiwa nyie hamumo wapo watu wengine wa mjini sasa tungeomba nipate jawabu za suala hili.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, ningezungumzia suala soko la Kinyasini ambalo limejengwa hivi karibuni na Mhe. Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, wananchi ambao waliokuwepo mwanzo katika suala la Kinyasini, Mhe. Waziri ningekuomba kwamba wahakikishe kwamba wizara yako kupitia halmashauri kwamba wananchi wale wapewe *priority* ambayo waweze kutumia wao milango ile mwanzo na ikibakia ndio wapewe watu ambao wamepeleka maombi mengine. Vile vile ningependelea zaidi hata kiwango ambacho mtakuja kuwapangia muwapangie kiwango kwa mujibu wa hali yao kisije kikapangwa kiwango ambacho kitawashinda.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba zikibakia dakika tatu zangu za mwisho unijulishe ili nipate nizungumze mambo yangu machache ambayo mengine yatakuwemo, Mhe. Mwenyekiti nitaomba niongee na Mhe. Waziri hapa kwenye suala la maduka haya ambayo siku nyingi tunaongela mjini, tumezungumza kipindi kikubwa kwamba usiku tunakuta baadhi ya maduka yanawekwa usiku asubuhi yashaanza kazi hasa maeneo ya Mbweni, ukija maeneo mengine ya kwa Mchina na sehemu nyenginezo watu wanatengeneza mabanda watengeneza zege usiku wanakuja kushushwa maduka.

Haya maduka yataondoshwa lini ya kiholela kwa sababu maduka ya bei rahisi yapo yanaharibu hadhi na mji, yanachafua hali ya madhari vibali hivi anatoa nani ya kuruhusu hii milango hii vibanda hivi ambavyo havina hadhi. Lakini tukienda Mhe. Mwenyekiti, nimwambie Mhe. Waziri kuna siku walitoa ahadi pale Mlandege kwa ndugu yetu yule Anuwar Abdalla Juma kwamba sehemu ya *buffer zone* ile maduka hayaruhusiwi kuanzia *quality super market* mpaka *Muzamil center* watu wote wenye nyumba pale maeneo ya mbele ni yao. Kina maduka maeneo ya pale sheli yameanza kuja hivi karibu maduka nane yanajengwa kiholela.

Mhe. Waziri kipindi cha nyumba uliongea na unayajua haya mambo kama utayavunja kabla ya Ramadhani cha kushangaza kipindi kile yalikua yako makontena na sasa safari hii yatatiwa zege kabisa. Kibali kile Mhe. Waziri ukija unieleze kibali kile katoa nani cha kuwaruhusu wale watu kwenye *buffer zone* kujenga kwa zege na hatimiliki kama wanazo najua hawana na kama wanazo hatimiliki wamepewa na nani. Kwa sababu kila mwenye nyumba kule nyuma sehemu ya mbele

ni yake kwa mujibu wa sheria na sehemu ni ya *buffer zone* hawaruhusiwi watu eneo lile kujenga kama vile.

Mhe. Waziri mimi naenda kwenye suala ambalo tuliwahi kufanya kamati ziara bahati nzuri ulikuwa kama kawaida yako wewe ni Waziri anakuwepo Naibu Waziri tulitembelea sehemu ya Wahindu hapo kwa Mhe. Rais nyumbani kwake ngazi mia. Sehemu ile ni sehemu ambayo ya makaburi kwa mujibu wa sheria zao za kidini yao ndugu zetu Wahindu Zanzibar, watoto walioko chini ya miaka 18 wanazikwa pale lakini ambao wamefikia miaka 18 wanachomwa moto kwa mujibu wa itikadi zao za dini yao.

Tulikiwenda kipindi cha nyuma sisi na kamati na Mhe. Mkuu wa Wilaya na kamati nzima tukakuta maeneo yale watu wanafanya mambo machafu kwenye masuala yao ya kidini hivi leo sisi waislamu au ndugu zetu wa kikirsto watu wende kufanya masuala ya mapenzi au wakafanye uchafu wanye, wakojoe kwenye makaburi ya Mwanakwerekwe au ya wenzetu upande wa pili tutakubali.

Wenzetu tumekwenda tumekuta pale uchafu wa kinyesi kwenye maji yao ya kufanya ibada watu wamekojoa wamekunya Mkuu wa Wilaya shahidi, lakini cha kushangaza kwamba Mkoa na Wilaya wamekuwa ndio wa mwanzo kushadidia kwamba watu wazidi kupita mle, kufanya mazoezi na mambo mengineyo. Hata mimi sikatai watu kwenda kufanya mazoezi lakini ifanywe utaratibu tuwaheshimu wao japo kuwa *commute* yao wapo kidogo lakini tuwaheshimu.

Hata sisi waislamu tunaambiwa kila dini ikiwa ndogo ikiwa kubwa tuiheshimu. Kwa nini serikali kupitia Mkoa na Wilaya imekuwa inawapa baadhi ya vitisho sijui watahamishwa, sijui hivi haya mambo hayafai, halafu walipokuwa wakipigiwa simu hichi ndio ambacho kimeniudhi zaidi. Imetoka kauli kwenye simu kwa sababu wale vijana walipokuwa wakipiga simu wakasema mbona kamati imekuja hapa tumekubaliana vizuri kwamba tufunge mpaka yatoke maagizo. Jibu lililotoka kwamba wale Wawakilishi Mhe. Nadir na Mhe. Machano wale watoto wadogo tu wale Wawakilishi tu wale wenye mamlaka Mkoa.

Mimi niwambie sisi Wawakilishi tumechaguliwa na wananchi mimi kwa mujibu wa sheria kwa jina jengine mimi ni Rais wa Jimbo, nina wananchi zaidi ya elfu thalathani nyuma wananitegea kwa kuwaongelea Mkuu wa Mkoa Mkuu wa Wilaya umeteuliwa tu iko siku wewe utakuja kutolewa tu uwe na nidhamu haiwezekani unamjibu mtu ambae mtu wa kawaida kwamba eti Mwakilishi ni mtu wa kawaida.

Nani anaekupitishieni bajeti hapa Mhe. Waziri leo tukisema leo bajeti yako tuigomee huna cha kufanya. Tungeomba Wakuu wa Mikoa kama wale tunaowana upande wa pili na sehemu nyenginezo wapo Wakuu wa Mkoa na Wakuu wa Wilaya ambao wana nidhamu lakini wapo Wakuu Mikoa na Wakuu wa Wilaya ambao hawana nidhamu ningeomba sana kupitia Wizara yako wajue Waheshimiwa Wawakilishi ni nani kamati ndio iliyokwenda pale, pale hakwenda Nadir hakwenda mwenyekiti suala lile linapigiwa simu nasikia kwenye *loud speaker* Mhe. Waziri.(*makofi*)

Mhe. Waziri tunadharauliwa suala pale tunazungumza wazi pale Mhe. Rais nyumba yake hairuhusiwi watu kwenda kufanya mazoezi tumekuta wavuta unga ushahidi Mkuu wa Wilaya

yako muulize. Lakini wanaambiwa watavunjiwa sijui watahamishwa wale kwa mujibu wa warka zao tokea enzi izo zaidi ya miaka 120 wapo pale. Si tatizo kuhamishwa watahamishwa kwa mujibu wa sheria ikibidi lakini tusiwatishe kwa maneno kuona wako kidogo tukaendelea.

Mimi Mhe. Waziri nimesema nikwambie hivi kwa sababu haya masuala naona kuna baadhi ya wateuzi wanakuwa wana dharau sana kwa Waheshimiwa. Lakini wafahamu kwamba sisi tuna hadhi yetu na wao wana hadhi yao na tunaheshimu sana na tunamuheshimu sana Mhe. Rais lakini ikibidi tutawagonga. Kwa sababu hatuwezi mimi nasema siku zote Mhe. Rais wetu amekamilika kwa mujibu wa ubinadamu wake hakuna mkamilifu 100% isipokuwa Mwenyezi Mungu. Lakini ikibidi kwenye utendaji wake aliowateuwa wakiwa wanaenda kinyume kama hivyo hatutowaachilia sisi tunafahamu aliyekosa sio Mhe. Rais waliokosa ni wateuzi na hii inatokana kwamba sifa nyingi, sifa zikizidi mambo yanaharibika hatuwezi tukenda hivyo.(*makofi*)

Mhe. nazungumza hivi Mkoa sasa hivi wa Mjini hauna usalama, tuzungumze ukweli kipindi cha nyuma mwezi uliopita mimi nakaa hapa Mbweni nyumba kumi na tatu zimevamiwa. Wazungu wenyewe kwa wenyewe na mapanga zaidi ya nane kumi na tano ndani ya mwezi mmoja. Mhe. Waziri ukija utueleze kamati ya ulinzi na usalama ya Mkoa haifai haiwezekani nyumba ndani ya mwezi mmoja kumi na tatu zinaingiliwa. Watu wanapigwa wanaingiliwa na mapanga wanaekwa chini ya ulinzi halafu hatujui mpaka leo kakamtwa nani watu wametapeliwa wamenyang'anya pesa zao tumeona mpaka barua kutoka nchi za nje zinasema kwa *alert* kwa Zanzibar sasa hivi hali sio nzuri.

Halafu tunakuja hapa tunamsifu nani tusisifu kitu ambacho hakipo tunasifu Mkoa tunamsifu nani wakati Mkoa hauna usalama. Tuzungumze ukweli mimi nasema tena ulinzi hauko vizuri siku atakayokuja kuingia kwangu mwezi ambae anayejifanya wa nguo hatotoka, nasema kabisa kwa sababu tumeshaona ulinzi hakuna. Mimi nitatumia nguvu zangu ninazozijua mwenyewe ninazo, siwezi kumruhusu mtu kuingia katika nyumba yangu halafu tukachekeana chekeana tu tukategemea ulinzi huu mbovu.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Kamanda Hassan Nassir leo kazungumza kwamba kwa kupitia mkoa suala ambalo mtu akimkoholea mwanamke ana kosa atamuweka ndani, kwa sababu ya mabodi na mambo mengine. Mimi niseme wazi wanawake wa Zanzibar wana heshima zao hawawezi kuvaa nguo hizo tunazozizungumza, wanaovaa nguo hizo ni watalii na ndugu zetu wengine ambao *design* zao ni tofauti na sisi. Sasa kama mtu kukohoa ni wajibu wake kukohoa, umeshanifahamu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mimi nasema dhahiri mashehe watafumba macho watafumba macho watalaani, lakini sisi tuliokuwa sio mashehe tutakohoa tu kwa sababu mtu kavaa vibaya, hatuwezi tukenda. Mtu anataka ajiheshimu, iwekwe barua *Airport* kwa watalii kwamba sasa hivi ni mwezi mtukufu watu wavae vizuri, lakini mjini watu wanatembea na chupi tutafanya nini. Zamani Darajani mtu anapigwa mikwaju, na mimi ningeomba *design* ile iendelee, akipita mwanamke uchi apigwe mikwaju, hakuna cha kukohoa wala kukoholewa, kwa sababu hivi hatwendi. Leo unataka sheria hiyo, mtu akikoholewa kama mtu ana ugonjwa wa kifua je kakohoa mbele ya mwanamke itakuwaje. Hizi sheria nyengine ziangalieni, mtu anajitakia mwenyewe tena unataka nini. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mimi niende kwenye suala la, Mhe. Mwenyekiti, dakika zangu watu wanacheka ningeomba ziwekwe kwa sababu sipati kuongea. Mhe. Mwenyekiti, mimi naendelea na hawa watu wanaouza vitu vidogo vidogo, ningemuomba Mheshimiwa kupitia wizara yake Mhe. Haji Omar Kheir, hawa watu wa chini angalau wasitoleshwe kodi mtu hii kodi ya shilingi 500 au 1,000 itasaidia nini kwenye serikali, waachilie wanyonge wauze tu vitu vya shilingi 500 kodi ya shilingi 1,000 kwa siku wawasamehe, wawatafute wafanyabiashara waliokuwa na maduka wanajiweza wanaweza wakalipa kidogo na wasikomolewe, walipe kwa mujibu wa haki yao. Lakini hawa wauza mikate ya boflo, tungule sijui viazi wanatoleshwa kodi ya shilingi 500 au 1,000 ya nini mnawatilisha *headache*. Nchi yenyewe maskini tunazidisha umaskini, kwa wao shilingi 1,000 ni sawa sawa na shilingi 100,000 kwa mtu aliyekuwa mnyonge. Kwa hivyo, tungeomba hasa kwa wakati huu wa mwezi wa Ramadhani kodi ile isiwepo.

Mhe. Mwenyekiti, nizungumzie suala jengine kwenye wizara hii. Kuhusu suala la kulipishwa malipo ya maegesho. Mhe. Waziri shilingi 500 na shilingi 1,000 ni nyingi kwa nchi hii. Hapo Dubai, Oman na nchi nyengine za Ulaya unatoleshwa kwa saa nzima haifiki kiasi hicho, inakuwaje Zanzibar mtu anaweka gari anapewa eti saa moja kwa shilingi 500, au ukienda Forodhani shilingi 1,000 kwa saa moja. Mtu kwa siku kama mizunguko yake ya mjini analipa shilingi 8,000 au 10,000 kwa mshahara gani wa Zanzibar mtu akalipe maegesho ya gari shilingi 10,000. Wapo watu wenye gari hapa maskini, sio kwamba watu wana mishahara mikubwa, mtu gari lakini uwezo wake ni mdogo. Kwa hivyo, tungeomba kiwango cha hizi ada za maegesho iwe shilingi 200 au 250 tena iwe kwa masaa matatu sio saa moja, tuangalie na hali tusiangalie kwenye kuchuma tu, tuangalie na hali ya wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naendelea na mchango wangu kwenye masuala ya mabango machafu. Kuna mabango yaani nyumba imeshamaliza kujengwa serikali miaka 10 bado lile bango lipo sijui linawekwa *memory* au watu waone kama kulijengwa sijui na mtu fulani. Kwa hivyo, tungeomba mabango machafu yakaondoshwa kuna mabango siku hizi ya kisasa *digital*, kuna yale ambayo yakusimamisha masafi, ya nini tunatoa mabango machafu kila kona mabango hayeshi na tumeshayazungumza sana lakini bado mabango yale yapo, mabango miaka 10 nyuma yameshamaliza kujengwa watu wameweka *show* tu yanaonekana.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, naomba zikikaribia dakika zangu tatu au tano uniambie kabla. Kuhusu taa za barabarani, Mhe. Mwenyekiti, *Airport* ni barabara ambayo ni muhimu na ni njia kubwa, taa za barabarani hadi hii leo hakuna kiza aibu na ndio njia ya mwanzo tu mtu akifika Zanzibar kutoka Uwanja wa Ndege anapita njia ile. Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri aje atuambie ana mpango gani wa kutia taa kwenye njia ile tena kwa njia nzuri, hili tunaliangalia vipi.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye suala jengine ambalo nataka kuzungumza suala la wizara kwa jumla, mimi nimeongea machache ambayo Mhe. Waziri ameyafahamu, nimshukuru sana Mhe. Waziri kwa kupitia wizara yako nzima kwa kuweza kushirikiana vizuri na kamati yetu kwa njia ya heshima kabisa kama nilivyoeleza. Katika wizara haiwezi kuwa imekamilika kwa asilimia 100 kwamba ni watiifu, lazima wapo waliotukosea na wapo tuliowakosea sisi na lazima wapo waliokwenda vizuri na sisi.

Mhe. Waziri, kwa kupitia Mhe. Naibu Waziri wako, viongozi wako wote na makamanda mlikuwa na nidhamu ya hali ya juu katika kutukaribisha kwenye kamati, tunachohitaji mnatuonesha na ambacho tunataka kuuliza mmekuwa mkitupa mstari wa mbele kwenye masuala hayo. Kwa suala hili lazima tuwe wawazi na tuwe wakweli kwa watu wanapofanya vizuri. Mimi nikiwa mjumbe wa kamati hii naweza kusema nakuageni rasmi siwezi kujua kwenye kamati hii nitarudi au sirudi. Lakini mimi mchango wangu wa mwisho kwenye kamati hii nikiwa mjumbe wa kamati nakupongezeni sana, lakini pia bila ya kumsahau Mhe. Mwenyekiti wangu, Makamu Mwenyekiti na wajumbe wote ambao tumefanyakazi kwa pamoja, nakushukuruni sana tumefanyakazi vizuri.

Kwa hivyo, niwaambie tu ndugu zangu katika wizara hii, tumefanya kazi zetu kwa uadilifu hatujampendelea mtu na ndio maana hapa ukakuta tunasifu lakini tunampiga mtu anapokosea, ndio kwenye sehemu yetu ya kuongea. Wale waliokuwa wamenuna waendelee kununa, mimi simpapatikii mtu kwa sababu nafanya kazi yangu, waliokwenda kuona sisi tumefanyakazi wafahamu kwamba tumefanyakazi kwa mujibu wa sheria na tuliokaa nao vizuri tutazidi kukaa nao vizuri. Mhe. Waziri, Mhe. Naibu Waziri, na watendaji wengi wako wewe tuko vizuri, tunawaheshimuni sana. Lakini tunapokuja kwenye kukugongeni tunataka mkasimamie wale ambao wanaharibu katika kupitia wizara.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ni mjumbe wa kamati sijataka niongee leo na nimeongea kidogo tu bado nimeheshimu kwa sababu ni mjumbe wa kamati. Kwa hivyo, nitai-*support* kwa asilimia 99.909, yaani ile 01 mimi ndio nataka uje unijibu yale majibu yangu kwa sababu wananchi wangu wananilalamikia mambo ambayo yaliyozungumzwa yana tuudhi na mambo ya dharau tuliyoyazungumza angalau tuje tupate jibu na masuala ya ulinzi na usalama.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo mimi nimeshataja zile asilimia zangu 99.909 hiyo 0.1 nitakuja kuisubiri hapo mbele. Nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wenzangu waunge mkono hotuba hii ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwanaasha Khamis Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi hii na pia nikupongeze kuwa mchangiaji wa mwanzo wa hotuba hii mwanamke kwa siku ya leo basi nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuipongeza sana wizara hii pamoja na watendaji wote akiwemo waziri katika wizara hii kwa kazi kubwa ambazo wanazifanya. Mhe. Mwenyekiti, mimi nitakuwa na michango sio mingi sana, lakini kidogo nitaanza kugusia katika kitabu cha Mhe. Waziri cha hotuba yake kwenye Idara ya Uratibu wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Mhe. Mwenyekiti, katika hili nadhani tulitunga sheria hapa namba 7 ya mwaka 2014 ambayo ni sheria ya Serikali za Mitaa, kwa hivyo hizi Serikali za Mitaa zipo kisheria. Nashukuru Mhe. Waziri kwa ujumla wake tayari zipo zile kanuni ambazo zitaongoza sheria hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, lakini cha kusikitisha mpaka hivi sasa wajumbe wenzangu wengi wamechangia, lakini nimuombe tu Mhe. Waziri aweze kuliona hili na kama hajalijua, lakini bado katika Mabaraza yetu ya Manispaa zile *by-law* hazipo. Nasema hivi kwa sababu hawawezi kufanyakazi zao kwa ufanisi kama hizi sheria ndogo ndogo hazipo. Mhe. Mwenyekiti, katika

Serikali za Mitaa ili zifanye kazi zao vizuri na watendaji wake, lazima sheria ndogo ziwepo na ndipo watakapofanya kazi zao kwa ufanisi.

Mhe. Mwenyekiti, suala la pili nilitaka niseme pia katika hizi Serikali za Mitaa Mhe. Waziri wa Serikali za Mitaa waongezewe fedha na kupatiwa hizo fedha kwa wakati. Tumeshuhudia na tumeona kuwa Serikali hizi za Mitaa zinafanya kazi, hasa katika masuala ya ugatuzi pia wanafanya kazi vizuri na wamejitahidi, ambapo kipindi cha mwanzo katika hivi vituo vya afya na skuli hizi za maandalizi na msingi kulikuwa na changamoto kubwa kabla ya ugatuzi, lakini sasa hivi wanajitahidi kutatua yale matatizo madogo madogo ambayo yanawakabili katika maeneo yale.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri katika huo Uratibu wa Serikali za Mitaa nimeona katika ukurasa wa 11 na kwenye 26 na 30 wameonesha ule utekelezaji wao na mikakati yao. Lakini niwakumbushe pia waweze kuwapa mafunzo, kupata mafunzo wale watu wetu wapate wataalamu kwanza wa fedha, wapate wataalamu wa mipango, lakini pia wapate wataalamu washauri au wanasheria pamoja na wahandisi katika hizi Serikali za Mitaa. Kwa nini Mhe. Mwenyekiti, nasema hivi. Sasa hivi ni ugatuzi, majukumu mengi tayari ziko kwenye Serikali za Mitaa, kama watakosa wataalamu hawa sifikirii kama tutafikia yale malengo ambayo tumeyakusudia.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, nimuombe sana Mhe. Waziri, katika kuratibu kwao hili pia walione na walichukuwe walifanyie kazi, ili tuone kwamba wale watu wetu katika Serikali za Mitaa basi waweze kufanyakazi zao kwa ufanisi.

Mhe. Mwenyekiti, lakini la tatu hapo hapo katika huo uratibu. Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa namuomba sana Mhe. Waziri wawawezeshe madiwani wetu, suala la ugatuzi linawahusu pia madiwani na wao ndio wasimamizi wakuu katika masuala yale. Kwa hivyo, naomba sana maeneo yamezidi katika ufuatiliaji. Namuomba sana Mhe. Waziri awaangalie madiwani wetu kwa jicho la huruma kwenye maslahi yao, lakini pia wawapatie usafiri.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, naomba sana madiwani wapewe mafunzo katika nchi tofauti ikiwezekana kwa suala la ugatuzi. Mhe. Mwenyekiti, hawa madiwani pia namuomba Mhe. Waziri sheria hii ipo ya Serikali za Mitaa, lakini watendaji wetu au madiwani wetu hawaijui kutokana na ile lugha sio wengi wanaoweza kuijua ile sheria. Kwa hivyo, naomba itafsiriwe au iwe na lugha nyepesi ambayo madiwani wetu ile sheria au watendaji wanaweza wakaifanyia kazi na wakajua ni kitu gani kinachotakiwa kwao wao, ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa usahihi. Kwa hivyo, nimuombe sana Mhe. Waziri hili alichukuwe katika kuratibu kwao wawaone hawa watendaji wetu waweze kufanyakazi.

Mhe. Mwenyekiti, pia twende kwa hawa watendaji hasa tukiwacha mbali hawa madiwani. Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri watendaji hasa wapewe mafunzo ya kazi, yaani *customer care*, ili waweze wale watendaji wetu wanapokwenda pengine katika kudai mapato au kodi mbali mbali, waweze kuwa na zile lugha ambazo zitawashawishi wale wafanyabiashara au watozwa kodi kushawishika katika kutoa kodi ili tuongeze mapato katika serikali yetu.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri wawe na usalama wale watendaji wetu. Mhe. Mwenyekiti, watendaji wanahangaika katika maeneo tofauti lakini usalama wao ni mdogo na chochote kinaweza kutokea kwao wao, kwa hivyo waangalie hilo la usalama wao.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye programu ya Idara Maalum. Mhe. Mwenyekiti, niipongeze wizara hii pamoja na waziri katika programu hii ya Idara Maalum. Lakini dogo nataka nichangie katika hili Jeshi la Kujenga Uchumi na nataka ninukuu katika kiambatanisho cha ukurasa wa 33 kuanzia kiambatanisho namba 3.
Mhe. Mwenyekiti, katika ukurasa huu wa 83 katika kiambatanisho namba 4a na kifungu cha d 02 Jeshi la Kujenga Uchumi, kama nitakuwa niko sahihi Jeshi la Kujenga Uchumi tayari linajenga uchumi na uchumi sote tunajua tafsiri yake ikoje.

Mhe. Mwenyekiti, katika makadirio na makusanyo kwa mwaka 2017/2018 nimeona kuwa kuna mapato ya mazao ambayo yalikadiriwa shilingi milioni 37 na makadirio ya makusanyo Julai 2017 yalikuwa ni milioni 37 na makusanyo halisi ilikuwa ni milioni 21. Kwa hivyo, niwapongeze kwa kiasi fulani wamevuka malengo kwa sababu wamefikia ile nusu ya asilimia.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye mapato ya mifugo. Pia katika mapato ya mifugo inawezekana labda, sio inawezekana ndivyo ilivyo kwa sababu katika kipindi kilichopita kwenye maonesho niliwaona hawa wa JKU wanafuga wanyama, kama kuku na ng'ombe. Lakini kwa mujibu wa hii takwimu hapa na hali halisi kidogo hairidhishi, labda kutakuwa kuna changamoto na kama kuna changamoto basi namuomba Mhe. Waziri azifuatilie ili tuone yale makusanyo yanafikia malengo.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika mapato ya wanafunzi naona wamefikia kiwango inapendeza. Lakini nije kwenye mapato ya bidhaa za thamani. Mhe. Mwenyekiti, labda Mhe. Waziri aje anieleze kwa nini labda makadirio na makusanyo haya ya Julai/Machi 2018 pana ziro. Kwa maana hiyo hakuna thamani zilizouzwa au hakuna kitu chochote kilichofanyika, kwa nini iwe hivyo. Niseme tu kwa bahati nzuri mimi nilikwenda katika yale maonesho na niliwakuta hawa watu wa JKU wana *furniture* nzuri sana, na wametengeneza vitu vingi tu vizuri sana, lakini matokeo yake inawezekana labda hawajapata ule ununuzi au havijanunuliwa. Niseme kwamba Mhe. Waziri inawezekana hata ile sadaka huanzia nyumbani basi pia haijafika kwa misingi hii, kwa nini.

Mhe. Mwenyekiti, tuna ofisi nyingi hususan kwenye wizara yake, sifikirii kama zile bidhaa ambazo hawa watu wa JKU au zile thamani kama zipo au wamezinunua, ndio maana nikasema hizi sadaka zinaanzia nyumbani. Sasa Mhe. Waziri atakapokuja anipe tu ufafanuzi, sasa kama ni hivyo ninavyofikiria basi ipo haja kujirekebisha ili yale mapato yaongezeke hapa, hata tukienda maofisini badala ya zile bidhaa za Kichina basi ziwe za kwetu. Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri atakapokuja labda anipe ufafanuzi wa suala hili, kwa nini hapa haya mapato hayajaongezeka na wakati vile vitu vipo na nimeviona na nimevishuhudia kwa macho yangu.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri awawezeshe au awawekee sehemu yatolewe matangazo tofauti, kwa sababu nimeona katika hii hapa kuna ada ya ulinzi na ada ya ulinzi wamefikia makusanyo ya mwaka 2017 karibu milioni 24. Lakini hapo hapo makadirio yalikuwa 18, kwenye makusanyo halisi wamepata 15, Mhe. Mwenyekiti, hii ni hatua nzuri na kwa nini,

kwa sababu wamejitangaza na wamejitangaza tumeona mpaka kwenye vyombo vya habari tunaona kuwa kumbe kuna ulinzi ndani ya JKU, kwa nini mambo ya thamani yasitangazwe, yasiweke wazi, kwa nini wasijenge maeneo ambayo yakafanya wale watu au hawa JKU na zile bidhaa zao.

Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri atakapokuja anitolee ufafanuzi kuhusiana na haya kwa nia ya kujenga, kwa sababu ni Jeshi la Kujenga Uchumi na ili uchumi wetu ukuwe basi kuna vitu tuvizingatie, lakini sio kukua tu hili. Jeshi la Kujenga Uchumi tuna vijana wengi ambao wanatoka katika maeneo tofauti tofauti wanakuwepo pale, wanapata mafunzo na wanapata kila kitu wanaondoka pale na ujuzi tofauti. Lakini kama tutawajengea mazingira yaliyokuwa bora basi ule uhalali wa vijana wetu wa kusema hawana ajira hakuna kazi, kwa kupitia hili Jeshi la Kujenga Uchumi basi kila kitu ina imani kitakwenda vizuri na wale vijana wetu wanaweza wakafika pahala lile kero la serikali haiwaajiri ikaondoka, kwa sababu watapata ajira wenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa na hayo. Lakini mwisho kabisa katika mchango wangu pia nataka nitowe pongezi katika hii Kamati ya Ulinzi na Usalama, ikiongozwa na Mwenyekiti, ambaye ni Mkuu wa Mkoa wa Mjini kwa upande wa mwengine. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, hii kamati inafanya kazi tena inafanyakazi kwa uadilifu, na lengo lake kubwa ni kuona hali ya usalama lakini pia na masuala ya udhalilishaji ya wanawake na watoto kwa maana hiyo kwa vile inafanyakazi vizuri basi niombe serikali pia ichukue juhudi za makusudi kufatilia na kuwa nao karibu katika vile vile vitengo vyao tafauti vya usalama ambavyo wanavyo kuhusiana na suala zima hasa la madawa ya kulevya kwasababu kwenye madawa ya kulevya tayari tunaona tunawapoteza vijana wengi wengi ambao ndio nguvu kazi. Kwa kiasi kikubwa, niipongeze sana serikali kwa jihada zao, kwa kiasi kikubwa ule uingizaji au madawa kutumiwa kiholela kama ilivyokuwa awali kwa kiasi fulani wamefanikiwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo niwaombe jitihada ziongezeke na ziongezeke huwezi kufanyakazi katika vitengo kama hatuna nyenzo za kufanyia kazi, waangalie vile vitengo vyote vinavyowakabili, au wanavyohusiana navyo katika ulinzi na usalama na hali ya nchi yetu, basi wazitazame zile changamoto zinazowakabili zikiwemo hao, kamati za ulinzi na usalama. Kwahivyo najua kuna Nyanja tofauti tofauti katika ulinzi na usalama.
Mhe. Mwenyekiti, Kwa hivyo yale mambo yanaweza kuleta changamoto yakaweza kuathiri kazi zao, niombe sana Wizara na Serikali kwa ujumla wawaangalie watu hao wafanyekazi kwa bidii.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho kabisa mimi nilikuwa na hayo tu machache ya kuongea na mpongeza sana Mhe. Waziri na watendaji wake wote wa serikali pamoja na Mhe. Rais kwa jitihada zao zote wanazozichukua ili kuona nchi yetu inaendelea na inaleta mafanikio.

Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia. Nakushukuru sana.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana kwa mchango wako. Sasa nnamwita Mhe. Salum Mohammed Simai na akifuatiwa na Mhe. Abdalla Ali Kombo.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Mwenyekiti, kwa faida ya *hansard* naomba nirudie jina langu ni Simai Mohammed Said, naomba unite tena ili tuweke sawa *record*. Naomba unite tena.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe Simai Mohammed Said.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Mwenyekiti, Ahsante sana, nakushukuru sana kwa nafasi uliyonipa. Nianze kwa kumtanguliza kumshukuru Mwenyezi Mungu, yeye ndie alotuumba sisi sote binaadamu na viumbe vyote tuliokuwa hai na huku tukiendea na mwezi mtukufu wa Ramadhani basi nitangulize maneno mazuri kuwatakia wanzanzibari wote na watanzania wenzetu mwezi mtukufu mwema wa Ramadhan nasema Ramadhan Karim. Lakini pia nichukue nafasi hii kwa kuniona na nimshukuru Mhe. Waziri kwa kuniona na nimshukuru Mhe. Waziri kwa hotuba yake alivyoisoma vizuri pamoja na Mwenyekiti wa Kamati husika na niwapongeze wajumbe wote wa Baraza hili la Wawakilishi waliohusika katika kamati hii.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kabla sijaanza kutoa mchango wangu naomba nichukue nafasi hii kutoa shukurani za pekee kwa wakuu wa Mikoa wote wa Unguja na Pemba, pamoja na halmashauri na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mchango wao na kwa umoja wao walioutoa wakati wa wapiganaji wetu walipofariki kule DRC na walipoletwa zile maiti zao huku Zanzibar kwa ajili ya kupekwa katika nyumba zao au kwa ajili ya maziko, basi na mimi pia nilipata nafasi ya kushiriki katika Mkoa wa kusini niliona mashirikiano mazuri ya viongozi wetu wa SMZ pamoja na wakuu wa Mikoa na Halmashauri zetu. Kwahivyo nawashukuru sana na tunawapongeza wote wapiganaji kwa umoja wao ule ni mfano mzuri na inshaalla Mwenyezi Mungu atawalinda wale waliotangulia mbele ya haki. Nasema *" Inna lillahi wa inna ilayhi rajiiun".*

Mhe. Mwenyekiti, Eee, nitaanza na maneno mawili matatu lakini nikuombe tu Mwenyekiti kwamba hali yangu sio nzuri nakohoa kohoa, kwahiyo nikikohoa sia nia mbaya yoyote utambue kuwa naumwa na kifua.

Mhe. Mwenyekiti, nitaanza kwa upande wa bajeti Mkoa wa Kusini, kwanza nimpongeze sana Mhe. Waziri, ukiangalia katika mwaka jana bajeti iliyoidhinishwa ya billion 4, million 191 na million 800 ambayo ameipata kwa uhakika na imeingia vizuri kama alivyoonesha katika buku lake ambalo sawasawa na asilimia 91 ya bajeti yote. Lakini pia ukiangalia katika fungu hilo hilo aliingiziwa pia katika fedha ambazo zilizoingizwa ni billioni 2, millioni 546, laki 8 na elfu 41 na ushei. Lakini ukiangalia katika fedha hizo shilingi billion 1, million 322, sawasawa na asilimia 65 ilikuwa ni mishahara. Na katika billion 1, million 224, laki 475, elfu na ushei kidogo zilikuwa katika matumizi mengineyo.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nataka niseme vitu viwili au vitatu, moja katika suala la bajeti nzima ukiangalia kwa upande wetu, ukiangalia hizi nchi za nje ambazo zimeendelea kwenye Halmashauri au kwenye Wizara kama hii mara nyingi suala inakuwa sio bajeti, suala inakuwa sio fedha, au uhaba, au fedha ambazo zinazopatikana katika Wizara. Inakuwa wakati mwengine kwamba matumizi ambayo umejipangia jee unaweza ukayafanya au ukaweza kuyafikia yale malengo yako. Lakini ukiangalia wizara hii ilivyo tunahitaji ubunifu na tunahitaji mapinduzi ya kifikra ili kuhakikisha kama hasa katika maeneo tofauti tunakuwa tunaweza kuyakamilisha.
Mhe. Mwenyekiti kwa mfano tuliongelea barabara ya Mpendae ya kutoka Kiembe Samaki mpaka uwanja wa *round-about* Mwanakwerekwe, tukazungumza umuhimu wa mwaka jana jinsi ya viongozi wanaopita na wananchi na maduka yalivyoshamiri katika maeneo yale, lakini waziri akatuahidi kwamba patabadilishwa mazingira yake yataboreshwa kuna mpango maalum.

Mhe. Mwenyekiti, Naibu Waziri pia katika anajibu masuali na majibu akanihakikishia lakini nafikiria mpango huu, unaposema mpango utakuwa uko njiani, na kuwa nashindwa kufahamu ni muda gani unachukua mpango huu kwanini mazingira haya tunaposema yaboreshwe tunakuwa tunapewa lugha ambayo jee, inakuwa ni ya kisiasa, au ni ahadi, hasa mimi nitafurahi sana atakapokuja Mhe. Waziri maana nipate kufahamu kwasababu nisitumie nguvu nyingi za kutoa mawazo na fikira kuishauri wizara alafu inakuwa napewa majibu ikafika pahala nikaona kama naondolewa njiani.

Mhe. Mwenyekiti, la pili nataka nizungumze kuhusu halmashauri yetu ya wilaya ya Kati, Mkoa wa Kusini ambayo pia ni jimbo langu la Tunguu lipo uko uko, moja katika kazi ambayo tunasimamia sisi tunaangalia katika uhaba au zote njia za fedha ambazo tulizokuwa tunazo kwamba ukiangalia pengine katika manispaa za mjini na maeneo mengine wana nafasi nzuri sana ya kutoza kodi na kupata fedha. Lakini kwa upande wa Wilaya ya kati na mazingira yetu tuliyokuwa tunayo, bado biashara nyingi ambazo zinatumika bado hazijashamiri kwa upande ule kule hasa katika sekta ya utalii na mengineyo. Kwahivyo bado tunatumia rasilimali ya nchi pamoja na ukanda wa Chwaka, Pongwe, na Uroa katika kidogo tunazo hoteli ambazo zimeanzwa kujengwa tofauti. Mhe. Mwenyekiti, sasa tunapopitisha bajeti katika halmashauri yetu bado ukiangalia katika utendaji na zile ahadi ambazo zinakuwa zinapangwa panakuwa bado pana uzito.

Mhe. Mwenyekiti, mfano barabara ya kutoka Jumbi kupanda juu kwendea Jumbi sekondari kwendea juu. Bado ile barabara ilipangiwa bajeti tena fedha ndogo kabisa na madiwani wetu na nilipewa taarifa lakini ukiangalia barabara mpaka leo za ndani hazijafanywa hazijatengenezwa na nilizungumza juzi katika kipindi cha masuala na majibu, umuhimu wa barabara za ndani, *unfortunately* au kwa bahati mbaya Mhe. waziri alipokuwa anajibu katika kipindi cha masuala na majibu alisema tunangalie mfuko wa maendeleo ambao tunautumia sisi wajumbe wa Baraza la wawakilishi ili kuboresha barabara za ndani.

Mhe. Mwenyekiti, Serikali hii ya Mapinduzi ya Zanzibar inakopa fedha kwa ajili ya kuendeleza barabara, hivi leo mfuko wa maendeleo wa Wawakilishi utaweza kuboresha barabara za ndani kweli na fedha zenyewe Mwenyekiti unazifahamu kwa sababu wewe pia ni mmoja wao wawakilishi wa kutegemea fedha hizi. Sasa tuwe wa kweli barabara za ndani tulizojenga kwa upande wa Tunguu tukubali kwamba wananchi tumewalazimisha, tumewafanya wende wakajenge kwa haraka wameweka fedha zao lakini sasa hivi hizi njia kwa kweli hazifai na tuna viongozi kabisa wengi wanaokaa katika maeneo haya unaambiwa hakuna bajeti, bajeti nitafute wapi mie, nitazipatia wapi. Wananchi wanatulaumu kesho kuwa tunakwenda 2020 na tuliwahidi kwamba wale wote watakaojenga kule kote tutaboresha njia zao.

Mhe. Mwenyekiti, ni sahihi sisi tupo tayari katika kueleza maeneo haya lakini ninachoomba Waziri ujitahidi sana kutumia njia za ubunifu basi angalau Mkoa Kusini katika maeneo kama haya halmashauri zetu ziko *weak* katika kutafuta fedha au katika mfumo mzima wa kupokea kodi, basi angalau tuongee na Mhe. Rais au Makamu wa Pili wa Rais tutafute mpango maalum kuboresha maeneo haya. Kwasababu wananchi wameitikia kile kilio kwamba twendeni tuungane mkono kujenga Jumbi na Tunguu Mji mpya, leo nyumba zinajengwa lakini barabara haziendani, lazima nyumba zilizojengwa katika maeneo ya Tunguu na Jumbi, mimi naitaTunguu mji mpya

naamini humu ndani sheria inaniruhusu pamoja na Jumbi mji mpya na *inshaallah* Mwenyezi Mungu akitujaaliwa iko siku waziri pamoja na Mkuu wa Mkoa atatangaza kwamba maeneo yale yanaitwa Tunguu-mji mpya, sio tena Jumbi –jaani, na Jumbi-mji mpya. Sasa mimi niombe tu basi kwamba tujenge, zile nyumba zilizojengwa maeneo ya Tunguu na Jumbi na zile barabara za ndani ziende sambasamba na maeneo yale yalivyo tuyaboreshe. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia ukenda katika upande wa JKU mwaka jana na mwaka juzi 2016/2017 nimezungumza, 2017/2018 nikachangia tena ukienda katika buku lako mwenyewe kwenye ukurasa wa (d)(1) unasema juu ya changamoto, changamoto na utatuzi wake, unasema JKU changamoto yake ni ukosefu wa miundombinu na uzalishaji katika mashamba ya viwanda lakini hapo hapo unasema kuwepo kwa uhaba wa wataalamu wa fani mbali mbali kama uzalishaji mali na walimu wa sayansi na ufundi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sioni hii ni kama changamoto moja, ya sifa ya wizara hii ambayo waliokuwa nayo ambao wengi hawana, wanarasilimali watu, unapokuwa na *labour* ina maana tayari wewe unaweza kufunga mkataba ili kuweza kuzalisha na nchi yoyote au pengine na kampuni yoyote. Nilitoa mawazo hapa kwamba mfano katika maeneo ya *furniture* tunaweza tukafungua viwanda vyetu vya *furniture* ili JKU hawa wakaingia mikataba na kampuni za kichina tukaweza kuingia katika soko la Afrika Mashariki. Lakini katika soko la wazanzibari kuwasaidia katika huduma, sasa haya unakuwa hupati majibu lakini tunatumia nguvu nyingi sana sisi Wajumbe wako wa Baraza la Wawakilishi kubuni mawazo kama haya kuyaleta.

Mhe. Mwenyekiti, sasa mimi naomba sana bora nipewe jibu kwamba kama haya mawazo ya fikra mbadala ili kuweza kuishauri Serikali tujibiwe tuseme tumeyapokea halafu tunayafanyia kazi halafu tupewe majibu. Sio panakuwa tumeyapokea na tutayafanyia kazi halafu hatupati jibu lolote, na mimi kwa uwezo wangu sina njia ya kuweza kuwasaidia JKU isipokuwa waingie mikataba kwasababu wao wana watu lakini ubunifu waliokuwa nao inawezekana kwamba uwezo wao waliokuwa nao wanahitaji waungane na nguvu ya mtu mwengine. Wachina, Wamalaysia, watu wa kutoka Korea ya Kusini, wana mawazo mingi sana katika mipango kama hiyo wamejiendeleza wao. Kwahivyo naamini mambo kama haya wakiingia, yataweza kuwasaidia.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia nataka niongelee suala la ulinzi na usalama katika nchi yetu. Mhe. Mwenyekiti, ukienda katika buku hili, ukisoma namba. (d) (ii) inasema kazi moja ya vikosi vyetu kama mfano JKU, ni kushirikiana na JWTZ pale inapohitajika kwa ajili ya ulinzi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Lakini (b)(c) kushirikiana na Jeshi la Polisi katika kudumisha amani na utulivu iwapo itaombwa kufanya hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, suala la ulinzi na usalama upo chini ya Polisi wetu na naamini vikosi vyetu pale wanapohitajika wanashirikiana. Lakini niombe pale ambapo nchi ipo salama imetulia haya mambo ambayo yakupita pita maeneo kuwatandika watu makwaju, na kuwafanyia vitu ambavyo havistahiki sijui anaefanya ni nani. Sinyooshei mkono lakini hisia za wananchi zinawaelekeza huko vyombo vyetu vinatumika vibaya wakati mwengine.

Mhe. Mwenyekiti, kwahivyo mimi naamini Mhe. Waziri kama kuna kasoro hizi kama kuna mtu yoyote ambayeikiwa si Mkuu wa Mkoa, ametoa agizo, au mkuu wa Wilaya, au mtu yoyote ambaye ndani ya kikosi, ambae yeye anajiamini kule anapeleka watu ambao wanatumia uniform

zetu basi ihakikishwe hili jambo sio kweli. Kwasababu polisi wanakataa lakini wananchi kama karibuni walivyoingiliwa maeneo ya Chukwani kwa kweli ni aibu kitendo ambacho cha akinamama kimewafikia ni udhalimu, ukatili wa hali ya juu kuwafanyia wale wasichana mambo kama yale, na ukenda katika katiba yetu ukisoma kifungu namba 23 kinasema kwamba kila mtu ana wajibu wa kufuata na kutii katiba hii na sheria ya Zanzibar na kuchukua hatua za kisheria kama zilivowekwa na Ofisi ya hifadhi ya Katiba hii na Sheria hii, lakini ukisoma kifungu cha 24 inasema haki na uhuru wa binaadamu ambao ni misingi yake imeorodheshwa katika katiba hii haitatumiwa na mtu mmoja kwa namna ambayo itasabishwa kuingiliwa kati, au kukatizwa kwa haki na uhuru wa mtu mwengine kwa maslahi ya Umma inaweza kubanwa na sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi, sisi ndio tunotunga sheria hizi hapa hatujampa mtu yoyote sheria ya kwenda kuwabana kama kuna mtu amekosea tunazo mahkama zetu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niombe sana amani tuliyokuwa nayo tusiichezee, wananchi wetu waendelee kulindwa vizuri. Mtu yoyote kama anajaribu kutia dosari katika vikosi vyetu basi tuhakikishe kwamba hili jambo na zitoke *statement* ikiwa siyo kama vikosi vyetu vinahusika basi wananchi wapewe taarifa, kwasababu huo ni unyonge na maneno yaliyokuwa chini kwa chini hayapendezi kwetu sisi kama wajumbe Wa Baraza la Wawakilishi, na sisi ndio wawakilishi wa wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, kwahivyo mimi naomba Mhe. Waziri mikwaju wananchi kuonewa onewa yaishe, ikiwa nchi yetu hatuko katika kipindi cha uchaguzi tunajua wakati taa ni nyekundu kila mwananchi mtu tunajua kipindi cha uchaguzi wale wadhalimu watu wabaya wanakuwa wanapenda kuchukua nafasi kama hizo ili kufanya mambo yaliyokuwa hayastahiki lakini pia

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. muda wako umemaliza.

Mhe. Simai Mohammed Simai: Mhe.Mwenyekiti bado dakika 3 tu naangalia nilikuwa naangalia saa tu hapa.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. muda wako umemaliza nakupa dakika 2.

Mhe. Simai Mohammed Simai: Ahsante Mhe.Mwenyekiti namalizia hizo dakika 3. Mhe. Mwenyekiti, lakini ukiangalia katika upande wa zimamoto nimeangalia katika kitabu chao, wananchi ambao wameokolewa ni 32 wale waliofariki ni watu 16. Lakini pia ukiangalia katika matukio ambayo yametokezea katika kuungua nyumba na majengo ya Taasisi kuna idadi ya nyumba 103, ajali ya ndege ndogo zilikuwa 5, moto wa sheli zilikuwa 4, lakini kwa kweli kwa takwimu hizo mlizoziweka na kama ni sahihi mimi ninawapongeza sana kwa upande wao kwa kazi nzuri na waendelee kutuletea taarifa kama hizi ili pale inapohitajika fedha tuweze kuwaunga mkono.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie tu Mhe. Waziri na mimi ni mdau wa Wizara yako, naona mwisho wamepongeza sana wengi wamekuunga mkono na mimi pia nimechangia katika japo ni kidogo lakini lengo langu ni kuhakikisha kwamba katika Mikoa yote tutakuwa tunaunga mkono, si vibaya na sisi pia ukawa unatugusa gusa katika ili bado huko wanatugusa gusa katika shukurani zako.

Chengine nimalizie tu katika sikukuu Mhe.Mwenyekiti, kule Jimboni kwetu Mkoa wetu wa Kusini tuna vijana ambao wanakuwa wanapiga piga miziki yao vijana tunajua, mjini ni mbali wakati mwengine. Kwahivyo Mhe. Waziri na Wakuu wako wa Mikoa wale ambao ni masheha wanakuwa wanaomba wanafanya michango yao wapige miziki katika maeneo yao husika ili washerehekee katika sikukuu. Kwa hivyo naomba sana muwaruhusu kwasababu inakuwa inatusumbua sana sisi wananchi vijana na wao wanastahiki kujirusha tuwaonee huruma na wao wapate.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo Mhe. mengine nitayapeleka kwa maandishi mimi sina lengo la kuzuia fungu la aina lolote nitampelekea maoni yangu mengine na mawazo yangu kwa maandishi kama utaratibu unavyoruhusu.

Nikushukuru wewe Mwenyekiti, kwa nafasi uliyonipa naunga mkono hoja mia juu ya mia Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe Simai, sasa namwita Mhe. Abdalla Ali Kombo akifuatiwa na Mhe. Asha Abdalla Mussa.

Mhe. Abdalla Ali Kombo: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako nakushukuru sana kwa nafasi uliyonipa kwanza mkono hoja ya kitabu hichi mia kwa mia sina tatizo nacho, na nina mawazo kidogo tu.

Mhe. Mwenyekiti, naanza na Wakuu wa Mikoa, wakuu wa Wilaya na Maofisa Tawala.
Mhe. Mwenyekiti, hawa ndio wasaidizi wakubwa au wakuu wa Mhe. Waziri wa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na ndio kucha kutwa ndio wanaofanyakazi za ulinzi, usalama, uzalishaji, na huduma za jamii. Lakini kwa bahati mbaya sana ni watu wanaotia huruma kuliko wote, usafiri wa watu hawa ni wa ajabu katika nchi hii. Imefika pahali imefikia *time* unamkuta Ofisa Tawala au Mkuu wa Wilaya gari yake imekwama mbovu inasukumwa aibu kubwa, ama imefika *time* ile namba ya DC wanavijibati hawa hubadilisha hapo hapo ikawa SMZ au ZNZ asifahamike kama Mheshimiwa lakini hiyo ni sawa sawa na kuazima nywele kwa Mhe. Jaku nikavaa ikiwa mimi muhindi lakini mswahili ndio yale yale.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo naomba tu watu hawa, Ma-*DC,* Ma-*RC,* Maafisa Tawala, kupitia Wizara hii naiomba serikali iwape usafiri. Kuna magari hapa yaliyokuwa ya Mawaziri mengine si mabaya wapewe angalau na wao waweke mkono juu kuliko kuchukua baadhi ya viongozi wakatumia majumbani mwao tuwape watu hawa. Hilo la kwanza.

Mhe. Mwenyekiti, nakuja tena jengine. Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, sisi tunachukua maoni kwa wananchi wala usishangae, kuna malalamiko ya wastaafu wetu wa JKU na mimi lazima niwaheshimu *intake* ya 10 nilikuwa nao na wengine walimu wangu. Wanalalamika sasa ukweli utakuwa unaujua wewe, kuna pesa zao hawajapewa mpaka leo. Sasa naomba tu Tume ya Utumishi ya Idara Maalum na nini wewe unayajua, sasa kama kuna chao basi tuwapeni. Watu hawa mara nyingi si wabaya lakini hawana dhamana kwa sababu kila kitu wanakijua. Zamani wakati huo askari wanaweza wakakupiga vishoka tisa kabla hujawasemesha lakini sasa hivi wanaweza wakakwambia shikamoo yakawa yamwekwisha. Kwa hiyo nadhani kama wana chao basi naomba tuwapeni. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nakuja ukurasa wa 62 kwenye mashamba ya JKU ya Unguja na Pemba. Mhe. Waziri katika Wizara yako una mkataba na Mwarabu mmoja ambaye ni Mtaalam wa Kilimo yuko Bambi, lakini ananitisha na mimi niliwahi kupitia ubwana shamba. Tumekwenda kwenye maonesho anatwambia hizi mbegu za muembe ambazo unaweza ukapanda mita nne kwa nne, sasa utaalam huo kama si mpunga wa Kibokwa sijawahi kuuona, imenitisha kidogo. Lakini baada ya kuwaita wale askari wa JKU vipi mbona yapo hivi, wanasema sisi hatumo yeye tu huyo. Sasa nikajua hapa ushirikiano haupo. Labda baadae Mhe. Waziri akija afafanue uhusiano wa mtaalam huyo kutoka Misri ukoje kwetu sisi na una tija gani kwa nchi. Maana yake sio tuna mtaalam tu hatuna tija lakini tunaliwa pesa zetu baadae akija mjini anatia shati ndio hayo tena tunakataza kwa ulimi inakuwa mashaka. Kwa hivyo, hili ukija kidogo Mheshimiwa utusaidie.

Mhe. Mwenyekiti, jengine umezungumza usafi kwenye kurasa za kitabu hiki kwenye Mamlaka za Mikoa, kuna mambo yalifanyika kidogo ningependa Wizara hasa Wakuu wa Mikoa pamoja na Mhe. Waziri na watu wa Halmashauri ama Manispaa mkakaa pamoja kuliko kila mtu kutoa amri kikundi hiki kifanye hivi, kikundi hiki kifanye hivi, hiki nitapata pesa hizi, hiki nitaajiri vipi tunawachanganya wananchi. Fahamu yangu mimi ni kwamba taka zote duniani ni Manispaa ama Halmashauri. Sasa kama kuna kingine chochote cha serikali basi kikae na Halmashauri kipange wananchi wetu hawajui taratibu zikoje. Haiwezekani wananchi wakachukua risiti zao na Halmashauri na risiti yao sasa hiyo itakuwa sio serikali itakuwa kijungu nje hicho ambayo tunapika mchuzi tunaonja kumbe sio. Sasa nadhani Wenyeviti, Waziri na Wakuu wa Mikoa na Wilaya wakae zoezi lifanyike lakini kwa utaratibu wa serikali na kanuni.

Mhe. Mwenyekiti, jengine kuna Baraza la Mji Mkoani nimesoma kitabu hiki katika ukurasa wa 51 wao wanasema wamewapa chakula wanafunzi 2,500 zaidi na halafu wamesimamia mashamba darasa 1,800 na kusimamia ekari 100 za mpunga. Ninawapa hongera lakini je, ugatuzi huu upo Baraza la Mkoani tu na wengine wanafanya hivyo? *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nakuja tena kwenye Wakala wa Ulinzi wa JKU ukurasa wa 19, moja kati kazi zao ni kuwalinda na kutoa ulinzi na kuwafundisha wawekezaji na watalii. Hapa ningeomba baadae ukija utufafanulie je, kwa wawekezaji wepi? Hoteli hizo 16 ni zipi na kiasi gani wametulipa hawa. Maana isije ikawa tuna askari wa kwenda kutoa ulinzi, wa kwenda kutoa huduma. Halafu ni askari wepi kuna vikosi vingi, kuna Valantia, kuna JKU, kuna KMKM, kuna Zimamoto, ni wepi askari ambao wanaofanya kazi hii.

Mhe. Mwenyekiti, kuna jengine fahamu yangu mimi kama nilivyozungumza mapema, Manispaa wanashughulika aidha na *low, medium* au *high* kwenye *residential,* yaani kwenye *populationa* na mengineyo. Lakini kwenye Manispaa zetu bado tuna maombi ya eka. Sasa je, kwenye Manispaa kuna eka? Mhe. Waziri akija naomba atupe ufafanuzi. Ninachojua mimi kwenye Manispaa huwa tunazungumza miji ile yenye watu wengi ya kati kati na midogo. Sasa Manispaa zetu tunakuwa na maombi ya eka. Je, kwenye Manispaa kunakuwa na maombi ya eka?

Mhe. Mwenyekiti, jengine kuna suala kidogo gumu la Halmashauri au Manispaa zetu hasa hizi za shamba uombaji wa kibali cha kujengea ukweli kabisa kina adha. Kwa nfano, Wilaya ya Kati kuna watu wanakaa Charawe, Uzi, mtu ameshauza kaa au mbaazi zake anakuja ofisini anaambiwa bwana wewe kwanza katafute *engineer*, uje na mafaili matatu, uende Forodhani,

kaonane na Sheha upate cheti cha uhaulishaji, sijui uende wapi. Sasa ninachoshauri tumezungumza mambo ya ugatuzi mimi sikatai hivi vitu kutokufanyika lakini watu hawa hebu na wakae pamoja wote. Mtu ametoka zake Charawe unamwambia nenda Forodhani mwisho wake Mwembedezo kwa gari ya wazi, si usumbufu huo. Ametoka Uzi ameshauza mbaazi zake unamwambia sasa uje na *engineer* na mafaili matatu. Ninachowaomba kaeni kitako Halmashauri au Manispaa wataalam wote wawepo halafu tajeni hizo pesa, suala sio pesa, suala ni usumbufu. Sasa kama mtaendelea na haya nakuhakikishieni watu watatoa pesa na watajenga. Kwa hivyo, hebu tuutafsiri huu ugatuzi kwa vitendo. Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Ardhi, Maji na Nishati tumezungumza nao juzi wanasema aa sisi hatumo, ni Halmashauri hizo au Manispaa. Kwa hivyo, ningeomba tu mkakaa pamoja.

Mhe. Mwenyekiti, nakuja tena swali langu labda ukija niulize hizi barabara kutengenezwa pamoja na taa hizi ni mjini tu maana yake watu wote wa Unguja Pemba wapo, lakini utatizama leo taa hizo mwisho wake barabara ya Uwanja wa Ndege/Amani. Ukenda huko mashamba ambako mnasema miji inakuzwa mmepeleka ugatuzi hakuna taa, sasa hiyo sio hii wanaita *bias*. Kwa mfano, ukenda Makunduchi sasa hivi ukitoka Kajengwa/Mzuri njia ile si yako, na kama mji wa kisasa si ule. Ukenda Gamba mle huko ndio njia ya Tumbatu kwa hivyo sisemi chochote. Mhe. Mwenyekiti, ningeomba tu hizi taa wakati mwengine mengine siyasemi nikaja nikaambiwa unachokoa watu lakini na mashamba mengine mambo yawemo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nakuja Kengeja mimi kesi ya Kengeja kwa kweli inaniuma. Kengeja nyumba zilizokuwepo ni za serikali zipo chini ya Wizara ya Ardhi, Maji na Nishati, lakini watu ambao wamo ni wako. Pale kuna Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya, Mkurugenzi wa Halmashauri au wa Mji wa Mkoani siyajui vizuri, wale watu mle ndani ya nyumba ni wako wewe si wa Wizara ya Ardhi, na sijui kama hizi nyumba umeshawahi kuziona wanazokaa watu wako. Sasa Mhe. Waziri ukija labda utasema nimewaona watu wangu ambao nategemea wazalishe, walinde na watoe kila kitu wanavyoishi. Ningekuomba ukakaa na serikali lakini wale watu mle ndani wahamishwe.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naona aibu kwamba Sheikh Mohammed Aboud Mohammed mheshimiwa namba sita tokea yupo, lakini leo anachukua wageni anakwenda kuwaonesha mimi raia wangu hawa kwa kweli haipendezi. Wale watu Mhe. Haji Omar Kheri si wako kama Haji, lakini wako kama Waziri. Serikali ikae na ukae nao watafutiwe pahala iwe Fukuchani, iwe Tumbe kokote lakini mle waondoke. *(Makofi)*

Mwisho sasa nakuja kwenye jimbo langu. Mhe. Mwenyekiti, katika Jimbo la Mwanakwerekwe Mhe. Haji Omar Kheri, Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara za SMZ hajabadilishwa bado na nilimlalamikia kwamba kuna watu wamejenga barabarani. Ukienda Amani humu sasa hivi mmewekwa *tiles* mnauzwa nini tulizungumza kwenye bajeti iliyopita lakini usemaji wa Mmasai jibu bila maana yake hakuna kitu. Sasa yale hajanionea huruma na kuna *pipe,* sasa hivi kuna mtu sina uhakika kama kupitia Halmashauri yake ama Wizarani kapewa kibali anauza mbao pale pale Mwanakwerekwe chini kuna *pipe* kubwa. Mhe. Mwenyekiti, wengine wanakaa visiwani, mimi tayari nimeshakuwa kisiwani Mwanakwerekwe sasa unataka kuniongezea mengine. Nakuomba mengine mwenyewe ulitangaza kwamba uuzaji wa mbao utakuwa Darajabovu, saa pale Darajabovu sipo, pale Mwanakwerekwe pana *pipe*, lakini kubwa zaidi pana Kambi yako ya Zimamoto wakitoka mle wanakwenda kuzima moto

watakuja kuponda watu. Sheikh Mohammed Aboud Mohammed atafika pale mapema maana yake ndio kazi yake hiyo atapiga hotuba ataweka sawa lakini watu wameshakufa tayari. Mhe. Mwenyekiti, vibali vyengine hivi vya hatima nasema tuvisamehe *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, lakini hapo hapo sasa hivi sina uhakika kuna ukuta wa Mohammed Hamza sasa yeye sijui kama *garage* ama *parking* au nini na sijui kama Halmashauri imeruhusu, naomba haya mengine tupunguziwe tuachiwe haya maji tu kwenye barabara.

Mhe. Mwenyekiti, la mwisho kabisa, naomba wote baba mmoja mama mmoja hawa Manispaa ya Mjini na Manispaa ya Magharibi "A" ikiwezekana na "B" wakae pamoja hebu wazungumze haya mapato kwenye masoko yao. Hii kesi imeanza zamani lakini hebu wakae pamoja na niyachukue wapi, niyachukue wapi, lakini pia wasafishe wapi, sasa wanagombania pesa tu, sasa hivi ukenda uchafu umezidi. Kwa hivyo, naomba nao pia wakae pamoja waje na jibu ambalo halitaiharibia sifa nchi yetu. Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Abdalla Ali Kombo sasa namwita Mhe. Asha Abdalla Mussa na Mhe. Mussa Foum Mussa pamoja na Mhe. Said Omar Said wajitayarishe.

Mhe. Asha Abdalla Mussa: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na mimi napenda kuchangia hotuba hii ya Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara za SMZ. Mhe. Mwenyekiti, napenda nimpongeze sana Mhe. Waziri pamoja na Naibu Waziri kwa kazi zao nzuri wanazozifanya za kila siku. Lakini pia niwapongeze Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hii pamoja na watendaji wake wote. Mhe. Mwenyekiti, pia niungane mkono na wajumbe wenzangu ambao wametangulia niiunge mkono hotuba hii ya Mhe. Waziri kwa asilimia mia moja.

Mhe. Mwenyekiti, niende moja kwa moja katika ukurasa wa 8 wa hotuba hii kuna miradi 10 ambayo wameitekeleza katika mwaka wa fedha 2017/2018. Mhe. Mwenyekiti, kati ya miradi ambayo imetekelezwa namuomba sana Mhe. Waziri atakapokuja anipe ufafanuzi ili na mimi niweze kufahamu hii miradi ambayo imetekelezwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa katika miradi 10 hii kuna ujenzi wa Chuo cha Kurekebishia Watoto ambacho kipo Hanyegwamchana. Mhe. Mwenyekiti, mradi huu nakumbuka tokea nilipoingia Barazani unaombewa fedha kwa ajili ya kutekeleza mradi huo.

Mhe. Mwenyekiti, mwaka 2017/2018 iliombwa fedha shilingi milioni 600 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu, lakini fedha walizopatiwa ni shilingi milioni 500,088,000/- ambazo wamepewa kwa ajili ya ujenzi sawa na asilimia 98. Mhe. Mwenyekiti, lakini kwa mwaka 2018/2019 mradi huu tena wameomba fedha shilingi milioni 700 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo. Mhe. Mwenyekiti, nilitaka kufahamu kwamba Mhe. Waziri huu mradi mpaka kumalizika utatumia gharama ya kiasi gani, lakini mpaka sasa mradi huu umetumia kiasi gani.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia kuna Mradi wa Kuimarisha Kiwanda cha Viatu (KVZ). Mhe. Mwenyekiti, mradi huu nao pia umekuwa kila mwaka unaombewa fedha. Kwa mwaka 2017/2018 ziliombwa fedha jumla ya shilingi milioni 400 lakini fedha walizopewa ni shilingi milioni 248,700,000/- sawa na asilimia 62. Lakni kwa mwaka huu 2018/2019 hakuna fedha

yoyote ambayo imetengwa kwa ajili ya mradi huu. Nilitaka kufahamu kwamba mradi huu tayari umeshakamilika, na kama haujakamilika ni sababu gani ambazo zimepelekea kwamba hazijatengewa fungu kwa ajili ya mradi huu.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye suala zima la Mradi wa Kupeleka Madaraka kwa Wananchi yaani Ugatuzi. Mhe. Mwenyekiti, niwapongeze sana watendaji wote wa Halmashauri zote za Unguja na Pemba kwa utekelezaji wao mzuri ambao ni mwaka tu toka ugatuzi huu uanze kutekelezwa. Kwa kweli wanafanya kazi kubwa na pia wanajitolea sana. Naomba sana hili fungu ambalo walitengewa mwaka jana jumla ya shilingi milioni 500 lakini pia walipewa fedha shilingi milioni 128 ambazo ni fedha kidogo sana. Lakini kwa mwaka huu wametengewa jumla ya shilingi bilioni 1,110,000,000/= kwa ajili ya utekelezaji wao. Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri wapatiwe fedha hizi kwa wakati ili waweze kutelekeza majukumu yao.

Mhe. Mwenyekiti, nije ukurasa wa 23 kuna Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo. Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2017/2018 kikosi hichi walikuwa wana programu mbili, programu ya kwanza ilikuwa ni ulinzi na uzuiaji wa magendo, na programu ya pili ilikuwa utawala na uendeshaji wa huduma za kikosi hichi. Lakini wamesema kwamba walifanya doria katika kanda za bahari na nchi kavu, lakini pia wamekamata walioweza kudhibitiwa ambao jumla ya shilingi bilioni 118,530,000,000/- ambazo zimeokolewa kupitia doria hizi. Mhe. Waziri atakapokuja nilitaka kufahamu kwamba hawa watu ambao walikamatwa kupitia bidhaa ambazo za magendo wamechukuliwa hatua gani, lakini pili Wizara ina mkakati gani kupitia hichi kikosi maalum ya kuhakikisha kwamba magendo haya yasiweze kuingizwa na kutolewa katika kisiwa chetu hichi cha Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, nitakuwa mkosefu wa fadhila kama sikuwapongeza sana Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya pamoja na Wakurugenzi wa Halmashauri zote za Unguja na Pemba kwa kazi ambazo wanazifanya wakati wote, lakini pia kamati za ulinzi na usalama za Mikoa na Wilaya zinafanya kazi kubwa sana tena za kuchukuliwa mfano katika maeneo yetu hususan katika Wilaya yangu ya Kaskazini (B) Unguja. Kamati hiyo ikiongozwa na DC mpya ambae Mhe. Rais hakukosea kututeuliwa DC wetu mpya ambae anafanya kazi usiku na mchana, nampongeza sana kwa kazi kubwa anayoifanya akishirikiana na Wawakilishi wote pamoja na Wabunge lakini pia pamoja na Madiwani na Masheha wote. Naomba sana Mwenyezi Mungu amjaalie awe na Afya njema lakini pia aweze kuzidisha juhudi katika kutekeleza majukumu yake.

Mhe. Mwenyekiti Wizara hii pia imeweza kujenga mahanga ambayo yataweza kutusaidia vikosi vyetu hivi ikiwemo katika kisiwa chetu cha Pemba, kwa kweli wanafanya kazi kubwa sana tena sana ya kujitolea na ambayo yenye mfano mkubwa. Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba katika fungu lao ambalo wamepangiwa basi naomba sana waongezewe ili waweze kutekeleza majukumu yao.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa kitabu hichi kwa upande wangu nimekipitia ukurasa kwa ukurasa lakini mengine haya yanajumuishwa katika Wizara nyingine ikiwemo suala zima la udhalilishaji kwa wanawake na watoto hili nitaliachia, ili itakapofika Wizara hii ya Wanawake na Watoto basi tutaichangia kwa kina.

Mhe. Mwenyekiti, kwa haya machache niseme naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mheshimiwa Asha Abdalla Mussa, sasa ninamuita Mhe. Mussa Foum Mussa akifuatiwa na Mhe. Said Omar Said Mheshimiwa Mussa karibu.

Mhe. Mussa Foum Mussa: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kunipa ruhusa ya kuchangia kidogo, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwepo hapa katika wakati huu wa usiku tukiwa katika hali ya utulivu na usalama. Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na Naibu Waziri, pamoja na Watendaji wake wote kwa kutuletea hutuba hii nzuri na kwa mashirikiano mazuri katika Wizara yao, baada ya maelezo hayo mimi nitaanza kuchangia ukurasa wa 28 program za Mamlaka za Mikoa.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza napenda kuwapongeza Wakuu wa Mikoa wote wa Zanzibar Unguja na Pemba pamoja na watendaji wake, pamoja na watendaji wao wote kwa mashirikiano makubwa wanayotupa sisi Waheshimiwa Wawakilishi, tumeshuhudia baadhi ya Mikoa yetu yote kwamba tunaishi vizuri, tunalala tunaamka bila ya matatizo usalama upo kwa hali yoyote ni kwamba usalama upo. Kwa hivyo kiupande wetu ni vyema tukatoa shukurani kwa Mwenyezi Mungu kutujaalia mpaka hivi sasa kuwa tuko katika hali ya utulivu na usalama katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile mimi nitoe pongezi maalum kwa Mkoa wangu wa Kusini Pemba kwanza nimpe pongezi Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba, kwa kweli mimi niseme katika jimbo langu takriban lilikuwa haliko katika hali ya utulivu wa usalama kwa vijana wavuta unga, wizi na walevi wa aina nyengine. Kwa mashirikiano makubwa ya Mkuu wa Mkoa wakati ule alikuwa Mkuu wa Wilaya lakini sasa hivi Mkuu wa Mkoa na Jeshi la Polisi la Mkoa wetu, pamoja na vijana wetu wa ulinzi shirikishi tumefanya kazi kubwa katika kupata utulivu katika jimbo letu la Kiwani. Mhe. Mwenyekiti hali ilikuwa mbaya lakini kwa mashirikiano makubwa nimpongeze tu Mhe. Mkuu wa Mkoa hivi sasa aendelee ili na ile hali iendelee kuimarika isije ikarudi nyuma.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile niendelee kusema kwamba nalipongeza pia Baraza la Mji Mkoani katika ukurasa wa 52 hapa tumeambiwa kwamba Baraza la Mji Mkoani kwa mwaka wa fedha 2017/2018 lilikadiriwa kukusanya Shilingi milioni 230 hadi kufikia Machi, 2018 limekusanya Shilingi 259, 959,485/= sawa na asilimia 113% hapa ni vyema tukampongeza Mkurugenzi wa Baraza la Mji Mkoani kwa jitihada yake kubwa aliyoifanya. Lakini tunamuomba tu kwamba mara hii basi apite lengo hili liendelee kuzidi ili tupate mafanikio makubwa.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile katika kulielezea suala hili pia Mikoa yetu ilijikita katika kuhakikisha masuala ya udhalilishaji wanayapiga vita, hapa ukifungua katika ukurasa wa 108 kiambatanisho namba 11 utaona kuna matokeo ya udhalilishaji yaliyoripotiwa kwa mwaka 2017/2018. Mhe. Mwenyekiti, ukianzia Mkoa wa Mjini Magharibi hapa utakuta namba ya kulawiti, kubaka, kutelekezwa, kukashifiwa, shambulio la kuumiza mwili mambo mengi hapa. Lakini katika jumla ya udhalilishaji hapa ni 113 katika Mkoa wa Mjini Magharibi. Mkoa wa Kusini Unguja ni 167, Mkoa wa Kaskazini Unguja 150, Mkoa wa Kusini Pemba 141 na Mkoa wa Kaskazini Pemba ni 142 jumla ya matokeo ni 713. Mhe. Mwenyekiti tukiiangalia hali kidogo si nzuri, kwa hivyo kwanza nawapongeza Wakuu wa Mikoa wote wajitahidi ili kupunguza hii idadi.

Lakini vile vile niseme tu katika Mkoa wa Kaskazini Unguja katika namba ya watu waliotelekezwa katika Mkoa Mzima wa Unguja tokeo la kutelekeza ni mtu mmoja, namba hii mimi hainiridhishi na utakapokuja tunataka maelezo mazuri. Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, juzi siku ya Jumamosi sisi kamati ya maendeleo ya wanawake na habari tulikuwepo Tumbatu, kwanza tumpongeze Mhe. Waziri kwa jitihada yake ya Jimbo lake la Tumbatu na tumekwenda kule kwa masuala haya ya udhalilishaji, siku ya pili Jumapili tulikuwepo Mkwajuni hali si nzuri na kuna wanawake wamelia kwa vile wanavyotelekezwa lakini hapa leo Mkoa mzima tunaiona nambari ya mtu mmoja hii nadhani Mhe. Mwenyekiti nadhani hata Mhe. Waziri anayehusika na wanawake atakapokuja hapa pengine anaweza kachangia hii hali anaweza ikawa na yeye haikubali, kwa hivyo nadhani Mhe. Waziri utakapokuja tunaomba tupate maelezo ya kuturidhisha.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mwenyekiti wangu wa Kamati pia watu wa Mkwajuni wamemuomba mwezi huu wa ramadhani turudie tena kwamba hali mbaya, sasa leo kuiona hii namba mimi siridhiki nayo lakini utakapokuja Mhe. Waziri atupe maelezo ili na sisi turidhike watu wa kamati hii ili tuendelee kufanya kazi vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, vilevile baada ya hapo niendelee kuzungumza katika vikosi vyetu vya SMZ, kwanza nivipongeze vikosi kwa jitihada zao kubwa wanazozifanya katika kuiweka nchi yetu katika hali ya usalama, mimi vile vile nizungumzie katika hichi kikosi cha KMKM juzi tulipokwenda Tumbatu hatujaondoka kule ilipigwa simu kwamba kuna watu wavuvi wameokotwa na meli ya mafuta inayokwenda Pemba, lakini wao hawawezi kurudi kwa hivyo walipigiwa KMKM kwamba waende wakawachukue kule wakatwambia twendeni haraka tufike Mkokotoni ili sasa sisi tunataka kutoka.

Lakini Mhe. Mwenyekiti Mhe. Waziri nakwambia tuliona huruma kwa kile chombo wanachokichukua pale kuwafuata wale wavuvi kwenda kuwachukua kule hali ilikuwa si nzuri, chombo hakihimili bahari. Mhe. Mwenyekiti, tunamuomba Mhe. Waziri wale KMKM waliokuwepo kule basi wapatiwe chombo kinachohimili bahari ya Nungwi, ili yatakapotokea yale matatizo makubwa kwa hivyo na wao wawe na chombo kinachohimili bahari, bahari ya Nungwi nzito ina mawimbi makubwa. Kwa hivyo tunakuomba Mhe. Waziri hii hali uifahamu na wao kule basi wawe wanakwenda katika shughuli zao hizi katika vyombo ambavyokuwa vinaaminika kidogo na vinavyohimili mikondo mikubwa.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo vile vile niendelee kuzungumzia barabara zilizojengwa kwa kupitia mradi wa *MIVAP* hapa Mhe. Waziri katika maelezo yake amesema kwamba wanafikiria barabara hizi kuziweka lami, Mheshimiwa Mwenyekiti na mimi nasema kwanza katika jimbo langu Kiwani tunayo barabara hii ambayo imetoka Ukutini mpaka Mtangani Bandarini, hizi barabara isizungumzwe kwamba tunafikiria izungumzwe kwamba tutazijenga kwa sababu hivi sasa ziko katika hali mbaya na ikiwa hazikujengwa kwa lami barabara hizi baada ya mategemeo makubwa ya wananchi basi tunaweza tukafika pahali pabaya na zile barabara zote zikapotea kwa maji. Tuzione hizi zawakati huu wa mvua zilivyo hivi sasa katika hili eneo letu la Mjini, je vipi zile ambazo kuwa zina kifusi.

Kwa hivyo tunamuomba Mhe. Waziri hili suala asiseme kwamba tutafikiria aseme tutazijenga kwa lami, wakati huo huo namuomba Mhe. Waziri watakapoleta uamuzi huo basi ile barabara yangu ya mwanzo iwe ya mwanzo kutoka Ukutini mpaka Mtangani Bandarini, namuomba Mhe. Waziri atoe *priority* katika barabara hii.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo vile vile nielezee ukatuzi hasa mimi nitazungumzia habari ya elimu hapa wamezungumzia kwamba pameandikishwa wanafunzi mwaka huu, mimi kwa kipindi kikubwa nina kilio katika skuli ya Mwambe Msingi. Kwanza niipongeze Serikali imeajiri walimu si kidogo lakini katika walimu hao tumepata walimu 13 katika skuli hiyo tulikuwa na upungufu wa walimu 30 tumepata walimu 13. Lakini wakati huo huo mwaka huu tumeandikisha watoto 985 ina maana hao walimu tuliopata kwa kipindi hiki wote kwa mkupuo huu wa kuandikisha wote wamekuwa wahaba hawa walioletwa ina maana ile hali imerudi pale pale au zaidi.

Sasa mimi ninachokiomba Mhe. Mwenyekiti, sizungumzii sana suala la uhaba wa walimu lakini suala ninalolizungumzia hapa suala la ugawaji wa walimu katika maskuli yetu kwa nini liwe hivi, kwa mfano skuli ya Mwambe imepakana na skuli ya Kengeja, Kiwani na Mtambile. Lakini kwa nini mfano Kengeja pawe na upungufu wa walimu sita lakini Mwambe walimu thalathini ugawaji gani huu hili linatuumiza, kwa sababu hivi sasa mwalimu mmoja ana madarasa mawili anayoyashughulikia madarasa mengine hayana walimu na wakati huo huo darasa la nne wanafanyiwa mitihani hapo tunategemea nini.

Kwa hivyo mimi nasema bado Serikali iendelee kuajiri walimu kwa sababu bado upungufu tunao mkubwa, lakini wakati huo huo Mzee wetu Mzee Karume alisema ni kheri kuwa na kidogo tu tugawana kidogo kidogo, kuliko kuwa na kingi tukaanza kukigombea. Sasa hii hali kwa nini ile *ratio* ya ugawaji wa walimu haiendi sambamba na mahitaji. Mimi sisemi kwamba hili suala sina nia ya kuzuia kifungu lakini nia yangu ni kuzungumza na hili suala nimeshalizungumza sana, hapa nalizungumza na itakapokuja Wizara ya Elimu nitasema tena, kwa hali yoyote nihakikishe kwamba hili suala mwaka huu Mhe. Mweyekiti basi tunapata mafanikio.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa muda wako umemaliza.

Mhe. Mussa Foum Mussa: La mwisho nasema kwamba Mhe. Waziri nimesoma hiki kitabu lakini katika mikoa yetu na Halmashauri zetu sikuona yale malengo yao kwamba kwa mfano watafanya kitu fulani, kitu fulani sasa najiuliza tu je, sisi Waheshimiwa Wawakilishi hatustahiki kuyajua hayo malengo yao.

Sasa nadhani hili suala utakapokuja hebu tueleze kwamba kwa mfano Baraza la Mji Mkoani mwaka huu wa fedha linakusudia kufanya mradi huu na huu hiyo kwa nini hatukuelezwa. Hata ingelielezwa kule kule kwenye Mkoa lakini tungelifahamu, lakini huku nyuma mwaka uliopita wa bajeti wameeleza mambo waliyoyafanya lakini sasa je hapa tutakuwa tunakwenda kama jongoo mpaka tukute maji ndio turudi. Sasa nadhani tuelezwe kwamba Baraza la Mji Mkoani kwa mwaka huu linakusudia kufanya mradi huu na huu ili tuje tupate kuhoji, lakini yameelezwa tu kwa pamoja kwamba tumepangiwa kwa mfano kupata kiasi kadhaa, lakini mnataka kufanyia nini na sisi ndio tunaoidhinisha pesa hiyo.

Mhe. Mwenyekiti baada ya maelezo hayo naunga mkono hoja mia juu ya mia ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mheshimiwa Mussa Foum Mussa sasa ninamuita Mhe. Said Omar Said na baadae atafutiwa na Mhe. Suleiman Makame Ali na wakati huo Mhe. Ame Haji ajitayarishe.

Mhe. Said Omar Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mwenyezi Jallah Subuhanahu wataallah kwa kuniwezesha kuwepo jioni hii katika kikao hichi nikiwa katika hali ya uzima.

Lakini pia nikushukuru na wewe kwa kunipa nafasi hii ya kuichangia hotuba ya Wizara ya Nchi Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum ya SMZ, nianze kumpongeza Mhe. Waziri Makini, Waziri muadilifu, Waziri ambae ameanzisha *Pentagon* kwa kipindi kilichopita wanamfahamu waliokuwepo wanajua maana ya *pentagon*, nimpongeze Mhe. Naibu Waziri nimpongeze Katibu Mkuu pamoja na Makamanda wetu wote kwa kutekeleza ahadi waliyoiweka ya kuilinda Zanzibar kwa hali yoyote. *(Makofi)*

Lakini nichukuwe nafasi hii ya pekee kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein kutokana na hekima zake, uadilifu wake na uvumilivu wake, ambao umechangia kutuletea neema kubwa Zanzibar, neema kutoka ndani ya Zanzibar na neema kutoka nje ya Zanzibar, ambapo ilikuwa hatutegemei, hatufikirii kutokana na hali iliyochafuka lakini ni kwa sababu ya unahodha wake. Huyu ni nahodha ambaye anaweza, ana nguvu, ana uwezo, ana uweledi kwa kuendesha chombo ndani ya mkondo katika bahari iliyochafuka kwenye mawimbi na kikafika salama salmin, tunampongeza sana. Mheshimiwa kabla ya kuchangia na mimi niseme naunga mkono hoja hii kwa asilimia 100.

Mhe. Mwenyekiti, nataka mchango wangu utakuwa mdogo sana nianze na Kikosi cha Zimamoto, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imejitahidi sana kuwawekea wapiganaji wetu mazingira mazuri ya kikazi lakini iliobakia, ni kuuzima moto bado hatujauzima huo moto kwa hivyo tunaomba kwa bajeti hii tuuzime na huu moto, yaani bajeti yetu tuieleze kwenye Kikosi cha Zimamoto na Uokozi.

Kwa kweli kama utakwenda kutembelea sehemu zao utashangaa kwa kweli, kwa hivyo tunaomba sana Serikali mara hii ijitutumuwe kidogo alau na wao Zimamoto vijana wetu wa nguvu, vijana wetu wa nguvu wanaofanya kazi kwa nguvu wanafanya kazi ngumu wanafanyakazi katika mazingira magumu lazima na wao angalau tulitupe pale jicho la huruma, kiasi ambacho waweze kujisikia na wao wana ofisi nzuri kama wenzao, waweze kujisikia kwamba wanavifaa vinavyolingana na kazi yao waepukane kama tulivyo kwenda wakuta, katika chumba kimoja wanawake, wanaume humo humo, hii kutokana na kukosekana kwa majengo, kwa hivyo tunaomba kwa kipindi hiki wafikiriwe, wakae katika majengo muwafaka kama wenzao.

Nije katika Mkoa wa Kaskazini Pemba, kwanza nimpongeze sana Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba, kwa kuendelea kudumisha usalama na amani, ya Mkoa wa Kaskazini kiasi ambacho sasa hivi aliyeondoka pale, pale Wete mjini pale, aliyeondoka kwa muda wa miaka 4 akaja pale akalala siku 3 atashangaa atasema lakini ndio Wete hii, leo ni Wete mpya, ni Wete

mpya. Nimpongeze kwa kudumisha amani, amani ambayo imeleta upendo baina ya jamii na jamii, amani ambayo imewafanya watu waungane ambao walikuwa wamebaguka, imani ambayo imewafanya wananchi wote washiriki katika maendeleo yao vizuri sana. Pia nimpongeze kwa jinsi anavyosimamia yaani miradi maendeleo kwa shehia zote za Kaskazini Pemba, akiwashirikisha Wakuu wake wa Wilaya ya Wete na Wilaya ya Micheweni. *(Makofi)*

Mheshimiwa napenda tena kuchukua nafasi hii ya kumpongeza Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba kwa utaratibu wake aliyejiwekea yaani kukutana na Waheshimiwa Wawakilishi kila kipindi ili kujadili maendeleo ya majimbo yao nimpongeze sana, kwa namna hiyo tutafikia pahala pazuri tunategemea.

Nije katika Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni, nimpongeze sana Mkurugenzi wetu wa Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni kutokana na miradi mingi tuliyoiona ambayo aliweza kuitekeleza kipindi kilichopita, lakini pia nimpongeze kwa ukusanyaji wa mapato. Kama tunavyoelewa, wilaya yetu ya Micheweni ndio ndogo kutokana na mapato, kwa sababu wakaazi wake mapato yao ni madogo kulingana na wilaya nyengine.

Lakini hata hivyo, ameweza wa kukusanya milioni mia moja na hamsini na tatu ambayo hiyo ni sawa na asilimia 90 kwa hivyo hongera sana Mkurugenzi ila moja tu, changamoto niliyoiona katika Halmashauri walipokuwa wanakusanya wenyewe zile fedha, kwa mfano fedha za mchanga walivyokuwa wanakusanya wenyewe kwa mwaka mmoja walikuwa wakiingiza milioni 40 mpaka 50 lakini hivi mwaka mzima wana milioni 10 walizopewa kutokana na hiyo kodi ya mchanga. Kodi hii ya mchanga walipewa si miezi mitatu, mwezi wa 7-8-9-2017, hii ni changamoto kwa hivyo twaomba hii ifanyiwe kazi ziko wakati wao wenyewe walikuwa wakikusanya 40 au 50 milioni.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie kwa kuwataja watendaji wetu. Watendaji wetu wa mwanzo katika Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar ni masheha, hawa ndio watendaji wetu wa mwanzo katika watendaji wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar wa mwanzo ni masheha, lakini leo utashangaa kutokana hali zao hata nyumba hawana, hata vipando hawana. Masheha wetu tunawaelewa jamani hawana nafasi hata ya kunywa maji kutokana na kazi zao, sheha huyo huyo mwalimu, sheha ni daktari, sheha ni hakimu hana nafasi saa zote na hatimae wako katika hali hiyo, na hawana hata uwezo pamoja na kwamba ni waajiriwa lakini hawana uwezo hata wa kwenda wakakopa vespa, kitu vespa ambao wafanyakazi wakakope tu, wana uwezo wa kwenda kukopa vespa, masheha wetu wako katika hali hiyo lakini kimya maana ndio sifa hiyo hawalalamiki, hawalalamiki, wako kimya wala hawana joto lakini sisi tunawaona mazingira yao ni magumu sana na mazito sana. *(Makofi)*

Twakuomba Serikali aa ifanye mpango wa makusudi ili kuwawezesha wale masheha waweze kwenda kukopa katika taasisi za kibenki yoyote ile, Serikali mnayo mipango mingi ya kuwafanyia wale wakapata mikopo na wao, ila nao wao alau wakajisikia wakapata angalau usafiri, saa zote wamo pirikani tu. Wengine wanaazima chombo akifika kishaharibika hawezi kujieleza hana cha kutengenezea matatizo. Mheshimiwa tunaomba sana tuangalie kwa jicho la huruma, kuna mtaalamu mmoja alisema kuiona mwanamke ndani hakuulizi chochote nipe hiki, nipe hiki hakwambii basi huyo ndio anayehitaji kumpa kila kitu. Masheha, Serikali inahitaji kuwapa masheha kila kitu.

Baada ya hayo Mheshimiwa nakushukuru. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Said Omar Said naomba nimwite Mhe. Suleiman Makame Ali na Mhe. Ame Haji Ali ajitayarishe.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti nakushukuru sana kwa kunipata nafasi hii ya kuweza kuchangia Hotuba hii ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum.

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kuchangia kwanza niwapongeze na nimpongeze sana Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote, kwa kukaa na kujadili kuhakikisha kwamba wanaleta bajeti yao ili kuangaliwa kwenye kasoro wapi parekebishwe ili kuhakikisha tunapata maendeleo katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kutoa shukurani zangu hizo, niende kwa Mhe. Waziri moja kwa moja kuwambia kwamba Mhe. Mawaziri katika Waheshimiwa Mawaziri katika Baraza la Wawakilishi hakuna Waziri mbaya wala Naibu mbaya wote Mawaziri wazuri na Manaibu wazuri. Lakini vile vile, wazingatie na wao kwamba na wao wanatoka kwenye majimbo baadhi yao, na uzuri wao walionao nao ni wawakilishi kama sisi tulioko huku nyuma. Kwa hiyo yale tunayowambia wasiyakalie, maana kuna wengine ukiwaambia kwamba tutayakalia tutayafanyia kazi, ukilikalia hilo ndio halendi Mhe. Mwenyekiti, wayafanyie kazi, ili wahakikishe kwamba yale tuliyowaambia siye na washauri wao wayafanyie kazi lengo ni kuleta maendeleo katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende moja kwa moja katika Baraza la Miji na Manispaa pamoja na Halmashauri, miye niwapongeze sana Mhe. Mwenyekiti kwa kazi kubwa wanayoifanya kugombana na watu huko mitaani, huko vijijini na sehemu nyengine lakini pia vile vile, na hii bajeti ambayo tunakwenda nayo Mhe. Mwenyekiti haipo mbaya sana kwa kiwango cha fedha kinazochopatika ni asilimia 90 na 95 na kwendea mbele.

Mhe. Mwenyekiti, lakini baada ya kuwa nishayapongeza Mabaraza ya Miji pia na wao wahakikishe kwamba lengo si kukushanya mapato tu, ni kuwapelekea wananchi huduma zile wanazozihitaji. Mhe. Mwenyekiti kwa mfano nitakwenda kwenye Baraza la Manispaa Magharibi B, hivi sasa Baraza la Magharibi B niseme kipindupindu kiko njiani kinakuja tujiandae. Baraza la Magharibi B lilikuwa wakikushanya taka wananchi pale maeneo ya tomondo, leo taka zile zote ziko majumbani hayachukuliwi na Baraza la Magharibi B wala hayachukuliwi na Baraza la vijana, baada ya kuondoa maradhi tunaweka maradhi, Mhe. Mwenyekiti inafika wakati mwengine wananchi wananun'gunika.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba sana tuangalie kwamba ikiwa kama kuna taratibu au kanuni hizi zilizopangwa Mhe. Mwenyekiti hii ni Serikali, hii sio kila mtu ajipangie utaratibu wake anaotaka mwenyewe hiyo sio Serikali ya sisimizi Mhe. Mwenyekiti, hii ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, hao sisimizi wana kiongozi wao. Sasa Mhe. Mwenyekiti, niliuliza siku moja nikaambiwa kwamba mabaraza ya vijana ndio watakaochukuwa taka zile, lakini mabaraza ya vijana wakapangiwa taratibu na Baraza la Manispaa wakasema hawataki taratibu hizo

walizopangiwa sasa Mhe. Mwenyekiti huo utaratibu unatokea wapi kwamba wewe unashungulikiwa na Baraza la Manispaa leo wewe mdogo lakini unapangiwa taratibu hutaki.

Mhe. Mwenyekiti, chengine Mabaraza ya Miji na Manispaa zetu zinachangamoto kubwa sana kwenye vitu vya nini vyanzo vya kuzoleya taka, nikisema hivyo nizungumzie kuhusu masuala ya usafiri, magari pamoja na vijiko vya kuzolea taka, Mhe. Mwenyekiti, kuna baadhi ya Baraza ya Miji hapa yanatumia shilingi milioni 10 kwa kila saa moja, wanatumia shilingi milioni moja kwa kukodi kijiko cha kuzolea taka, ukitumia masaa kumi ni milioni 10 sasa Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka mmoja ni bilioni ngapi?

Leo kijiko thamani yake ni shilingi milioni moja kijiko cha kawaida tu, cha *used* kwenda kununua ni shilingi milioni 100, lakini leo ndani ya mwaka unatumia si chini ya milioni na milioni 200 na kwa kuzowa taka Mhe. Mwenyekiti hili ni tatizo kubwa kwa hivyo naishauri sana wizara nakuiomba sana Wizara pamoja na mabaraza ya miji wahakikishe kwamba wanapanga bajeti zao vizuri na pia wanatafuta ufadhili wowote, kutakuta kuhakikisha kwamba vile vitu gari pamoja na vijiko vya kuzolea taka wanavyo wao wenyewe waache na ile kukodi.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende moja kwa moja kwenye vikosi vyetu vya SMZ, Vikosi vya SMZ nao niwapongezea sana kwa kazi nzito wanayoifanya,wana kazi kubwa ya kuhakikisha kulinda amani katika nchi yetu, lakini Mhe. Mwenyekiti, vikosi wanafika *time* nyengine kama walivyosema Mhe. Said kwamba wana matatizo. Leo vikosi wamepangiwa kukushanya mapato ukenda kuwatembelea kwenye taasisi zao pale pa kupumzika hawana. Sasa Mhe. Mwenyekiti, vyanzo hivi vya mapato hawana kama Chuo cha Mafunzo tulikwenda kukagua bwawa la ufugaji samaki, kuna wale samaki aina ya mwatiko ambao kwamba wamewafuga tangu tumbili wapo watu mpaka leo samaki wale wameshindwa kuvua hayo ndio mapato yao.

Lakini leo utakuta vikosi hivi vimepangiwa milioni 100, milioni sabiini, milioni sitini mapato kwa nini, mimi nimeunga sana mkono kwamba wakushanye mapato lakini ikiwezekana hayo mapato waweze kutumia wenyewe kutatua zile changamoto zao. Kwa sababu vikosi hivi inafika mpaka ile bajeti wanaopangiwa kwa mwaka wanaitumia yote, inamalizika wanabakia kuhangaika naomba sana, kwamba mapato wakusanye lakini kile wanachokusanya waweze kutumia wenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende moja kwa moja kwenye barabara za ndani, bajeti ya mara hii haina barabara za ndani hata moja itakayotengenezwa, kuna kitabu cha mwaka 2016 hichi hapa, kwenye barabara za vijijini zilizofanyiwa mkakati wa kitathmini, ikiwemo barabara yangu ya Ndagoni, Mhe. Doholo kanigeuza jina ananiita roho ya Pemba, nasema hivi kwa sababu Ndagoni katika hizi barabara zilizofanyiwa tathmini barabara 32 kwa bajeti 2016 barabara ya Ndagoni ina kilomita 9.8 ni barabara kubwa yote, ni barabara kubwa kuniko barabara zote za Zanzibar nzima zilizofanyiwa tathmini huku kwenye kitabu hiki.

Mhe. Mwenyekiti, sababu ya kunita Mhe. Doholo mimi nikakubali, kwa sababu sote tuhakikishe kwamba kule Pemba umeme upo Ndagoni, ukizimwa umeme Ndagoni Pemba ni kiza hakuna atakayeona, hakuna atayeoga maana mpaka maji yatoke, sasa umeme nguzo imeanguka utakwenda nini? Kwa hiyo roho ya Pemba imo Ndagoni naomba sana, lakini pia vile vile,

kwamba Mhe. Waziri alituambia kwamba Mfuko wa Barabara umewapa shilingi milioni 4,600,000,000/- inataka kutengenezwa barabara ipi mbona humu hatukuoneshwa hiyo barabara itakayotengenezwa kwa hizi milioni 4,600,000,000. Mimi nilitaka nijuwe hizi milioni 4,600,000,000 ni barabara gani itakayotengezwa, kwa sababu yule angetuainishia wakatwambia Ndagoni kwa sababu nasema Ndagoni ndio vifaa vinapotoka. Lsakini vile vile, nikasema Mhe. Hindi kuna barabara kule kwake ningesema pengine na Pangawe angesema na Kijitoupele tukapata kuona humu. Lakini sasa mimi nikuwa najiuliza kwamba hii milioni 4,600,000,000 pengine Mhe. Waziri atakuja kutufafanulia zaidi wanataka kutengeneza barabara ipi.

Mhe. Mwenyekiti nikitoka hapo niende tena kwenye Baraza ya Miji, kuhakikisha sasa hivi tumekwenda kwenye ugatuzi, na lengo la ugatuzi ni kukasimu madaraka ukayapeleka kwa wananchi, vituo vya afya vyote, skuli zote za msingi ziko kwenye ugatuzi. Mhe. Mwenyekiti, baadhi ya vituo vya afya havina hata *panadol* ndani ya majimbo yetu, mwakilishi anapewa shilingi milioni 20 kwa mwaka, Mwakilishi huyo afanye mangapi. Ndio pale niliposema kwamba Mawaziri wote ni wazuri, lakini wafikirie kwamba na wao ni wawakilishi wanatoka majimboni wanakamatwa mikia kama tunavyokamatwa sisi, kwa sababu huko nje watu wanafikiri labda Mwakilishi anapewa mabilioni ya mapesa, kumbe sivyo hivyo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa naomba kama lengo ni kupeleka madaraka na nampongeza sana tena sana, siku ya Mei Mosi alisema kuwataka wananchi wote wa Zanzibar wasikae vibarazani na kunung'unika, wapeleke kero zao kwa Wawakilishi wao ili waweze kuwawakilishia kero zao, mimi nampongeza sana. Sasa niombe kwamba lile agizo la Rais lifanyiwe kazi. Maana Mhe. Mwenyekiti, tukisema hapa kuna kuna wengine wanaona wakasema yule nani aliyesema hapa "yammaliza, yansoza" ni Mhe. Jaku Hashim Ayoub, kwa hivyo naomba sana yafanyiwe kazi.

Vile vile tukenda huko kwenye masuala ya ugatuzi Mhe. Mussa alisema Mwambe ana tatizo la walimu 35, Mhe. Mwenyekiti, elimu gani itakayopatikana hapa. Lakini sio Mhe. Mussa tu na majimbo yote changamoto hii ipo. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti mimi naomba kwamba kile haba kinachopatikana basi kiweze kugaiwa ili kuhakikisha kwamba kila sehemu inayohitajika wapewe wale walimu pamoja na vifaa tiba, bila ya tiba kusema la ukweli ni mtihani. Mimi naomba sana.

Mhe. Mwenyekiti kidogo niende kwenye mpango wa Maendeleo aliowasilisha Mhe. Dkt. Khalid hapa kwamba alisema kuimarisha miundombinu ya maeneo ya uingiaji nchini, barabara na nishati. Kwenye mpango huu wa maendeleo, lakini sasa ili mapato yapatikane kuna baadhi ya maeneo mengine, majimbo mengine kuna vyanzo vya utalii vya mapato yanatoka huko. Leo mimi nashangaa, tena nashangaa sana, kuona hivi vyanzo vya mapato huko kwenye barabara zenyewe ndio hazimo, sasa ndio tunakwenda wapi, hatuwezi kufika.

Mhe. Mwenyekiti, mimi namuomba sana Mhe. Waziri kwamba kuhakikisha kwamba zile barabara alizozifanyia upembuzi zihakikishwe zinatengenezwa, kwa sababu kwa hiyo miaka mitano itapita mitano, ije tena mitano, hazimaliziki.

Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono kwa sababu bajeti hii ni kamati yangu naunga mkono kwa asilimia mia kwa mia, lakini nasisitiza tena niwaombe Mawaziri kuhakikisha kwamba zile

changamoto majimboni mwetu wanazifanyia kazi kwa sababu na wao wanatoka huko huko. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako, sasa namwita Mhe. Ame Haji Ali.

Mhe. Ame Haji Ali: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi, awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kuniwezesha jioni hii kusimama katika chombo hichi na mimi kutoa mchango wangu. Nianze kwa kuwashukuru Waziri na watendaji wake wote wa Wizara hii kwa kutuletea hotuba hii yenye mambo mengi sana kwa maendeleo ya nchi yetu.

Sambamba na hayo niushukuru uongozi wangu wote wa Mkoa wa Kaskazini Unguja ukiongozwa na Mhe. Mkuu wa Mkoa na watendaji wake wote, kwa juhudi na kazi kubwa wanazozifanya katika Mkoa wetu na mashirikiano yao yanatupa faraja sana katika mkoa na kwa kweli mpaka sasa mkoa wetu upo salama.

Sambamba na hayo Mhe. Mwenyekiti, nitakuwa mchache wa fadhila kama sitoishukuru Halmashauri yetu ya Wilaya ya Kaskazini A. Kwa dhati kabisa niishukuru Halmashauri ya Wilaya kwa mambo mengi ambayo wameyaratibu, lakini kubwa kuliko yote ni kwa uwezo wao mkubwa wa kukusanya mapato ambayo yamepelekea mafanikio tuliyonayo na baadhi yake ambayo mimi nimeyaona katika jimbo langu. Kipekee niishukuru halmashauri kwa kazi kubwa waliyoifanya ya kukarabati kile kituo changu cha Afya pale Tazari.

Sambamba na hilo wanaendelea na ujenzi wa nyumba ya daktari, nawashukuru sana watu wa Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini. Sambamba na hayo niwashukuru pia kwa wazo lao la kuendesha matamasha haya ya wafanyabiashara, wajasiri amali wetu. Jambo hili ni zuri na kwa kweli linawafanya wafanyabiashara wetu wadogo wadogo ambao ni wajasiri amali wanapowaweka pamoja katika matamasha haya katika Wilaya yanajenga umoja wa uwelewao na wanapata nafasi ya kubadilishana mawazo. Jambo hili nawaomba Halmashauri waliendeleze kwa sababu ni moja kati ya jambo ambalo ni la kimaendeleo sana kwa wafasiri amali hawa walio wengi ambao ni wadogo wadogo.

Sambamba na hayo niwaombe Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini A walitupie macho sana jambo la barabara za ndani. Ukweli usiofichika eneo la jimbo langu ni eneo la utalii, lakini inasikitisha na inavunja moto hali za barabara zetu za ndani kufikia katika hayo maeneo tunayoyataka ni jambo ambalo hili kwa pamoja tunapaswa kulitizama kwa sote tumeelekeza nguvu zetu katika katika Sekta ya Utalii, lakini kwa kweli hali ya barabara zetu za ndani kwa sasa hazipitiki na mbovu kupita maelezo haya ninayoyasema mimi.

Mhe. Mwenyekiti, niiombe sana Halmashauri yetu kwa dhati kabisa walitizame jambo hili kwa jicho pana sana ili tuweze sasa kuona kwamba njia hizi zinapitika vizuri na watalii wetu wanafika katika maeneo yao kama vile walivyotarajia.

Mhe. Mwenyekiti, mimi katika mchango wangu nivitizame sasa vikosi vyetu vya SMZ sana mimi nitazungumzia kule jimboni kwangu kuna vikosi vya KMKM, kuna kikosi cha Zima Moto. Nikianza na Kikosi cha KMKM kilichopo pale Nungwi, Mhe. Waziri nakushukuru kile kikosi

kiko vizuri sana na ni lazima tuishukuru serikali. Tatizo moja lililokuwepo pale ni kwamba kile Kituo kipo karibu sana na bahari na wanahitaji vifaa vya kwenda kuwaokoa watu. Sote tukubaliane kwamba bahari yetu ni kali sana pale. Matokeo yanayojitokeza pale wao tunawategemea watusaidie katika kwenda kuyafikia yale matokeo kuwaokoa watu, Mheshimiwa kasema pale hivi tukiwa na viboti vidogo vidogo tunataka kwenda kuwafikia watu tunafikaje. Bahari ile ukali wake hakuna asiyeijua.

Mhe. Waziri pamoja na kuweka kile kituo cha Uwokozi pake ile ilikuwa ni kazi moja, kazi nyengine sasa ni kuwawezesha kuwapatia vifaa vya kikweli na vya kisasa ili waweze kuifanya ile kazi kwa ukamilifu, hili naliomba sana Mhe, Waziri tulichukulie kwa uzito wake kwa sababu kile kituo ni muhimu sana. Sambamba na hicho kuna kituo chetu chengine cha KMKM Kibwengo, kile kituo kinasikitisha sana, miundombinu yake yote ni mibaya sana, ukianza na ujenzi wenyewe wa kile kituo, kile kituo hakina umeme, kile kituo hakina maji, kile kituo hakina huduma yoyote. Pale tumewaweka wapiganaji wetu ambao hawa tunawategemea wafanye kazi ya kulinda lakini mazingira wanayoishi pale sio mazuri sana na sio rafiki sana. Hii ni mara yangu ya pili kusimama katika bajeti hii kukizungumzia kituo kile.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri kituo cha Kibwengo hakipo katika hali nzuri, wanahitaji msaada wa hali ya juu. Kwa bahati mbaya sana mazingira ya eneo lile pale pa Fukuchani yote ni ya chumvi wale wanajeshi wetu pale wanapata tabu hata maji ya kunywa, kwa sababu umeme upo mbali sana, wamejitahidi hata wao wenyewe binafsi kuchimba kisima lakini matokeo yake wamepata maji ya chumvi. Sasa njia pekee ya kuwaokoa ni kusogeza umeme pale, kwa sababu vipo visima jirani ambavyo wanaweza wakavitumia na nina hakika wataepukana na tatizo hilo. Sasa nakuomba sana Mhe. Waziri kwa mara nyengine tena kile kituo tukitizame kwa jicho la huruma.

Mhe. Mwenyekiti tukirudi tena kuna kituo chetu Kigunda cha Zimamoto kile kituo kipo vizuri lakini bado tunahitaji tuwaongezee vifaa kwa sababu majanga katika Wilaya yetu yamekuwa mara kwa mara na kwa kweli wanahitaji kupatiwa vifaa ili wafikie matokeo haraka iwezekanavyo kutokana na ukubwa wa eneo letu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niseme sasa nashukuru sana eneo hili la ugatuzi kuja katika Halmashauri zetu. Lakini nataka nizungumzie sana suala la elimu. Kati ya Wilaya zinazofanya vibaya sana katika Zanzibar ni Wilaya ya Kaskazini katika eneo la elimu. Maana mara zote tunakuwa wa tisa au wa kumi. Lakini zipo sababu kubwa mbili ambazo nimeziona mimi katika kipindi changu hichi cha uongozi.

Sababu ya kwanza tulikuwa tuna uhaba mkubwa wa madarasa katika eneo hili, lakini sababu ya pili kubwa ni uhaba mkubwa wa walimu katika maeneo haya. Mimi baada ya kupata nafasi hii nimesema nichukue jitihada za makusudi sana kuhakikisha kwamba tunapunguza uhaba wa madarasa. Kwa taarifa hivi sasa najenga madarasa 21 katika jimbo langu. Ni imani yangu nitakapoyamaliza madarasa 21 nawaomba Halmashauri sana wanisikie waje wanisaidie ili tumalize haya madarasa. Tukimaliza madarasa 21 katika jimbo langu nina imani tutakuwa tumepunguza kwa kiasi kikubwa upungufu wa madarasa. Lakini tunarudi katika upungufu wa walimu, hili nalo ni tatizo na nawaomba wahusika wote walichukue jamani katika Jimbo la

Nungwi kuna uhaba mkubwa, zaidi ya ukubwa wa walimu katika skuli zangu zote. Hili naliomba sana kupitia Baraza hili na kupitia bajeti hii tulichukue kwa uzito unaostahiki.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nimetaka niyaseme hayo lakini kwa sababu leo, ni mara yangu ya mwanzo katika kikao hichi kusimama naomba sasa niwape pole wananchi wote wa Zanzibar ambao wamekutwa na maafa ya mvua hizi zinazoendelea. Kwa bahati miongoni mwa waathirika wa matatizo haya ya mvua miongoni mwao ni watu wa jimbo langu, Nawapa pote wote walioathirikma na mvua, Mwenyezi Mungu atawapa subra na waone kwamba hiyo ni mipango yake. Na mimi kama Mwakilishi wao nasema siku zote tupo pamoja katika kufanya kila lile litakalokuwa limo ndani ya uwezo wangu na siku zote najua changamoto zao na mimi niko tayari kila wakati nawahakikishia kwamba sitowaangusha katika hili.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nimalizie mchango wangu kwa kuishukuru tena familia yangu kwa kuwa karibu nami kunifariji na hata pale wanaponikosa katika baadhi ya wakati kunivumilia. Nawashukuru sana. ahsante Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe wetu wa mwisho kwa leo atakaechangia ni Mhe. Hussein Ibrahim Makungu. Mheshimiwa karibu sana.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu: Mhe. Mwenyekiti, ahsante, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kufika hapa jioni hii kuchangia hotua hii muhimu sana. Nikushukuru na wewe Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi adhimu ya mwisho kuchangia hotuba ya Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Idara Maalum.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa kazi yake kubwa anayoifanya kwa Wizara hii na kujitahidi kwa umakini mkubwa sana na uzoefu aliokuwa nao. Pia nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri kwa kazi yake nzuri na watendaji wake wote kwa kazi yao nzuri wanayoifanya.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze kidogo kuwapongeza Wakuu wa Mikoa wote kwa kazi yao nzuri sana na Wakuu wa Wilaya wote wanaofanya kazi na watendaji wao wote wanaofanya kazi pamoja na Halmashauri zetu zote wanaofanya kazi zao hizo katika Mikoa yetu. Mimi nianzie hapa katika kuwapongeza hawa ndugu zetu wa Idara maalum kwa kufanya kazi yao kubwa hasa KMKM katika jengo la hospitali. Sasa hivi kama mnavyoona kazi imeshakamilika bado kununua vifaa vya tiba tu kidogo ili kumalizia hosptali yetu, mimi nawapongeza sana.

Mhe. Mwenyekiti, hospitali ile imo ndani ya jimbo langu na ikifanikiwa kumalizika mimi nitafaidika sana na wananchi wote wa Zanzibar watakuja pale. Pia niipongeze serikali sana kwa juhudi zao kubwa KMKM kuweza kununua boti ya uokozi kwa ajili yakitokezea maafa au majanga baharini wanaweza kujitahidi kwa sababu boti hii ya kasi na serikali kuweza kuona janga hili kuweza kununua.

Pia niwapongeze JKU, KVZ, Kikosi cha Zima Moto niipongeze sana serikali kwa kununua boti kwa ajili ya majanga hasa kwa upande wa baharini. Mimi nilisema katika Baraza lililopita kikosi cha Zima Moto kina kazi kubwa, lakini tuwaangalie sana Serikali iwapatie bima hawa ndugu zetu. Sasa sijui kama kazi hii Mhe. Waziri kama imeshafanyika lakini naomb sana tuwapatie

Bima kwa sababu linapotokea janga wanajitolea maisha yao kusaidia janga kuhatarisha maisha yao.

Mhe. Mwenyekiti, nipongeze Kikosi cha Mafunzo, Kikosi cha Valantia pia niwapongeze kwa kazi yao nzuri. Mimi nianzie katika ukurasa wa 78 huu mradi wa CCTV camera TV. Mimi hii mara ya pili nasema mradi huu mimi nilikwenda China kwenda kuukubali, na mnilikwenda sehemu nyingi hawa wenzetu wa ZTE walituonesha. Mradi huu kuna bilioni 20 hapa zinatakiwa zilipwe. Huu mradi serikali azma yake imalize kwa sababu hizi camera zinasaidia kwa ajili ya watalii. Kisiwa chetu hichi Zanzibar watalii wanaingia masaa 24, wanakuja na wanatembea. Camera hii itakapokuwa tayari itatusaidia, hivi camera zinafungwa katika nchi zilizoendelea Marekani, Uingereza Canada na sehemu mbali mbali. Kwa hivyo na sisi tukifanikiwa Mhe. Waziri kufunga hizi tutafanikiwa, watalii wetu watajua usalama wao upo tena wa uhakika. Hizi camera kama tunavyoziona ni wireless camera hata ukiwa nje ya nchi unaweza kuona matukio.

Mhe. Mwenyekiti, kama tunavyojua nchi yetu ni utalii na Mji Mkongwe ni sura ya Zanzibar, na hizi camera zimefungwa nyingi sana Mji Mkongwe. Kwahivyo mimi naomba sana wajumbe wasione shida kutoa hizi bilioni 20 kuupitisha mradi huu na pia zikalipwa kwa serikali yetu. Kwa sababu mipango imepangwa mingi sana mizuri kwa ajili ya camera hizi kununua sisi.

Mhe. Mwenyekiti, niseme kuhusu hizi barabara zetu sasa hivi vimeharibika sana. Kama tunavyojua hawa ndugu zetu wa Serikali za Mitaa washughulikie barabara hizi, Kama barabara hii ya *Airport* watalii wanakuja wanaingia. Juzi nimesema mashimo mengi njia mbaya, lakini ukiangalia Serikali za Mitaa watakuwa hawana fedha hasa Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharib fedha zake ajengee barabara zote kwa ajili ya hizi barabara za Mjini zote zimeharibika sasa hivi na hii ni sura ya Zanzibar. Naomba Wizara ya Mawasiliano iwashike mkono, isaidie kujenga hizi barabara isiwe wanatupiwa mzigo wao, hili suala la Zanzibar ni la taifa letu, na hii ni nchi yetu, wanapokuja wageni wanaona mashimo njia mbaya inakuwa haileti picha nzuri na kesho kutwa *season* inaanza mwezi wa sita.

Kwa hivyo mimi naomba sana tujitahidi Wizara ya Mawasiliano na Serikali za Mitaa, Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi pamoja wasaidiane na Wizara ya Mawasiliano wazuie mashimo na kuziweka hizi barabara vizuri sana. Ukiangalia na barabara za ndani kama wajumbe walivyosema sasa hivi hakuna kwenye bajeti hii. Naomba sana Mheshimiwa tuangalie barabara yangu ya Mwanyanya jimbo langu la Mtoni huu mwaka wa pili imetiwa kifusi na serikali za Mitaa na Halmashauri, naomba mara hii tuangalie itiwe lami barabara ile ya Mwanyanya kutoka kwa Hanzari mpaka kutokea kwa Kisasa ni mbaya mbaya. Jana mimi nimekwenda usiku Mheshimiwa gari nimeiwacha pahali nimeshindwa kupita. Kwa hivyo naomba sana hii mara ya pili serikali inatia kifusi njia ile inaharibika.

Niipongeze sana serikali kwa juhudi zao kubwa kutia taa za barabarani. Ukiangalia njia hii ya Amani ukishusha chini ya njia ya Gulioni, Mwembeladu kunang'ara taa zinawaka, ukenda Darajani, Mnazi Mmoja niipongeze sana serikali hizi taa mwaka jana zilikuwa hamna lakini serikali imejitahidi. Bado njia hii naomba serikali ijaalie kutoka *Airport* mpaka hapa Mjini ifanye haraka hara itie kwa sababu watalii wakishuka wanapitia njia hii. Naishukuru Serikali za Mitaa imeweza na Halmashauri zetu Mkuu wa Mkoa wa Mjini kwa kutia hizi taa katika sehemu mbali mbali za Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika Mkoa wa Mjini Magharibi kuhusu madawa ya kulevya. Mimi kwanza nataka nimpongeze sana Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi kwa kazi yake nzuri ya kupunguza haya mambo ya majanga ya madawa ya kulevya, tatizo limekuwa ni kubwa sana. Mimi nitoe mfano mzuri Mhe. Mkuu wa Mkoa ana rai nzuri sana sasa hivi ya kuvuta vijana na juzi juzi hapa kafanya tamasha Kisonge mziki pamoja na Zenji FM na yeye alikuwa mgeni Rasmi pale, tamasha likafanyika, vijana wengi walijaa lakini agizo kubwa au maelezo makubwa yalikuwa kuhusu Madawa ya Kulevya. Mimi nampongeza na akifanya tamasha kama hivi vijana wengi unawaelimisha pale wanakuwa wanaridhika bila ya kuwatumilia nguvu na kuweza kuwambia madhara ya madawa ya kulevya na alitoa *speech* nzuri na akawafahamisha na mimi nilikuwepo pale nikawa nialiona lile tamasha linavyofanyika.

Nampongeza sana na matamasha kama yale yaendelee kufanyika kwa vijana kwa sababu vijana ndio wanaoangamia kwenye madawa ya kulevya. Kwa hivyo wakipewa taaluma kama hii na viongozi wetu wanafarijika na wanafurahi, na kama kuna mambo mazuri wanaambiwa pale kama ajira kwa hivyo wanaingia tamaa wanakuwa na hamu na Serikali yao wanaipenda zaidi, kwa hivyo mimi nampongeza lakini Mheshimiwa madawa ya kulevya hapa tumeona kwenye kitabu cha bajeti karibu watu 25 wamekamatwa na kesi ipo Mahakamani. Lakini sasa mahkamani hawa watu wanaweza wakatoka bila ya kufungwa au kupewa adhabu yoyote. Sasa tuangalie serikali watu hawa waangaliwe kwa ushahidi mzuri kwa sababu tukisema tunawaachia kidogo hawa watu wataachiwa bila ya kupewa adhabu yoyote au faini yoyote. Mimi naomba sana serikali na Mahakama waangalie vizuri, huku tutafanya kazi vizuri kwenye serikali zetu za Mitaa na kwenye Mikoa lakini wakifika Mahakamani wanaachiwa. Naomba sana hili tuliangalie vizuri sana.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika ukurasa wa 29 niipongeze sana serikali kama kwenye kitabu kilivyoandika humu wazee 7881 wamepewa pencheni katika Wilaya ya Mjini Magharibu tu. Hili ni jambo la kupongezwa Serikali za Mkoa wa Mjini Magharibi lakini niipongeze Serikali ya Zanzibar na Mhe. Rais kwa kuliona hili wazee hawa wanapata Sh. 20,000/= kila mwezi. Kwa hivyo mimi nashukuru na azma ya Rais hii iende vizuri. Namshukuru Mkuu wa Mkoa wa Mjini kwa malengo haya anayoyafanya na nia yake nzuri. Hizi fedha zinafikwa kwa walengwa mia kwa mia, hakuna malalamiko kwa wazee aliyekuwa hapati fedha hizi.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika ukurasa wa 29 katika matamasha haya. Pia Mkuu wa Mkoa ana rai nyengine nzuri sana. Juzi hapa ilikuwa siku ya Jumamosi mimi nilikuwa na Semina Kariakoo ZSSF, kulikuwa kunatamasha kubwa sana pale kisonge. Kulikuwa kuna mziki, umewekwa pale na palikuwa na vijana wengi tangu saa 3;00 nimepita pale kushajaa watu. Lakini hapo walikuwa watu wanachangishwa damu, watu wanatoa damu kwa hiari zao. Siku ile mimi nilikuwa nikatoe damu kweli kweli lakini muda nilikuwa sijaupata nikuwa nipo kwenye Semina. Ilikuwa ukiangalia pale asilimia kubwa walikuwa ni vijana wanaotoa damu zile, kwa hiari na kwa kutaka wenyewe.

Ukiangalia kitabu katika ukurasa huu tumeona karibu jumla ya *packet* 1132 ya damu imekusanywa. Mheshimiwa tumpongeze sana kwa kazi anayoifanya. Kwa sababu hii kuchangia damu kwa hiari mtu kutoa sio kazi ndogo lakini utakuta vijana, kuanzia miaka 15 kwenda juu ndiyo wanaotoa damu, kuchangia. Damu ile inasaidia katika Hospitali zetu zote za rufaa kama

Mnazi Mmoja na sehemu nyengine. Mimi naipongeza sana kazi hii na serikali tuunge mkono sote jumla na viongozi mbali mbali, tujitahidi kuunga mkono hatua hizi zinazofanyika.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika habari ya ukurasa wa 29 niende katika kuchangia Mkuu wa Mkoa katika jimbo langu kuna skuli ya Sharifumsa katika kitabu kimesema kuna skuli ya madara manene na vyoo viwili vimejengwa. Mimi nimpongeze sana Mkuu wa Mkoa kwa kazi yake nzuri na kunijengea hii Skuli ya Sharimsa. Wananchi wangu wote wananisikia kuwa hii skuli Mkuu wa Mkoa kasema atajenga, na jambo la kumpongeza sana kwa kuwa na imani na watoto wetu waweze kusoma pale. Ingawa kuna changamoto ya maji safi na salama na pia madawati 250 na ameweza kujitahidi kuyapata madawati hayo. Nimpongeze kwa juhudi zake kubwa.

Mhe. Mwenyekiti, pia nimpongeze kwa skuli yangu ya Bububu ya Primary kachangia mifuko 100 ya saruji. Si jambo dogo la kumpongeza sana Mheshimiwa kwani hizi *Primary school* ndiyo zenye shida njia sasa hivi ni nyingi na wanafunzi ni wengi. Kwa hivyo juhudi yake kubwa hii mimi niipongeze. Kama walivyosema wenzangu Mhe. Asha Abdalla Mussa kasema kwamba bajeti zao wapate haraka hawa watu, sasa hivi kuna ugatuzi wa madaraka, bila ya kuwapa hizi fedha hawa Wakuu wa Mikoa hawatofanya kazi yoyote Mheshimiwa.

Mimi naomba bajeti yao hii tuipitishe bajeti hii, ikishakupita Mheshimiwa fedha zao wapewe haraka ili watufanyie kazi zetu kwa sababu tumewapa kazi ya kutusaidia kwenye mji wetu huu, kila Mkoa na Bajeti yao.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie haraka haraka kwenye ukurasa wa 31 Mkoa wa Mjini Magharibi huu ulipanga kukusanya karibu milioni 45, mimi nasema bado makusanyo yaliyokusanywa ni kidogo, Mkoa wa Mjini una vianzio vingi vya mapato. Mimi naomba sana tuangalie mapato gani wanaweza kukusanya mapato zaidi. Kama tunavyojua Mkoa wa Mjini watalii wengi wanaingia na kuna vianzio vya kitalii vingi. Kwa hivyo tujue mapato yanavyoingia utalii unakuwaje. Tuseme hata Mji Mkongwe watalii kuingia pia walipe, sisi tunataka mapato kwa sababu nchi yetu inaendeshwa na utalii, bila ya utalii hata mishahara yetu sisi tusingeipata, kwa sababu bajeti yetu karibu asilimia 70 tunapata kwenye pato la utalii. Naomba sana Mheshimiwa tuangalie hivi vianzio vya mapato.

Mhe. Mwenyekiti, niseme wenzangu wamesema hawa ma RC wetu Afisi zao ndogo, ukitizama Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi kwa kazi yake kubwa anashughulikia watu mpaka usiku saa 7 saa nane usiku yupo ofisini, watu wanakuwa wengi, ofisi ndogo, nafasi ndogo, hata usafiri wake saa nyengine inakuwa siyo wa uhakika gari yake, naomba sana na wenzangu wamesema tutafute gari japo za Mawaziri tuwape hawa Wakuu wa Mikoa watatu kwanza gari nzuri. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kumpa Mkuu wa Mkoa V8 ndiyo heshima yake ya mjini hapa aendeshe V8 kama magari ya mawaziri, sasa nafikiri kuna gari zilizobakia bakia Mheshimiwa japo tatu wapewe hawa wakuu wa Mikoa kwa heshima yao na kazi wanayoifanya ni kubwa kwa nchi yetu. Mimi naomba sana kwa heshima kwa Serikali na Mhe. Mohammed About, Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais japo Wakuu wa Mikoa wa watatu wa Unguja na watatu wa Pemba wapewe usafiri wa uhakika, Mkoa wa Mkoa anaingia hapa anaingia na gari yake ya maana kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo mimi muda najua hakuna lakini nishukuru sana na mimi naunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia kwa mia. Naomba Waheshimiwa Wajumbe wote tusipige buti bajeti hii, ipite kwa salama kwa sababu wana kazi kubwa ndugu zetu kutekeleza katika mikoa yetu.

Baada ya kusema hayo ahsante sana Mwenyekiti, nakushukuru.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe nawashukuru sana kwa kutimiza wajibu wetu vyema kwa kuchangia hotuba hii leo na hadi sasa naomba niakhirishe Baraza hili hadi kesho saa 3:00 pamoja majaaliwa ahsanteni sana.

(Saa 1:45 usiku Baraza liliakhirishwa mpaka tarehe 16/5/2018 saa 3:00 asubuhi)